JAMHURI YA KENYA

Mali ya
Serikali ya Kenya

HAKIUZWI

# Kiswahili 2

## Mazoezi ya Lugha

### Mwongozo wa Mwalimu



KIMEIDHINISHWA

KICD

KIMEAINISHWA KWA MTAALA ULIOJIKITA KWENYE UFARISI

Tusome Early Literacy Programme

# Kiswahili 2
## Mazoezi ya Lugha
### Mwongozo wa Mwalimu

# Yaliyomo


Utangulizi ........ ii
Dibaji ........ ii
Mwongozo kwa mwalimu ........ iii
Utangulizi ........ v
Mwongozo wa Mwalimu wa Kiswahili kwa Gredi ya 2 ........ vi
Tathmini ........ viii
Kamusi ya Kiswahili ........ ix
Michoro ya Kuashiria ........ xii
Shuleni 1 ........ 1
(Kipindi cha 1 hadi 5)
Shuleni 1 ........ 11
(Kipindi cha 6 hadi 10)
Haki zangu 1 ........ 21
(Kipindi cha 11 hadi 15)
Haki zangu 1 ........ 30
(Kipindi cha 16 hadi 20)
Usafi ri 1 ........ 35
(Kipindi cha 21 hadi 25)
Familia 1 ........ 40
(Kipindi cha 26 hadi 30)
Familia 2 ........ 45
(Kipindi cha 31 hadi 35)
Usalama wangu 1 ........ 50
(Kipindi cha 36 hadi 40)
Hali ya anga 1 ........ 55
(Kipindi cha 41 hadi 45)
Lishe bora 1 ........ 60
(Kipindi cha 46 hadi 50)
Marejeleo 1 ........ 65
(Kipindi cha 51 hadi 55)
Mnyama nimpendaye 1 ........ 70
(Kipindi cha 56 hadi 60)
Mnyama nimpendaye 2 ........ 75
(Kipindi cha 61 hadi 65)
Shuleni 2 ........ 80
(Kipindi cha 66 hadi 70)
Shuleni 2 ........ 85
(Kipindi cha 71 hadi 75)
Haki zangu 2 ........ 92
(Kipindi cha 76 hadi 80)
Haki zangu 2 ........ 97
(Kipindi cha 81 hadi 85)
Usafiri 2 ........ 102
(Kipindi cha 86 hadi 90)
Familia 2 ........ 107
(Kipindi cha 91 hadi 95)
Familia 2 ........ 112
(Kipindi cha 96 hadi 100)
Marejeleo 2 ........ 117
(Kipindi cha 101 hadi 105)
Usalama wangu 2 ........ 122
(Kipindi cha 106 hadi 110)
Usalama wangu 2 ........ 127
(Kipindi cha 111 hadi 115)
Hali ya anga 2 ........ 132
(Kipindi cha 116 hadi 120)
Hali ya anga 2 ........ 137
(Kipindi cha 121 hadi 125)
Lishe bora 2 ........ 142
(Kipindi cha 126 hadi 130)
Mnyama nimpendaye 3 ........ 147
(Kipindi cha 131 hadi 135)
Shuleni 3 ........ 152
(Kipindi cha 136 hadi 140)
Shuleni 3 ........ 158
(Kipindi cha 141 hadi 145)
Marejeleo 3 ........ 164
(Kipindi cha 146 hadi 150)



© 2021 ya RTI International kwa nchi zote isipokuwa Jamhuri ya Kenya.

RTI International ni alama na jina la kibiashara la Research Triangle institute.

Haki ya Kunakili ya Jamhuri ya Kenya inashikiliwa na wizara ya elimu Kenya.



Chapisho hili limefanikishwa kupitia kwa ufadhili kutoka kwa shirika la kimataifa na maendeleo la America (USAID) kupitia mradi wa USAID -Tusome.



Kazi hii inapatikana chini ya leseni ya Attribution-NonCommercial-NoDerivatives 4.0 International (CC BY-NC-ND 4.0). Ili kuona nakala ya leseni hii, tembelea https://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/4.0/ ama tuma barua kwa Creative Commons, sanduku la posta 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

**Kunukuu na kutambua kazi asili** — Ukinakili na kusambaza kazi hii tafadhali nukuu kama ifuatavyo: *Imenakiliwa kutokana na kazi asili ya RTI International na kuruhusiwa chini ya leseni ya Attribution-NonCommercial-NoDerivatives 4.0 International (CC BY-NC-ND 4.0).*

**Si ya Biashara** — Usitumie kazi hii kwa nia ya biashara.

**Si ya Kuigaiga na Kusambazwa** — Usisambaze kazi hii kama utaifanyia mabadiliko kazi asili pamoja na kuichanganya na kazi nyingine, kuitumia kama msingi wa kazi nyingine au kuibadilisha kwa njia yoyote ile.

**Kazi ya Mtu wa Tatu** — Sio lazima RTI International kumiliki kila kipengele cha maudhui yaliyomo katika kazi hii. Hivyo basi, RTI international haikuhakikishii ya matumizi ya kipengele chochote cha kazi ya mtu mwingine au baadhi ya kazi yake haitakiuka haki za watu hao. Utawajibika kutokana na hatari ya kudaiwa kutokana na kuingilia haki za wengine. Ukitaka kutumia tena kipengele cha kazi hii, ni jukumu lako kuamua kama imeruhusiwa kutumia tena na kupata ruhusa kutoka kwa mwenye hati ya kunakili. Baadhi ya mifano ya vipengele hivi ni majedwali, maumbo na picha.



Kimechapishwa nchini Kenya kwa ufadhili kutoka kwa USAID (U.S. Agency for International Development) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

ISBN: 978 9966 110 11 4

Toleo la Kwanza

Kimechapishwa 2018

# Utangulizi

Serikali ya Kenya imejitolea kutoa elimu bora kama haki ya kimsingi kwa wanafunzi wote. Azma hii inaambatana na majukumu ya kitaifa na kimataifa yanayohitaji kila nchi kuyakimu mahitaji ya kielimu na kijamii ya raia wake. Ingawa juhudi zimefanywa kuhakikisha elimu inapatikana kwa urahisi, lengo kuu la serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata elimu bora. Serikali ya Kenya imewekeza zaidi katika kuboresha vifaa vya kielimu, miundomsingi pamoja na wafanyakazi ili kuinua kiwango cha elimu inayotolewa katika viwango vyote vya elimu nchini. Mfumo wa elimu unaolengwa umebuniwa kutokana na matokeo ya utafiti wa kina. Kadhalika umejumuisha mbinu zingine zinazokubalika na kutumiwa kimataifa. Msukumo uliopo katika mageuzi ya elimu unatokana na haja ya kuifanya elimu nchini Kenya kuwa kwenye kiwango cha kimataifa na kuwa ya manufaa kiuchumi katika jamii. Serikali inahakikisha kwamba kupitia elimu, wananchi watakuwa wabunifu na kupata stadi za karne ya 21 ikiwemo utafiti, kutatua matatizo, kufikiria kwa kina na kufanya kazi katika hali zote.

Vitabu vya Tusome vimeshirikisha maadili ya mtaala mpya na vimeandikwa ili kuimarisha uwezo wa kujua kusoma na kuandika, uwezo ambao ni stadi ya kimsingi katika elimu bora. Kitabu hiki kitatumika katika Gredi ya 2 kujifunza na kufundishia Kiswahili katika mtaala mpya. Mpangilio wa kitabu hiki unatilia maanani maantiki na mikakati inayotokana na utafiti ili kukuza stadi za kusoma na kuandika. Vilevile, mpangilio huu utahakikisha kuwa wanafunzi wanapata umilisi ambao ni muhimu kwa viwango vyao.

Ninawasihi washikadau wote kuendelea kuunga mkono mageuzi yanayoshughulikiwa katika sekta ya elimu nchini Kenya ili kufikia matokeo bora.

[redacted]

Waziri wa Elimu

# Dibaji

Wizara ya Elimu imejitolea kuwapa Wakenya elimu bora kama ilivyo katika Katiba ya Kenya, ya mwaka wa 2010. Mabadiliko yanayoendelea katika elimu yanalenga kushughulikia uwepo wa elimu bora. Mipango ya utafiti kama vile Tathmini ya Kitaifa ya Ufuatiliaji wa Mafanikio ya Masomo (NASMLA) na Muungano wa Kusini na Mashariki ya Afrika wa Kufuatilia Ubora wa Elimu (SACMEQ) imeangazia mianya ambayo inafaa kushughulikiwa ili kuboresha matokeo ya elimu.

Matukio ya hivi punde katika mfumo wa elimu yanasisitiza uwezo wa kusoma na kufanya hesabu kama nguzo ya kujifunza katika darasa tangulizi. Umakinifu katika elimu umechangia hatua ambazo zimeimarisha matokeo ya kusoma na kufanya hesabu. Mradi wa kitaifa wa Tusome umeimarisha uwezo wa mwanafunzi wa kusoma na kuandika katika Gredi ya 1 na ya 2. Matokeo haya bora yamechangia kuendelezwa kwa mradi huu hadi gredi ya 3. Kitabu hiki kimeandikwa ili kuelekeza mafunzo ya Kiswahili kiwango cha Gredi ya 2 katika mtaala mpya. Mbinu za ubunifu katika kujifunza na kufundisha pamoja na Masuala Mtambuko yameangaziwa kulingana na mtaala mpya.

Wizara ya Elimu inatambua usaidizi wa kifedha kutoka kwa shirika la usaidizi la Marekani (USAID). Kadhalika, ningependa kutoa shukrani zangu kwa washirika na washikadau wengine kwa mchango wao katika uandishi na uchapishaji wa kitabu hiki.

[redacted]

Wizara ya Elimu.

# Mwongozo kwa mwalimu

Mwongozo huu wa mwalimu umejikita kwenye mfumo wa kufundisha wa moja kwa moja. Mbinu hii humsaidia mwalimu kufundisha wanafunzi akitumia ujuzi wa kimsingi ambao unahitajika katika kuboresha ufasaha wa kusoma, kufahamu na kuandika. Mbinu hii huzingatia hatua tatu rahisi: kuonyesha kwa mfano, maongozi kwenye mazoezi na mazoezi huru au tathmini. Kwa kutumia mbinu hii, mwalimu huweka mikakati iliyosawazishwa ya kufundishia na kuonyesha mkusanyiko wa shughuli ndani ya darasa. Mbinu hii huruhusu ubunifu wa mwalimu. Japo matayarisho ya mwalimu ni muhimu kufanikisha somo akitumia mwongozo huu, mwalimu anahimizwa kubuni, kutayarisha na kutumia nyenzo za kufundishia zinazolingana na muktadha utakaoboresha umilisi wa maudhui yanayofundishwa. Nyenzo hizi zinaweza kujumuisha vifaa halisi, vifaa vya kidijitali, picha, ramani, kamusi na kadhalika.

Matumizi ya ubao ni muhimu na yanatiliwa mkazo katika mwongozo huu. Hata hivyo, inampasa kila mwanafunzi kuwa na kitabu chake mwenyewe ili kuongeza uzoefu wake wa kusoma. Zaidi ya hayo, kuna mazoezi kwenye kitabu cha mwanafunzi ambayo yanawahitaji wanafunzi kuyafanya peke yao darasani. Kazi ya ziada pia imejumuishwa ili wanafunzi wafanye mazoezi wakiwa nyumbani. Lengo kuu haswa ni kuhakikisha kuwa mlezi au mzazi anashirikishwa katika jitihada za kumwezesha mwanafunzi kufaulu masomoni. Walimu wanahimizwa kuangalia kazi ya wanafunzi ili kuhakikisha kuwa mazoezi yote yanafanywa na kutoa tathmini yenye maana kwa wakati ufaao. Ni vyema kukumbuka pia kwamba walimu hawapaswi kuhisi kuwa wamezuiwa kuwapa wanafunzi kazi nyingine zifaazo za ziada. Ikiwa wanahisi kuwa wanafunzi wanahitaji mazoezi zaidi, wanapaswa kutumia uamuzi wao kutoa mazoezi yanayofaa kama kazi ya ziada.

Walimu pia wanahimizwa kuchagua shughuli zitakazofanikisha uelewa wa wanafunzi wa dhana zinazofundishwa. Shughuli hizi zinajumuisha maonyesho, maigizo au maelezo kwa kutumia maneno mafupi, rahisi na yanayoeleweka.

Mwongozo huu pia umeshughulikia masuala yaliyopewa kipau mbele katika mtaala mpya kama vile umilisi wa kimsingi, masuala mtambuko na maadili, nk. Vile vile mwongozo huu wa mwalimu umeundwa kwa njia inayoondoa vizuizi vya ujifunzaji bora. Hivyo basi, mwongozo huu unakidhi mahitaji ya wanafunzi wote (hata wenye ulemavu) kwa kuzingatia viwango vyao vya kuelewa na changamoto zao. Wanafunzi kama hawa wanaweza kusaidiwa na walimu kwa njia kadha wa kadha. Zifuatazo ni baadhi ya njia anazoweza kutumia mwalimu kuwasaidia wanafunzi wenye changamoto tofauti za kujifunza.

Namna ya kushughulikia wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

1. Mwalimu anapaswa kutafuta mbinu ya kushughulikia wanafunzi wenye mahitaji maluum. Baadhi ya mahitaji haya ni kama vile:
   a) matatizo ya kusikia.
   b) matatizo ya kuona.
   c) udhaifu wa kusoma, kuandika na kuelewa mambo haraka.
   d) udhaifu wa kuwasiliana. Kwa mfano, mtoto aliye na kigugumizi na kadhalika.
   e) udhaifu au ulemavu wa viungo vya mwili.
   f) walio wepesi katika kuelewa mambo haraka kuliko wale wa wastani.
2. Ni muhimu kwa mwalimu kutambua uwezo na udhaifu wa kila mwanafunzi kabla ya, wakati wa na baada ya somo. Kufanya hivi kutamwezesha kushughulikia mahitaji hayo kwa njia inayofaa ili yasiathiri mafanikio ya somo. Mifano ya mahitaji maalumu na namna ya kuyashughulikia imetolewa katika Jedwali la 1.

**Jedwali la 1: mahitaji maalum ya wanafunzi na mapendekezo na namna ya kuyashughulikia**

| Mahitaji | Mapendekezo na Namna ya Kuyashughulikia |
|---|---|
| a) Matatizo ya kutosikia | - Tumia lugha ya ishara inapowezekana.<br>- Mwanafunzi aketi karibu na mwalimu au pale anapoweza kusikia vizuri.<br>- Himiza matumizi ya vipazasauti inapowezekana.<br>- Matumizi ya vifaa halisi yanahimizwa. |
| b) Matatizo ya kutoona vyema | - Mwanafunzi aketi karibu au mbali na ubao kulingana na mahitaji yake.<br>- Himiza matumizi ya breli (braille) inapofaa.<br>- Jadili na wazazi au walezi matumizi ya miwani au vioo vya kukuza kimo cha maandishi.<br>- Epuka ama ondoa vifaa vinavyoathiri uwezo wa kuona.<br>- Mwanafunzi aketi karibu au mbali na mwangaza kulingana na mahitaji yake.<br>- Matumizi ya vifaa halisi yanahimizwa. |
| c) Udhaifu wa kusoma, kuandika na kuelewa mambo kwa haraka | - Wape wanafunzi hawa muda mwingi wa ziada kuliko wanafunzi wengine.<br>- Watengewe muda maalumu wa kurejelea waliyosoma baada ya somo.<br>- Gawa somo kwa hatua fupi fupi kuanzia nyepesi hadi hatua tatanishi.<br>- Wape mazoezi ya ziada.<br>- Mwalimu awakinge wanafunzi walio na udhaifu dhidi ya kudunishwa kwa njia yoyote ile. |
| d) Udhaifu wa kuwasiliana/ kigugumizi | - Wape wanafunzi muda wa kuwasilisha mawazo yao.<br>- Mwalimu aepukane na vitendo vinavyoweza kuathiri hisia au maono ya wanafunzi.<br>- Mwalimu atumie mbinu tofauti za mawasiliano ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi. |
| e) Udhaifu au ulemavu wa viungo vya mwili | - Mwanafunzi apewe muda wa ziada ili kukidhia upungufu (ulemavu) wake.<br>- Wapewe vifaa vya kidijitali ikiwezekana au vya kubuniwa kulingana na hali ya ulemavu ili kuongeza uwezo wa utenda kazi wao.<br>- Mwalimu anaweza kushauriana na wahudumu wa walemavu kwa usaidizi zaidi. |
| f) Walio wepesi katika kuelewa mambo haraka kuliko wale wa wastani | - Wanafunzi wapewe kazi ya ziada ili watumie muda wao vyema.<br>- Wanafunzi wapewe nafasi za kukuza vipawa vyao.<br>- Wanafunzi wapewe kazi zenye changamoto zaidi ili kufanyisha kazi akili zao na kuwapa fursa ya kutumia wepesi wao wa kuelewa. |

# Utangulizi

Mwongozo huu umendaliwa kwa maelekezo ya wataalamu wa kimataifa na wa hapa nchini wa kusoma na wa lugha kwa kufuata mchakato uliopangwa kwa utaratibu. kwenye warsha ya kwanza ya maafisa wa Wizara ya Elimu na ya Taasisi ya Mitaala ya Kenya, upeo na mpangilio ulibuniwa ambao umekuwa ramani kwa kuendeleza mpangilio wa somo. kwenye warsha hiyo, maamuzi yaliafikiwa kuhusu ujuzi wa kukuzwa miongoni mwa wanafunzi kwa kila muhula na shughuli maalum ambazo zingetumiwa kutimiza malengo ya ufundishaji na ujifunzaji.

Kuna jaribio la wazi la kuwa na mwendelezo wa herufi na sauti kutoka kwa gredi ya 2. Vilevile kuna msisitizo wa kusoma maneno magumu zaidi yenye uwiano tata kati ya herufi na sauti na kuwasilisha kwa mwanafunzi mikakati mingine ya kusoma maneno.

Matini kwenye masomo yanawiana kimandhari na silibasi ya Taasisi ya Mitaala ya Kenya. Matini zimeundwa kwa uangalifu ili mwanafunzi aelewe aina tofauti ya maandishi huku pia akitilia maanani misamiati ya kimandhari. Kila matini inajumuisha mifumo ya maneno na miundo husika ya lugha. Ili kuboresha ufahamu wa wanafunzi wa matini, baadhi ya mbinu za ufahamu zinazolingana na kiwango chake zimetumiwa ili kumpa mwanafunzi mbinu tofauti za kuelewa matini.

Kila mpango wa somo unajumuisha shughuli tofauti zilizopangwa ili kukuza ujuzi na ufahamu wa mwanafunzi wa lugha ya Kiswahili. Shughuli za somo ni simulizi na za kuandika zikizingatia stadi nne za lugha (kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika). Katika masomo manne ya kwanza, wanafunzi hujifunza na kufanya mazoezi ya matumizi ya maneno, kusoma hadithi, ufahamu na sarufi. Somo la tano linazingatia marejeleo na shughuli za kutathmini zitakazosaidia mwalimu kufuatiliza maendeleo ya mwanafunzi. Mambo haya yametolewa, japo kwa muhtasari katika Jedwali la 3.



Hakiuzwi

## Mapendekezo ya mgawanyiko wa muda wa kila somo

### (Gredi ya 2, Kipindi cha 1-150)

| Sehemu | Utangulizi 1 | Kipindi cha mazoezi 1 | Utangulizi 2 | Kipindi cha mazoezi 2 | Kipindi cha marejeleo (Tathmini) |
|---|---|---|---|---|---|
| Utambuzi wa sauti | 3 | | 3 | | |
| Jina laherufi na sauti | 3 | 3 | 3 | 3 | 2 |
| Silabi | 3 | | 3 | | |
| Kusoma maneno kwa kutumia silabi | 3 | | 3 | | |
| Kusoma maneno marefu | | 4 | | 4 | |
| Jedwali la silabi | | | | | 5 |
| Sarufi | | 9 | | 9 | 5 |
| **Hadithi ya mwanafunzi** | | | | | |
| Kabla ya kusoma hadithi | 4 | 3 | 4 | 3 | |
| Wakati wa kusoma hadithi | 5 | 6 | 5 | 6 | |
| Baada ya kusoma hadithi | 4 | | 4 | | |
| **Hadithi ya mwalimu** | | | | | |
| Kabla ya kusoma hadithi | | | | | 5 |
| Wakati wa kusoma hadithi | | | | | 5 |
| Baada ya kusoma hadithi | | | | | 3 |
| Kuandika | | | | | 5 |
| Zoezi | 5 | 5 | 5 | 5 | |
| | **30** | **30** | **30** | **30** | **30** |

# Mwongozo wa Mwalimu wa Kiswahili kwa Gredi ya 2

| Utangulizi 1 | Kipindi cha mazoezi 1 | Utangulizi 2 | Kipindi cha mazoezi 2 | Kipindi cha marejeleo (Tathmini) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | 32 | 33 | 34 | 35 |
| 36 | 37 | 38 | 39 | 40 |
| 41 | 42 | 43 | 44 | 45 |
| 46 | 47 | 48 | 49 | 50 |
| 51 | 52 | 53 | 54 | 55 |
| 56 | 57 | 58 | 59 | 60 |
| 61 | 62 | 63 | 64 | 65 |
| 66 | 67 | 68 | 69 | 70 |
| 71 | 72 | 73 | 74 | 75 |
| 76 | 77 | 78 | 79 | 80 |
| 81 | 82 | 83 | 84 | 85 |
| 86 | 87 | 88 | 89 | 90 |
| 91 | 92 | 93 | 94 | 95 |
| 96 | 97 | 98 | 99 | 100 |
| 101 | 102 | 103 | 104 | 105 |
| 106 | 107 | 108 | 109 | 110 |
| 111 | 112 | 113 | 114 | 115 |
| 116 | 117 | 118 | 119 | 120 |
| 121 | 122 | 123 | 124 | 125 |
| 126 | 127 | 128 | 129 | 130 |
| 131 | 132 | 133 | 134 | 135 |
| 136 | 137 | 138 | 139 | 140 |
| 141 | 142 | 143 | 144 | 145 |
| 146 | 147 | 148 | 149 | 150 |



Hakiuzwi

## Tathmini

Mfumo mpya wa elimu unadhamiria kuhakikisha kuwa matokeo ya mafunzo ni ujenzi wa umilisi utakaomwezesha mwanafunzi kutumia ujuzi wake kujiendeleza. Kutokana na hayo, mwongozo huu umezingatia tathmini katika kila kipindi na mwishoni mwa kila wiki.

| Mada | Mada Ndogo | Mapendekezo ya tathmini |
|---|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | Kusikiliza kwa makini | - Tathmini matumizi ya mwanafunzi ya ishara.<br>- Uliza maswali |
| | matamshi | - Tathmini anavyotamka maneno.<br>- Tathmini matumizi ya maneno katika mazungumzo. |
| | Msamiati | - Tathmini anavyotamka msamiati lengwa na anavyotumia msamiati huo kujieleza au kutunga setensi na katika maandishi. |
| | Muundo wa lugha na matumizi yake. | - Tathmini anavyotunga sentensi katika miktadha tofautitofauti na ikiwa anazingatia muundo mwafaka wa lugha katika mazungumzo na katika maandishi.<br>- Unaweza kutumia maswali kupima uelewa wao wa muundo lengwa wa lugha. |
| Kusoma | Ufahamu wa jina na sauti ya herufi. | - Tathmini ufahamu wao wa jina na sauti ya herufi lengwa na anavyotumia ujuzi huo kusoma maneno mapya. |
| | Kusoma maneno | - Tathmini ufasaha wao wa kusoma maneno, kucheza michezo ya maneno na mbinu wanazotumia kusoma maneno mapya. |
| | Kusoma matini kwa ufasaha. | - Tathmini ufasaha wao wanaposomeana wakiwa wawiliwawili, katika darasa zima au akiwa peke yake.<br>- Tathmini iwapo anazingatia shadda na kiimbo wakati wa usomaji. |
| | Ufahamu | - Waulize wanafunzi watabiri kabla ya kusoma hadithi na uhakiki utabiri huo baada ya kusoma hadithi.<br>- Tathmini pia wanavyosimulia hadithi waliyoisoma, jibu maswali ya ufahamu au kujadili wahusika na muktadha wa matini lengwa. |
| Kuandika | Hati | - Tathmini nakala zao za maneno na sentensi au michoro hasa wakati wa imla na kuandika. Zingatia maumbo na mpangilio mwafaka wa maneno. Tumia kazi zao kujadili kuhusu hati nadhifu. |
| | Tahajia | - Tathmini ikiwa wamezingatia tahajia katika maandishi yao. Unaweza kutumia kadi za herufi na kamusi katika tathmini hiyo. |
| | Uakifishaji | - Tathmini usahihi wa uakifishaji wao (herufi kubwa/ ndogo, koma, kituo na kiulizi) katika maandishi na ikiwa wanaweza kutambua alama lengwa za uafikishaji. |
| | Mwongozo wa uandishi. | - Tathmini mazoezi yao yanayozingatia kujaza nafasi katika sentensi, kuandika sentensi kutokana na picha au hadithi. Zingatia usahihi wa sentensi zao katika maandishi. |

# Kamusi ya Kiswahili

| **Msamiati** | | **Maana** |
|---|---|---|
| Ajali | – | tukio lenye madhara linalotokea ghafla bila kupangwa. |
| Akatuzwa | – | akapewa zawadi. |
| Amu | – | kaka wa baba. |
| Anga | – | uwazi ulioko juu ya dunia. |
| Babu | – | mzazi wa kiume wa baba au mama. |
| Baridi | – | hali ya kutokuwa na joto; hali ya kupoa. |
| Basi | – | gari kubwa la kubebea abiria/neno la kuashiria kikomo au mwisho wa jambo. |
| Bendeji | – | kitambaa cheupe kinachotumiwa kufungia jeraha, donda au mahali palipoumia. |
| Bendera | – | kitambaa chenye rangi maalum au nembo kinachotambulisha nchi. |
| Binafsi | – | wewe mwenyewe, peke yako. |
| Binamu | – | mtoto wa mjomba au shangazi au ami. |
| Binti | – | mtoto wa kike. |
| Bustani | – | mahali pa kupumzika palipopandwa miti au maua. |
| Chakula | – | ni kile kinacholiwa na watu kwa kudumisha maisha yao. |
| Chumvi | – | madini meupe ambayo hutiwa katika chakula wakati au baada ya kupika ili kuongeza ladha. |
| Dada | – | ndugu wa kike. |
| Daraja | – | kivuko kilichojengwa kwa ajili ya kuvukia mto au bahari. |
| Darasa | – | chumba cha mafunzo shuleni. |
| Dawa | – | kitu anachopewa mgonjwa ili kutibu ugonjwa aalionao. |
| Dhuluma | – | kumtendea mtu mambo maovu au kumnyima haki yake. |
| Elimu | – | mpango wa mafunzo yanayopatikana shuleni, vyuoni, maishani, n.k. |
| Familia | – | watu wa ukoo mmoja. |
| Farasi | – | mnyama wa jamii ya punda lakini mkubwa zaidi anayetumiwa kubeba watu au mizigo. |
| Fisi | | – mnyama wa porini mwenye rangi ya kijivu na anayekula mizoga |
| Gwaride | – | paredi. |
| Haki | – | kitu au jambo mtu anastahili kupata. |
| Hakuhitimu | – | hakufaulu. |
| Halati | – | dada wa mama. |
| Hewa | – | upepo mwororo unaozunguka ardhi na ambao unavutwa na viumbe. |
| Hodari | – | mtu aliye na ujuzi wa kufanya jambo vizuri kuliko wengine. |
| Hongera | – | pongezi. |
| Huduma ya kwanza | – | msaada wa tiba anaopewa mgonjwa au majeruhi kabla ya kupelekwa hospitali au kwa daktari. |
| Humlinda | – | humweka salama; angalia ili kuepusha na madhara au hasara. |
| Huogopa | – | hushindwa kukabili jambo. Hupata hofu. |
| Iligongwa | – | ilipigwa na kitu kingine kwa nguvu hadi ikatoa mlio au kikavunjuka au kubonyee. |
| Jua | – | gimba kubwa lenye nuru kali lililoko angani ambalo hutoa mwanga na joto. |
| Kaka | – | ndugu wa kiume. |
| Kamanda | – | kiongozi wa polisi. |
| Kame | – | eneo au sehemu isiokuwa na maji ya kuotesha mimea. Eneo kavu. |
| Katiba | – | jumla ya sheria ambazo huiwezesha serikali itawale. |



Hakiuzwi

Kikivuja gesi – gesi kutoka kwenye mtungi wake.

Kipenga – kitu kinachotoa sauti kinapopulizwa.

Kiranja – kiongozi au mwakilishi wa wanafunzi shuleni au darasani.

Kivukio cha barabara – mahali ambapo pametengwa kuvukia barabara.

Kupewa jina – hali ya kumpa jina mtoto anapozaliwa.

Kutuarifu – kutujulisha/kutufahamisha/kutupasha.

Kuzama maji – kuingia ndani ya maji na kwenda chini.

Kuzingatia – kutilia maanani.

Lishe bora – aina mbali mbali ya vyakula vilivyo muhimu kwa kuimarisha afya yetu.

Madini – vitu vinavyopatikana kwenye vyakula au vinavyotiwa kwenye vyakula kama vile chumvi ili kuongeza ladha, n.k.

Maganda – sehemu za nje za matunda, mahindi, n.k (umoja - ganda, wingi - maganda)

Magonjwa – maradhi, hali ya watu kutosikia vizuri mwilini; kuwa na afya mbaya.

Majeraha – mikato au michubuko ilio katika mwili ambayo haijatunga usaha.

Maktaba – mahali mnamohifadhiwa vitabu ambamo watu huruhusiwa kuvisoma au kuviazima kwa muda.

Malezi bora – ukuzaji wa mtoto kwa kutarajiwa na kufuata tabia na mwenendo unaostahili.

Mama – mzazi wa kike.

Mama mdogo – dada mdogo wa mama.

Matatu – basi dogo linalobeba abiria mijini nchini Kenya, hasa kwa safari fupifupi.

Matibabu – dawa na huduma inayotolewa kwa mgonjwa na daktari.

Matone – sehemu ndogo ya kitu kiowevu kinachodondoka.

Mavazi – nguo tunazovaa.

Mbuzi – mnyama mkubwa kiasi wa miguu minne anayefugwa kwa ajili ya kutoa nyama au maziwa.

Meli – chombo kikubwa cha baharini kilichoundwa kwa chuma na kinachokwenda juu ya maji.

Mjomba – ndugu wa kiume wa mama.

Mkanda – kamba ya ngozi au nguo inayovaliwa kiunoni.

Mkoba – mfuko mdogo unaotumiwa kubeba mizigo, bidhaa.

Moto – joto kali linaloweza kuunguza.

Mpwa – mtoto wa dada au kaka.

Mshindo – sauti kubwa na nzito inayosababishwa na mgongano, mwanguko wa kitu kizito au mlipuko.

Mvua – matone ya maji yanayodondoka kutoka kwenye mawingu.

Mwalimu mkuu – kiongozi wa walimu ambaye anasimamia shule.

Ndege – chombo cha angani cha kusafiria abiria au kusafirishia mizigo, chenye injini na mabawa. Eropleni.

Ngamia – mnyama mkubwa mwenye nundu, ambaye hutumika katika safari za jangwani. Huishi sehemu kame.

Ng’ombe – mnyama mkubwa wa miguu minne wa kufugwa nyumbani kwa ajili ya maziwa au nyama.

Nyanya – mzazi wa kike wa baba au mama.

Ofisi – chumba ambacho wafanyikazi hukaa na kuhudumia watu

Paa – sehemu ya juu ya nyumba.

Pikipiki – chombo cha usafiri kinachofanana na baiskeli lakini kinachoendeshwa kwa nguvu za mota na petroli au dizeli

| | | |
|---|---|---|
| Potovu | – | kitu chenye sifa mbaya. |
| Protini | – | madini yanayopatikana katika aina mbalimbali za vyakula k.v nyama, mayai ambayo ni muhimu katika kujenga misuli ya mwili. |
| Punda | – | mnyama wa nyumbani anaetumiwa kubeba mizigo. |
| Sare | – | mavazi yanayofanana ambayo huvaliwa na vikundi vya watu kama vile wanafunzi. |
| Shangazi | – | ndugu wa kike wa baba. |
| Sifa | – | umaarufu. |
| Stadi | – | hodari; anayejua mambo. |
| Tabuleti | – | chombo cha kidijitali cha mawasiliano mfano wa simu. |
| Talanta | – | kuwa na ujuzi wa kufanya jambo |
| Tamaduni | – | mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani. |
| Tembe | – | kidonge cha dawa |
| Trafiki | – | askari ambaye anaangalia usalama barabarani. |
| Trafiki | – | kitu kinachohusu usafiri na barabara |
| Tulivu | – | iliyotulia |
| Ukosefu | – | hali ya kutokuwa na kitu fulani. |
| Upepo | – | hewa isiyotulia na aghalau huenda kwa kasi, hewa hii huvuma kwa nguvu na huweza kuleta hasara na uharibifu wa mali. |
| Upungufu | – | hali ya kutokuwa na viwango vya kutosha vya madinini fulani ya chakula mwilini. |
| Utahatarisha | – | tia katika hatari. |
| Utamaduni | – | desturi za kundi la jamii fulani, mila. |
| Uwanjani | – | eneo linalotumika kucheza michezo mbalimbali. |
| Vita | – | mapigano baina ya watu, wanyama au mataifa. |
| Vitamini | – | ni kirutubishi kinachohitajika na mwili kwa kujenga afya yake. Hupatikana hasa kwenye matunda kama machungwa n.k |
| vitamini | – | madini yanayopatikana katika aina mbalimbali ya vyakula ambayo ni muhimu kuufanya mwili uwe na afya kinga dhidi ya maradhi. |
| Vyoo | – | mahali pa kwenda haja. |
| Waangalifu | – | wawe makini |
| Wakihatarisha | – | wakitia katika mashaka au taabu. |
| Wanga | – | ni sehemu muhimu ya chakula katika vyakula kama ugali, ndizi, viazi, pasta na mkate. |
| Washa moto | – | kufanya moto uwake. |
| Yamepambwa | – | yamerembeshwa. |
| Zahanati | – | mahali pa kutolea matibabu ya magonjwa madogo madogo; hospitali ndogo. |
| Zizi | – | boma lililojengwa maalumu kwa kufugia/hifadhi mifugo kama vile ng’ombe, mbuzi na kondoo. |
| Vyoo | – | Mahali pa kwenda haja. |
| Waangalifu | – | Wawe makini |
| Wakihatarisha | – | Wakitia katika mashaka au taabu. |
| Wanga | – | Ni sehemu muhimu ya chakula katika vyakula kama ugali, ndizi, viazi, pasta na mkate. |
| Washa moto | – | Kufanya moto uwake |
| Yamepambwa | – | Yamerembeshwa |
| Zahanati | – | Mahali pa kutolea matibabu ya magonjwa madogo madogo; hospitali ndogo. |
| Zizi | – | Mahali ambapo ng'ombe, mbuzi na kondoo hulala. |

# Michoro ya Kuashiria

| | |
|---|---|
| Ufahamu wa fonimu | |
| Ufahamu wa herufi | |
| Kusoma silabi | |
| Kusoma maneno kwa kutumia silabi | |
| Kusoma maneno marefu | |
| Sarufi | |
| Kabla ya kusoma | |
| Kusoma hadithi | |
| Maswali | |
| Kuandika | |
| Kazi ya ziada | |
| Zoezi | |
| Jedwali la silabi | |
| Msamiati | |
| Hadithi ya mwalimu | |
| Kutazama na kujadili picha | |
| Kuimba wimbo | |
| Kuandika maneno | |

Kipindi cha 1 na 2 **Shuleni 1**

**Kipindi 1**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**r**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ra** **re** **ri** **ro** **ru**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ra fi ki | re fu | ru hu sa | ru di |
|---|---|---|---|
| **rafiki** | **refu** | **ruhusa** | **rudi** |

**Kipindi 2**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**R** **r**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li rudi | a li m ruhusu | a li regesha |
|---|---|---|
| **walirudi** | **alimruhusu** | **aliregesha** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma sentensi hizi.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mwalimu **wako** | Walimu **wenu** |
| 2. | Kalamu **yako** | Kalamu **zenu** |
| 3. | Kitabu **chako** | Vitabu **vyenu** |
| 4. | Kiti **chako** | Viti **vyenu** |
| 5. | Shule **yako** | Shule **zenu** |
| 6. | Elimu **yako** | Elimu **yenu** |

1 Hakiuzwi

## Utambuzi wa sauti

Tutajifunza sauti za Kiswahili leo. Kwanza tutataja sauti kisha neno. Sauti ni /r/. Ikiwa neno lina sauti /r/ mwanzoni nitaonyesha kidole juu. Ikiwa neno halina sauti /r/ mwanzoni nitaonyesha kidole chini.

**Ninafanya:** Sauti ni /r/. Neno la kwanza ni 'raba'. Neno hili linaanza kwa sauti /r/ kwa hivyo nitaonyesha kidole juu. Neno jingine ni 'darasa'. Neno hili halianzi kwa sauti /r/. Kwa hivyo naonyesha kidole chini.

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Sauti ni /r/. Sauti ni gani? Sauti ni /r/. Sasa nitataja neno. Ikiwa neno limeanza kwa sauti /r/, tutaonyesha kidole juu. Ikiwa halianzi kwa sauti /r/, tutaonyesha kidole chini. Neno la kwanza ni 'raba'. *Mwalimu na wanafunzi wanaonyesha kidole juu.*

Endelea na maneno; *yafuatayo:* rafiki, darasa.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Sauti ni /r/. Onyesha kidole juu ikiwa neno linaanza kwa sauti /r/. Ikiwa halianzi kwa sauti /r/ onyesha kidole chini. *Tumia maneno yafuatayo:* raba, rafiki, darasa, gwaride.

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'r' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.*

Jina la herufi hii ni 'r'. Sauti yake ni /r/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'r'. Sauti yake ni /r/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'r'. Sauti yake ni /r/.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 1.** Taja jina la herufi na utamke sauti.

Mwanafunzi afinyange umbo la herufi 'r'.

## Kusoma silabi

*Andika silabi 'ra' ubaoni au utumie kadi za herufi.*

**Ninafanya:** Leo tutaunda silabi kwa kuunganisha sauti. Nitataja sauti kisha nitamke silabi. Sauti hizi ni /r//a/. Naunganisha sauti zote mbili. Silabi ni 'ra'.

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Tutatamka sauti kisha tutataja silabi pamoja. Sauti ni /r/ /a/. Silabi ni 'ra'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Tamka sauti kisha utataja silabi. Sauti ni /r/ /a/. Silabi ni gani? 'ra'

*Rudia hatua 1-3 kwa kutumia silabi re, ri, ro, ru.* Soma silabi kwenye **ukurasa wa 1.**

## Kusoma maneno kwa kutumia silabi

**Ninafanya:** *Andika neno 'rafiki' ubaoni.* Nitazameni: ra fi ki. Neno ni 'rafiki'.

**Tunafanya:** Hebu tusome sote. Tutatamka silabi, kisha tusome. *Pitisha kidole chini ya kila silabi huku ukisoma pamoja na wanafunzi.* Silabi ni? 'ra fi ki'. Neno ni? 'rafiki'.

**Unafanya:** Sasa zamu yako. Tamka silabi kisha usome neno. *Hakikisha unapitisha kidole kwa kila silabi huku wanafunzi wakisoma.* Silabi ni? 'ra fi ki'. Neno ni 'rafiki'. *Rudia hatua ya 3 na maneno yafuatayo*: refu, ruhusa.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 1.** Tamka silabi kisha uyasome maneno.

## Msamiati

**Ninafanya:** *Andika neno 'gwaride' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi*. Neno hili ni 'gwaride'. *Lisome polepole mara mbili.*

**Tunafanya:** Ni wangapi wamelisikia neno hili 'gwaride'? Wangapi wanajua maana yake? *Eleza maana ya neno.* **Ninafanya:** Nitatunga sentensi nikitumia neno 'gwaride'. *Tunga sentensi ukituma neno.*

**Unafanya:** Ni nani anayeweza kutunga sentensi kwa kutumia neno 'gwaride'? *Chagua baadhi ya wanafunzi watunge sentensi wakitumia neno gwaride.*

*Tumia hatua hizi kufunza maneno yafuatayo:* **maktaba, kumi na sita.**

**Unafanya**: Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 2.** Someni maneno ambayo tumejifunza kwenye hadithi.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 1: Shuleni 1

Kipindi cha 1 na 2 **Shuleni 1**

### Kusoma hadithi



**Shule ya Msingi ya Mutuma**

Shule ya Msingi ya Mutuma haikuwa kubwa. Kila darasa lilikuwa na wanafunzi kumi na sita. Wanafunzi hao walipenda kusoma lakini hawakuwa na vitabu vya kutosha. Wanafunzi watano walitumia kitabu kimoja. Shule hii pia haikuwa na maktaba. Vitabu viliwekwa katika ofisi kwenye maboksi kumi na moja.

Siku moja mgeni alifika shuleni asubuhi. Wanafunzi walikuwa katika gwaride. Mgeni aliwasalimia na kusema, "Habari ya asubuhi?" Mimi ni mkuu wa elimu. Serikali itailetea shule yenu vitabu. Utakapopokea kitabu chako, kitunze.". Wanafunzi walifurahi sana.

Mali ya Serikali ya Kenya 2

*Tumia chati iliyo na nambari 11 - 20. Hakikisha umewafunza nambari hizo zingine.*

### Kabla ya kusoma

**Tunafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 2.** Kichwa cha hadithi ni 'Shule ya msingi ya Mutuma'. Hadithi hii inahusu shule. Je, katika shule yenu kuna maktaba? *Chagua wanafunzi 3-4 wajibu.*

Weka kidole chako kwenye kichwa cha hadithi. Tusome kichwa pamoja.

Tazama picha kitabuni. Unaona nini? *Pata majibu kutoka kwa wanafunzi 3-4.*

Fungeni vitabu. Mgeukie mwenzako na umweleze kitu kimoja unafikiri kitafanyika katika hadithi. Nani atatueleza kile mwenzake alisema. *Waulize wanafunzi 2-3 wajibu. Andika utabiri wao ubaoni.*

### Hadithi ya mwanafunzi

**Ninafanya:** Fungua kitabu chako tena kwenye **ukurasa wa 2.** Tutasoma hadithi ili tuone iwapo yale mliyosema yangefanyika yatafanyika. Kwanza nitawasomea huku mkisikiliza. Weka kidole chako kwenye kichwa cha hadithi na ufuatilize ninaposoma. *Somea wanafunzi hadithi.*

**Tunafanya:** Sasa tusome hadithi pamoja. Fuatiliza kwa kutumia kidole. *Soma hadithi pamoja na wanafunzi.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Someni hadithi na mwenzako. *Zunguka darasani ili kuhakikisha kila mwanafunzi anasoma.*

### Maswali

**Ninafanya:** Taja jina la shule inayozungumziwa katika hadithi. *(Mutuma). Onyesha jinsi ya kutafuta jibu kwenye hadithi.*

**Tunafanya:** Kila darasa lilikuwa na wanafunzi wangapi? *(Kumi na sita.) Elekeza wanafunzi jinsi ya kutafuta jibu kwenye hadithi.*

**Unafanya:** Ukisalimiwa 'habari ya asubuhi', utajibu vipi? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

*Andika vifungu vifuatavyo ubaoni.*

1. Maboksi kumi na moja
2. Vitabu kumi na tisa
3. Rula kumi na nne
4. Wanafunzi kumi na sita

Mwanafunzi amsomee mwenzake vifungu hivi.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike nambari zifuatazo: 11, 12, 13, 14,15, 16, 17, 18, 19, 20 na kumsomea mzazi au mlezi wake nyumbani.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 1 na 2 **Shuleni 1**

**Kipindi 1**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **r**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  **ra** **re** **ri** **ro** **ru**

- Soma maneno ukitumia silabi.

  ra fi ki — **rafiki**  re fu — **refu**  ru hu sa — **ruhusa**  ru di — **rudi**

**Kipindi 2**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **R** **r**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  wa li rudi — **walirudi**  a li m ruhusu — **alimruhusu**  a li regesha — **aliregesha**

**Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma sentensi hizi.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mwalimu **wako** | Walimu **wenu** |
| 2. | Kalamu **yako** | Kalamu **zenu** |
| 3. | Kitabu **chako** | Vitabu **vyenu** |
| 4. | Kiti **chako** | Viti **vyenu** |
| 5. | Shule **yako** | Shule **zenu** |
| 6. | Elimu **yako** | Elimu **yenu** |

1 Hakiuzwi

Kipindi cha 1 na 2 **Shuleni 1**

**Kusoma hadithi**



**Shule ya Msingi ya Mutuma**

Shule ya Msingi ya Mutuma haikuwa kubwa. Kila darasa lilikuwa na wanafunzi kumi na sita. Wanafunzi hao walipenda kusoma lakini hawakuwa na vitabu vya kutosha. Wanafunzi watano walitumia kitabu kimoja. Shule hii pia haikuwa na maktaba. Vitabu viliwekwa katika ofisi kwenye maboksi kumi na moja.

Siku moja mgeni alifika shuleni asubuhi. Wanafunzi walikuwa katika gwaride. Mgeni aliwasalimia na kusema, “Habari ya asubuhi?” Mimi ni mkuu wa elimu. Serikali itailetea shule yenu vitabu. Utakapokipokea kitabu chako, kitunze.”. Wanafunzi walifurahi sana.

Mali ya Serikali ya Kenya 2

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi ‘R’ ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.* Jina la herufi hii ni ‘R’. Hii ni herufi kubwa. Sauti yake ni /r/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni ‘R’. Sauti yake ni /r/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni ‘R’. Sauti yake ni /r/.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 1.** Taja jina la herufi na utamke sauti.

## Kusoma maneno marefu

**Ninafanya:** *Andika neno ‘walirudi’ ubaoni.* Nitazameni: wa li rudi. Neno ni ‘walirudi’.

**Tunafanya:** Hebu tusome pamoja. Tutasoma sehemu za neno, kisha tusome neno lote kwa upesi. *Pitisha kidole chini ya kila silabi huku ukisoma pamoja na wanafunzi.* Sehemu za neno ni? ‘wa li rudi’. Neno ni? ‘walirudi’.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tamka sehemu za neno kisha usome neno. *Hakikisha unapitisha kidole chini ya kila sehemu ya neno huku wanafunzi wakisoma.* Sehemu za neno ni? ‘wa li rudi’ Neno ni ‘walirudi’. *Rudia hatua ya 3 na maneno yafuatayo*: alimruhusu, walirefusha, aliregesha.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 1.** Soma sehemu za neno na neno lote.

## Kabla ya kusoma

*Rejelea msamiati – kumbusha mwanafunzi maana ya maneno:* **gwaride, maktaba, kumi na sita.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**Unafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 2.** Somea mwenzako hadithi. Kumbuka kufuatiliza kidole chini ya kila neno unaposoma.

## Sarufi

**Matumizi ya: -ako na –enu**

*Andika -ako na –enu ubaoni.*

**Ninafanya:** Leo tutajifunza kuhusu vimilikishi. *Onyesha ‘–ako’.* Tunatumia ‘-ako’ kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano: Kitabu chako kimepotea. *Onyesha ‘-enu.’* ‘-enu’ hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano: Vitabu vyenu vimepotea. Nitatunga sentensi nikitumia –ako na –enu. Kiatu chako ni kizuri. Viatu vyenu ni vizuri.

**Tunafanya:** Fungua kitabu chako **ukurasa wa 2.** Ningetaka tusome sentensi inayoonyesha vimilikishi kwenye hadithi.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 1 na 2 **Shuleni 1**

**Kipindi 1**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**r**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ra** **re** **ri** **ro** **ru**

- Soma maneno ukitumia silabi.

ra fi ki — re fu — ru hu sa — ru di

**rafiki** **refu** **ruhusa** **rudi**

**Kipindi 2**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**R** **r**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li rudi — a li m ruhusu — a li regesha

**walirudi** **alimruhusu** **aliregesha**

**Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma sentensi hizi.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mwalimu **wako** | Walimu **wenu** |
| 2. | Kalamu **yako** | Kalamu **zenu** |
| 3. | Kitabu **chako** | Vitabu **vyenu** |
| 4. | Kiti **chako** | Viti **vyenu** |
| 5. | Shule **yako** | Shule **zenu** |
| 6. | Elimu **yako** | Elimu **yenu** |

1 Hak uzwi

Kipindi cha 1 na 2 **Shuleni 1**

**Kusoma hadithi**



**Shule ya Msingi ya Mutuma**

Shule ya Msingi ya Mutuma haikuwa kubwa. Kila darasa lilikuwa na wanafunzi kumi na sita. Wanafunzi hao walipenda kusoma lakini hawakuwa na vitabu vya kutosha. Wanafunzi watano walitumia kitabu kimoja. Shule hii pia haikuwa na maktaba. Vitabu viliwekwa katika ofisi kwenye maboksi kumi na moja.

Siku moja mgeni alifika shuleni asubuhi. Wanafunzi walikuwa katika gwaride. Mgeni aliwasalimia na kusema, "Habari ya asubuhi?" Mimi ni mkuu wa elimu. Serikali itailetea shule yenu vitabu. Utakapokipokea kitabu chako, kitunze.". Wanafunzi walifurahi sana.

Mali ya Serikali ya Kenya 2

*Mwalimu asome sentensi iliyopigiwa mstari kwenye hadithi pamoja na wanafunzi.*

**Ninafanya:** Nitatunga sentensi nikitumia kimilikishi, '-enu.' Chakula chenu ni kizuri. Nitatunga sentensi nyingine nikitumia kimilikishi '-enu.' Vitabu vyenu ni vizuri.

**Unafanya:** Ninataka sasa mtunge sentensi mkitumia '-ako na '-enu.'

*Waagize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia vimilikishi; '–ako' na '-enu.'*

### Zoezi

Fungua kwenye **ukurasa wa 1** kwenye sarufi. Soma sentensi hizo.

*Zunguka darasani ili kuhakikisha kila mwanafunzi anasoma.*

### Kazi ya ziada

Jaza pengo ukizingatia -ako na -enu.

1. Mwalimu wako — Walimu ________
2. Kalamu _______ — Kalamu zenu
3. Kitabu chako — Vitabu _________

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 3 na 4 **Shuleni 1**

**Kipindi 3**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

j r

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

je ji jo ju

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ja na | ma je ngo | ju zi | ja di li |
| **jana** | **majengo** | **juzi** | **jadili** |

**Kipindi 4**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

J j

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a li jenga | wa li juana | a li jaliwa | tu li jaribu |
| **alijenga** | **walijuana** | **alijaliwa** | **tulijaribu** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Jaza mapengo kwa kutumia **-ako** na **-enu**.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Dawati _____ ni zuri. | Madawati _____ ni mazuri. |
| 2. | Kifutio _____ ni chekundu. | Vifutio ____ ni vyekundu. |
| 3. | Sare _____ ni safi. | Sare _____ ni safi. |
| 4. | Mgeni _____ amefika. | Wageni _____ wamefika. |
| 5. | Bendera ____ inapepea. | Bendera _____ zinapepea. |

3 Hak uzwi

## Utambuzi wa sauti

Tutajifunza sauti za Kiswahili leo. Kwanza tutataja sauti kisha neno. Sauti ni /j/. Ikiwa neno lina sauti /j/ mwanzoni nitaonyesha kidole juu. Ikiwa neno halina sauti /j/ mwanzoni nitaonyesha kidole chini.

**Ninafanya:** Sauti ni /j/. Neno la kwanza ni 'jana'. Neno hili linaanza kwa sauti /j/ kwa hivyo nitaonyesha kidole juu. Neno jingine ni 'majengo'. Neno hili halianzi kwa sauti /j/. Kwa hivyo naonyesha kidole chini.

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Sauti ni /j/. Sauti ni gani? Sauti ni /j/. Sasa nitataja neno. Ikiwa neno limeanza kwa sauti /j/, tutaonyesha kidole juu. Ikiwa halianzi kwa sauti /j/, tutaonyesha kidole chini. Neno la kwanza ni 'jana'. *Mwalimu na wanafunzi wanaonyesha kidole juu.*

Endelea na maneno; *yafuatayo: juzi, lala.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Sauti ni /j/. Onyesha kidole juu ikiwa neno linaanza kwa sauti /j/. Ikiwa halianzi kwa sauti /j/ onyesha kidole chini. *Tumia maneno yafuatayo:* jana, majengo, jadili.

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'j' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.*

Jina la herufi hii ni 'j'. Sauti yake ni /j/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'j'. Sauti yake ni /j/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'j'. Sauti yake ni /j/.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 3.** Taja jina la herufi na utamke sauti.

## Kusoma silabi

*Andika silabi 'ja' ubaoni au utumie kadi za herufi.*

**Ninafanya:** Leo tutaunda silabi kwa kuunganisha sauti. Nitataja sauti kisha nitamke silabi. Sauti hizi ni /j//a/. Naunganisha sauti zote mbili. Silabi ni 'ja'.

*Hakikisha unapitisha kidole chini ya kila herufi unapoitamka.*

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Tutatamka sauti kisha tutataja silabi pamoja. Sauti ni /j/ /a/. Silabi ni 'ja'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Tamka sauti kisha utataja silabi. Sauti ni /j/ /a/. Silabi ni gani? 'ja'.
*Rudia hatua 1-3 kwa kutumia silabi je, ji, jo, ju.* Soma silabi kwenye **ukurasa wa 3**.

## Kusoma maneno kwa kutumia silabi

**Ninafanya:** *Andika neno 'jana' ubaoni.* Nitazameni: ja na. Neno ni 'jana'.

**Tunafanya:** Hebu tusome sote. Tutatamka silabi, kisha tusome. *Pitisha kidole chini ya kila silabi huku ukisoma pamoja na wanafunzi.* Silabi ni? 'ja na'. Neno ni? 'jana'.
**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tamka silabi kisha usome neno. Silabi ni 'ja na', Neno ni 'jana'. *Rudia hatua ya 3 na maneno yafuatayo*: majengo, juzi, jadili.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 3**. Tamka silabi kisha uyasome maneno.

## Msamiati

**Ninafanya:** *Andika neno 'bustani' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi*. Neno hili ni 'bustani'. *Lisome polepole mara mbili.*

**Tunafanya:** Ni wangapi wamelisikia neno hili 'bustani'? Wangapi wanajua maana yake? *Eleza maana ya neno.*
**Ninafanya:** Nitatunga sentensi nikitumia neno 'bustani'. *Tunga sentensi ukituma neno.*

**Unafanya:** Ni nani anaweza kutunga sentensi kwa kutumia neno 'bustani'? *Chagua baadhi ya wanafunzi watunge sentensi wakitumia neno 'bustani'.*

*Tumia hatua hizi kufunza maneno* **bendera, vyoo, ishirini na saba.**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________



Hakiuzwi

Kipindi cha | 3 na 4 | **Shuleni 1**

**Kusoma hadithi**



**Shule ya Msingi ya Mlimani**

Shule ya Mlimani inajulikana kwa usafi. Shule hii ina madarasa ishirini na moja. Maktaba ina madirisha makubwa. Madirisha huleta hewa safi. Maktabani kuna meza ishirini na saba na rafu thelathini. Kuna ofisi moja ya mwalimu mkuu. Kuna bustani yenye maua ya kupendeza. Mlingoti wa bendera ni wa chuma. Wanafunzi hupanga foleni katika gwaride. Wanafunzi huimba wimbo wa taifa. Kando ya uwanja kuna vyoo ishirini na tisa. Ilani nje ya choo imeandikwa, "Nawa mikono yako ukitoka msalani!"

Mali ya Serikali ya Kenya 4

**Unafanya**: Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 4.** Someni maneno ambayo tumejifunza kwenye hadithi.

*Tumia chati iliyo na nambari 21 - 30. Hakikisha umewafunza nambari hizo zingine.*

### Kabla ya kusoma

**Tunafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 4.** Kichwa cha hadithi ni 'Shule ya msingi ya Mlimani'. Hadithi hii inahusu shule. Je, shuleni mna nini? *Chagua wanafunzi 3-4 wajibu.*

Weka kidole chako kwenye kichwa cha hadithi. Tusome kichwa pamoja.

Tazama picha kitabuni. Unaona nini? *Pata majibu kutoka kwa wanafunzi 3-4.*

Fungeni vitabu. Mgeukie mwenzako na umweleze kitu kimoja unafikiri kitafanyika katika hadithi. Nani atatueleza kile mwenzake alisema. *Waulize wanafunzi 2-3 wajibu. Andika utabiri wao ubaoni.*

### Hadithi ya mwanafunzi

**Ninafanya:** Fungua kitabu chako tena kwenye **ukurasa wa 4.** Tutasoma hadithi ili tuone iwapo yale mlisema yangefanyika yatafanyika. Kwanza nitawasomea huku mkisikiliza. Weka kidole chako kwenye kichwa cha hadithi na ufuatilize ninaposoma. *Somea wanafunzi hadithi.*

**Tunafanya:** Sasa tusome hadithi pamoja. Fuatiliza kwa kutumia kidole. *Soma hadithi pamoja na wanafunzi.*

**Unafanya:** Sasa ni wakati wenu. Someni hadithi na mwenzako. *Zunguka darasani ili kuhakikisha kila mwanafunzi anasoma.*

### ? Maswali

**Ninafanya:** Kwa nini madirisha ya maktaba ni makubwa? *(Ili yalete hewa safi.) Onyesha jinsi ya kutafuta jibu kwenye hadithi.*

**Tunafanya:** Maktabani kuna meza ngapi? *(Ishirini na saba) Elekeza wanafunzi jinsi ya kutafuta jibu kwenye hadithi.*

**Utafanya:** Kwa nini wanafunzi husimama wima wanapoimba wimbo wa taifa? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi asome nambari hizi: 21-30.

### Kazi ya ziada

*Mwanafunzi aandike sentensi zifuatazo ubaoni. Agiza wanafunzi waziandike kwenye vitabu vyao kisha wawasomee wazazi au walezi wao nyumbani.*

1. Dawati lako ni nzuri.
   Madawati yenu ni mazuri.
2. Kifutio chako ni chekundu.
   Vifutio vyenu ni vyekundu.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 4: Shuleni 1

Kipindi cha 3 na 4 **Shuleni 1**

**Kipindi 3**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  j  r

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  je  ji  jo  ju

- ★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ja na | ma je ngo | ju zi | ja di li |
|---|---|---|---|
| **jana** | **majengo** | **juzi** | **jadili** |

**Kipindi 4**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  J  j

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li jenga | wa li juana | a li jaliwa | tu li jaribu |
|---|---|---|---|
| **alijenga** | **walijuana** | **alijaliwa** | **tulijaribu** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Jaza mapengo kwa kutumia **-ako** na **-enu**.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Dawati _____ ni zuri. | Madawati _____ ni mazuri. |
| 2. | Kifutio _____ ni chekundu. | Vifutio _____ ni vyekundu. |
| 3. | Sare _____ ni safi. | Sare _____ ni safi. |
| 4. | Mgeni _____ amefika. | Wageni _____ wamefika. |
| 5. | Bendera _____ inapepea. | Bendera _____ zinapepea. |

3  Hak uzwi

Kipindi cha 3 na 4 **Shuleni 1**

**Kusoma hadithi**



**Shule ya Msingi ya Mlimani**

Shule ya Mlimani inajulikana kwa usafi. Shule hii ina madarasa ishirini na moja. Maktaba ina madirisha makubwa. Madirisha huleta hewa safi. Maktabani kuna meza ishirini na saba na rafu thelathini. Kuna ofisi moja ya mwalimu mkuu. Kuna bustani yenye maua ya kupendeza. Mlingoti wa bendera ni wa chuma. Wanafunzi hupanga foleni katika gwaride. Wanafunzi huimba wimbo wa taifa. Kando ya uwanja kuna vyoo ishirini na tisa. Ilani nje ya choo imeandikwa, "Nawa mikono yako ukitoka msalani!"

Mali ya Serikali ya Kenya  4

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'J' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.* Jina la herufi hii ni 'J'. Hii ni herufi kubwa. Sauti yake ni /j/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'J'. Sauti yake ni /j/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'J' Sauti yake ni /j/.

Rudia hatua ya 1-3 kwa kutumia herufi 'r'.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 3.** Taja jina la herufi na utamke sauti.

## Kusoma maneno marefu

**Ninafanya:** *Andika neno 'alijenga' ubaoni.* Nitazameni: 'a li jenga'. Neno ni 'alijenga'.

**Tunafanya:** Hebu tusome pamoja. Tutatamka sehemu za neno, kisha tusome neno lote kwa upesi. *Pitisha kidole chini ya kila sehemu huku ukisoma pamoja na wanafunzi.* Sehemu za neno ni 'a li jenga'. Neno ni 'alijenga'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu. Tamka sehemu za neno kisha usome neno. Sehemu za neno ni 'a li jenga'. Neno ni 'alijenga'. *Rudia hatua ya 3 na maneno yafuatayo*: walijuana, alijaliwa, majaribu.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 3.** Soma sehemu za neno na neno lote.

## Kabla ya kusoma

Mkumbushe mwanafunzi maana ya maneno **bendera, gwaride, vyoo, bustani, foleni**

## Hadithi ya mwanafunzi

**Unafanya**: Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 4.** Somea mwenzako hadithi. Kumbuka kufuatiliza kidole chini ya kila neno unaposoma.

## Sarufi

**Matumizi ya -ako na -enu**

*Andika -ako na –enu ubaoni.*

**Ninafanya:** Leo tutajifunza kuhusu vimilikishi. *Onyesha '–ako'.* Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano; Kalamu yako ni fupi. *Onyesha '-enu.'* '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano; Kalamu zenu ni fupi.

**Tunafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 4.** Ningetaka tusome sentensi inayoonyesha vimilikishi kwenye hadithi. *Mwalimu asome sentensi iliyopigiwa mstari kwenye hadithi pamoja na wanafunzi.*

**Ninafanya:** Nitatunga sentensi nikitumia kimilikishi, '-enu.'

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Hakiuzwi

Kipindi cha | 3 na 4 | **Shuleni 1**

**Kipindi 3**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

j r

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

je ji jo ju

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ja na | ma je ngo | ju zi | ja di li |
| **jana** | **majengo** | **juzi** | **jadili** |

**Kipindi 4**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

J j

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a li jenga | wa li juana | a li jaliwa | tu li jaribu |
| **alijenga** | **walijuana** | **alijaliwa** | **tulijaribu** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Jaza mapengo kwa kutumia **-ako** na **-enu**.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Dawati _____ ni zuri. | Madawati _____ ni mazuri. |
| 2. | Kifutio _____ ni chekundu. | Vifutio _____ ni vyekundu. |
| 3. | Sare _____ ni safi. | Sare _____ ni safi. |
| 4. | Mgeni _____ amefika. | Wageni _____ wamefika. |
| 5. | Bendera _____ inapepea. | Bendera _____ zinapepea. |

3 Hakiuzwi

Kipindi cha | 3 na 4 | **Shuleni 1**

**Kusoma hadithi**



**Shule ya Msingi ya Mlimani**

Shule ya Mlimani inajulikana kwa usafi. Shule hii ina madarasa ishirini na moja. Maktaba ina madirisha makubwa. Madirisha huleta hewa safi. Maktabani kuna meza ishirini na saba na rafu thelathini. Kuna ofisi moja ya mwalimu mkuu. Kuna bustani yenye maua ya kupendeza. Mlingoti wa bendera ni wa chuma. Wanafunzi hupanga foleni katika gwaride. Wanafunzi huimba wimbo wa taifa. Kando ya uwanja kuna vyoo ishirini na tisa. Ilani nje ya choo imeandikwa, "Nawa mikono yako ukitoka msalani!"

Mali ya Serikali ya Kenya 4

Viti vyenu ni vizuri.

**Unafanya:** Ninataka sasa mtunge sentensi mkitumia '-ako na '-enu.'

*Waulize wanafunzi watunge sentensi wakitumia vimilikishi; ' –ako' na '-enu'.*

### Zoezi

Fungua kwenye **ukurasa wa 3** kwenye sarufi. Jaza mapengo ukitumia -ako na -enu kwa usahihi.
*Sahihisha kazi ya mwanafunzi ukizingatia majibu haya:*

*1. lako/yenu*

*2. chako/vyenu*

*3. yako/zenu*

*4. wako/wenu*


*5. yako/zenu*

### Kazi ya ziada

*Andika maneno yafuatayo ubaoni. Mwanafunzi aandike na achore kwenye daftari lake.*

1. Dawati
2. Ubao
3. Bendera
4. Meza
5. Rafu

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________


Kipindi cha 5 Shuleni 1

Kipindi 5

Taja jina la herufi na utamke sauti.

J j R r

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: zi a ra – ziara**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ra | na | je | ru | ju |
| li | ja | zi | a | di |

**Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma na uandike vifungu hivi ukitumia **-ako** na **-enu**.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mwalimu **wako** | Walimu **wenu** |
| 2. | Mwanafunzi **wako** | Wanafunzi **wenu** |
| 3. | Bendera **yako** | Bendera **zenu** |

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Shule ya Nasifu**

**Kuandika**

Andika majina ya vitu vitatu vinavyopatikana shuleni mwenu.

5 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'J' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.* Jina la herufi hii ni 'J'. Hii ni herufi kubwa. Sauti yake ni /j/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'J'. Sauti yake ni /j/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'J'. Sauti yake ni /j/.

*Rudia hatua ya 1-3 kwa kutumia herufi 'j' 'R' 'r'.*

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 5**. Taja jina la herufi na utamke sauti.

### Jedwali la silabi

*Chora jedwali la silabi kwenye ubao.*

**Ninafanya:** Leo tutatumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno. *Soma silabi zote.*

**Tunafanya:** Sasa tutasoma silabi pamoja. *Soma silabi pamoja na wanafunzi.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako kuzisoma silabi. *Wanafunzi wasome silabi zote.*

**Ninafanya:** Nitatumia silabi 'ru' 'di' 'a' 'na' kuunda neno 'rudiana'. *Andika neno 'rudiana' ubaoni.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Unda maneno sahihi pamoja na mwenzako. *Wanafunzi waunde maneno. Andika maneno 3-4 ya wanafunzi ubaoni. Wanafunzi wasome maneno yote.*

### Msamiati wa hadithi ya mwalimu

Kabla ya kusoma tutajifunza kuhusu maneno mapya. Neno la kwanza ni 'ofisi'. Je, unafikiri neno '**ofisi**' lina maana gani? *Wachague wanafunzi 2-3 wachangie swali kwa kusema maana ya neno.* Neno hili lina maana ya chumba ambacho walimu hukaa wakati wanapojitayarisha kwenda darasani.

*Rudia hatua hizi kufunza maneno haya:* **madarasa, maktaba.**

### Kabla ya kusoma

**Tunafanya:** Fungua kwenye **ukurasa wa 5.**

Leo, nitawasomea hadithi huku mkisikiliza. Kabla ya kusoma, tutazungumzia zaidi kuhusu hadithi yenyewe. *Wasomee wanafunzi kichwa cha hadithi.*

Kichwa cha hadithi ni 'Shule ya Nasifu'. Tazama picha. Je, mnaona nini kwenye picha? *Wachague wanafunzi 2-3 waseme kile wanachokiona kwenye picha.*

Hadithi hii inahusu Shule ya Nasifu. Ni nini tunachojua kuhusu shule? *Wape wanafunzi 2-3 nafasi ya kujibu au kuchangia.*

Mweleze mwenzako kile unachofikiri tutajifunza kwenye hadithi? *Wachague wanafunzi 2-3 kuchangia somo kwa kutoa utabiri wao.*

### Hadithi ya mwalimu

Nitawasomea hadithi huku mkiitazama picha ya hadithi yenyewe. Iwapo utalisikia neno 'madarasa', inua mkono wako wa kulia, iwapo utasikia neno 'maktaba' inua mkono wako wa kushoto.

*Soma hadithi kwa utaratibu huku ukitumia ishara na hisia iwezekanavyo. Badilisha sauti unaporejelea wahusika tofauti kwenye hadithi. Tulia kwanza, kabla ya kusoma jambo la kufurahisha na utoe maelezo mafupi kulihusu.*

**Shule Ya Nasifu**

Shule ya msingi ya Nasifu inapatikana mjini Akilimali. Shule hii inasifika kwa umaarufu wake katika masomo na michezo. Karibu na lango kuu kuna ofisi ya mwalimu mkuu, Bi. Neema. Ofisi hii ina madirisha makubwa yenye vioo. Karibu na ofisi hiyo kuna bustani ya maua yanayopendeza. Kila mara, mwalimu mkuu hutuhimiza kubisha mlango wa ofisi kabla ya kuingia.

Katika shule hii kuna madarasa mengi. Zaidi ya madarasa kuna vyoo vya walimu na wanafunzi. Vyoo hivi vimejengwa karibu na maktaba ya shule.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 5 **Shuleni 1**

**Kipindi 5**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

J j R r

Jedwali la silabi
Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
**Kwa mfano: zi a ra – ziara**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ra | na | je | ru | ju |
| li | ja | zi | a | di |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**
Soma na uandike vifungu hivi ukitumia **-ako** na **-enu**.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mwalimu **wako** | Walimu **wenu** |
| 2. | Mwanafunzi **wako** | Wanafunzi **wenu** |
| 3. | Bendera **yako** | Bendera **zenu** |

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Shule ya Nasifu**



**Kuandika**
Andika majina ya vitu vitatu vinavyopatikana shuleni mwenu.

5 Hakiuzwi

Sasa tumeisoma hadithi. Je, yale ulitabiri yametimia? Mweleze mwenzako kuhusu utabiri uliotoa. Waulize wanafunzi kadhaa kujadili matokeo ya utabiri wao iwapo ulitimia.

### Maswali

**Ninafanya:** Shule ya Nasifu inapatikana wapi? *(Mjini Akilimali)*

**Tunafanya:** Taja vitu vinavyopatikana katika shule ya Nasifu. *(Ofisi ya mwalimu mkuu, madarasa, vyoo, maktaba)*

**Unafanya:** Je, unafikiria ni kwa nini mwalimu mkuu alisisitiza kuhusu usafi wa vyoo? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Kuandika

**Ninafanya:** Leo tutaandika majina ya vitu vinavyopatikana shuleni. *Andika neno 'dawati' ubaoni.*

**Tunafanya:** Sasa mtaniambia majina ya vitu vingine vinavyopatikana shuleni. *Chagua wanafunzi 2-3 wakutajie majina huku ukiandika kwenye ubao.*

**Unafanya:** Sasa angalia sehemu ya kuandika kwenye kitabu chako kwenye **ukurasa wa 5.** Tunaelezwa tuandike majina ya vitu vitatu vinavyopatikana shuleni. Chukua daftari lako uandike kwa hati nadhifu.

### Sarufi

**Tunafanya:** Nani anakumbuka tuliyojifunza jana kuhusu sarufi? *Wape wanafunzi nafasi kujibu.*

Tulijifunza kuhusu matumizi ya vimilikishi; '-ako' na '-enu.' Tunatumia '-ako.' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano: Pipa lako. Tunatumia '-enu' kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano: Mapipa yenu.

Nitawafundisha kutunga sentensi kwa kutumia '-ako' na '-enu.' *Waongoze wanafunzi kutunga sentensi.*

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 5.** Soma na uziandike sentensi zenye '-ako' na '-enu'.

### Zoezi

*Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 5**.*

### Kazi ya ziada

*Waeleze wanafunzi wakusanye picha za maneno yafuatayo, kisha wabandike kwenye vitabu vyao vya kuchora.*

1. Kalamu
2. Bendera
3. Gwaride
4. Kifutio
5. Basi la shule

### Kazi ya nyongeza

*Katika makundi ya wawili wawili, wanafunzi wajadiliane kuhusu umuhimu wa salamu.*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 6 na 7 **Shuleni 1**

**Kipindi 6**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**g** **j**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ge** **gi** **go** **gu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| tu li pi ga | wa ge ni | ga ri ni | ga nda |
| **tulipiga** | **wageni** | **garini** | **ganda** |

**Kipindi 7**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**G** **g**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| wa li pangana | a li gawanya | a li pongeza |
| **walipangana** | **aligawanya** | **alipongeza** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma sentensi hizi.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mgeni **wako** amefika. | Wageni **wenu** wamefika. |
| 2. | Tabuleti **yako** ni nzuri. | Tabuleti **zenu** ni nzuri. |
| 3. | Kitabu **chako** ni kizuri. | Vitabu **vyenu** ni vizuri. |
| 4. | Mwalimu **wako** ameenda. | Walimu **wenu** wameenda. |
| 5. | Darasa **lako** limefungwa. | Madarasa **yenu** yamefungwa. |

Mali ya Serikali ya Kenya

6

### Utambuzi wa sauti

Tutajifunza sauti za Kiswahili leo. Kwanza tutataja sauti kisha neno. Sauti ni /g/. Ikiwa neno lina sauti /g/ mwanzoni nitaonyesha kidole juu. Ikiwa neno halina sauti /g/ mwanzoni nitaonyesha kidole chini.

**Ninafanya:** Sauti ni /g/. Neno la kwanza ni 'gani'. Neno hili linaanza kwa sauti /g/ kwa hivyo nitaonyesha kidole juu. Neno jingine ni 'tulipiga'. Neno hili halianzi kwa sauti /g/. Kwa hivyo naonyesha kidole chini.

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Sauti ni /g/. Sauti ni gani? Sauti ni /g/. Sasa nitataja neno. Ikiwa neno limeanza kwa sauti /g/, tutaonyesha kidole juu. Ikiwa halianzi kwa sauti /g/, tutaonyesha kidole chini. Neno la kwanza ni 'gani'. *Mwalimu na wanafunzi wanaonyesha kidole juu.*

Endelea na maneno; yafuatayo: gani, tulipiga.

**Unafanya:** Sasa ni wakati wenu kujaribu. Sauti ni /g/. Onyesha kidole juu ikiwa neno linaanza kwa sauti /g/. Ikiwa halianzi kwa sauti /g/ onyesha kidole chini. *Tumia maneno yafuatayo:* garini, tulipiga, ganda.

### Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'g' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.* Jina la herufi hii ni 'g'. Sauti yake ni /g/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'g'. Sauti yake ni /g/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'g'. Sauti yake ni /g/.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 6.** Taja jina la herufi na utamke sauti.

### Kusoma silabi

*Andika silabi 'ga' ubaoni au utumie kadi za herufi.*

**Ninafanya:** Leo tutaunda silabi kwa kuunganisha sauti. Nitataja sauti kisha nitamke silabi. Sauti hizi ni /g//a/. Naunganisha sauti zote mbili. Silabi ni 'ga'.

*Hakikisha unapitisha kidole chini ya kila herufi unapoitamka.*

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Tutatamka sauti kisha tutataja silabi pamoja. Sauti ni /g/ /a/. Silabi ni 'ga'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Tamka sauti kisha utataja silabi. Sauti ni /g/ /a/. Silabi ni gani? 'ga'

*Rudia hatua 1-3 kwa kutumia silabi ge, go, gi, gu.* Soma silabi kwenye **ukurasa wa 6.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

**Ninafanya:** *Andika neno 'tulipiga' ubaoni.* Nitazameni: 'tu li pi ga'. Neno ni 'tulipiga'.

**Tunafanya:** Hebu tusome pamoja. Tutatamka silabi, kisha tusome. *Pitisha kidole chini ya kila silabi huku ukisoma pamoja na wanafunzi.* Silabi ni? 'tu li pi ga'. Neno ni? 'tulipiga'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tamka silabi kisha usome neno. Silabi ni? 'tu li pi ga' Neno ni 'tulipiga'. *Rudia hatua ya 3 na maneno yafuatayo*: wageni, garini.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 6.** Tamka silabi kisha uyasome maneno.

### Msamiati

**Ninafanya:** *Andika neno 'tarakilishi' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi.* Neno hili ni 'tarakilishi'. *Lisome polepole mara mbili.*

**Tunafanya:** Ni wangapi wamelisikia neno hili 'tarakilishi'? Wangapi wanajua maana yake? *Eleza maana ya neno.*

**Ninafanya:** Nitatunga sentensi nikitumia neno 'tarakilishi'. *Tunga sentensi ukituma neno.*

**Unafanya:** Ni nani anaweza kutunga sentensi kwa kutumia neno 'tarakilishi'? *Chagua baadhi yao watunge sentensi wakitumia neno 'tarakilishi'.*

Tarehe: ________________________ Muda: ________________ Idadi: ________________




Hakiuzwi

Kipindi cha | 6 na 7 | **Shuleni 1**

**Kusoma hadithi**



**Wageni shuleni**

Kengele ya kuenda gwaride ilipigwa. Wageni arubaini walikuwa wamefika. Walikaribishwa na mwalimu mkuu. Walituletea tarakilishi thelathini na nne. Walitueleza umuhimu wa tarakilishi walizotuletea.

Mwalimu mkuu alisema, "Ni jukumu lako sasa kutia bidii. Serikali imetimiza matarajio yenu ya kupata tarakilishi." Tulifurahi tulipoambiwa tungezitumia darasani. Mgeni mmoja alitumia tarakilishi kutuonyesha video, na vibonzo vilivyokuwa vinacheza mchezo wa tarakimu. Tulimpigia makofi kwa shangwe. Tarakilishi hizo ziliwekwa katika maktaba. Siku hizi kila mwanafunzi anasoma kwa kutumia tarakilishi.

7

Hakiuzwi

*Tumia hatua hizi kufunza maneno* **arubaini, darasani.**

**Unafanya**: Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 7**. Someni maneno ambayo tumejifunza kwenye hadithi.

*Tumia kadi za nambari kufunza 31 - 40. Hakikisha umewafunza nambari hizo zingine.*

### Kabla ya kusoma

**Tunafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 7**. Kichwa cha hadithi ni 'Wageni shuleni'. Hadithi hii inahusu wageni. Umewahi kupata wageni? Ilikuwaje? *Chagua wanafunzi 3-4 wajibu.*

Weka kidole chako kwenye kichwa cha hadithi. Tusome kichwa pamoja.

Tazama picha kitabuni. Unaona nini? *Pata majibu kutoka kwa wanafunzi 3-4*.

Fungeni vitabu. Mgeukie mwenzako na umweleze kitu kimoja unafikiri kitafanyika katika hadithi. Nani atatueleza kile mwenzake alisema. *Waulize wanafunzi 2-3 wajibu. Andika utabiri wao ubaoni.*

### Hadithi ya mwanafunzi

**Ninafanya:** Fungua kitabu chako tena kwenye **ukurasa wa 7**. Tutasoma hadithi ili tuone iwapo yale mlisema yangefanyika yatafanyika. Kwanza nitawasomea huku mkisikiliza. Weka kidole chako kwenye kichwa cha hadithi na ufuatilize ninaposoma. *Somea wanafunzi hadithi*.

**Tunafanya:** Sasa tusome hadithi pamoja. Fuatiliza kwa kutumia kidole. *Soma hadithi pamoja na wanafunzi*.

**Unafanya:** Sasa ni wakati wenu. Someni hadithi na mwenzako. *Zunguka darasani ili kuhakikisha kila mwanafunzi anasoma*.

### Maswali

**Ninafanya:** Kengele ya nini ilipigwa? *(Kuenda gwarideni). Onyesha jinsi ya kutafuta jibu kwenye hadithi.*

**Tunafanya:** Wageni walileta tarakilishi ngapi? *(Thelathini na nne). Elekeza wanafunzi jinsi ya kutafuta jibu kwenye hadithi.*

**Unafanya:** Unafikiria tarakilishi zina umuhimu gani shuleni? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Wanafunzi watazame vibonzo vikicheza mchezo wa nambari kwenye tabuleti au tarakilishi.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi afinyange maumbo ya herufi 'g' na aandike maneno matano yenye herufi 'g'.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 6 na 7 **Shuleni 1**

**Kipindi 6**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**g** **j**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ge** **gi** **go** **gu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| tu li pi ga | wa ge ni | ga ri ni | ga nda |
| **tulipiga** | **wageni** | **garini** | **ganda** |

**Kipindi 7**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**G** **g**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| wa li pangana | a li gawanya | a li pongeza |
| **walipangana** | **aligawanya** | **alipongeza** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma sentensi hizi.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mgeni **wako** amefika. | Wageni **wenu** wamefika. |
| 2. | Tabuleti **yako** ni nzuri. | Tabuleti **zenu** ni nzuri. |
| 3. | Kitabu **chako** ni kizuri. | Vitabu **vyenu** ni vizuri. |
| 4. | Mwalimu **wako** ameenda. | Walimu **wenu** wameenda. |
| 5. | Darasa **lako** limefungwa. | Madarasa **yenu** yamefungwa. |

Mali ya Serikali ya Kenya

6

Kipindi cha 6 na 7 **Shuleni 1**

**Kusoma hadithi**



**Wageni shuleni**

Kengele ya kuenda gwaride ilipigwa. Wageni arubaini walikuwa wamefika. Walikaribishwa na mwalimu mkuu. Walituletea tarakilishi thelathini na nne. Walitueleza umuhimu wa tarakilishi walizotuletea.

Mwalimu mkuu alisema, "Ni jukumu lako sasa kutia bidii. Serikali imetimiza matarajio yenu ya kupata tarakilishi." Tulifurahi tulipoambiwa tungezitumia darasani. Mgeni mmoja alitumia tarakilishi kutuonyesha video, na vibonzo vilivyokuwa vinacheza mchezo wa tarakimu. Tulimpigia makofi kwa shangwe. Tarakilishi hizo ziliwekwa katika maktaba. Siku hizi kila mwanafunzi anasoma kwa kutumia tarakilishi.

7 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'G' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.* Jina la herufi hii ni 'G'. Hii ni herufi kubwa. Sauti yake ni /g/

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'G'. Sauti yake ni /g/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'G'. Sauti yake ni /g/.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 6.** Taja jina la herufi na utamke sauti.

### Kusoma maneno marefu

**Ninafanya:** *Andika neno 'walipanga' ubaoni.* Nitazameni: 'wa li panga'. Neno ni 'walipanga'.

**Tunafanya:** Hebu tusome pamoja. Tutatamka sehemu za neno, kisha tusome neno lote kwa upesi. *Pitisha kidole chini ya kila sehemu huku ukisoma pamoja na wanafunzi.* Sehemu za neno ni? 'wa li panga'. Neno ni? 'walipanga'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tamka sehemu za neno kisha usome neno. Sehemu za neno ni? 'wa li panga' Neno ni 'walipanga'. *Rudia hatua ya 3 na maneno yafuatayo*: aligawanya, ilinguruma, waligonga.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 6.** Soma sehemu za neno na neno lote.

### Kabla ya kusoma

*Mkumbushe mwanafunzi maana ya maneno:* **tarakilishi, arubaini, darasani.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**Unafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 7.** Somea mwenzako hadithi. Kumbuka kufuatiliza kidole chini ya kila neno unaposoma.

### Sarufi

**Matumizi ya -ako na -enu**

*Andika -ako na –enu ubaoni.*

**Ninafanya:** Leo tutajifunza kuhusu vimilikishi. *Onyesha '–ako'.* Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano, Mchi wako. *Onyesha '-enu.'* '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano, Michi yenu.

**Tunafanya:** Fungua kitabu chako **ukurasa wa 6.** Ningetaka tusome sentensi inayoonyesha vimilikishi kwenye hadithi. *Mwalimu asome sentensi iliyopigiwa mstari kwenye hadithi pamoja na wanafunzi.*

**Ninafanya:** Nitatunga sentensi nikitumia kimilikishi, '-ako' na '-enu'. Mche wako ni mfupi. Miche yenu ni mifupi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

**Kipindi 6**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**g** **j**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ge** **gi** **go** **gu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| tu li pi ga | wa ge ni | ga ri ni | ga nda |
|---|---|---|---|
| **tulipiga** | **wageni** | **garini** | **ganda** |

**Kipindi 7**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**G** **g**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li pangana | a li gawanya | a li pongeza |
|---|---|---|
| **walipangana** | **aligawanya** | **alipongeza** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma sentensi hizi.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mgeni **wako** amefika. | Wageni **wenu** wamefika. |
| 2. | Tabuleti **yako** ni nzuri. | Tabuleti **zenu** ni nzuri. |
| 3. | Kitabu **chako** ni kizuri. | Vitabu **vyenu** ni vizuri. |
| 4. | Mwalimu **wako** ameenda. | Walimu **wenu** wameenda. |
| 5. | Darasa **lako** limefungwa. | Madarasa **yenu** yamefungwa. |





**Kusoma hadithi**



**Wageni shuleni**

Kengele ya kuenda gwaride ilipigwa. Wageni arubaini walikuwa wamefika. Walikaribishwa na mwalimu mkuu. Walituletea tarakilishi thelathini na nne. Walitueleza umuhimu wa tarakilishi walizotuletea.

Mwalimu mkuu alisema, "Ni jukumu lako sasa kutia bidii. Serikali imetimiza matarajio yenu ya kupata tarakilishi."

Tulifurahi tulipoambiwa tungezitumia darasani. Mgeni mmoja alitumia tarakilishi kutuonyesha video, na vibonzo vilivyokuwa vinacheza mchezo wa tarakimu. Tulimpigia makofi kwa shangwe. Tarakilishi hizo ziliwekwa katika maktaba. Siku hizi kila mwanafunzi anasoma kwa kutumia tarakilishi.



**Unafanya:** Ninataka sasa mtunge sentensi mkitumia '-ako' na '-enu'.

*Waagize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia vimilikishi; '-ako' na '-enu'*

### Zoezi

Fungua kwenye **ukurasa wa 6** kwenye sarufi. Soma sentensi kwa usahihi.

*Zunguka darasani kuhakikisha mwanafunzi anasoma.*

### Kazi ya ziada

Tunga sentensi ukitumia maneno yafuatayo.

1. Arubaini
2. Maktaba
3. Mgeni
4. Thelathini na nne

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 8 na 9 **Shuleni 1**

**Kipindi 8**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**d** **g**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**de** **di** **do** **du**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| mu da | da ra sa | da ra ja | da da |
|---|---|---|---|
| **muda** | **darasa** | **daraja** | **dada** |

**Kipindi 9**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**D** **d**

★ Soma sehemu ya neno na neno lote.

| i na tubidi | a li dondoa | wa li badilika |
|---|---|---|
| **inatubidi** | **alidondoa** | **walibadilika** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Tunga sentensi tatu ukitumia **-ako** na **-enu.**

**Kwa mfano:**

| **Umoja -ako** | **Wingi -enu** |
|---|---|
| Mkoba **wako** ni mpya. | Mikoba **yenu** ni mipya. |
| Jina **lako** ni refu. | Majina **yenu** ni marefu. |
| Darasa **lako** ni kubwa. | Madarasa **yenu** ni makubwa. |
| Daraja **lako** limejengwa. | Madaraja **yenu** yamejengwa. |

Mali ya Serikali ya Kenya 8

### Utambuzi wa sauti

Tutajifunza sauti za Kiswahili leo. Kwanza tutataja sauti kisha neno. Sauti ni /d/. Ikiwa neno lina sauti /d/ mwanzoni nitaonyesha kidole juu. Ikiwa neno halina sauti /d/ mwanzoni nitaonyesha kidole chini.

**Ninafanya:** Sauti ni /d/. Neno la kwanza ni 'darasa'. Neno hili linaanza kwa sauti /d/ kwa hivyo nitaonyesha kidole juu. Neno jingine ni 'twiga'. Neno hili halianzi kwa sauti /d/. Kwa hivyo naonyesha kidole chini.

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Sauti ni /d/. Sauti ni gani? Sauti ni /d/. Sasa nitataja neno. Ikiwa neno limeanza kwa sauti /d/, tutaonyesha kidole juu. Ikiwa halianzi kwa sauti /d/, tutaonyesha kidole chini. Neno la kwanza ni 'dawati'. *Mwalimu na wanafunzi wanaonyesha kidole juu.*

Endelea na maneno; *yafuatayo:* dada, daraja, muda.

**Unafanya:** Sasa ni wakati wenu kujaribu. Sauti ni /d/. Onyesha kidole juu ikiwa neno linaanza kwa sauti /d/. Ikiwa halianzi kwa sauti /d/ onyesha kidole chini. *Tumia maneno yafuatayo:* daraja, ngamia, dada, ganda.

### Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'd' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.* Jina la herufi hii ni 'd'. Sauti yake ni /d/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'd'. Sauti yake ni /d/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'd'. Sauti yake ni /d/.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 8.** Taja jina la herufi na utamke sauti.

### Kusoma silabi

*Andika silabi 'da' ubaoni au utumie kadi za herufi.*

**Ninafanya:** Leo tutaunda silabi kwa kuunganisha sauti. Nitataja sauti kisha nitamke silabi. Sauti hizi ni /d//a/. Naunganisha sauti zote mbili. Silabi ni 'da'.

*Hakikisha unapitisha kidole chini ya kila herufi unapoitamka.*

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Tutatamka sauti kisha tutataja silabi pamoja. Sauti ni /d/ /a/. Silabi ni 'da'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Tamka sauti kisha utataja silabi. Sauti ni /d/ /a/. Silabi ni gani? 'da'.

*Rudia hatua 1-3 kwa kutumia silabi de, di, do, du.* Soma silabi kwenye **ukurasa wa 8.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

**Ninafanya:** *Andika neno 'muda' ubaoni.* Nitazameni: mu da. Neno ni 'muda'.

**Tunafanya:** Hebu tusome pamoja. Tutatamka silabi, kisha tusome. *Pitisha kidole chini ya kila silabi huku ukisoma pamoja na wanafunzi.* Silabi ni? 'mu da'. Neno ni? 'muda'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tamka silabi kisha usome neno. Silabi ni 'mu da'. Neno ni 'muda'. *Rudia hatua ya 3 na maneno yafuatayo*: darasa, daraja.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 8.** Tamka silabi kisha uyasome maneno.

### Msamiati

**Ninafanya:** *Andika neno 'darasa' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi.* Neno hili ni 'darasa'. *Lisome polepole mara mbili.*

**Tunafanya:** Ni wangapi wamelisikia neno hili 'darasa'? Wangapi wanajua maana yake? *Eleza maana ya neno.*
**Ninafanya:** Nitatunga sentensi nikitumia neno 'darasa'. *Tunga sentensi ukituma neno.*

**Unafanya:** Ni nani anaweza kutunga sentensi kwa kutumia neno 'darasa'? *Chagua baadhi yao watunge sentensi wakitumia neno 'darasa'.*

*Tumia hatua hizi kufunza maneno* **ofisini, maktabani, hamsini.**

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 8 na 9 **Shuleni 1**

**Kusoma hadithi**




**Mwalimu wetu**

Jina langu ni Kajuzi. Ninasoma katika Shule ya Msingi ya Mkombozi. Niko katika darasa la pili. Mwalimu wetu mkuu anaitwa Bi. Ng'ara. Ana umri wa miaka arubaini na tisa. Yeye huvalia nadhifu kila siku. Ana mkoba wa kupendeza. Kiti chake ofisini kiko karibu na mlango. Mwalimu Ng'ara hutufunza kusoma na kuandika. Sisi tunajua kuchora kwa njia ya kipekee. Bi. Ng'ara hutupeleka maktabani pia. Maktabani kuna vitabu zaidi ya hamsini. Unapoenda pale, unachagua kitabu chako mwenyewe. Muda unapoisha mwalimu husema, "Rudisheni vitabu vyenu kwenye rafu."

9 Hakiluzwi

**Unafanya**: Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 9**. Someni maneno ambayo tumejifunza kwenye hadithi.

*Tumia kadi za nambari kufunza 41 - 50. Hakikisha umewafunza nambari hizo zingine.*

### Kabla ya kusoma

**Tunafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 9**. Kichwa cha hadithi ni 'Mwalimu wetu'. Hadithi hii inahusu mwalimu. Unamjua mwalimu wenu? Anaitwaje? *Chagua wanafunzi 3-4 wajibu.*

Weka kidole chako kwenye kichwa cha hadithi. Tusome kichwa pamoja.

Tazama picha kitabuni. Unaona nini? *Pata majibu kutoka kwa wanafunzi 3-4.*

Fungeni vitabu. Mgeukie mwenzako na umweleze kitu kimoja unafikiri tutajifunza katika hadithi. Nani atatueleza kile mwenzake alisema. *Waulize wanafunzi 2-3 wajibu. Andika utabiri wao ubaoni.*

### Hadithi ya mwanafunzi

**Ninafanya:** Fungua kitabu chako tena kwenye **ukurasa wa 9.** Tutasoma hadithi ili tuone iwapo yale mlisema yangefanyika yatafanyika. Kwanza nitawasomea huku mkisikiliza. Weka kidole chako kwenye kichwa cha hadithi na ufuatilize ninaposoma. *Somea wanafunzi hadithi.*

**Tunafanya:** Sasa tusome hadithi pamoja. Fuatiliza kwa kutumia kidole. *Soma hadithi pamoja na wanafunzi.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Someni hadithi na mwenzako. *Zunguka darasani ili kuhakikisha kila mwanafunzi anasoma.*

### Maswali

**Ninafanya:** Mwalimu ana umri wa miaka mingapi? *(Arubaini na tisa.) Onyesha jinsi ya kutafuta jibu kwenye hadithi.*

**Tunafanya:** Mwalimu wa darasa anaitwa nani? *(Bi. Ng'ara). Elekeza wanafunzi jinsi ya kutafuta jibu kwenye hadithi.*

**Unafanya:** Unafikiria ni vitu vipi vinavyopatikana katika maktaba? *(vitabu, tarakilishi, n.k)*

### Zoezi

Andika silabi kutokana na herufi zifuatazo:

1. ch_____ 2. dh_____
3. l_____ 4. b_____

### Kazi ya ziada

**Jaza pengo ukitumia -ako na -enu.**

1. Darasa _____ ni kubwa.
   Madarasa _______ ni makubwa.
2. Vyoo ________ ni safi.
   Vyoo _________ ni safi.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Kipindi cha 8 na 9 **Shuleni 1**

**Kipindi 8**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**d** **g**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**de** **di** **do** **du**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| mu da | da ra sa | da ra ja | da da |
|---|---|---|---|
| **muda** | **darasa** | **daraja** | **dada** |

**Kipindi 9**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**D** **d**

★ Soma sehemu ya neno na neno lote.

| i na tubidi | a li dondoa | wa li badilika |
|---|---|---|
| **inatubidi** | **alidondoa** | **walibadilika** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Tunga sentensi tatu ukitumia **-ako** na **-enu.**

**Kwa mfano:**

| Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|
| Mkoba **wako** ni mpya. | Mikoba **yenu** ni mipya. |
| Jina **lako** ni refu. | Majina **yenu** ni marefu. |
| Darasa **lako** ni kubwa. | Madarasa **yenu** ni makubwa. |
| Daraja **lako** limejengwa. | Madaraja **yenu** yamejengwa. |

Mali ya Serikali ya Kenya

8

Kipindi cha 8 na 9 **Shuleni 1**

**Kusoma hadithi**




**Mwalimu wetu**

Jina langu ni Kajuzi. Ninasoma katika Shule ya Msingi ya Mkombozi. Niko katika darasa la pili. Mwalimu wetu mkuu anaitwa Bi. Ng'ara. Ana umri wa miaka arubaini na tisa. Yeye huvalia nadhifu kila siku. Ana mkoba wa kupendeza. Kiti chake ofisini kiko karibu na mlango. Mwalimu Ng'ara hutufunza kusoma na kuandika. Sisi tunajua kuchora kwa njia ya kipekee. Bi. Ng'ara hutupeleka maktabani pia. Maktabani kuna vitabu zaidi ya hamsini. Unapoenda pale, unachagua kitabu chako mwenyewe. Muda unapoisha mwalimu husema, "Rudisheni vitabu vyenu kwenye rafu."

9 Hakiuzwi

### ■ Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'D' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.* Jina la herufi hii ni 'D'. Hii ni herufi kubwa. Sauti yake ni /d/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'D'? Sauti yake ni /d/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'D' Sauti yake ni /d/.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 8.** Taja jina la herufi na utamke sauti.

### ★ Kusoma maneno marefu

**Ninafanya:** *Andika neno 'inatubidi' ubaoni.* Nitazameni: 'i na tubidi'. Neno ni 'inatubidi'.

**Tunafanya:** Hebu tusome pamoja. Tutatamka sehemu za neno, kisha tusome lote kwa upesi. *Pitisha kidole chini ya kila sehemu huku ukisoma pamoja na wanafunzi.* Sehemu za neno ni? 'i na tubidi'. Neno ni? 'inatubidi'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tamka sehemu za neno kisha usome neno. Sehemu za neno ni? 'i na tubidi' Neno ni 'inatubidi'. *Rudia hatua ya 3 na maneno yafuatayo*: walibadilika, iwalidondoa.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 8.** Soma sehemu za neno na neno lote.

### Kabla ya kusoma

Mkumbushe mwanafunzi maana ya maneno, **darasa, ofisini, maktabani, hamsini.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**Unafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 9.** Somea mwenzako hadithi. Kumbuka kufuatiliza kidole chini ya kila neno unapolisoma.

### ♦ Sarufi

**Matumizi ya vimilikishi -ako na -enu**

*Andika -ako na –enu ubaoni.*

**Ninafanya:** Leo tutajifunza kuhusu vimilikishi. *Onyesha '–ako'.* Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano: Kiti chako. *Onyesha '-enu.'* '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano: Viti vyenu.

**Tunafanya:** Fungua kitabu chako **ukurasa wa 9.** Ningetaka tusome sentensi inayoonyesha vimilikishi kwenye hadithi. *Mwalimu asome sentensi iliyopigiwa mstari kwenye hadithi pamoja na wanafunzi.*

**Ninafanya:** Nitatunga sentensi nikitumia kimilikishi, '-ako na '-enu'. Kiatu chako kimepatikana. Viatu vyenu vimepatikana.

**Unafanya:** Ninataka sasa mtunge sentensi mkitumia '-ako'

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 9: Shuleni 1

Kipindi cha 8 na 9 **Shuleni 1**

**Kipindi 8**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**d** **g**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**de** **di** **do** **du**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| mu da | da ra sa | da ra ja | da da |
| **muda** | **darasa** | **daraja** | **dada** |

**Kipindi 9**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**D** **d**

★ Soma sehemu ya neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| i na tubidi | a li dondoa | wa li badilika |
| **inatubidi** | **alidondoa** | **walibadilika** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Tunga sentensi tatu ukitumia **-ako** na **-enu.**

**Kwa mfano:**

| Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|
| Mkoba **wako** ni mpya. | Mikoba **yenu** ni mipya. |
| Jina **lako** ni refu. | Majina **yenu** ni marefu. |
| Darasa **lako** ni kubwa. | Madarasa **yenu** ni makubwa. |
| Daraja **lako** limejengwa. | Madaraja **yenu** yamejengwa. |



Kipindi cha 8 na 9 **Shuleni 1**

**Kusoma hadithi**




**Mwalimu wetu**

Jina langu ni Kajuzi. Ninasoma katika Shule ya Msingi ya Mkombozi. Niko katika darasa la pili. Mwalimu wetu mkuu anaitwa Bi. Ng'ara. Ana umri wa miaka arubaini na tisa. Yeye huvalia nadhifu kila siku. Ana mkoba wa kupendeza. Kiti chake ofisini kiko karibu na mlango. Mwalimu Ng'ara hutufunza kusoma na kuandika. Sisi tunajua kuchora kwa njia ya kipekee. Bi. Ng'ara hutupeleka maktabani pia. Maktabani kuna vitabu zaidi ya hamsini. Unapoenda pale, unachagua kitabu chako mwenyewe. Muda unapoisha mwalimu husema, "Rudisheni vitabu vyenu kwenye rafu."



na '-enu'.

*Waagize wanafunzi kutunga sentensi wakitumia vimilikishi; '–ako' na '-enu'*

### Zoezi

Fungua **ukurasa wa 8**. Tunga sentensi tatu ukitumia -ako na -enu na uziandike kwenye daftari lako.

### Kazi ya ziada

*Mwanafunzi aandike sentensi zaidi akitumia maneno: gwaride, maktaba, ofisi, bendera, mwalimu mkuu. Baadaye awasomee wazazi au walezi wake.*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 10 **Shuleni 1**

**Kipindi 10**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

D d G g

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: da ra sa - darasa**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| da | ja | sa | ga | tu |
| ra | mu | ge | li | pa |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Jaza mapengo ukitumia **-ako** na **-enu**.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Choo _____ ni safi. | Vyoo _____ ni safi. |
| 2. | Kiti _____ ni kikubwa. | Viti _____ ni vikubwa. |
| 3. | Kiatu _____ ni kipya. | Viatu _____ ni vipya. |

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Shule yetu**



**Kuandika**

Andika maneno haya kitabuni na uyatungie sentensi fupi.

1. tarakilishi
2. maktaba
3. darasani

Mali ya Serikali ya Kenya

10

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'D' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.* Jina la herufi hii ni 'D'. Hii ni herufi kubwa. Sauti yake ni /d/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'D'. Sauti yake ni /d/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'D' Sauti yake ni /d/.

*Rudia hatua ya 1-3 kwa kutumia herufi 'd' 'G' 'g'.*

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 10.** Taja jina la herufi na utamke sauti.

## Jedwali la silabi

*Chora jedwali la silabi kwenye ubao.*

**Ninafanya:** Leo tutatumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno. *Soma silabi zote.*

**Tunafanya:** Sasa tutasoma silabi pamoja. *Soma silabi pamoja na wanafunzi.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako kuzisoma silabi. *Wanafunzi wasome silabi zote.*

**Ninafanya:** Nitatumia silabi 'da' 'ra' 'sa' kuunda neno 'darasa'. *Andika neno 'darasa' ubaoni.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Unda maneno pamoja na mwenzako. *Wanafunzi waunde maneno. Andika maneno 3-4 ya wanafunzi ubaoni. Wanafunzi wasome maneno yote.*

## Msamiati wa hadithi ya mwalimu

Kabla ya kusoma tutajifunza kuhusu maneno mapya. Neno la kwanza ni 'gwaride'. Je, unafikiri neno 'gwaride' lina maana gani? *Wachague wanafunzi 2-3 wachangie swali kwa kusema maana ya neno. Waeleze wanafunzi maana ya neno.*

*Rudia hatua hizi kufunza maneno haya:* **bendera, wimbo wa taifa.**

## Kabla ya kusoma

**Tunafanya:** Fungua kwenye **ukurasa wa 10.**

Leo, nitawasomea hadithi huku mkisikiliza. Kabla ya kusoma, tutazungumzia zaidi kuhusu hadithi yenyewe. *Wasomee wanafunzi kichwa cha hadithi.*

Kichwa cha hadithi ni 'Shule yetu'. Tazama picha. Je, mnaona nini kwenye picha? *Wachague wanafunzi 2-3 waseme kile wanachoona kwenye picha.*

Hadithi hii inahusu Shule yetu. Ni nini tunachojua kuhusu shule yetu? *Wape wanafunzi 2-3 nafasi ya kujibu au kuchangia.*

Mweleze mwenzako kile unachofikiri kitatendeka kwenye hadithi? *Wachague wanafunzi 2-3 kuchangia somo kwa kutoa utabiri wao.*

## Hadithi ya mwalimu

Nitawasomea hadithi huku mkiitazama picha ya hadithi yenyewe.

*Soma hadithi kwa utaratibu huku ukitumia ishara na hisia*

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 10 **Shuleni 1**

**Kipindi 10**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

D d G g

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: da ra sa – darasa**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| da | ja | sa | ga | tu |
| ra | mu | ge | li | pa |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Jaza mapengo ukitumia **-ako** na **-enu**.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Choo _____ ni safi. | Vyoo _____ ni safi. |
| 2. | Kiti _____ ni kikubwa. | Viti _____ ni vikubwa. |
| 3. | Kiatu _____ ni kipya. | Viatu _____ ni vipya. |

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Shule yetu**



**Kuandika**

Andika maneno haya kitabuni na uyatungie sentensi fupi.

1. tarakilishi
2. maktaba
3. darasani

Mali ya Serikali ya Kenya 10

*iwezekanavyo. Badilisha sauti unaporejelea wahusika tofauti kwenye hadithi. Tulia kwanza, kabla ya kusoma jambo la kufurahisha na utoe maelezo mafupi kulihusu.*

**Shule yetu**

Jumatatu na Ijumaa ni siku za gwaride. Wanafunzi huvalia sare safi. Wanafunzi hupanga foleni ili wakaguliwe na walimu wao. Walimu huwapongeza wanafunzi wanaovaa sare safi. Walimu pia huwakosoa na kuwaelekeza wasiodumisha usafi.

Kipawa alikuwa mwanafunzi wa gredi ya sita. Yeye alikuwa na ujuzi wa kupandisha bendera. Ijumaa moja bendera ilichelewa kupandishwa kwa sababu Kipawa hakuja shuleni. Ilimbidi mwalimu mmoja aipandishe. Aliwaomba wanafunzi wasimame wima na akawaongoza kuimba Wimbo wa Taifa.

Baada ya Wimbo wa Taifa, Mwalimu Mkuu Bi.Mwema alisimama na kusema, “Ni vizuri mtambue talanta zenu.Kuna wanafunzi wengi walio na uwezo wa kupandisha bendera kama Kipawa. Kuanzia wiki ijayo wanafunzi wote wanaombwa kujiunga na vikundi mbalimbali ili kutunza talanta zenu. Vikundi hivi vitakuwa vikikutana kila Ijumaa saa tisa kamili.” Ijumaa iliyofuata wanafunzi wengi walijiandikisha katika kikundi cha wanaskauti.

Sasa tumeisoma hadithi. Je, yale ulitabiri yametimia? Mweleze mwenzako kuhusu utabiri uliotoa. Waulize wanafunzi kadhaa kujadili matokeo ya utabiri wao iwapo ulitimia.

### Maswali

**Ninafanya:** Wanafunzi huenda kwenye gwaride siku gani? *(Ijumaa na Jumatatu)*

**Tunafanya:** Kwa nini wanafunzi hujiunga na vikundi mbalimbali shuleni? *(Ili kukuza talanta zao)*

**Unafanya:** Taja vikundi mbalimbali katika shule yenu? *(Kubali jibu sahihi)*

### Kuandika

**Ninafanya:** Leo tutatunga na kuandika sentensi fupi. *Andika sentensi fupi ukitumia neno ‘darasani’ ubaoni.*

**Tunafanya:** Sasa mtatunga sentensi fupi mkitumia neno darasani. *Chagua wanafunzi 2-3 watunge sentensi huku ukiziandika kwenye ubao.*

**Unafanya:** Sasa angalia sehemu ya kuandika kwenye kitabu chako kwenye **ukurasa wa 10**. Chukua daftari lako utunge sentensi ukitumia maneno hayo. Andika kwa hati nadhifu.

### Sarufi

**Matumizi ya -ako na -enu**

**Tunafanya:** Nani anakumbuka tuliyojifunza jana kuhusu sarufi?

Tulijifunza kuhusu matumizi ya vimilikishi; ‘-ako’ na ‘-enu’. Tunatumia ‘-ako’ kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano: Kitabu chako ni kizuri. Tunatumia ‘-enu’ kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano: Vyakula vyenu ni vizuri.

Nitawafundisha kutunga sentensi kwa kutumia ‘-ako’ na ‘-enu.’ *Waongoze wanafunzi kutunga sentensi.*

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 10.** Fanya zoezi kuhusu sarufi kwa kujaza mapengo ukitumia ‘-ako’ na ‘-enu’.

Majibu: 1. chako/vyenu 2. chako/vyenu 3. chako/vyenu

### Kazi ya ziada

*Eleza mwanafunzi aandike maneno yafuatayo kisha achore kwenye daftari lake la ziada.*


1. Sare 2. Tarakilishi 3. Ubao 4. Kitabu 5. Mpira

### Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi aweze kujadiliana na mlezi wake nyumbani kuhusu umuhimu wa kwenda shuleni kusoma.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 11: Haki zangu 1



Kipindi cha 11 na 12 **Haki zangu 1**

**Kipindi 11**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**p** **d**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**pe** **pi** **po** **pu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ku pe wa | ku pa ta | a fi ka po | hu mwe pu sha |
|---|---|---|---|
| **kupewa** | **kupata** | **afikapo** | **humwepusha** |

**Kipindi 12**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**P** **p**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu patiwa | a na po lia | a li po teuliwa | a li panda |
|---|---|---|---|
| **hupatiwa** | **anapolia** | **alipoteuliwa** | **alipanda** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Igiza vitendo vifuatavyo ukitumia **vibaya** na **vizuri**.

1. Andika vizuri.
2. Chora vibaya.
3. Kula vizuri.
4. Simama vibaya.
5. Keti vizuri.
6. Tembea vibaya.

11 Hakiuzwi

## Utambuzi wa sauti

Tutajifunza sauti za Kiswahili leo. Kwanza tutataja sauti kisha neno. Ikiwa neno lina sauti /p/ mwanzoni nitaonyesha kidole juu. Ikiwa neno halina sauti /p/ mwanzoni nitaonyesha kidole chini.

**Ninafanya:** Sauti ni /p/. Neno la kwanza ni 'pata'. Neno hili linaanza kwa sauti /p/ kwa hivyo nitaonyesha kidole juu. Neno jingine ni 'rudi'. Neno hili halianzi kwa sauti /p/. Kwa hivyo naonyesha kidole chini.

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Sauti ni /p/. Sauti ni gani? Sauti ni /p/. Sasa nitataja neno. Ikiwa neno limeanza kwa sauti /p/, tutaonyesha kidole juu. Ikiwa halianzi kwa sauti /p/, tutaonyesha kidole chini. Neno la kwanza ni 'pata'. *Mwalimu na wanafunzi wanaonyesha kidole juu.*

Endelea na maneno; *yafuatayo:* punda, bundi, pita.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Sauti ni /p/. Onyesha kidole juu ikiwa neno linaanza kwa sauti /p/. Ikiwa halianzi kwa sauti /p/ onyesha kidole chini. *Tumia maneno yafuatayo:* pata, rudi, pokea, duka.

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'p' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.* Jina la herufi hii ni 'p'. Sauti yake ni /p/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'p'. Sauti yake ni /p/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'p'. Sauti yake ni /p/.
Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 11.** Taja jina la herufi na utamke sauti.

## Kusoma silabi

*Andika silabi 'pe' ubaoni au utumie kadi za herufi.*

**Ninafanya:** Leo tutaunda silabi kwa kuunganisha sauti. Nitataja sauti kisha nitamke silabi. Sauti hizi ni /p//e/. Naunganisha sauti zote mbili. Silabi ni 'pe'.

*Hakikisha unapitisha kidole chini ya kila herufi unapoitamka.*

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Tutatamka sauti kisha tutataja silabi pamoja. Sauti ni /p/ /e/. Silabi ni 'pe'.
**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Tamka sauti kisha utataja silabi. Sauti ni /p/ /e/. Silabi ni gani? 'pe'

*Rudia hatua 1-3 kwa kutumia silabi pi, po, pu.* Soma silabi kwenye **ukurasa wa 11.**

## Kusoma maneno kwa kutumia silabi

**Ninafanya:** *Andika neno 'kupewa' ubaoni.* Nitazameni: 'ku pe wa'. Neno ni 'kupewa'.

**Tunafanya:** Hebu tusome pamoja. Tutatamka silabi, kisha tusome. *Pitisha kidole chini ya kila silabi huku ukisoma pamoja na wanafunzi.* Silabi ni? 'ku pe wa'. Neno ni? 'kupewa'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tamka silabi kisha usome neno. Silabi ni? 'ku pe wa'. Neno ni 'kupewa'. *Rudia hatua ya 3 na maneno yafuatayo*: kupata, afikapo.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 11.** Tamka silabi kisha uyasome maneno.

## Msamiati

**Ninafanya:** *Andika neno 'matibabu' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi*. Neno hili ni 'matibabu'. *Lisome polepole mara mbili.*

**Tunafanya:** Ni wangapi wamelisikia neno hili 'matibabu'? Wangapi wanajua maana yake? *Eleza maana ya neno.*
**Ninafanya:** Nitatunga sentensi nikitumia neno 'matibabu'. *Tunga sentensi ukituma neno.*

**Unafanya:** Ni nani anaweza kutunga sentensi kwa kutumia neno 'matibabu'? *Chagua baadhi yao watunge sentensi wakitumia neno 'matibabu'.*

*Tumia hatua hizi kufunza maneno* **haki, kupewa jina.**

**Unafanya**: Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 12.**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Kipindi cha 11 na 12 Haki zangu 1

Kusoma hadithi

Haki za mtoto

Mtoto anapozaliwa anastahili kupewa haki zake. Anapozaliwa watu hufurahi na kumletea zawadi. Kupewa jina ni haki. Malaika huyu anapolia mama humnyonyesha. Miezi sita ya kwanza chakula chake ni maziwa. Maziwa humsaidia mtoto kukua vizuri. Afikapo miezi sita mtoto hupewa vyakula vingine. Ni lazima mtoto apelekwe hospitalini kupata chanjo. Pia akiwa mgonjwa anapaswa kupewa matibabu. Ni vibaya kumpa mtoto dawa bila maagizo ya daktari. Usafi wa mtoto huwa muhimu. Yeye huogeshwa na kuvalishwa mavazi mazuri na safi. Usafi humwepusha na magonjwa.

Mali ya Serikali ya Kenya 12

Someni maneno ambayo tumejifunza kwenye hadithi.

### Kabla ya kusoma

**Tunafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 12**. Kichwa cha hadithi ni 'Haki za mtoto'. Hadithi hii inahusu haki za mtoto. Nani anajua haki za mtoto? *Chagua wanafunzi 3-4 wajibu.*

Weka kidole chako kwenye kichwa cha hadithi. Tusome kichwa pamoja.

Tazama picha kitabuni. Unaona nini? *Pata majibu kutoka kwa wanafunzi 3-4.*

Fungeni vitabu. Mgeukie mwenzako na umweleze kitu kimoja unafikiri tutajifunza katika hadithi. Nani atatueleza kile mwenzake alisema. *Waulize wanafunzi 2-3 wajibu. Andika utabiri wao ubaoni.*

### Hadithi ya mwanafunzi

**Ninafanya:** Fungua kitabu chako tena kwenye **ukurasa wa 12.** Tutasoma hadithi ili tuone iwapo yale mlisema tutajifunza tumejifunza. Kwanza nitawasomea huku mkisikiliza. Weka kidole chako kwenye kichwa cha hadithi na ufuatilize ninaposoma. *Somea wanafunzi hadithi.*

**Tunafanya:** Sasa tusome hadithi pamoja. Fuatiliza kwa kutumia kidole. *Soma hadithi pamoja na wanafunzi.*

**Unafanya:** Sasa ni wakati wenu. Someni hadithi na mwenzako. *Zunguka darasani ili kuhakikisha kila mwanafunzi anasoma.*

### Maswali

**Ninafanya:** Mtoto anapozaliwa anastahili kupewa nini? *(Haki zake). Onyesha jinsi ya kutafuta jibu kwenye hadithi.*

**Tunafanya:** Ni nani humpa mtoto jina? *(Wazazi wake). Elekeza wanafunzi kutafuta jibu kwenye hadithi.*

**Unafanya:** Kwa nini mtoto hupewa maziwa anapozaliwa? *(Awe na afya nzuri)*

### Zoezi

Mtajie mwenzako jina na sauti za herufi zifuatazo:

1. p
2. f
3. v
4. g

*Zunguka darasani ili kuhakikisha kila mwanafunzi anataja jina na kutamka sauti za herufi.*

### Kazi ya ziada

Mhadithie mlezi wako hadithi uliyoisoma.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 12: Haki zangu 1

Kipindi cha | 11 na 12 | **Haki zangu 1**

**Kipindi 11**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**p** **d**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**pe** **pi** **po** **pu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ku pe wa | ku pa ta | a fi ka po | hu mwe pu sha |
|---|---|---|---|
| **kupewa** | **kupata** | **afikapo** | **humwepusha** |

**Kipindi 12**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**P** **p**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu patiwa | a na po lia | a li po teuliwa | a li panda |
|---|---|---|---|
| **hupatiwa** | **anapolia** | **alipoteuliwa** | **alipanda** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Igiza vitendo vifuatavyo ukitumia **vibaya** na **vizuri**.

1. Andika vizuri.
2. Chora vibaya.
3. Kula vizuri.
4. Simama vibaya.
5. Keti vizuri.
6. Tembea vibaya.

11 Hakiuzwi

Kipindi cha | 11 na 12 | **Haki zangu 1**

**Kusoma hadithi**



**Haki za mtoto**

Mtoto anapozaliwa anastahili kupewa haki zake. Anapozaliwa watu hufurahi na kumletea zawadi. Kupewa jina ni haki. Malaika huyu anapolia mama humnyonyesha. Miezi sita ya kwanza chakula chake ni maziwa. Maziwa humsaidia mtoto kukua vizuri.

Afikapo miezi sita mtoto hupewa vyakula vingine. Ni lazima mtoto apelekwe hospitalini kupata chanjo. Pia akiwa mgonjwa anapaswa kupewa matibabu. Ni vibaya kumpa mtoto dawa bila maagizo ya daktari. Usafi wa mtoto huwa muhimu. Yeye huogeshwa na kuvalishwa mavazi mazuri na safi. Usafi humwepusha na magonjwa.

Mali ya Serikali ya Kenya 12

### Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'P' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.* Jina la herufi hii ni 'P'. Hii ni herufi kubwa. Sauti yake ni /p/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'P'? Sauti yake ni /p/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'P' Sauti yake ni /p/.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 11**. Taja jina la herufi na utamke sauti.

### Kusoma maneno marefu

**Ninafanya:** *Andika neno 'hupatiwa' ubaoni.* Nitazameni: 'hu patiwa'. Neno ni 'hupatiwa'.

**Tunafanya:** Hebu tusome pamoja. Tutatamka sehemu za neno, kisha tusome lote kwa upesi. *Pitisha kidole chini ya kila sehemu huku ukisoma pamoja na wanafunzi.* Sehemu za neno ni? 'hu patiwa'. Neno ni? 'hupatiwa'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tamka sehemu za neno kisha usome neno. Sehemu za neno ni? 'hu patiwa' Neno ni 'hupatiwa'. *Rudia hatua ya 3 na maneno yafuatayo*: anapolia, alipoteuliwa, alipanda. Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 11**. Soma sehemu za neno na neno lote.

### Kabla ya kusoma

Mkumbushe mwanafunzi maana ya maneno; **matibabu, haki** na **kupewa jina.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**Unafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 12**. Somea mwenzako hadithi. Kumbuka kufuatiliza kidole chini ya kila neno unapolisoma.

### Sarufi

**Matumizi ya vizuri na vibaya**

*Andika vivumishi 'vizuri' na 'vibaya.' Ubaoni.*

**Ninafanya:** Tutajifunza kuhusu vielezi; 'vizuri' na 'vibaya'. *Onyesha neno 'vizuri', ubaoni.* Tunatumia neno 'vizuri' kuonyesha jambo linafanywa kwa njia inayopendeza. *K*wa mfano; Zainabu alicheza vizuri akashinda.

Neno 'vibaya' linamaanisha kuwa jambo halikufanyika vizuri. Kwa mfano; Zainabu alicheza vibaya akashindwa.

**Tunafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 12.** Tusome sentensi iliyopigiwa msitari kwenye hadithi pamoja.

**Ninafanya:** Nitawatungia sentensi nikitumia vielezi: 'vizuri' na 'vibaya.'

Sikiza. Baba alinifunza kuimba vizuri.

Mtoto alicheza mchezo vibaya.

**Unafanya:** Sasa ninataka utunge sentensi ukitumia vielezi, 'vizuri' na 'vibaya'. *Mwanafunzi atunge sentensi akitumia vielezi ; 'vizuri' na 'vibaya.'*

### Zoezi


Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 11.**

### Kazi ya ziada

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. Matibabu 2. Haki 3. Pewa jina

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________


Kipindi cha 13 na 14 **Haki zangu 1**

**Kipindi 13**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

f p

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

fe fi fo fu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ku fi chu a | fu ra hi | fo mu | fu ngwa |
| **kufichua** | **furahi** | **fomu** | **fungwa** |

**Kipindi 14**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

F f

★ Soma sehemu ya neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a li safisha | a na po funguliwa | a li po fika |
| **alisafisha** | **anapofunguliwa** | **alipofika** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Soma sentensi na kujaza mapengo kwa kutumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Mwanafunzi anafaa kuandika __________.
2. Dereva asiendeshe gari __________.
3. Mtoto anafaa kulelewa __________.
4. Mwalimu anafaa afundishe __________.
5. Mwanafunzi asiketi __________.
6. Mtoto anafaa atibiwe __________.

13 Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tutajifunza sauti za Kiswahili leo. Kwanza tutataja sauti kisha neno. Sauti ni /f/. Ikiwa neno lina sauti /f/ mwanzoni nitaonyesha kidole juu. Ikiwa neno halina sauti /f/ mwanzoni nitaonyesha kidole chini.

**Ninafanya:** Sauti ni /f/. Neno la kwanza ni 'fungwa'. Neno hili linaanza kwa sauti /f/ kwa hivyo nitaonyesha kidole juu. Neno jingine ni 'tunza'. Neno hili halianzi kwa sauti /f/. Kwa hivyo naonyesha kidole chini.

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Sauti ni /f/. Sauti ni gani? Sauti ni /f/. Sasa nitataja neno. Ikiwa neno limeanza kwa sauti /f/, tutaonyesha kidole juu. Ikiwa halianzi kwa sauti /f/, tutaonyesha kidole chini. Neno la kwanza ni 'fungwa'. *Mwalimu na wanafunzi wanaonyesha kidole juu.*

*Endelea na maneno; yafuatayo:* fuata, vuta, futa.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Sauti ni /f/. Onyesha kidole juu ikiwa neno linaanza kwa sauti /f/. Ikiwa halianzi kwa sauti /f/ onyesha kidole chini. *Tumia maneno yafuatayo:* funza, usafi, funzo.

### Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'f' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.*

Jina la herufi hii ni 'f'. Sauti yake ni /f/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'f'. Sauti yake ni /f/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'f'. Sauti yake ni /f/.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 13.** Taja jina la herufi na utamke sauti.

### Kusoma silabi

*Andika silabi 'fe' ubaoni au utumie kadi za herufi.*

**Ninafanya:** Leo tutaunda silabi kwa kuunganisha sauti. Nitataja sauti kisha nitamke silabi. Sauti hizi ni /f//e/. Naunganisha sauti zote mbili. Silabi ni 'fe'.

*Hakikisha unapitisha kidole chini ya kila herufi unapoitamka.*

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Tutatamka sauti kisha tutataja silabi pamoja. Sauti ni /f/ /e/. Silabi ni 'fe'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Tamka sauti kisha utataja silabi. Sauti ni /f/ /e/. Silabi ni gani? 'fe'.

*Rudia hatua 1-3 kwa kutumia silabi fi, fo, fu.* Soma silabi kwenye **ukurasa wa 11.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

**Ninafanya:** *Andika neno 'kufichua' ubaoni.* Nitazameni: ku fi chu a. Neno ni 'kufichua'.

**Tunafanya:** Hebu tusome sote. Tutatamka silabi, kisha tusome. *Pitisha kidole chini ya kila silabi huku ukisoma pamoja na wanafunzi.* Silabi ni? 'ku fi chu a'. Neno ni? 'kufichua'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tamka silabi kisha usome neno. Silabi ni 'kufichua'. Neno ni 'kufichua'. *Rudia hatua ya 3 na maneno yafuatayo*: funzo, fomu, fungwa.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 13.** Tamka silabi kisha uyasome maneno.

### Msamiati

**Ninafanya:** *Andika neno 'chakula' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi*. Neno hili ni 'chakula'. *Lisome polepole mara mbili.*

**Tunafanya:** Ni wangapi wamelisikia neno hili 'chakula'? Wangapi wanajua maana yake? *Eleza maana ya neno.*
**Ninafanya:** Nitatunga sentensi nikitumia neno 'chakula'. *Tunga sentensi ukituma neno.*

**Unafanya:** Ni nani anaweza kutunga sentensi kwa kutumia neno 'chakula'? *Chagua baadhi yao watunge sentensi wakitumia neno 'chakula'.*

*Tumia hatua hizi kufunza maneno* **mavazi, kupewa jina.**

**Unafanya**: Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 14.** Someni maneno ambayo tumejifunza kwenye hadithi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 13 na 14 **Haki zangu 1**

**Kusoma hadithi**



**Haki hizi haki gani?**

Kuzaliwa ni kuzuri, kupewa jina ni haki,
Sitaki kuitwa wewe, daima nitambulike,
Haki hizi haki gani, nizitaje uzijue?

Chakula haki ya pili, lishe bora niipate,
Watoto wafurahi, kuteseka ni vibaya,
Haki hizi haki gani, nizitaje uzijue?

Serikali imetangaza, elimu bila malipo,
Shuleni nihudhurie, nipate elimu bora,
Haki hizi haki gani, nizitaje uzijue?

Mavazi haki nyingine, nivae nguo vizuri,
Niwe kama wengine, uchi wangu kufichia,
Haki hizi haki gani, nizitaje uzijue?

Mali ya Serikali ya Kenya 14

### Kabla ya kusoma

**Tunafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 14.** Kichwa cha shairi ni 'Haki hizi haki gani'. Shairi hili inahusu haki za mtoto. Je, unajua haki za mtoto? *Chagua wanafunzi 3-4 wajibu.*

Weka kidole chako kwenye kichwa cha shairi. Tusome kichwa pamoja.

Tazama picha kitabuni. Unaona nini? *Pata majibu kutoka kwa wanafunzi 3-4.*

Fungeni vitabu. Mgeukie mwenzako na umweleze kitu kimoja unafikiri tutajifunza katika shairi. Nani atatueleza kile mwenzake alisema. *Waulize wanafunzi 2-3 wajibu. Andika utabiri wao ubaoni.*

### Hadithi ya mwanafunzi

**Ninafanya:** Fungua kitabu chako tena kwenye **ukurasa wa 14.** Tutasoma shairi ili tuone iwapo yale tulisema tutajifunza tumejifunza. Kwanza nitawasomea huku mkisikiliza. Weka kidole chako kwenye kichwa cha shairi na ufuatilize ninaposoma. *Somea wanafunzi shairi.*

**Tunafanya:** Sasa tusome shairi pamoja. Fuatiliza kwa kutumia kidole. *Soma shairi pamoja na wanafunzi.*

**Unafanya:** Sasa ni wakati wenu. Someni shairi na mwenzako. *Zunguka darasani ili kuhakikisha kila mwanafunzi anasoma.*

### Maswali

**Ninafanya:** Kwa nini mtoto anapaswa kupewa jina? *(Ni haki yake). Onyesha jinsi ya kutafuta jibu kwenye hadithi.*

**Tunafanya:** Haki ya pili kama ilivyotajwa katika shairi ni gani? *(Lishe bora) Elekeza wanafunzi jinsi ya kutafuta jibu kwenye hadithi.*

**Unafanya:** Taja aina mbalimbali ya vyakula vyenye lishe bora. *(Matunda, mboga, mihogo, viazi vitamu)*

### Zoezi

*Andika maneno yafuatayo ubaoni.* Soma maneno yafuatayo kwa kutumia silabi:

1. Viazi
2. Mavazi
3. Shule
4. Nyumba

### Kazi ya ziada

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. Kupewa jina
2. Elimu
3. Mavazi
4. Afya

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 14: Haki zangu 1

Kipindi cha 13 na 14 **Haki zangu 1**

**Kipindi 13**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

f p

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

fe fi fo fu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ku fi chu a | fu ra hi | fo mu | fu ngwa |
|---|---|---|---|
| **kufichua** | **furahi** | **fomu** | **fungwa** |

**Kipindi 14**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

F f

★ Soma sehemu ya neno na neno lote.

| a li safisha | a na po funguliwa | a li po fika |
|---|---|---|
| **alisafisha** | **anapofunguliwa** | **alipofika** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Soma sentensi na kujaza mapengo kwa kutumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Mwanafunzi anafaa kuandika ___________.
2. Dereva asiendeshe gari ___________.
3. Mtoto anafaa kulelewa ___________.
4. Mwalimu anafaa afundishe ___________.
5. Mwanafunzi asiketi ___________.
6. Mtoto anafaa atibiwe ___________.

13 Hakiuzwi

Kipindi cha 13 na 14 **Haki zangu 1**

**Kusoma hadithi**



**Haki hizi haki gani?**

Kuzaliwa ni kuzuri, kupewa jina ni haki,
Sitaki kuitwa wewe, daima nitambulike,
Haki hizi haki gani, nizitaje uzijue?

Chakula haki ya pili, lishe bora niipate,
Watoto wafurahi, kuteseka ni vibaya,
Haki hizi haki gani, nizitaje uzijue?

Serikali imetangaza, elimu bila malipo,
Shuleni nihudhurie, nipate elimu bora,
Haki hizi haki gani, nizitaje uzijue?

Mavazi haki nyingine, nivae nguo vizuri,
Niwe kama wengine, uchi wangu kufichia,
Haki hizi haki gani, nizitaje uzijue?

Mali ya Serikali ya Kenya 14

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'F' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.* Jina la herufi hii ni 'F'. Hii ni herufi kubwa. Sauti yake ni /f/

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'F'. Sauti yake ni /f/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'F'. Sauti yake ni /f/.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 13.** Taja jina la herufi na utamke sauti.

## Kusoma maneno marefu

**Ninafanya:** *Andika neno 'alisafisha' ubaoni.* Nitazameni: 'a li safisha'. Neno ni 'alisafisha'.

**Tunafanya:** Hebu tusome pamoja. Tutatamka sehemu za neno, kisha tusome neno lote kwa upesi. *Pitisha kidole chini ya kila sehemu huku ukisoma pamoja na wanafunzi.* Sehemu za neno ni 'a li safisha'. Neno ni 'alisafisha'.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tamka sehemu za neno kisha usome neno. Sehemu za neno ni 'a li safisha'. Neno ni 'alisafisha'. *Rudia hatua ya 3 na maneno yafuatayo*: anapofunguliwa, walipofungua.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 13.** Soma sehemu za neno na neno lote.

## Kabla ya kusoma

Mkumbushe mwanafunzi maana ya maneno; **chakula, mavazi** na **kupewa jina.**

## Kusoma shairi

**Unafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 14.** Somea mwenzako shairi. Kumbuka kufuatiliza kidole chini ya kila neno unapolisoma.

## Sarufi

**Matumizi ya vizuri na vibaya**

*Andika 'vizuri' na 'vibaya' ubaoni.*

**Ninafanya:** Tutajifunza kuhusu vielezi; 'vizuri' na 'vibaya'. *Onyesha neno 'vizuri', ubaoni.* Tunatumia neno 'vizuri' kuonyesha jambo linafanywa kwa njia inayopendeza. *K*wa mfano; Mwalimu alitufunza vizuri.

Neno 'vibaya' linamaanisha kuwa jambo halikufanyika vizuri. Kwa mfano; Dereva aliendesha gari vibaya likaanguka.

**Tunafanya:** Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 14.** Tusome sentensi iliyopigiwa msitari kwenye shairi pamoja.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 14: Haki zangu 1

Kipindi cha 13 na 14 **Haki zangu 1**

**Kipindi 13**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

f p

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

fe fi fo fu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ku fi chu a | fu ra hi | fo mu | fu ngwa |
|---|---|---|---|
| **kufichua** | **furahi** | **fomu** | **fungwa** |

**Kipindi 14**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

F f

★ Soma sehemu ya neno na neno lote.

| a li safisha | a na po funguliwa | a li po fika |
|---|---|---|
| **alisafisha** | **anapofunguliwa** | **alipofika** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Soma sentensi na kujaza mapengo kwa kutumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Mwanafunzi anafaa kuandika ___________.
2. Dereva asiendeshe gari ___________.
3. Mtoto anafaa kulelewa ___________.
4. Mwalimu anafaa afundishe ___________.
5. Mwanafunzi asiketi ___________.
6. Mtoto anafaa atibiwe ___________.

13 Hakiuzwi

Kipindi cha 13 na 14 **Haki zangu 1**

**Kusoma hadithi**



**Haki hizi haki gani?**

Kuzaliwa ni kuzuri, kupewa jina ni haki,
Sitaki kuitwa wewe, daima nitambulike,
Haki hizi haki gani, nizitaje uzijue?

Chakula haki ya pili, lishe bora niipate,
Watoto wafurahi, kuteseka ni vibaya,
Haki hizi haki gani, nizitaje uzijue?

Serikali imetangaza, elimu bila malipo,
Shuleni nihudhurie, nipate elimu bora,
Haki hizi haki gani, nizitaje uzijue?

Mavazi haki nyingine, nivae nguo vizuri,
Niwe kama wengine, uchi wangu kufichia,
Haki hizi haki gani, nizitaje uzijue?

Mali ya Serikali ya Kenya 14

**Ninafanya:** Nitawatungia sentensi nikitumia vielezi: 'vizuri' na 'vibaya.'

Sikiza. Mama alipika chakula vizuri.

Fundi alijenga nyumba vibaya.

**Unafanya:** Sasa ninataka utunge sentensi ukitumia vielezi, 'vizuri' na 'vibaya'. *Mwanafunzi atunge sentensi akitumia vielezi ; 'vizuri' na 'vibaya.'*

### Zoezi

Fungua kwenye **ukurasa wa 13** kwenye sarufi. Jaza mapengo kwa kutumia 'vizuri' au 'vibaya'.

*Sahihisha kazi ya mwanafunzi.*

**Majibu:**

1. vizuri
2. vibaya
3. vizuri
4. vizuri
5. vibaya
6. vizuri

### Kazi ya ziada

1. Finyanga maumbo ya herufi **p** na **f**.
2. Andika haki nne za watoto.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 15 **Haki zangu 1**

**Kipindi 15**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

P p F f

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: pa cha - pacha**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| fu | cha | ka | pe | ta |
| wa | fi | a | ku | pa |

◆ Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya

Andika sentensi hizi.

1. Zari hucheza mpira **vizuri**.
2. Alianguka akaumia **vibaya**.
3. Mwizi alipigwa **vibaya**.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Mashaka**



**Kuandika**

Tunga sentensi tatu ukitumia neno vibaya.

15 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi 'D' ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi au ufinyange umbo la herufi na uionyeshe.* Jina la herufi hii ni 'D'. Hii ni herufi kubwa. Sauti yake ni /d/.

**Tunafanya:** Sasa tutaje jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni 'D'. Sauti yake ni /d/.

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Jina la herufi hii ni 'D'. Sauti yake ni /d/.

*Rudia hatua ya 1-3 kwa kutumia herufi 'd' 'G' 'g'.*

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 10**. Taja jina la herufi na utamke sauti.

## Jedwali la silabi

*Chora jedwali la silabi kwenye ubao.*

**Ninafanya:** Leo tutatumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno. *Soma silabi zote.*

**Tunafanya:** Sasa tutasoma silabi pamoja. *Soma silabi pamoja na wanafunzi.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako kuzisoma silabi. *Wanafunzi wasome silabi zote.*

**Ninafanya:** Nitatumia silabi 'da' 'ra' 'sa' kuunda neno 'darasa'. *Andika neno 'darasa' ubaoni.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Unda maneno pamoja na mwenzako. *Wanafunzi waunde maneno. Andika maneno 3-4 ya wanafunzi ubaoni. Wanafunzi wasome maneno yote.*

## Msamiati wa hadithi ya mwalimu

Kabla ya kusoma tunaenda kujifunza kuhusu maneno mapya. Neno la kwanza ni 'malezi bora'. Je, unafikiri 'malezi bora' lina maana gani? *Wachague wanafunzi 2-3 wachangie swali kwa kusema maana ya neno. Waeleze wanafunzi maana ya neno.*

*Rudia hatua hizi kufunza maneno haya:* **matibabu, haki.**

## Kabla ya kusoma

**Tunafanya:** Fungua kwenye **ukurasa wa 10.**

Leo, nitawasomea hadithi huku mkisikiliza. Kabla ya kusoma, tutazungumzia zaidi kuhusu hadithi yenyewe. *Wasomee wanafunzi kichwa cha hadithi.*

Kichwa cha hadithi ni 'Mashaka'. Tazama picha. Je, mnaona nini kwenye picha? *Wachague wanafunzi 2-3 waseme kile wanachoona kwenye picha.*

Hadithi hii inahusu mtoto aliyeitwa Mashaka. Ni nini tunachojua kuhusu Mashaka? *Wape wanafunzi 2-3 nafasi ya kujibu au kuchangia.*

Mweleze mwanzako kile unachofikiri kitatendeka kwenye hadithi? *Wachague wanafunzi 2-3 kuchangia somo kwa kutoa utabiri wao.*

## Hadithi ya mwalimu

Nitawasomea hadithi huku mkiitazama picha ya hadithi yenyewe.

*Soma hadithi kwa utaratibu huku ukitumia ishara na hisia iwezekanavyo. Badilisha sauti unaporejelea wahusika tofauti kwenye hadithi. Tulia kwanza, kabla ya kusoma jambo la kufurahisha na utoe maelezo mafupi kulihusu.*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 15 Haki zangu 1

Kipindi 15

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

P p F f

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: pa cha - pacha**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| fu | cha | ka | pe | ta |
| wa | fi | a | ku | pa |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Andika sentensi hizi.

1. Zari hucheza mpira **vizuri**.
2. Alianguka akaumia **vibaya**.
3. Mwizi alipigwa **vibaya**.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Mashaka**



**Kuandika**

Tunga sentensi tatu ukitumia neno vibaya.

15 Hakiuzwi

**Mashaka**

Mashaka alikuwa mtoto wa Bi. na Bw. Heshima. Wazazi walimpenda mwana wao Mashaka. Walimpa Mashaka malezi bora na mavazi maridadi. Walimfunza kuwaheshimu wakubwa kwa wadogo. Walimshauri asome kwa bidii na kucheza kwa uangalifu.

Maisha ya Mashaka yalibadilika baada ya mama yake kufariki. Baba yake alioa bibi mwingine aliyeanza kumtesa Mashaka. Alimlazimisha kuacha masomo ili awatunze ndugu zake. Chakula chake kikawa ni makombo. Alimlazimisha alalie gunia bila blanketi wala shuka ya kujifunika. Alimchapa bila kosa. Mashaka alipougua hakumpeleka hospitalini kupata matibabu. Alimkataza pia kucheza na watoto wengine.

Majirani walipopata habari hii, walikasirika na kumshitaki mama huyo kwa chifu. Chifu alimkamata mama huyo na kusema, “Asanteni kwa kumwokoa Mashaka. Kila mtoto ana haki ya kutoteswa. Nawaomba tuendelee kuhakikisha watoto wote wamepata haki zao.”

Sasa tumeisoma hadithi. Je, yale ulitabiri yametimia? Mweleze mwenzako kuhusu utabiri uliotoa. Waulize wanafunzi kadhaa kujadili matokeo ya utabiri wao iwapo ulitimia.

## ? Maswali

**Ninafanya:** Mashaka alikuwa mtoto wa nani? *(Bi. na Bw. Heshima)*

**Tunafanya:** Mama wa kambo alimtesa vipi Mashaka? *(Alimuachisha shule, alimlazimisha alalie gunia, hakumpeleka hospitalini kupata matibabu)*

**Unafanya:** Mtoto anaponyimwa haki zake anafaa kufanya nini? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Kuandika

**Ninafanya:** Leo tutatunga na kuandika sentensi tukitumia neno ‘vibaya’. *Andika sentensi ukitumia neno ‘vibaya’ ubaoni.*

**Tunafanya:** Sasa mtatunga sentensi mkitumia neno ‘vibaya’. *Chagua wanafunzi 2-3 watunge sentensi huku ukiziandika kwenye ubao.*

**Unafanya:** Sasa angalia sehemu ya kuandika kwenye kitabu chako kwenye **ukurasa wa 15.** Chukua daftari lako utunge sentensi ukitumia neno ‘vibaya’. Andika kwa hati nadhifu.

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya ‘vizuri’ na ‘vibaya’**

**Tunafanya:** Nani anakumbuka tuliyojifunza jana kuhusu sarufi?

Tulijifunza kuhusu matumizi ya ‘vizuri’ na ‘vibaya’. Tunatumia neno ‘vizuri’ kuonyesha jambo linafanywa kwa njia inayopendeza. Kwa mfano; Kaka alikimbia vizuri. Neno ‘vibaya’ linamaanisha kuwa jambo halikufanyika vizuri. Kwa mfano; Wanafunzi waliimba vibaya.

Fungua kitabu chako kwenye **ukurasa wa 15.** Fanya zoezi la sarufi kwa kuandika sentensi kwenye daftari lako kwa hati nadhifu.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aakifishe sentensi zifuatazo kwa kutumia herufi kubwa na kikomo.

1. shule ya chewa ni nzuri sana
2. mwalimu wetu fatuma ni mzuri
3. mji wa wote ni mkubwa
4. mashaka alikuwa mtoto wa bi na bw heshima

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi amsikilize mgeni wa haki za watoto kuhusu umuhimu wa kufahamu haki zao.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 16 na 17 **Haki zangu 1**

**Kipindi 16**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  v f

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  ve vi vo vu

- Soma maneno ukitumia silabi.

| vi le vi le | vi a zi | vi mba | vu mbi |
|---|---|---|---|
| **vilevile** | **viazi** | **vimba** | **vumbi** |



**Kipindi 17**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  V v

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li vimbiwa | vi ka haribiwa | vi li lowa | a li vi sikia |
|---|---|---|---|
| **alivimbiwa** | **vikaharibiwa** | **vililowa** | **alivisikia** |

**Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Soma sentensi na kujaza mapengo kwa kutumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Ukiwa mgonjwa unahisi ________.
2. Alipewa zawadi baada ya kusoma ________.
3. Mwalimu alifundisha ________.
4. Walishindwa kwa sababu walicheza ________.
5. Watoto wana haki ya kutunzwa ________.

Kipindi cha 16 na 17 **Haki zangu 1**

**Kusoma hadithi**



**Haki za watoto**

Katiba ya Kenya inamlinda mtoto. Humlinda kutokana na dhuluma mbalimbali. Kila mtoto ambaye amefikisha umri wa miaka sita anapaswa kuwa shuleni. Watoto hawaruhusiwi kufanya kazi ya kulipwa. Hawafai kutunzwa vibaya. Ni makosa kumwadhibu mtoto kwa kumchapa. Watoto pia wana haki ya kulindwa vizuri. Anafaa kupata matibabu bora na mavazi. Vilevile, apate haki ya kusikilizwa. Watoto wanafaa kufurahia maisha yao.



### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti /v/. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** vumbi, papa

**U:** Endela na maneno vumbi, papa, vunja na punda.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** v

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 16**.

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /v/ /a/ silabi ni va

**U:** Endelea na silabi ve, vi, vo

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 16**.

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** vi le vi le- vilevile

**U:** Endelea na maneno; viazi, vimba, vumbi.

Katika vikundi vya wawili, wanafunzi wasomeane maneno kwenye **ukurasa wa 16**.

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **katiba**, **dhuluma**, **matibabu**.

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 17**.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Katiba ya Kenya inapendekeza mtoto wa miaka sita afanyiwe nini? *(Kuwa shuleni)*

**T:** Watoto hawaruhusiwi kufanya kazi ya aina gani? *(Kazi ya kulipwa)*

**U:** Taja haki zingine za mtoto unazozijua. *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi achague neno lililo sahihi.

1. Chakula na mavazi ni ________ ya watoto. (haki, hadithi)
2. ________ hupatia watoto afya bora. (Shule, Chakula)
3. Mtoto mgonjwa hupelekwa wapi? ________ (hospitalini, uwanjani)

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi ahadithie wengine nyumbani hadithi aliyosoma darasani.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 17: Haki zangu 1

Kipindi cha | 16 na 17 | **Haki zangu 1**

**Kipindi 16**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

v f

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ve vi vo vu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| vi le vi le | vi a zi | vi mba | vu mbi |
|---|---|---|---|
| **vilevile** | **viazi** | **vimba** | **vumbi** |

**Kipindi 17**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

V v

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li vimbiwa | vi ka haribiwa | vi li lowa | a li vi sikia |
|---|---|---|---|
| **alivimbiwa** | **vikaharibiwa** | **vililowa** | **alivisikia** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Soma sentensi na kujaza mapengo kwa kutumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Ukiwa mgonjwa unahisi ________.
2. Alipewa zawadi baada ya kusoma ________.
3. Mwalimu alifundisha ________.
4. Walishindwa kwa sababu walicheza ________.
5. Watoto wana haki ya kutunzwa ________.

Mali ya Serikali ya Kenya



Kipindi cha | 16 na 17 | **Haki zangu 1**

**Kusoma hadithi**



**Haki za watoto**

Katiba ya Kenya inamlinda mtoto. Humlinda kutokana na dhuluma mbalimbali. Kila mtoto ambaye amefikisha umri wa miaka sita anapaswa kuwa shuleni. Watoto hawaruhusiwi kufanya kazi ya kulipwa. Hawafai kutunzwa vibaya. Ni makosa kumwadhibu mtoto kwa kumchapa. Watoto pia wana haki ya kulindwa vizuri. Anafaa kupata matibabu bora na mavazi. Vilevile, apate haki ya kusikilizwa. Watoto wanafaa kufurahia maisha yao.



Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** V

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti katika kitabu chao kwenye **ukurasa wa 16.**

### Kusoma maneno marefu

Andika neno 'alivimbiwa' ubaoni.

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'a li vimbiwa' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'alivimbiwa' upesi.

**U:** Endelea na maneno; vikaharibiwa, alivisikia. Eleza mwanafunzi asome kwenye **ukurasa wa 16.**

### Kabla ya kusoma

Wakumbushe wanafunzi maana ya msamiati: **katiba, dhuluma, matibabu**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya vizuri na vibaya**

Andika maneno 'vizuri' na 'vibaya'.

'Vizuri' ni neno linalotumika kumaanisha jambo linapendeza au limefanyika kwa njia inayofurahisha. Kwa mfano: Mwalimu alitufundisha vizuri. 'Vibaya' lina maana kuwa jambo halipendezi au linafanyika kwa njia isiyofurahisha. Kwa mfano: Dereva aliendesha gari vibaya likaanguka.

Mwelekeze mwanafunzi kusoma sentensi zilizo na vizuri au vibaya kwenye hadithi.

### Zoezi

*Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi* kwenye **ukurasa wa 16.**

**Majibu:** 1. vibaya 2. vizuri 3. vizuri 4. vibaya 5. vizuri

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi anakili herufi v na maneno yafuatayo:

1. Viazi
2. Vimba
3. Vumbi

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha | 18 na 19 | **Haki zangu 1**

**Kipindi 18**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

f v

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

fe fi fo fu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| hu fa ri ki | fu ra ha | fi si | fi cha |
|---|---|---|---|
| **hufariki** | **furaha** | **fisi** | **ficha** |

**Kipindi 19**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

F f

★ Soma sehemu ya neno na neno lote.

| hu fichuka | a li fundisha | a na furahisha | a li filisika |
|---|---|---|---|
| **hufichuka** | **alifundisha** | **anafurahisha** | **alifilisika** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Soma sentensi na kujaza mapengo kwa kutumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Dereva anafaa kuendesha gari ________.
2. Alipigiwa makofi baada ya kusoma ________.
3. Mwanafunzi alijeruhiwa ________.
4. Watoto wanafaa kusoma ________ darasani.
5. Watoto hawafai kuvalia nguo ________.

Mali ya Serikali ya Kenya 18

Kipindi cha | 18 na 19 | **Haki zangu 1**

**Kusoma hadithi**



**Watoto wa mitaani**

Watoto wote ni wazuri. Wakipewa malezi bora hufaulu maishani. Watoto wote ni sawa hata wawe wa mitaani. Watoto wanaorandaranda hunyimwa haki zao. Kuna wale waliokosa pahali pa kulala. Hao hulala nje mitaani. Wengine hukosa mavazi bora. Wao huvaa vibaya. Mavazi yao huwa chafu na yaliyoraruka. Pia hawapati matibabu. Wengine huwa wezi. Wengine hufa njaa. Ni vizuri watoto wapewe haki zao.

19 Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti /f/. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** fungwa, ngazi

**U:** Endelea na maneno; funza, katiba na funzo.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja herufi. Tamka sauti. **N/T/U:** f

Mwanafunzi ataje jina la herufi na sauti kwenye **ukurasa wa 18.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti. Soma silabi.

**N/T/U**: /f/ /a/ silabi ni fa

**U:** Endelea na silabi; fe, fi, fo. Joa

Mwanafunzi wasome silabi kwenye **ukurasa wa 18.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi za kila neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** fu ra ha- furaha

**U:** Endelea na maneno; hufariki, fisi

Katika vikundi vya wawili wawili. Wape wanafunzi nafasi wasomeane maneno kwenye **ukurasa wa 18.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **haki, mavazi, malezi bora.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Watoto wakipewa malezi bora hufanya nini maishani? *(hufaulu maishani)*

**T:** Watoto wa mitaani hukosa nini maishani? *(haki zao)*

**U:** Taja haki nyingine ambazo mtoto anafaa kupata? *(elimu, lishe bora, mavazi)*

### Zoezi

Mwanafunzi atunge sentensi mbili akitumia maneno haya:

1. Haki 2. Mavazi

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi asimulie mzazi/mlezi wake hadithi aliyosoma.

Tarehe: ________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 19: Haki zangu 1

Kipindi cha 18 na 19 **Haki zangu 1**

**Kipindi 18**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

f v

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

fe fi fo fu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| hu fa ri ki | fu ra ha | fi si | fi cha |
|---|---|---|---|
| **hufariki** | **furaha** | **fisi** | **ficha** |

**Kipindi 19**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

F f

★ Soma sehemu ya neno na neno lote.

| hu fichuka | a li fundisha | a na furahisha | a li filisika |
|---|---|---|---|
| **hufichuka** | **alifundisha** | **anafurahisha** | **alifilisika** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Soma sentensi na kujaza mapengo kwa kutumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Dereva anafaa kuendesha gari ________.
2. Alipigiwa makofi baada ya kusoma ________.
3. Mwanafunzi alijeruhiwa ________.
4. Watoto wanafaa kusoma ________ darasani.
5. Watoto hawafai kuvalia nguo ________.

Mali ya Serikali ya Kenya 18

Kipindi cha 18 na 19 **Haki zangu 1**

**Kusoma hadithi**



**Watoto wa mitaani**

Watoto wote ni wazuri. Wakipewa malezi bora hufaulu maishani. Watoto wote ni sawa hata wawe wa mitaani. Watoto wanaorandaranda hunyimwa haki zao. Kuna wale waliokosa pahali pa kulala. Hao hulala nje mitaani. Wengine hukosa mavazi bora. Wao huvaa vibaya. Mavazi yao huwa chafu na yaliyoraruka. Pia hawapati matibabu. Wengine huwa wezi. Wengine hufa njaa. Ni vizuri watoto wapewe haki zao.

19 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** F

Mwanafunzi ataje jina la herufi na sauti yake kwenye **ukurasa wa 18.**

### Kusoma maneno marefu

Andika neno 'hufichuka' ubaoni.

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'hu fichuka' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'hufichuka' upesi.

**U:** Endelea na maneno; alifundisha, anafurahisha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 18.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **haki, mavazi na malezi bora.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya vizuri na vibaya**

Andika maneno 'vizuri' na 'vibaya'.

'Vizuri' ni neno linalotumika kumaanisha jambo linapendeza au limefanyika kwa njia inayofurahisha kwa mfano: Mwanafunzi alisoma hadithi vizuri. 'Vibaya' lina maana kuwa jambo halipendezi au linafanyika kwa njia isiyofurahisha kwa mfano: Mwanafunzi alisoma hadithi vibaya.

Mwelekeze mwanafunzi kusoma sentensi zilizo na matumizi ya vizuri na vibaya kwenye hadithi.

### Zoezi

*Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi* kwenye **ukurasa wa 18.**

**Majibu:** 1. vizuri 2. vizuri 3. vibaya 4. vizuri 5. vibaya

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi afinyange maumbo ya herufi p, f, v.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 20 **Haki zangu 1**

**Kipindi 20**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

V v F f

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ra ha - raha.**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| vi | fi | a | fu | mba |
| ra | le | ha | cha | zi |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Andika sentensi zifuatazo.

1. Zari hucheza mpira **vizuri**.
2. Ni **vibaya** kupiga kelele darasani.
3. Mtoto aliumia **vibaya** alipoanguka.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Usiwadharau wenye ulemavu**



**Kuandika**

Tunga sentensi nne ukitumia maneno vizuri na vibaya.

Mali ya Serikali ya Kenya 20

### ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** V, v, F, f.

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 20.**

### Jedwali

Chora jedwali la silabi. **T:** Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'raha'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

### Hadithi ya mwalimu

Funza maana ya maneno: **ulemavu, kubaguliwa.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

Soma hadithi. Mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

**Usiwadharau wenye ulemavu**

Katika kijiji cha Matumaini kulikuwa na familia ya Bw. na Bi. Imani. Walibarikiwa na watoto pacha. Pacha hawa walipewa majina Dhahabu na Baraka. Dhahabu na Baraka hawakuwa na uwezo wa kuongea wala kusikia. Kulingana na mila za eneo la Matumaini iliaminika kuwa pacha walileta mikosi.

Siku moja Bwana Imani aliandamana na pacha wake hadi shule ya Wote ili wapate haki ya kuelimishwa. Walipofika, Bwana Imani alimwelezea mwalimu mkuu kuhusu hali ya watoto wake. Mwalimu mkuu alimhakikishia Bwana Imani kuwa, watoto hao wangesoma bila kubaguliwa. Mwalimu mkuu alimwita mwalimu wa lugha ya ishara Bi. Malasi. Bi. Malasi aliwakaribisha pacha hao darasani.

Shuleni waliwasiliana na wenzao kutumia lugha ya ishara. Pacha hao walifaulu katika masomo na michezoni. Sifa zao zikaenea kote kijijini Matumaini. Wanakijiji walielewa umuhimu wa kuwatunza wenye ulemavu.

### ? Maswali

**N:** Watoto wa Bw. na Bi. Imani hawakuwa na uwezo wa nini? *(kuongea na kusikia)*

**T:** Pacha waliotajwa katika hadithi waliwasiliana vipi na wenzao? *(kwa kutumia lugha ya ishara)*

**U:** Taja jinsi unavyoweza kumsaidia mtoto aliye na ulemavu? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Kuandika

**N:** Andika sentensi ukitumia neno 'vizuri'.

**T:** Mwongoze mwanafunzi kuandika sentensi akitumia neno 'vizuri'.

**U:** Mwanafunzi atunge na aandike sentensi tatu akitumia neno 'vizuri'.

### ◆ Sarufi

**Matumizi ya vizuri na vibaya**

**N:** 'Vizuri' ni neno linalotumika kumaanisha jambo linapendeza au limefanyika kwa njia inayofurahisha kwa mfano: Mama alipika vizuri. 'Vibaya' lina maana kuwa jambo halipendezi au linafanyika kwa njia isiyofurahisha kwa mfano: Babu alibomoa nyumba vibaya.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 20.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi akitumia maneno yafuatayo.

1. Walemavu
2. Matibabu
3. Malezi bora

### Kazi ya nyongeza

Mwalimu afanye yafuatayo ikiwa atapata muda.

- **Michoro:** Wanafunzi wachore picha kuonyesha matukio katika hadithi ya mwalimu. Picha zinaweza kupangwa ili zisaidie kusimulia hadithi tena.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 21: Usafiri 1

Kipindi cha 21 na 22 **Usafiri 1**

**Kipindi 21**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **ch** **v**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  **che** **chi** **cho** **chu**

- ★ Soma maneno ukitumia silabi.

| cha ku la | chu ku a | chi fu | chu ma |
|---|---|---|---|
| **chakula** | **chukua** | **chifu** | **chuma** |

**Kipindi 22**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **CH** **ch**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li chora | a li cho panda | wa li chungulia |
|---|---|---|
| **alichora** | **alichopanda** | **walichungulia** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Tambua matumizi ya herufi kubwa katika sentensi hizi.

1. **B**asi letu lina rangi ya manjano.
2. **J**umatatu ni siku ya kuimba wimbo wa taifa.
3. **A**tieno na **M**waura wako darasa la pili.
4. **T**utaenda **K**itale kwa basi.
5. **N**chi ya **K**enya huwa na kiangazi mwezi wa **J**anuari.



Kipindi cha 21 na 22 **Usafiri 1**

**Kusoma hadithi**




**Riakanao**

Katika kijiji cha Mpungani, kulikuwa na basi. Basi hilo liliitwa Riakanao. Basi hilo lilibeba abiria na mizigo. Hakukuwa na chombo kingine cha usafiri Mpungani. Meli au ndege hazikupatikana. Siku moja wanakijiji waliliabiri basi hilo. Basi lilikuwa likienda polepole. Abiria walianza kulalamika. Walimtaka dereva aliendeshe kwa kasi. Walimpigia kelele.

"Basi hili haliwezi kuendeshwa haraka. Limewekwa vidhibiti mwendo," dereva alisema. Aliwaeleza umuhimu wa kuendesha polepole. Abiria walivumilia. Baada ya kukaa sana barabarani, walifika salama.



### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ch/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti **/ch/** mwanzoni mwa neno au aonyeshe vidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** chakula, penda

**U:** Endelea na maneno; chakula, penda, changa, chifu na chuma.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ch, v

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 21**.

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti. Soma silabi.

**N/T/U:** /ch/ /a/ silabi ni cha

**U:** Endelea na silabi; che, chi, cho, chu.

Eleza mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 21**.

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila sauti katika kila neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** cha nga - changa

**U:** Endelea na maneno; chukua, chifu.

Katika vikundi vya wawili, wanafunzi wasomeane maneno kwenye **ukurasa wa 21**.

### Msamiati

Funza maana ya maneno **basi**, **meli**, **ndege**.

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 22**.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kijiji kilichotajwa katika hadithi kinaitwaje? *(Mpungani)*

**T:** Basi lililotajwa lilibeba nini? *(abiria na mizigo)*

**U:** Unafikiria ni kwa nini basi lilikuwa likienda polepole? *(abiria wafike salama)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike silabi kutokana na herufi zifuatazo:

1. ch  2. dh  3. l  4. b

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi ajadiliane na walezi wake kuhusu umuhimu wa vyombo vya usafiri.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 22: Usafiri 1

Kipindi cha 21 na 22 **Usafiri 1**

**Kipindi 21**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ch** **v**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**che** **chi** **cho** **chu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| cha ku la | chu ku a | chi fu | chu ma |
|---|---|---|---|
| **chakula** | **chukua** | **chifu** | **chuma** |

**Kipindi 22**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**CH** **ch**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li chora | a li cho panda | wa li chungulia |
|---|---|---|
| **alichora** | **alichopanda** | **walichungulia** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Tambua matumizi ya herufi kubwa katika sentensi hizi.

1. Basi letu lina rangi ya manjano.
2. Jumatatu ni siku ya kuimba wimbo wa taifa.
3. Atieno na Mwaura wako darasa la pili.
4. Tutaenda Kitale kwa basi.
5. Nchi ya Kenya huwa na kiangazi mwezi wa Januari.

21 Hakiuzwi

Kipindi cha 21 na 22 **Usafiri 1**

**Kusoma hadithi**




**Riakanao**

Katika kijiji cha Mpungani, kulikuwa na basi. Basi hilo liliitwa Riakanao. Basi hilo lilibeba abiria na mizigo. Hakukuwa na chombo kingine cha usafiri Mpungani. Meli au ndege hazikupatikana. Siku moja wanakijiji waliliabiri basi hilo. Basi lilikuwa likienda polepole. Abiria walianza kulalamika. Walimtaka dereva aliendeshe kwa kasi. Walimpigia kelele.

"Basi hili haliwezi kuendeshwa haraka. Limewekwa vidhibiti mwendo," dereva alisema. Aliwaeleza umuhimu wa kuendesha polepole. Abiria walivumilia. Baada ya kukaa sana barabarani, walifika salama.

Mali ya Serikali ya Kenya 22

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** CH, ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti yake kwenye **ukurasa wa 21.**

### Kusoma maneno marefu

Andika neno 'alichora' ubaoni.

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'a li chora' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'alichora' upesi.

**U**: Endelea na neno: alichopanda.

Mwanafunzi asome kwenye **ukurasa wa 21.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **basi, meli, ndege.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U**: Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya herufi kubwa**

Eleza matumizi ya herufi kubwa. Tunatumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi . Andika ubaoni. 'Dhahabu hung'aa sana'. Waonyeshe wanafunzi herufi kubwa.

Pia herufi kubwa hutumiwa mwanzoni mwa majina ya vitu au mahali. Andika sentensi zifuatazo na uonyeshe wanafunzi herufi kubwa.

Shule ya Chewa ni nzuri sana. Mwalimu wetu Fatuma ni mzuri. Mji wa Nairobi ni mkubwa.

Mwongoze mwanafunzi kusoma sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 21.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia maneno yafuatayo. Tunatumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi. Kwa mfano: Dhahabu hung'ara sana.

1. Matatu
2. Basi
3. Pikipiki
4. Ndege

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 23 na 24 — **Usafiri 1**

**Kipindi 23**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  dh ch

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  dhe dhi dho dhu

- Soma maneno ukitumia silabi.

| ba a dhi | dha ti | dhi di | dho ru ba |
|---|---|---|---|
| **baadhi** | **dhati** | **dhidi** | **dhoruba** |

**Kipindi 24**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  DH dh

- Soma sehemu ya neno na neno lote.

| wa li m dhulumu | a li m dhania | a li mu adhibu |
|---|---|---|
| **walimdhulumu** | **alimdhania** | **alimuadhibu** |

**Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Katika vikundi vya wanafunzi wawili, soma sentensi zifuatazo. Andika herufi kubwa zilizotumiwa.

1. **B**asi limebeba abiria na mizigo.
2. **B**i. **Z**awadi amefika kwa gari dogo.
3. **A**pesa na **S**ifa wako shuleni.
4. **B**aba ameninunulia pikipiki dogo.
5. **A**biria walifika **M**ombasa usiku sana.



Kipindi cha 23 na 24 — **Usafiri 1**

**Kusoma hadithi**




**Apesa azawadiwa**

Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Apesa na Sifa walikuwa shuleni. Usafiri ulitatizika. Jioni, Apesa na Sifa waliamua kutembea. Mto ulikuwa umejaa na kufurika. Walipokuwa wakivuka mto, Sifa aliteleza na kuanguka mtoni. Apesa alijua kuogelea.

Aliruka mtoni kumtoa ili asizame. Wakati huo huo wanakijiji walikuwa washafika. Walimsaidia Apesa kumwokoa Sifa.

Wanakijiji walifurahi sana. Waliamua kumfanyia Apesa sherehe.

Baadhi ya wageni walisafiri kwa mabasi. Wengine walitumia matatu na pikipiki. Mbunge alifika kwa gari dogo. Alimpa Apesa zawadi. Aliwaahidi kutengeneza daraja hilo.



### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/dh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** dhahabu, haki

**U:** Endelea na maneno; dhoruba, darasa na dhiki.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** dh, ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 23.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti. Soma silabi.

**N/T/U:** /dh//a/, silabi ni dha

**U:** Endelea na silabi; dhe, dhi, dho.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 23.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi kwa kila neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** dho ru ba – dhoruba

**U:** Endelea na maneno; baadhi, dhati

Katika vikundi vya wawili wawili wanafunzi wasomeane maneno kwenye **ukurasa wa 23.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **matatu, pikipiki, gari dogo.** Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kwa nini mto ulikuwa umejaa maji? *(Mvua kubwa ilinyesha)*

**T:** Apesa na Sifa walikuwa wapi? *(Walikuwa shuleni)*

**U:** Unafikiria ni njia gani za usafiri ambazo Apesa na Sifa wangetumia badala ya kutembea? *(Pikipiki, gari)*

### Zoezi

Mwanafunzi asome maneno yafuatayo wakiwa katika vikundi kisha waandike silabi katika kila neno:

1. lori – lo ri
2. matatu – ma ta tu
3. pikipiki – pi ki pi ki
4. garimoshi – ga ri mo shi

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi afinyange maumbo ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa, 'dh' na 'ch'.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 24: Usafiri 1

Kipindi cha 23 na 24 | **Usafiri 1**

**Kipindi 23**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**dh** **ch**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**dhe** **dhi** **dho** **dhu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ba a dhi | dha ti | dhi di | dho ru ba |
| **baadhi** | **dhati** | **dhidi** | **dhoruba** |

**Kipindi 24**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**DH** **dh**

★ Soma sehemu ya neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| wa li m dhulumu | a li m dhania | a li mu adhibu |
| **walimdhulumu** | **alimdhania** | **alimuadhibu** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Katika vikundi vya wanafunzi wawili, soma sentensi zifuatazo. Andika herufi kubwa zilizotumiwa.

1. **B**asi limebeba abiria na mizigo.
2. **B**i. **Z**awadi amefika kwa gari dogo.
3. **A**pesa na **S**ifa wako shuleni.
4. **B**aba ameninunulia pikipiki dogo.
5. **A**biria walifika **M**ombasa usiku sana.

23

Hakiuzwi

Kipindi cha 23 na 24 | **Usafiri 1**

**Kusoma hadithi**




**Apesa azawadiwa**

Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Apesa na Sifa walikuwa shuleni. Usafiri ulitatizika. Jioni, Apesa na Sifa waliamua kutembea. Mto ulikuwa umejaa na kufurika. Walipokuwa wakivuka mto, Sifa aliteleza na kuanguka mtoni. Apesa alijua kuogelea.

Aliruka mtoni kumtoa ili asizame. Wakati huo huo wanakijiji walikuwa washafika. Walimsaidia Apesa kumwokoa Sifa.

Wanakijiji walifurahi sana. Waliamua kumfanyia Apesa sherehe.

Baadhi ya wageni walisafiri kwa mabasi. Wengine walitumia matatu na pikipiki. Mbunge alifika kwa gari dogo. Alimpa Apesa zawadi. Aliwaahidi kutengeneza daraja hilo.

Mali ya Serikali ya Kenya

24

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

N/T/U: DH, dh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 23.**

## Kusoma maneno marefu

Andika neno 'walimdhulumu' ubaoni.

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'wa li m dhulumu' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'walimdhulumu' upesi.

**U:** Endelea na maneno; alimdhania, alimdharau.

Eleza mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 23.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **matatu**, **pikipiki**, na **gari ndogo**.

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya herufi kubwa**

Andika herufi 'DH' na 'CH' ubaoni.

Eleza matumizi ya herufi kubwa. Tunatumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi. Andika ubaoni. 'Basi limebeba abiria'. Waonyeshe wanafunzi herufi kubwa.

Pia herufi kubwa hutumiwa mwanzoni mwa majina ya vitu au mahali. Andika sentensi zifuatazo na uonyeshe wanafunzi herufi kubwa.

1. Mji wa Kisumu ni mkubwa.
2. Baba yangu anaitwa Hosea.
3. Rafiki yangu anaishi Kitutu.

Mwongoze mwanafunzi kusoma sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 23.**

**Majibu**

1. Basi – mwanzoni mwa sentensi.
2. Bi. Zawadi – mwanzoni mwa sentensi ni jina la mtu.
3. Apesa na Sifa – mwanzoni mwa sentensi na majina ya watu.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aakifishe sentensi zifuatazo kwa kutumia herufi kubwa.

1. basi letu lina rangi ya manjano.
2. atieno na mwaura wako katika darasa la pili.
3. tutasafiri mombasa kwa basi.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 25: Usafiri 1

Kipindi cha 25 **Usafiri 1**

**Kipindi 25**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

DH dh CH ch

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: che za - cheza**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| dha | fi | dhu | mu | mbi |
| ra | lu | che | cha | za |

◆ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Akifisha sentensi zifuatazo ukitumia herufi kubwa.

1. kipindi cha kiswahili kilikuwa kizuri.
2. basi la kwenda kwa babu linaitwa maisha.
3. garimoshi limepeleka mizigo mombasa.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Safari katika basi la shule**




**Kuandika**

Chora maumbo ya vyombo hivi vya usafiri.

1. Baiskeli 2. Basi 3. Pikipiki

25 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** DH, dh, CH, ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 25.**

## Jedwali

**N:** Chora jedwali la silabi.

**T:** Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'cheza'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza maneno mapya: **mabasi, magari madogo, matatu.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi. Mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

**Safari katika basi la shule**

Shule yetu ya Ushindi ilikuwa ikishiriki katika mashindano ya michezo ya mipira. Michezo hii ilikuwa katika shule ya Afuraha iliyokuwa mbali na shule yetu. Tulianza safari yetu mapema kwani michezo ilikuwa ianze saa tatu asubuhi.

Tulitumia basi la shule. Kila mwanafunzi alijifunga mkanda wa usalama.

Tulifurahia kuyaona magari mengine kama vile, matatu, mabasi na magari madogo. Madereva wengine waling'ang'ana kuyapita magari mengine. Jambo hili lilisababisha msongamano wa magari.

Baadaye polisi wa trafiki alifika na kuyaelekeza magari ili kupunguza msongamano. Alikuwa na simu ya rununu aliyoitumia kuwasiliana na polisi wenzake. Wanafunzi wengi waliogopa walipoona malori yakikaribia basi letu. Tulitamani kusafiri kwa pikipiki kwa sababu zilikuwa zikitupita kwa mwendo wa kasi. Hatimaye, tulifika katika shule ya Afuraha na michezo ikaendelea.

## Maswali

**T:** Basi la shule lilikuwa likielekea wapi? *(Shule ya Afuraha)*

**U:** Ni nani aliyesaidia kupunguza msongamano wa magari? *(Polisi wa trafiki)*

**U:** Je, ni aina gani ya usafiri unayoipenda zaidi? Eleza ni kwa nini? *(Kubali jibu sahihi)*

## Kuandika

**N:** Chora umbo la chombo kimoja cha kusafiri.

**T:** Waongoze wanafunzi wachore chombo cha kusafiria.

**U:** Wanafunzi wachore baisikeli, basi na pikipiki.

## Sarufi

**Matumizi ya herufi kubwa**

Andika herufi 'DH' na 'CH' ubaoni.

Eleza matumizi ya herufi kubwa. Tunatumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi. Andika ubaoni. 'Chama cha maskauti kimesafiri'. Waonyeshe wanafunzi herufi kubwa.

Pia herufi kubwa hutumiwa mwanzoni mwa majina ya vitu au mahali. Andika sentensi zifuatazo na uonyeshe wanafunzi herufi kubwa. Shamba la Chalo ni kubwa; Yaya wetu anaitwa Cheruto; Kijiji cha Chanzu ni kidogo.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 25.**

**Majibu:**

1. Kipindi cha Kiswahili kilikuwa kizuri.
2. Basi la kwenda kwa babu linaitwa Maisha.
3. Garimoshi limepeleka mizigo Mombasa.

## Kazi ya ziada

Andika maneno haya kisha uchore vyombo hivi vya usafiri.

1. Ndege
2. Basi
3. Meli

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 26: Familia 1

Kipindi cha 26 na 27 **Familia 1**

**Kipindi 26**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

gh dh

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ghe ghi gho ghu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| gha ra ma | ma gha ri bi | dho ru ba | cho mbo |
|---|---|---|---|
| **gharama** | **magharibi** | **dhoruba** | **chombo** |

**Kipindi 27**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

Gh gh

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| ma ghorofa | hu gharimu | a li chafuka | a li ghairi |
|---|---|---|---|
| **maghorofa** | **hugharimu** | **alichafuka** | **alighairi** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya maneno yanayoashiria vitendo**

Igiza vitendo hivi.

1. Simama
2. Tembea
3. Cheka
4. Ruka
5. Andika
6. Osha nguo
7. Piga mswaki

Mali ya Serikali ya Kenya 26

Kipindi cha 26 na 27 **Familia 1**

**Kusoma hadithi**



**Arusi ya kufana**

Ilikuwa siku ya Jumamosi mwezi uliopita. Nilibahatika kuhudhuria arusi ya kufana mjini. Ami yangu Gholika alikuwa akifunga ndoa. Aliandaa karamu kubwa. Watu walifika kwa wingi. Nilifurahi na kucheka nilipokutana na ndugu na marafiki. Shangazi yangu anayeishi ng'ambo alikuwa amefika. Mjomba Ngatia alifika pamoja na familia yake. Bwana na bibi arusi walisimama na kupewa zawadi nyingi. Mama na baba waliwapa pikipiki. Ilikuwa sherehe ya shangwe na nderemo.

27 Hakluzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti /gh/. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** gharama, maji.

**U:** Endelea na maneno; ghala, ugali, gari na magharibi.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** gh, dh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 26.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /gh/ /a/ silabi ni gha

**U:** Endelea na silabi; ghe, ghi, gho.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 26.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** gha ra ma – gharama

**U:** Endelea na maneno; magharibi, dhoruba.

Katika vikundi vya wawili wawili, wanafunzi wasomeane maneno kwenye **ukurasa wa 26.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **ami, shangazi, mjomba.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 27**.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Harusi ilifanyika siku gani? *(Jumamosi)*

**T:** Ni nani alikuwa akifunga ndoa? *(Gholika)*

**U:** Unafikiri shangazi aliishi nchi gani? *(Kubali jibu lolote sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aunde silabi kwa kutumia herufi zifuatazo katika vikundi vys wawili wawili.

1. ny 2. ng' 3. gh 4. ng

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi ajadiliane na walezi wake kuhusu watu hawa:

1. Mjomba 2. Shangazi 3. Ami

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 27: Familia 1

Kipindi cha 26 na 27 **Familia 1**

**Kipindi 26**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**gh** **dh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ghe** **ghi** **gho** **ghu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| gha ra ma | ma gha ri bi | dho ru ba | cho mbo |
|---|---|---|---|
| **gharama** | **magharibi** | **dhoruba** | **chombo** |

**Kipindi 27**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**Gh** **gh**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| ma ghorofa | hu gharimu | a li chafuka | a li ghairi |
|---|---|---|---|
| **maghorofa** | **hugharimu** | **alichafuka** | **alighairi** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya maneno yanayoashiria vitendo**

Igiza vitendo hivi.

1. Simama
2. Tembea
3. Cheka
4. Ruka
5. Andika
6. Osha nguo
7. Piga mswaki

Mali ya Serikali ya Kenya

26

Kipindi cha 26 na 27 **Familia 1**

**Kusoma hadithi**



**Arusi ya kufana**

Ilikuwa siku ya Jumamosi mwezi uliopita. Nilibahatika kuhudhuria arusi ya kufana mjini. Ami yangu Gholika alikuwa akifunga ndoa. Aliandaa karamu kubwa. Watu walifika kwa wingi. Nilifurahi na kucheka nilipokutana na ndugu na marafiki. Shangazi yangu anayeishi ng'ambo alikuwa amefika. Mjomba Ngatia alifika pamoja na familia yake. Bwana na bibi arusi walisimama na kupewa zawadi nyingi. Mama na baba waliwapa pikipiki. Ilikuwa sherehe ya shangwe na nderemo.

27 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** GH, gh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 26.**

### Kusoma maneno marefu

Andika neno 'maghorofa' ubaoni.

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'ma ghorofa' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'maghorofa' upesi.

**U:** Endelea na maneno; hugharimu, alichafuka. Eleza mwanafunzi asome maneno yaliyo kwenye **ukurasa wa 26.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **ami, shangazi, mjomba.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U**: Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya maneno yanayoashiria vitendo**

Andika maneno haya ubaoni: 'simama', 'tembea', 'andika', 'cheka', 'oga' na 'chana'.

Eleza maana ya maneno ya vitendo. Maneno ya vitendo ni yale yanaonyesha kutendeka kwa jambo fulani. Kama vile simama, tembea, cheka, chana. Maneno haya huonyesha vitendo.

Waongoze wanafunzi kutaja maneno yanayoonyesha vitendo. Wanafunzi watambue na wasome maneno yanayoonyesha vitendo kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 26.**

Mwanafunzi aigize vitendo.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aigize matumizi ya maneno haya akiwa na mlezi wake.

1. Hodi
2. Naomba
3. Karibu

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha | 28 na 29 | **Familia 1**

**Kipindi 28**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ny** **gh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**nyi** **nyo** **nyu** **gho**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | |
|---|---|---|
| nya nya | ku fa nya | nye u pe |
| **nyanya** | **kufanya** | **nyeupe** |

**Kipindi 29**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NY** **ny**

★ Soma sehemu ya neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ku kanya | a li kunywa | wa nyama | hu nyolewa |
| **kukanya** | **alikunywa** | **wanyama** | **hunyolewa** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya maneno yanayoashiria vitendo**

Jaza mapengo ukitumia neno moja kati ya uliyopewa.

1. Babu alitu________ nyumbani kwetu. (soma, tembelea)
2. Mwalimu alitu________ Kiswahili. (ruka, fundisha)
3. Ami ana________ shambani. (lima, osha)
4. Halati ata__________nywele. (fagia, chana)
5. Binamu ali _______ kucha. (panda, kata)

Mali ya Serikali ya Kenya

28

Kipindi cha | 28 na 29 | **Familia 1**

**Kusoma hadithi**



**Likizo mashambani**

Likizo iliyopita mimi na dada yangu tulienda mashambani. Nyanya yangu alifurahi kutuona. Tulimsaidia kufanya kazi shambani. Tulihakikisha ng'ombe wake wameshiba. Babu alifurahishwa na kazi zetu. Baada ya kazi tulioga na kuchana nywele zetu. Nyanya alihakikisha tulipata lishe bora. Wakati wa kurudi nyumbani ulifika. Binamu walitoa mahindi ndani ya ghala. Walitupatia tukampelekea mama yetu. Tulipata mafunzo mengi mashambani.

29 Hakluzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti /**ny**/. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** nyanya, binamu

**U:** Endelea na maneno; nyeupe, kiti, nyekundu na alinyang'anya.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ny, gh

Mwanafunzi ataje jina La herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 28.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi. **N/T/U:** /ny/ /a/ silabi ni nya

**U:** Endelea na silabi; nyi, nyo, nyu, gho.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 28.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** nyi ngi - nyingi

**U:** Endelea na maneno; nyanya, kufanya na nyeupe.

Katika vikundi vya wawili wawili wanafunzi wasomeane maneno kwenye **ukurasa wa 28.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **nyanya, babu, binamu.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Wakati wa likizo dada alienda wapi? *(Mashambani)*

**T:** Ni kwa nini babu alifurahi? *(Kwa kazi waliyofanya)*

**U:** Je, unafikiria ni mafunzo gani walijifunza mashambani? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aunde maneno kwa kutumia silabi zenye herufi:

1. ny 2. ng' 3. gh

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya.

1. Lala 2. Soma 3. Enda

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha | 28 na 29 | **Familia 1**

**Kipindi 28**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ny** **gh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**nyi** **nyo** **nyu** **gho**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | |
|---|---|---|
| nya nya | ku fa nya | nye u pe |
| **nyanya** | **kufanya** | **nyeupe** |

**Kipindi 29**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NY** **ny**

★ Soma sehemu ya neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ku kanya | a li kunywa | wa nyama | hu nyolewa |
| **kukanya** | **alikunywa** | **wanyama** | **hunyolewa** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya maneno yanayoashiria vitendo**

Jaza mapengo ukitumia neno moja kati ya uliyopewa.

1. Babu alitu________ nyumbani kwetu. (soma, tembelea)
2. Mwalimu alitu________ Kiswahili. (ruka, fundisha)
3. Ami ana________ shambani. (lima, osha)
4. Halati ata__________nywele. (fagia, chana)
5. Binamu ali _______ kucha. (panda, kata)



Kipindi cha | 28 na 29 | **Familia 1**

**Kusoma hadithi**



**Likizo mashambani**

Likizo iliyopita mimi na dada yangu tulienda mashambani. Nyanya yangu alifurahi kutuona. Tulimsaidia kufanya kazi shambani. Tulihakikisha ng'ombe wake wameshiba. Babu alifurahishwa na kazi zetu. Baada ya kazi tulioga na kuchana nywele zetu. Nyanya alihakikisha tulipata lishe bora. Wakati wa kurudi nyumbani ulifika. Binamu walitoa mahindi ndani ya ghala. Walitupatia tukampelekea mama yetu. Tulipata mafunzo mengi mashambani.



## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NY, ny

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 28.**

## Kusoma maneno marefu

Andika neno 'alikunywa' ubaoni.

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'a li kunywa' kisha unganisha sehemu hizo na usome neno 'alikunywa' upesi.

**U:** Endelea na maneno; kukanya, wanyama.

Eleza mwanafunzi asome kwenye **ukurasa wa 28.**

## Msamiati

Mkubushe mwanafunzi maana ya msamiati **nyanya, babu, binamu.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya maneno yanayoashiria vitendo**

**T:** Elezea kuhusu vitenzi. Maneno ya vitendo ni yale ambayo yanaonyesha kutendeka kwa jambo fulani. Kwa mfano, imba, cheka, soma. Mwaongoze mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mpe mwanafunzi nafasi ya kufanya zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 28.**

**Majibu**

1. tembelea
2. fundisha
3. lima
4. chana
5. kata

## Kazi ya ziada

Jibu maswali haya

1. Dada wa baba yako anaitwa nani? (shangazi)
2. Mzazi wa kike wa baba anaitwa nani? (nyanya)
3. Mzazi wa kiume wa baba anaitwa nani? (babu)
4. Watoto wa shangazi wanaitwa nani? (binamu)

Tarehe: ________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 30: Familia 1

Kipindi cha 30 **Familia 1**

**Kipindi 30**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

GH gh NY ny

▦ Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa Mfano: gha la – ghala**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ma | ka | gha | na | ri |
| bi | nya | bu | la | mu |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Soma sentensi hizi.

1. Mama **anasimama** mlangoni.
2. Binamu **anakula** vibaya.
3. Mtoto **alimsalimia** babu kwa heshima.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Familia ya Pendo**



**Kuandika**

Taja watu watatu wa familia unaowajua.

Mali ya Serikali ya Kenya

30

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** GH, gh, NY, ny

Mwanafunzi ataje jina la herufi na sauti kwenye **ukurasa wa 30.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi.

**T:** Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'ghala'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza maneno mapya: **nyanya, babu, mjomba.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi. Mwanafunzi asikilize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

**Familia ya Pendo**

Siku moja Pendo alitumwa kwa nyanya na babu yake. Alifurahi kwani alipenda kuitembelea jamaa. Alioga na kuvalia nguo safi. Akitabasamu alimwambia mama yake, "Niko tayari mama. Je, kuna zawadi ya kumpelekea nyanya?" Mama akamjibu, "Naam", na kumpa mzigo. Kwa haraka Pendo alijitwika mzigo na kuanza safari.

Nyanya na babu waliishi ng'ambo ya Mto Tana. Kwa bahati mbaya Pendo alipofika kando ya mto aliteleza. Mzigo ulianguka mtoni. Pendo alisimama na kulia kwa sauti, "Uuuuiiiii! Uuuuiiii!" Huku akitetemeka kwa uwoga. Mjomba wake aliyeishi karibu na Mto Tana alimsikia akilia akaenda kumsaidia, "Usilie, nitatumia kijiti hiki kirefu kuuvuta mzigo wako." Mjomba akasema. Mjomba alisaidiana na Pendo kuuvuta mzigo hadi ukingoni mwa mto. Pendo alifurahi. Alimshukuru mjomba wake.

## Maswali

**N:** Ni nini kilichomfurahisha Pendo? *(Kuwatembelea babu na nyanya)*

**T:** Ni nini kilifanyika alipofika kando ya mto? *(Pendo aliteleza)*

**U:** Je, kuna hatari gani kwa watoto kuingia ndani ya mto? *(Kubali majibu sahihi kama vile kuzama)*

## Kuandika

**N:** Andika jina la mtu mmoja wa familia.

**T:** Waongoze wanafunzi waandike jina la mtu moja wa familia.

**U:** Mwanafunzi ataje na aandike majina matatu ya watu wa familia.

## Sarufi

**Matumizi ya maneno yanayoashiria vitendo**

**T:** Elezea kuhusu vitenzi. Maneno ya vitendo ni yale ambayo yanaonyesha kutendeka kwa jambo fulani. Kwa mfano, simama, kula, oga n.k.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 30.** Mwanafunzi asome sentensi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya.

1. Ruka
2. Lima
3. Cheza
4. Keti

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

# Kipindi cha 31: Familia 2

Kipindi cha | 31 na 32 | **Familia 2**

**Kipindi 31**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ch gh dh f v

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

gha dhe ghu cha

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| gha li | gha sia | gha ra ma | gha la |
|---|---|---|---|
| **ghali** | **ghasia** | **gharama** | **ghala** |

**Kipindi 32**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

Ch ch

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li ghadhabika | hu gharimu | a li fua | ali ghairi |
|---|---|---|---|
| **alighadhabika** | **hugharimu** | **alifua** | **alighairi** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Soma sentensi zifuatazo.

1. Shemeji **anapenda** watoto.
2. Okitoi **alimpelekea** baba yake picha.
3. Nyanya **hupika** chai.
4. Mimi **humtembelea** binamu yangu.
5. Kaka yangu **anaendesha** baiskeli.
6. Yaya **alifua** nguo zote.

31 Hakiuzwi

Kipindi cha | 31 na 32 | **Familia 2**

**Kusoma hadithi**



**Okitoi**

Okitoi anaishi katika kijiji cha Ghamba. Yeye humtembelea shemeji yake Amina. Amina ameolewa na ndugu yake Okitoi.

Okitoi na ndugu yake walipelekwa na mjomba wao kwenye mbuga ya wanyama. Hiyo mbuga iko ng'ambo ya Ziwa Viktoria. Mara Okitoi alimkumbuka baba yake na kusema, "Baba angefurahi sana kuwaona wanyama hawa."

Mjomba alimwambia, "Nitakupa picha za wanyama umpelekee baba yako." Okitoi alimshukuru mjomba.

Mali ya Serikali ya Kenya 32

## Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ch/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** /ch/, chimba, soma

**U:** Endelea na maneno; choma, sima, cheka.

Endelea na sauti: /gh/: ghali, gari, ghalika, basi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** gh, ch, dh

Mwanafunzi asome jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 31.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /gh/ / a/ silabi ni gha

**U:** Endelea na silabi dhe, ghu, cha.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 31.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** chi mba – chimba

**U:** Endelea na maneno; Ghamba, ghasia, gharama.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 31.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno: **shemeji, ndugu, mjomba.** Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 32.**

## Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Okitoi anaishi wapi? *(Ghamba)*

**T:** Mbuga ya wanyama ilikuwa wapi? *(Ng'ambo ya ziwa viktoria)*

**U:** Unafikiri baba ya Okitoi alihisi vipi alipopelekewa picha? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Zoezi

Tamkia mwenzako sauti za herufi zifuatazo:

1. ny 2. ng' 3. gh 4. ng

## Kazi ya ziada

Chora watu wa familia yako na uandike majina yao.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 32: Familia 2

Kipindi cha 31 na 32 **Familia 2**

**Kipindi 31**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ch** **gh** **dh** **f** **v**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**gha** **dhe** **ghu** **cha**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| gha li | gha sia | gha ra ma | gha la |
| **ghali** | **ghasia** | **gharama** | **ghala** |

**Kipindi 32**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**Ch** **ch**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a li ghadhabika | hu gharimu | a li fua | ali ghairi |
| **alighadhabika** | **hugharimu** | **alifua** | **alighairi** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Soma sentensi zifuatazo.

1. Shemeji **anapenda** watoto.
2. Okitoi **alimpelekea** baba yake picha.
3. Nyanya **hupika** chai.
4. Mimi **humtembelea** binamu yangu.
5. Kaka yangu **anaendesha** baiskeli.
6. Yaya **alifua** nguo zote.

31

Hakiuzwi

Kipindi cha 31 na 32 **Familia 2**

**Kusoma hadithi**



**Okitoi**

Okitoi anaishi katika kijiji cha Ghamba. Yeye humtembelea shemeji yake Amina. Amina ameolewa na ndugu yake Okitoi.

Okitoi na ndugu yake walipelekwa na mjomba wao kwenye mbuga ya wanyama. Hiyo mbuga iko ng'ambo ya Ziwa Viktoria. Mara Okitoi alimkumbuka baba yake na kusema, "Baba angefurahi sana kuwaona wanyama hawa."

Mjomba alimwambia, "Nitakupa picha za wanyama umpelekee baba yako." Okitoi alimshukuru mjomba.

Mali ya Serikali ya Kenya

32

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

N/T/U: ch

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na kutamka sauti zake kwenye **ukurasa wa 31.**

## ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno 'alighadhabika' ubaoni.

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno alighadhabika kwa upesi.

a li ghadhabika - alighadhabika

**U:** Endelea na maneno; hugharimu, alifua.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 31.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **shemeji, ndugu, mjomba.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya vitenzi**

**N:** Eleza maana ya vitenzi. Vitenzi ni maneno yanayoonyesha kutendeka kwa jambo fulani, kama vile pika, imba, kimbia.

Maneno haya huonyesha kitendo.

**T:** Mwongoze mwanafunzi kusoma sentensi zinazoonyesha vitenzi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi lililo kwenye **ukurasa wa 31.**

Mwanafunzi asome sentensi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi amwambie mlezi wake amfunze wimbo au shairi kuhusu familia.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 33 na 34 **Familia 2**

**Kipindi 33**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng'** **ny**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ng'i** **ng'o** **ng'u** **nyu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng'a ra | nu ng'u ni ka | ng'a mu a | ng'o a |
| **ng'ara** | **nung'unika** | **ng'amua** | **ng'oa** |

**Kipindi 34**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG'** **ng'**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| wa li nung'unika | hu ng'ang'ana | a li ng'arisha |
| **walinung'unika** | **hung'ang'ana** | **aling'arisha** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Jaza mapengo kwa kutumia kitenzi.

1. Wazazi ___________ watoto. (hulea, shangazi)
2. Watoto wanapenda _________ (nyumba, kucheza)
3. Nyumbani sisi sote ________ kufanya kazi. (husaidiana, kaka)
4. Baba yangu __________ kazi nzuri. (hununua, hufanya)
5. Dada yangu __________ mimea. (alipalilia, aliosha)

33 Hakiuzwi

Kipindi cha 33 na 34 **Familia 2**

**Kusoma hadithi**



**Jamaa yangu**

Nyakati zimefika, wimbo nauandika,
Wa baba na mama, wazazi walionilea,
Majina ya jamaa, wote nitawaelezea,
Asante Mungu, baraka kuniletea.

Kaka, dada umenipa, ni ndugu zangu,
Marafiki umenipa, tucheze bila ghasia,
Binamu pia watoto, wa mjomba na shangazi,
Asante Mungu, baraka kuniletea.

Amu ninayempenda, kaka yake baba.
Halati mema hutenda, ni dada yake mama.
Msaada hutuma, bila kunung'unika
Asante Mungu, baraka kuniletea.

Mali ya Serikali ya Kenya 34

## Utambuzi wa sauti

Tamka sauti. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T:** /ng'/ ng'ara, nung'unika, ng'amua

**U:** Endelea na sauti /ny/: nyanya, ngara, nyoa, ngamia

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng', ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti katika kitabu chake kwenye **ukurasa wa 33.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /ng'/ /a/ silabi ni ng'a

**U:** Endelea na silabi ng'i, ng'o, ng'u, nyu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 33.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** ng'o a – ng'oa

**U:** Endelea na maneno; ng'ara, ng'amua.

Mwanafunzi asome maneno yaliyo kwenye **ukurasa wa 33.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **amu, halati, shangazi.** Mwanafunzi asome maneno kwenye hadithi.

## Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha shairi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Kusoma shairi

**N/T/U:** Soma shairi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Baba na mama pia huitwaje? *(Wazazi)*

**T:** Binamu ni nani? *(Watoto wa mjomba)*

**U:** Unafikiri ni mambo gani mema ambayo halati hutenda? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Zoezi

Andika maneno haya ubaoni. Mwanafunzi asome kwa kutumia silabi

1. Nyanya 2. Gharama 3. Ng'ombe 4. Ngoma

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maana ya maneno haya:

1. Halati 2. Mjukuu 3. Shemeji 4. Nyanya

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

Kipindi cha | 33 na 34 | **Familia 2**

**Kipindi 33**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng'** **ny**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ng'i** **ng'o** **ng'u** **nyu**

- Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng'a ra | nu ng'u ni ka | ng'a mu a | ng'o a |
| **ng'ara** | **nung'unika** | **ng'amua** | **ng'oa** |

**Kipindi 34**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG'** **ng'**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| wa li nung'unika | hu ng'ang'ana | a li ng'arisha |
| **walinung'unika** | **hung'ang'ana** | **aling'arisha** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Jaza mapengo kwa kutumia kitenzi.

1. Wazazi __________ watoto. (hulea, shangazi)
2. Watoto wanapenda _________ (nyumba, kucheza)
3. Nyumbani sisi sote ________ kufanya kazi. (husaidiana, kaka)
4. Baba yangu __________ kazi nzuri. (hununua, hufanya)
5. Dada yangu __________ mimea. (alipalilia, aliosha)

33 Hak uzwi

Kipindi cha | 33 na 34 | **Familia 2**

**Kusoma hadithi**



**Jamaa yangu**

Nyakati zimefika, wimbo nauandika,
Wa baba na mama, wazazi walionilea,
Majina ya jamaa, wote nitawaelezea,
Asante Mungu, baraka kuniletea.

Kaka, dada umenipa, ni ndugu zangu,
Marafiki umenipa, tucheze bila ghasia,
Binamu pia watoto, wa mjomba na shangazi,
Asante Mungu, baraka kuniletea.

Amu ninayempenda, kaka yake baba.
Halati mema hutenda, ni dada yake mama.
Msaada hutuma, bila kunung'unika
Asante Mungu, baraka kuniletea.

Mali ya Serikali ya Kenya 34

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NG', ng'

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 33.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** wa li nung'unika - walinung'unika

**U:** Endelea na maneno; hung'ang'ana, aling'arisha.

Mwanafunzi asome maneno yaliyo kwenye **ukurasa wa 33.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **shangazi, amu, halati.**

## Kusoma shairi

**U:** Somea mwenzako shairi.

## Sarufi

**Matumizi ya vitenzi**

**N:** Eleza maana ya vitenzi. Vitenzi ni maneno yanayoonyesha kutendeka kwa jambo fulani, kama vile cheka, cheza, lala.

Maneno haya huonyesha kitendo.

**T:** Mwongoze mwanafunzi kusoma sentensi zinazoonyesha vitenzi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 33.**

**Majibu:**

1. lea
2. kucheza
3. husaidiana

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya:

1. Shangazi
2. Amu
3. Halati

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 35: Familia 2

Kipindi cha 35 **Familia 2**

**Kipindi 35**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng'　　　ch

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ndu gu – ndugu**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| a | ha | ndu | mbe | ti |
| che | gu | la | ng'o | mu |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Andika sentensi zifuatazo.

1. Ni vizuri **kufuata** tamaduni nzuri.
2. Wanafunzi **husimama** mwalimu **anapoingia** darasani.
3. Shangazi wetu **huishi** Nairobi.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Kemboi na Mamba**



**Kuandika**

Andika sentensi mbili fupi kuhusu hadithi uliyoisoma ya **Okitoi**.

35　Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng', ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 35.**

### Jedwali

Chora jedwali la silabi.

**T:** Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'ndugu'.

**U:** Wanafunzi waunde maneno.

### Hadithi ya mwalimu

Funza maneno mapya: **nyanya, mjukuu.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi. Mwanafunzi asikilize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

**Kemboi na mamba**

Wakati wa likizo mimi na dada yangu tulimtembelea nyanya na babu. Kila jioni, nyanya alitusimulia hadithi kabla ya chakula. Jioni moja, nyanya alituhadithia hadithi ya mamba na Kemboi. Kemboi alikuwa mjukuu wa mzee Masumbuko. Alizoea kucheza na marafiki zake karibu na mto.

Siku moja Kemboi na rafiki yake walipokuwa wakirusha mawe mtoni, mamba alitokea ghafla. Kemboi alianguka majini chubwi! Mamba akaona amepata kitoweo. Akaogelea kwa kasi kumwelekea Kemboi. Mzee Masumbuko alitimua mbio huku akipiga nduru kwa kutaka msaada. Alimchukua Kemboi na kumrusha nje ya maji. Binamu Wasike aliyekuwa amewaleta ng'ombe mtoni alimpa Kemboi huduma ya kwanza. Mzee Masumbuko alimbeba Kemboi na kumpeleka nyumbani. Kila mtu alifurahia kumwona Kemboi akiwa salama salmini.
Tulimuahidi nyanya kuwa waangalifu na daima kuepuka wanyama hatari.

### Maswali

**T:** Kila jioni nyanya alifanya nini? *(Kusimulia hadithi)*

**U:** Taja mambo yaliyofanyika wakati mamba alipotokea. *(Kemboi alianguka majini)*

**U:** Unafikiri tunaweza kufanya mambo gani kuzuia hatari tunapovua samaki mitoni? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Kuandika

**N:** Andika sentensi kuhusu hadithi ya Kemboi na mamba.

**T:** Mwongoze mwanafunzi kuandika sentensi kuhusu hadithi ya Kemboi na mamba.

**U:** Mwanafunzi aandike sentensi mbili kuhusu hadithi ya Kemboi na mamba.

### Sarufi

**Matumizi ya vitenzi**

**N:** Eleza maana ya vitenzi. Vitenzi ni maneno yanayoonyesha kutendeka kwa jambo fulani, kama vile tembea, andika, futa.
Maneno haya huonyesha kitendo.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi lililopo kwenye **ukurasa wa 35.**
Mwanafunzi anakili sentensi.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi nne akitumia maneno yafuatayo:

1. Ruka　　2. Cheza
3. Andika　　4. Pika

Tarehe: ______________________　Muda: ________________　Idadi: ________________

# Kipindi cha 36: Usalama wangu 1

Kipindi cha 36 na 37 **Usalama wangu**

**Kipindi 36**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

sh v

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

shi sho shu vu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| hu ha ta ri sha | wa na o e nde sha | shu le ni |
|---|---|---|
| **huhatarisha** | **wanaoendesha** | **shuleni** |

**Kipindi 37**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

SH sh

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa thibitishe | ku rekebisha | tu na shiriki | tu na vuta |
|---|---|---|---|
| **wathibitishe** | **kurekebisha** | **tunashiriki** | **tunavuta** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi mkitumia vitenzi vifuatavyo pamoja na **huyo** au **hao**.

1. Cheza
2. Vunja
3. Soma
4. Keti
5. Lima
6. Osha

Mali ya Serikali ya Kenya 36

Kipindi cha 36 na 37 **Usalama wangu**

**Kusoma hadithi**



**Siku ya michezo**

Siku ya michezo tulifika shuleni mapema. Tuliitwa pamoja na kuelezwa jinsi tutakavyoshiriki katika michezo. Kwanza tulienda kuogelea katika kidimbwi cha shule. Mwalimu alisimama karibu ili tusije kuzama majini. Baadaye mwalimu aliwatuma Hamisi na Lewi darasani kuchukua mpira. Lo! Alikuta kizima-moto cha darasa kikivuja gesi. Wanafunzi hao walimwita mwalimu ili athibitishe kisa hicho. Mwalimu alienda hima na kurekebisha kifaa hicho. Hamisi alisema kuwa huyo mwalimu alikuwa mzuri.

37 Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/sh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** /sh/ shambani, anguka

**U:** Endelea na maneno; shangazi, shuka, mchanga, angukia.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** sh, v

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zilizo kwenye **ukurasa wa 36.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /sh/ /a/ silabi ni sha

**U:** Endelea na silabi; shi, sho, shu, vu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 36.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** shu hu di a – shuhudia

**U:** Endelea na maneno; shuleni, huhatarisha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 36.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kuzama majini, kikivuja gesi, kizima-moto.** Mwanafunzi asome maneno kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 37**.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Ni mchezo gani uliochezwa kwanza? *(Kuogelea)*

**T:** Ni nini kilichofanyika Hamisi alipoingia darasani? *(Alikuta kizima moto cha darasa kikivuja gesi)*

**U:** Wewe unapenda mchezo gani? *(Kubali jinbu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi afinyange maumbo ya herufi hizi:

1. sh 2. th 3. ng 4. ny

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi anakili maneno haya kisha atasomea walezi wake nyumbani.

1. Huhatarisha 2. Wanaoendesha 3. Shuleni

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 37: Usalama wangu 1

Kipindi cha 36 na 37 **Usalama wangu**

**Kipindi 36**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  sh v

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  shi sho shu vu

- Soma maneno ukitumia silabi.

  hu ha ta ri sha — **huhatarisha**
  wa na o e nde sha — **wanaoendesha**
  shu le ni — **shuleni**

**Kipindi 37**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  SH sh

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  wa thibitishe — **wathibitishe**
  ku rekebisha — **kurekebisha**
  tu na shiriki — **tunashiriki**
  tu na vuta — **tunavuta**

**Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi mkitumia vitenzi vifuatavyo pamoja na **huyo** au **hao**.

1. Cheza
2. Vunja
3. Soma
4. Keti
5. Lima
6. Osha

Mali ya Serikali ya Kenya 36

Kipindi cha 36 na 37 **Usalama wangu**

**Kusoma hadithi**



**Siku ya michezo**

Siku ya michezo tulifika shuleni mapema. Tuliitwa pamoja na kuelezwa jinsi tutakavyoshiriki katika michezo. Kwanza tulienda kuogelea katika kidimbwi cha shule. Mwalimu alisimama karibu ili tusije kuzama majini. Baadaye mwalimu aliwatuma Hamisi na Lewi darasani kuchukua mpira. Lo! Alikuta kizima-moto cha darasa kikivuja gesi. Wanafunzi hao walimwita mwalimu ili athibitishe kisa hicho. Mwalimu alienda hima na kurekebisha kifaa hicho. Hamisi alisema kuwa huyo mwalimu alikuwa mzuri.

37 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** SH, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 36.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** wa na oendeshwa - wanaoendeshwa

**U:** Endelea na maneno; wathibitishe, kurekebisha, tunashiriki.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 36.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **kuzama majini, kizima-moto, kivuja gesi.**

## Hadithi ya mwanafunzi

Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya 'huyo' na 'hao'**

N: Fafanua maana ya 'huyo' na 'hao'.

'Huyo' hutumika kuonyesha/kuashiria mtu au kiumbe chenye uhai kilicho mbali kidogo katika umoja.

**Kwa mfano:** Mtoto **huyo** ni wangu.
Kondoo **huyo** ni mweusi.

'Hao' hutumiwa kama wingi wa 'huyo'. Hutumiwa kuashiria wingi wa majina ya watu au viumbe wenye uhai.

**Kwa mfano:** Watoto **hao** wanaogelea.
Kondoo **hao** ni wetu.

**T:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 36.**

## Kazi ya ziada

Tumia **hao** au **huyo** kujaza mapengo kwa usahihi.

1. Kijana _____________ni mwerevu. (huyo)
2. Wanafunzi__________walichelewa. (hao)
3. Mtoto______________analia. (huyo)
4. Wazima moto_________walifika. (hao)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 38: Usalama wangu 1

Kipindi cha 38 na 39 **Usalama wangu**

**Kipindi 38**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

th sh

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

the thi tho thu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| a tha ri | the ma ni ni | a thi bi ti she | the la thi ni |
|---|---|---|---|
| **athari** | **themanini** | **athibitishe** | **thelathini** |

**Kipindi 39**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

TH th

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa na o endesha | u li thibitiwa | hu sababisha |
|---|---|---|
| **wanaoendesha** | **ulithibitiwa** | **husababisha** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Soma sentensi zifuatazo.

1. Dereva **huyo** anaendesha gari vizuri.
2. Wanafunzi **hao** ni wa darasa gani?
3. Mtoto **huyo** anatumia kivukio cha barabara.
4. Walimu **hao** walitufundisha vizuri.
5. Kiranja **huyo** alikusanya vitabu.
6. Mwalimu **huyo** alitupatia zawadi.
7. Polisi **hao** waliwakamata wezi.

Mali ya Serikali ya Kenya

38

Kipindi cha 38 na 39 **Usalama wangu**

**Kusoma hadithi**




**Jamaa yangu**

Ijumaa mwalimu wetu alitufundisha kuhusu usalama. Alisema kuwa ni vizuri kutumia kivukio cha barabara. Aliongeza kuwa vidaraja husaidia kukiwa na mafuriko. Mwalimu huyo alieleza kuwa ajali husababishwa na kutofuata sheria barabarani. Kwa mfano, madereva wa magari na pikipiki wanapoendesha kwa kasi. "Watu kama hao huhatarisha maisha ya kila mtu," mwalimu alisema.

Alituhimiza tuwafundishe jamaa zetu kuhusu umuhimu wa usalama.

39

Hakluzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/th/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** thamani, athari

**U:** Endelea na maneno; themanini, athibitishe.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** th, sh. Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 38.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.
**N/T/U:** /th/ /a/ silabi ni tha
**U:** Endelea na silabi the, thi, tho, thu.
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 38.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi kwa kila neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.
**N/T/U:** thu lu thi – theluthi
**U:** Endelea na maneno; athari, themanini, athibitishe.
Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 38.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **vidaraja, kivukio cha barabara, pikipiki.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 39.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Mwalimu aliwafundisha wanafunzi kuhusu usalama siku gani? *(Ijumaa)*

**T:** Taja vitu viwili vinavyosaidia kupunguza ajali. *(Kutumia vivukio, kutumia vidaraja wakati wa mafuriko)*

**U:** Ni vitu gani vingine vinavyohatarisha maisha ya watu? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi achore:

1. alama ya kivukio cha barabara 2. pikipiki 3. mto

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi nne akitumia **huyu** na **hao**.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 39: Usalama wangu 1

Kipindi cha 38 na 39 **Usalama wangu**

**Kipindi 38**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**th** **sh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**the** **thi** **tho** **thu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a tha ri | the ma ni ni | a thi bi ti she | the la thi ni |
| **athari** | **themanini** | **athibitishe** | **thelathini** |

**Kipindi 39**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**TH** **th**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| wa na o endesha | u li thibitiwa | hu sababisha |
| **wanaoendesha** | **ulithibitiwa** | **husababisha** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Soma sentensi zifuatazo.

1. Dereva **huyo** anaendesha gari vizuri.
2. Wanafunzi **hao** ni wa darasa gani?
3. Mtoto **huyo** anatumia kivukio cha barabara.
4. Walimu **hao** walitufundisha vizuri.
5. Kiranja **huyo** alikusanya vitabu.
6. Mwalimu **huyo** alitupatia zawadi.
7. Polisi **hao** waliwakamata wezi.

Mali ya Serikali ya Kenya

38

Kipindi cha 38 na 39 **Usalama wangu**

**Kusoma hadithi**




**Jamaa yangu**

Ijumaa mwalimu wetu alitufundisha kuhusu usalama. Alisema kuwa ni vizuri kutumia kivukio cha barabara. Aliongeza kuwa vidaraja husaidia kukiwa na mafuriko. Mwalimu huyo alieleza kuwa ajali husababishwa na kutofuata sheria barabarani. Kwa mfano, madereva wa magari na pikipiki wanapoendesha kwa kasi. "Watu kama hao huhatarisha maisha ya kila mtu," mwalimu alisema.

Alituhimiza tuwafundishe jamaa zetu kuhusu umuhimu wa usalama.

39 Hakiuzwi

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** TH, th

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 38.**

## ★ Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo na usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li thubutu – alithubutu

**U:** Endelea na maneno; wanaoendesha, ulithibitiwa.

Mwanafunzi asome maneno yaliyo kwenye **ukurasa wa 38.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **kivuko cha barabara, vidaraja, pikipiki.**

## Hadithi ya mwanafunzi

Somea mwenzako hadithi.

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya 'huyo' na 'hao'**

**N:** Rejelea maelezo kuhusu matumizi ya 'huyo' na 'hao'. 'Huyo' hutumika kuonyesha/kuashiria mtu au kiumbe mwenye uhai aliye mbali kidogo katika hali ya umoja. Kwa mfano, 'Mbuzi huyo ni wangu'. 'Hao' hutumiwa kama wingi wa 'huyo'. Hutumiwa kuashiria wingi wa majina ya watu au viumbe wenye uhai. Kwa mfano, 'Watoto hao wanacheza'.

Mwongoze mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 38.**

Mwanafunzi asome sentensi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya:

1. Ajali
2. Michezoni
3. Kivukio cha barabara

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 40: Usalama wangu 1

Kipindi cha 40 **Usalama wangu**

Kipindi 40

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

SH sh TH th

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: sha mba – shamba**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| sha | a | mba | ri | li |
| i | tha | nga | na | ma |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Igiza vitendo vifuatavyo ukitumia huyo au hao.

1. Endesha 2. Vuka 3. Fundisha

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Mkutano mtaani**



**Kuandika**

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. Vita 2. Ajali 3. Vidaraja 4. Kivukio cha barabara

Mali ya Serikali ya Kenya 40

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** SH, sh, TH, th

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 40.**

## ★ Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'shamba'. Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **kivukio cha barabara, moto, vidaraja.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi. Mwanafunzi asikilize huku wakitazama picha. Hakiki utabiri.

**Mkutano mtaani**

Hali ya wasiwasi ilitanda katika mtaa wa Kamenya. Hii ni kwa sababu ya ripoti za ajali zilizokuwa zikitokea mara kwa mara. Hivyo basi, chifu aliamua kuita mkutano Jumamosi moja ili kupata suluhisho. Wanakijiji wote waliitikia mwito wa chifu huyo aliyeheshimiwa na wengi. Wote walihudhuria, wakubwa kwa wadogo.

Chifu alianza kwa kuwakaribisha na kuwapongeza kwa kuiitikia mwito huo. Alieleza kuwa ajali nyingi zilisababishwa na hali mbalimbali. Kwa mfano moto, kutozingatia alama za barabara na mafuriko hasa wakati wa masika. Kila mwanakijiji alithibitisha kuwa aliyoyasema chifu yalikuwa ya kweli kabisa. Chifu aliwahimiza wanakijiji hao watoe mapendekezo ya kutatua hali hiyo. Kijana mmoja alipendekeza kuwa ni muhimu kwa kila familia kuhakikisha kuwa viberiti vimewekwa mbali na watoto. Vilevile, vifaa vingine kama nyaya za umeme ziangaliwe kila mara. Mama mwingine naye alipendekeza kuwa kila barabara iwe na kivukio cha barabara. Aliwahimiza wanakijiji kushirikiana na chifu na kuhakikisha kuwa sehemu zote zilizoathiriwa na mafuriko zimejengewa vidaraja. Alieleza kuwa hivi vingemaliza ajali zinazotokea tunapovuka barabara na wakati wa mafuriko.

Wanakijiji walifurahi na kuchagua kikundi cha watu thelathini ambao wangemsaidia chifu kutekeleza jukumu hilo. Hatua hizo zilileta mafanikio baada ya siku chache na kila mmoja alifurahia matunda ya ushirikiano huo.

## ? Maswali

**T:** Ni nani aliitisha mkutano wa wanakijiji? *(Chifu)*

**U:** Madereva wa magari na wa pikipiki husababisha ajali kwa njia gani? *(Kutojali alama za barabarani, kuendesha kwa haraka.)*

**U:** Je, unafikiri ajali zinaweza kupunguzwa vipi? *(Kufuata sheria za barabarani.)*

## Kuandika

**N:** Tunga sentensi ukitumia kifungu 'kivukio cha barabara'.

**T:** Mwongoze mwanafunzi kuandika sentensi akitumia kifungu 'kivukio cha barabara'.

**U:** Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno vita, ajali, vidaraja.

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya 'huyo' na 'hao'**

N: Rejelea matumizi ya 'huyo' na 'hao'. 'Huyo' hutumika kuonyesha/kuashiria mtu au kiumbe mwenye uhai aliye mbali kidogo katika hali ya umoja. Kwa mfano, 'Sungura huyo alipotea'. 'Hao' hutumiwa kama wingi wa 'huyo'. Hutumiwa kuashiria wingi wa majina ya watu au viumbe wenye uhai. Kwa mfano, 'Paka hao wamelala'.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 40.** Mwanafunzi aigize vitendo huku akitumia **huyo au hao.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore maumbo yanayowasilisha.

1. Alama za barabara 2. Vidaraja 3. Moto

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 41 na 42 **Hali ya anga 1**

**Kipindi 41**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**gh** **g** **h** **j**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ghu** **ji** **hu** **ga**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| gha la | gha fla | gha ra ma | gho ro fa |
|---|---|---|---|
| **ghala** | **ghafla** | **gharama** | **ghorofa** |

**Kipindi 42**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**GH** **G** **H** **J**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li gawa | a li ji sifu | hu makinika | wa li kata |
|---|---|---|---|
| **aligawa** | **alijisifu** | **humakinika** | **walikata** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili**

Mkiwa wawili, tungeni sentensi tatu mkitumia **wewe** na **nyinyi** katika wakati uliopita.

**Kwa mfano:** **Wewe** ulipanda mti.
**Nyinyi** mlipanda miti.
**Wewe** ulikata nyasi.
**Nyinyi** mlikata nyasi.
**Wewe** ulinyeshewa.
**Nyinyi** mlinyeshewa.

41 Hakiuzwi

Kipindi cha 41 na 42 **Hali ya anga 1**

**Kusoma hadithi**



**Paa la shule lang'olewa**

Asubuhi na mapema ndege waliimba mtini. Hewa ilikuwa safi. Walifurahia wakati jua lilipochomoza. Pasaka aliamka na kukimbia shuleni. Alipofika shuleni alipata paa la darasa lao limeng'olewa na upepo. Hii ilikuwa hasara ya gharama kubwa.

Wanafunzi walihamia darasa lingine. Mvua kubwa ilinyesha sana siku hiyo. Baadaye wote walitoka nje kwenda kupanda miti. Walifurahia sana kurembesha shule yao. Mwalimu aliwapongeza kisha akawapa maji wanawe mikono. Baadaye walirudi nyumbani.

"Mlinyeshewa sana?" Mama alituuliza.

"Wewe ulinyeshewa sana," Pasaka alimwambia dadake.

Mama alitwambia pole.

Mali ya Serikali ya Kenya 42

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/gh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** ghala, dhati

**U:** Endelea na maneno; ghorofa, chuma, gharama.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** gh, g, h, j

Mwanafunzi asome jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 41.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /gh/ / e/ silabi ni ghe

**U:** Endelea na silabi gha, ga, hu, ji, ghu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 41.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** gha li – ghali

**U:** Endelea na maneno; ghala, ghafla, gharama.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 41.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno **hewa, jua, upepo.**

Tumia nyenzo zinazoashiria hali za anga unapofunza maana ya maneno.

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 42.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kwa nini ndege walifurahi? *(Kwa sababu jua lilichomoza.)*

**T:** Pasaka alifanya nini? (Alikimbia shuleni.)

**U:** Taja madhara yanayoletwa na mvua nyingi na upepo. *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi achore picha kuonyesha hali hizi za anga.

1. Wakati wa upepo  2. Wakati wa jua  3. Mvua

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi ambatanishe maneno na michoro aliyochora darasani. 1. Jua  2. Upepo  3. Mvua

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

Kipindi cha 41 na 42 **Hali ya anga 1**

**Kipindi 41**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.
  gh g h j
- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.
  ghu ji hu ga
- ★ Soma maneno ukitumia silabi.

| gha la | gha fla | gha ra ma | gho ro fa |
|---|---|---|---|
| **ghala** | **ghafla** | **gharama** | **ghorofa** |

**Kipindi 42**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.
  GH G H J
- Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li gawa | a li ji sifu | hu makinika | wa li kata |
|---|---|---|---|
| **aligawa** | **alijisifu** | **humakinika** | **walikata** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili**

Mkiwa wawili, tungeni sentensi tatu mkitumia **wewe** na **nyinyi** katika wakati uliopita.

**Kwa mfano:** **Wewe** ulipanda mti.
**Nyinyi** mlipanda miti.
**Wewe** ulikata nyasi.
**Nyinyi** mlikata nyasi.
**Wewe** ulinyeshewa.
**Nyinyi** mlinyeshewa.

41 Hakiuzwi

Kipindi cha 41 na 42 **Hali ya anga 1**

**Kusoma hadithi**



**Paa la shule lang'olewa**

Asubuhi na mapema ndege waliimba mtini. Hewa ilikuwa safi. Walifurahia wakati jua lilipochomoza. Pasaka aliamka na kukimbia shuleni. Alipofika shuleni alipata paa la darasa lao limeng'olewa na upepo. Hii ilikuwa hasara ya gharama kubwa.

Wanafunzi walihamia darasa lingine. Mvua kubwa ilinyesha sana siku hiyo. Baadaye wote walitoka nje kwenda kupanda miti. Walifurahia sana kurembesha shule yao. Mwalimu aliwapongeza kisha akawapa maji wanawe mikono. Baadaye walirudi nyumbani.

"Mlinyeshewa sana?" Mama alituuliza.

"Wewe ulinyeshewa sana," Pasaka alimwambia dadake.

Mama alitwambia pole.

Mali ya Serikali ya Kenya 42

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** GH, G, H, J

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 41.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li gawa – aligawa.

**U:** Endelea na maneno; alijisifu, walikata.

Mwanafunzi asome maneno yaliyopo **ukurasa wa 41.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **hewa, jua, upepo.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Fafanua maana ya nafsi ya pili na wakati uliopita. 'Wewe' hutumiwa katika nafsi ya pili hali ya umoja. Ni hali ya kuonyesha mtu wa pili baada ya wa kwanza, 'mimi'. Kwa mfano: Wewe ulikula chakula. Wewe ulisoma kitabu. 'U' hutumiwa pamoja na wewe kuonyesha umoja. 'li' hutumiwa kuonyesha wakati uliopita.

'Wewe' inapotumiwa na wakati uliopita huwa inaonyesha kuwa jambo lilitendeka wakati uliopita.

'Nyinyi' na 'm' hutumiwa kama hali ya wingi wa nafsi ya pili. 'Li' hutumiwa pamoja na 'nyinyi' na 'm' kuonyesha wingi katika wakati uliopita. Kwa mfano: Nyinyi mlikula chakula. Nyinyi mlisoma vitabu. Waongoze wanafunzi kusoma sentensi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi lililo kwenye **ukurasa wa 41.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi zifuatazo akitumia wakati uliopita.

1. Mwalimu anaota jua.
2. Mvua itanyesha kesho.
3. Miti imepandwa shuleni.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 43 na 44 **Hali ya anga 1**

**Kipindi 43**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

l j

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

la le li lo

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| wa li we ka | u ku lima | la la mi ka | ki li ku wa |
| **waliweka** | **ukulima** | **lalamika** | **kilikuwa** |

**Kipindi 44**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

L l

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a ta lala | hu legea | a li jitahidi | wa li jumuika |
| **atalala** | **hulegea** | **alijitahidi** | **walijumuika** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili**

Igiza vitendo katika sentensi hizi ukiwa na mwenzako.

1. Nyinyi mnaruka kamba.
2. Wewe unacheka.
3. Nyinyi mnasoma kitabu.
4. Wewe unasugua meno.
5. Nyinyi mnachana nywele.
6. Wewe unakimbia.
7. Nyinyi mnaketi.

43 Hakiuzwi

Kipindi cha 43 na 44 **Hali ya anga 1**

**Kusoma hadithi**



**Mvua yang'oa miti**

Kijiji cha Patapata kilikuwa maarufu kwa ukulima. Wanakijiji walivuna na kuweka mavuno maghalani. Wanakijiji wengine walikata miti ovyoovyo. "Nyinyi mtajiletea shida," chifu wao Kondiri alionya. Hawakuzingatia wasia wa chifu. Siku moja, mawingu meusi yalitanda. Mvua kubwa ilinyesha. Miti iling'oka na kuharibu udongo. Baridi ilikuwa nyingi. Mwaka huo watu hawakupata mavuno kama kawaida. Wazee waliweka amri ya kutokata miti. Waliandika onyo kila pahali, 'Msikate miti bila ruhusa.' Zaidi ya kutokata mti, ni lazima wangepanda miti miwili kila mmoja. Hii sheria imedumu hadi leo.

Mali ya Serikali ya Kenya 44

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/l/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** lima, ukuta

**U:** Endelea na maneno; lala, lipa, mkono, ulimi, leta.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** l, j

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 43.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /j / /a/ silabi ni ja; /l/ /a/ silabi ni la.

**U:** Endelea na silabi le, li, lo.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 43.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** ka la mu – kalamu

**U:** Endelea na maneno; waliweka, ukulima, lalamika, kilikuwa.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 43.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **mvua, mawingu, baridi.** Mwanafunzi asome maneno kwenye hadithi.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri

### Maswali

**N:** Kwa nini kijiji cha Patapata kilikuwa maarufu? *(Ukulima)*

**T:** Mavuno yaliwekwa wapi? *(Ghalani)*

**U:** Je, unafikiri madhara ya kukata miti ni gani? *(Ukosefu wa mvua)*

### Zoezi

Mwanafunzi atumie maneno yafuatayo kutunga sentensi.

a) Upepo b) Mvua c) Jua

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi tatu kwa umoja akitumia **wewe.**

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 44: Hali ya anga 1

Kipindi cha 43 na 44 **Hali ya anga 1**

**Kipindi 43**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

l j

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

la le li lo

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| wa li we ka | u ku lima | la la mi ka | ki li ku wa |
|---|---|---|---|
| **waliweka** | **ukulima** | **lalamika** | **kilikuwa** |

**Kipindi 44**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

L l

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a ta lala | hu legea | a li jitahidi | wa li jumuika |
|---|---|---|---|
| **atalala** | **hulegea** | **alijitahidi** | **walijumuika** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili**

Igiza vitendo katika sentensi hizi ukiwa na mwenzako.

1. Nyinyi mnaruka kamba.
2. Wewe unacheka.
3. Nyinyi mnasoma kitabu.
4. Wewe unasugua meno.
5. Nyinyi mnachana nywele.
6. Wewe unakimbia.
7. Nyinyi mnaketi.

43 Hakiuzwi

Kipindi cha 43 na 44 **Hali ya anga 1**

**Kusoma hadithi**



**Mvua yang'oa miti**

Kijiji cha Patapata kilikuwa maarufu kwa ukulima. Wanakijiji walivuna na kuweka mavuno maghalani. Wanakijiji wengine walikata miti ovyoovyo. "Nyinyi mtajiletea shida," chifu wao Kondiri alionya. Hawakuzingatia wasia wa chifu. Siku moja, mawingu meusi yalitanda. Mvua kubwa ilinyesha. Miti iling'oka na kuharibu udongo. Baridi ilikuwa nyingi. Mwaka huo watu hawakupata mavuno kama kawaida. Wazee waliweka amri ya kutokata miti. Waliandika onyo kila pahali, 'Msikate miti bila ruhusa.' Zaidi ya kutokata mti, ni lazima wangepanda miti miwili kila mmoja. Hii sheria imedumu hadi leo.

Mali ya Serikali ya Kenya 44

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** L, l

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 41.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo na usome neno kwa upesi.

**N/T/U: a ta lala – atalala**

**U:** Endelea na maneno; hulegea, alijitahidi.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 43.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **mawingu, mvua, baridi.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya nafsi ya pili**

**N:** Rejelea ufafanuzi wa maana ya nafsi ya pili. 'Wewe' hutumiwa katika nafsi ya pili. Ni hali ya kuonyesha mtu wa pili baada ya wa kwanza, 'mimi'. Kwa mfano: Wewe unapika chakula. 'U' hutumiwa pamoja na wewe kuonyesha umoja.

'Nyinyi' na 'm' hutumiwa kama hali ya wingi wa nafsi ya pili. Kwa mfano: Nyinyi mnapika chakula.

**T:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi lililopo kwenye **ukurasa wa 43.**

Mmoja wao asome sentensi huku wengine wakiigiza vitendo. Hakikisha wametofautisha wewe na nyinyi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi hizi kwa hati nadhifu.

1. Upepo ulivuma sana.
2. Mvua ilinyesha.
3. Mawingu ni meusi.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 45: Hali ya anga 1

Kipindi cha 45 **Hali ya anga1**

**Kipindi 45**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

gh l

Jedwali la silabi

Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: he ma – hema**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| m | ra | gha | ma | a |
| ju | pe | vu | he | la |

♦ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Soma na uandike sentensi hizi.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Wewe uliandika. | Nyinyi mliandika. |
| 2. | Wewe ulinyeshewa. | Nyinyi mlinyeshewa. |
| 3. | Wewe ulipanda mti. | Nyinyi mlipanda miti. |

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Mvua yanyesha**



**Kuandika**

Andika sentensi tatu kutokana na hadithi ya mvua yang'oa miti.

45 Hakiuzwi

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** gh, GH, l, L

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 45.**

## ★ Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'hema'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza maneno mapya: **upepo**, **jua**, **mawingu**, **mvua**. Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi wanafunzi wasikilize huku wakitazama picha. Hakiki utabiri.

**Mvua yanyesha**

Jumatatu asubuhi ndege waliimba kwa furaha huku upepo ukivuma. Kijana Monari aliyelala na kaka yake Nduti aligeuka kitandani na kusema, "Aaah! Kumekucha." Vijana hao ambao walipenda masomo waliamka haraka na kujitayarisha. "Wewe shati lako linang'ara kama theluji!" Nduti alimwambia Monari. "Aaah! Lako pia," Monari alisema.

Jua lilipochomoza, vijana hao walikimbia hadi shuleni. Monari alijiunga na wanafunzi wengine na kusafisha darasa lao. Nduti naye alipangusa kiti na meza ya mwalimu na kisha akapanguza ubao. Baadaye, kiranja alihimiza kila mwanafunzi kuketi na kutulia. Mara walisikia sauti mlangoni, ngo! ngo! ngo! Kiranja alipofungua, wote walifurahi kumwona mwalimu wao.

Wakati wa mapumziko ulipofika, wanafunzi walienda kucheza uwanjani. Michezo yao ilikatika haraka mawingu mazito yalipotanda angani. Kwa ghafla, matone mazito ya mvua yalianza kuanguka. Kila mwanafunzi alikimbia kujikinga. Mvua ilipoisha, wote walienda nyumbani.

## ? Maswali

**T:** Monari na Nduti walifanya nini walipoamka? *(Kujitayarisha kwenda shuleni.)*

**U:** Taja mambo yaliyofanywa na Monari na Nduti walipofika darasani. *(Monari alijiunga na wenzake kusafisha darasa. Nduti alipanguza kiti na meza ya mwalimu.)*

**U:** Je, unafikiri Monari na Nduti walikuwa wanafunzi wa darasa gani? *(La pili.)*

## Kuandika

**N:** Andika sentensi kutokana na hadithi ya 'Mvua yang'oa miti'.

**T.** Mwongoze mwanafunzi kuandika sentensi kutokana na hadithi.

**U:** Mwanafunzi aandike sentensi tatu kuhusu hadithi ya 'Mvua yang'oa miti'.

## ♦ Sarufi

**Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

N: Rejelea kufafanua maana ya nafsi ya pili wakati uliopita. 'Wewe' hutumiwa katika nafsi ya pili hali ya umoja. Huonyesha hali ya mtu wa pili baada ya wa kwanza, 'mimi'. Kwa mfano, Wewe ulikula chakula. Wewe ulilima shambani. 'U' hutumiwa pamoja na wewe kuonyesha umoja. 'li' hutumiwa kuonyesha wakati uliopita. 'Wewe' inapotumiwa na wakati uliopita huwa inaonyesha kuwa jambo lilitendeka wakati uliopita. 'li' hutumiwa kuonyesha wakati uliopita.

'Nyinyi' na 'm' hutumiwa kama hali ya wingi wa nafsi ya pili. 'Li' hutumiwa pamoja na 'nyinyi' na 'm' kuonyesha wingi. Kwa mfano; Nyinyi mlilima mashamba. Nyinyi mliosha nguo.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi lililopo kwenye **ukurasa wa 45.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aeleze hali mbalimbali za anga kwa kutumia michoro au picha.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 46 na 47 **Lishe bora 1**

**Kipindi 46**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ch    l

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

chi    cho    chu    lo

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| che ma | che za | li si cho ke | cho mbo |
| **chema** | **cheza** | **lisichoke** | **chombo** |

**Kipindi 47**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

CH    ch    L    l

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ki na cho patia | wa ki changanya | a li chimba | hu lima |
| **kinachopatia** | **wakichanganya** | **alichimba** | **hulima** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya hiki na hivi**

Onyesha vitu mbalimbali na utunge sentensi tatu ukitumia **hiki** au **hivi**. Fanyeni zoezi hili mkiwa wawili wawili.

**Kwa mfano:**


Kitabu **hiki** ni kizuri. – Vitabu **hivi** ni vizuri.

| Umoja -hiki | Wingi -hivi |
|---|---|
| Kiti **hiki** ni kidogo. | Viti **hivi** ni vidogo. |
| Kiatu **hiki** ni cheusi. | Viatu **hivi** ni vyeusi. |
| Kioo **hiki** chavutia. | Vioo **hivi** vyavutia. |

Mali ya Serikali ya Kenya    46

Kipindi cha 46 na 47 **Lishe bora 1**

**Kusoma hadithi**




**Afya ulimwenguni**

Ilikuwa siku ya afya ulimwenguni. Daktari Walukhano aliwaita watu pamoja kijijini. Alitaka kuwaeleza umuhimu wa chumvi mwilini. Alianza, "Naomba mnisikilize kwa makini. Maji katika kijiji hiki yana chumvi nyingi. Hivyo basi, vyakula vinavyopikwa huwa na chumvi tayari. Vyakula hivi havifai kuongezwa chumvi. Havina ukosefu wowote wa chumvi. Kwa hivyo, hakuna aliye na upungufu wa chumvi mwilini." Watu wote walifurahia habari hiyo.

47    Hakiuzwi

## Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ch/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** chombo, jembe

**U:** Endelea na maneno; lisichoke, cheza, chema.

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ch, l

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 46.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /ch/ /a/ silabi ni cha

**U:** Endelea na silabi chi, cho, chu, lo.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 46.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** cho ka – choka

**U:** Endelea na maneno; chema, cheza, lisichoke.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 46.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno **chumvi, ukosefu, upungufu.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 47.**

## Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Jina la daktari aliyewaita watu ni nani? *(Walukhano)*

**T:** Daktari alikutana na watu siku gani? *(Siku ya afya)*

**U:** Unafikiri ni kwa nini watu walifurahia habari ya daktari? *(Aliwaelimisha)*

## Zoezi

Mwanafunzi atunge sentensi kutumia maneno yafuatayo akiwa katika vikundi vya wawili.

a) Vitamini    b) Protini    c) Lishe bora

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi sahihi wakitumia:

1. chumvi    2. upungufu    3. ukosefu

Tarehe: ____________    Muda: ____________    Idadi: ____________

# Kipindi cha 47: Lishe bora 1

Kipindi cha 46 na 47 **Lishe bora 1**

**Kipindi 46**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

ch l

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

chi cho chu lo

- Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| che ma | che za | li si cho ke | cho mbo |
| **chema** | **cheza** | **lisichoke** | **chombo** |

**Kipindi 47**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

CH ch L l

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ki na cho patia | wa ki changanya | a li chimba | hu lima |
| **kinachopatia** | **wakichanganya** | **alichimba** | **hulima** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya hiki na hivi**

Onyesha vitu mbalimbali na utunge sentensi tatu ukitumia **hiki** au **hivi**. Fanyeni zoezi hili mkiwa wawili wawili.

**Kwa mfano:**

Kitabu **hiki** ni kizuri. – Vitabu **hivi** ni vizuri.


| Umoja -hiki | Wingi -hivi |
|---|---|
| Kiti **hiki** ni kidogo. | Viti **hivi** ni vidogo. |
| Kiatu **hiki** ni cheusi. | Viatu **hivi** ni vyeusi. |
| Kioo **hiki** chavutia. | Vioo **hivi** vyavutia. |

Mali ya Serikali ya Kenya

46

Kipindi cha 46 na 47 **Lishe bora 1**

**Kusoma hadithi**




**Afya ulimwenguni**

Ilikuwa siku ya afya ulimwenguni. Daktari Walukhano aliwaita watu pamoja kijijini. Alitaka kuwaeleza umuhimu wa chumvi mwilini. Alianza, "Naomba mnisikilize kwa makini. Maji katika kijiji hiki yana chumvi nyingi. Hivyo basi, vyakula vinavyopikwa huwa na chumvi tayari. Vyakula hivi havifai kuongezwa chumvi. Havina ukosefu wowote wa chumvi. Kwa hivyo, hakuna aliye na upungufu wa chumvi mwilini." Watu wote walifurahia habari hiyo.

47 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** CH, ch, L, l

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 46.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li cho tamka - alichotamka

**U:** Endelea na maneno; kinachopatia, wakichanganya, alichimba.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 46.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **chumvi, ukosefu, upungufu.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya 'hiki' na 'hivi'**

**N:** Fafanua maana ya 'hiki' na 'hivi'. 'Hiki' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kikiwa karibu na majina ya vitu yanayoanza na ki-vi. Kwa mfano: Kiatu hiki ni changu.

Chakula hiki ni chetu. 'Hivi' hutumiwa kuonyesha vitu vikiwa karibu na majina yanayoanza na ki-vi. Kwa mfano; Viatu hivi ni vyetu. Vyakula hivi ni vyetu. Waulize wanafunzi wasome sentensi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 46.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike katika hali ya umoja au wingi.

| | |
|---|---|
| 1. Kijiko hiki | 1. ________ (Vijiko hivi) |
| 2. ________ | 2. Viazi hivi (kiazi hiki) |
| 3. Kikapu hiki | 3. ________ (Vikapu hivi) |
| 4. ________ | 4. Vitabu hivi (kitabu hiki) |

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________



Hakiuzwi

Kipindi cha 48 na 49 **Lishe bora 1**

**Kipindi 48**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng ch

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ngi ngo ngu cho

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| u li mwe ngu | u pu ngu fu | za ngu | chu ngwa |
|---|---|---|---|
| **ulimwengu** | **upungufu** | **zangu** | **chungwa** |

**Kipindi 49**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

NG ng CH ch

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| na i pongeza | hu punguza | wa li ingiza | ali chota |
|---|---|---|---|
| **naipongeza** | **hupunguza** | **waliingiza** | **alichota** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya hiki na hivi**

Soma sentensi zifuatazo.

1. Chakula **hiki** ni kitamu.
2. Vyakula **hivi** ni vitamu.
3. Kiazi **hiki** ni kitamu.
4. Viazi **hivi** ni vitamu.
5. Kijiji **hiki** ni kidogo.
6. Vijiji **hivi** ni vidogo.
7. Kiatu **hiki** ni kizuri.

Mali ya Serikali ya Kenya 48

Kipindi cha 48 na 49 **Lishe bora 1**

**Kusoma shairi**



**Lishe bora**

Ndugu zangu sikizeni, wosia niwapatie,
Wote mtie akilini, umuhimu wa vyakula,
Kwanza kuna protini, hiki hujenga mwili,
Lishe bora muhimu, wananchi tuzingatie.

Pili ni vitamini, inayozuia magonjwa,
Huletwa mwilini, na mboga na matunda,
Wapishi mtie akilini, vitamini tusikose,
Lishe bora muhimu, wananchi tuzingatie.

Wanga pia muhimu, nguvu hutupatia,
Mahindi na chapati, hivi vya manufaa,
Kazi twaifanya, maisha kuendeleza,
Lishe bora muhimu, wananchi tuzingatie.

49 Hakluzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ng/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** ulimwengu, watu

**U:** Endelea na maneno; zangu, chungwa, langu, leta.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng, ch

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 48.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /ng//e/ silabi ni nge

**U:** Endelea na silabi ngi, ngo, ngu, cho.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 48.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi kwa kila neno.Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** nga o - ngao

**U:** Endelea na maneno; upungufu, zangu, chungwa.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 48.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **protini, wanga, vitamini.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha shairi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Kusoma shairi

**N/T/U:** Soma shairi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Mwandishi aliwapa watu wosia gani? *(Umuhimu wa chakula mwilini)*

**T:** Protini husaidia mwili na nini? *(Inajenga mwili)*

**U:** Taja vyakula vingine viwili vinavyoleta wanga mwilini? *(Mihogo, mchele na vinginevyo)*

### Zoezi

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno yafuatayo:

1. Wanga 2. Upungufu 3. Lishe bora

### Kazi ya ziada

Wanafunzi wajaze mapengo kwa kutumia 'hiki' au 'hivi'.

1. Vyakula ________. 2. Kikombe ________.
3. Kiti ____________ . 4. Viti ________.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 49: Lishe bora 1

Kipindi cha 48 na 49 **Lishe bora 1**

**Kipindi 48**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng ch

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ngi ngo ngu cho

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| u li mwe ngu | u pu ngu fu | za ngu | chu ngwa |
| **ulimwengu** | **upungufu** | **zangu** | **chungwa** |

**Kipindi 49**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

NG ng CH ch

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| na i pongeza | hu punguza | wa li ingiza | ali chota |
| **naipongeza** | **hupunguza** | **waliingiza** | **alichota** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya hiki na hivi**

Soma sentensi zifuatazo.

1. Chakula **hiki** ni kitamu.
2. Vyakula **hivi** ni vitamu.
3. Kiazi **hiki** ni kitamu.
4. Viazi **hivi** ni vitamu.
5. Kijiji **hiki** ni kidogo.
6. Vijiji **hivi** ni vidogo.
7. Kiatu **hiki** ni kizuri.

Mali ya Serikali ya Kenya 48

Kipindi cha 48 na 49 **Lishe bora 1**

**Kusoma shairi**



**Lishe bora**

Ndugu zangu sikizeni, wosia niwapatie,
Wote mtie akilini, umuhimu wa vyakula,
Kwanza kuna protini, hiki hujenga mwili,
Lishe bora muhimu, wananchi tuzingatie.

Pili ni vitamini, inayozuia magonjwa,
Huletwa mwilini, na mboga na matunda,
Wapishi mtie akilini, vitamini tusikose,
Lishe bora muhimu, wananchi tuzingatie.

Wanga pia muhimu, nguvu hutupatia,
Mahindi na chapati, hivi vya manufaa,
Kazi twaifanya, maisha kuendeleza,
Lishe bora muhimu, wananchi tuzingatie.

49 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NG, ng', CH, ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 48.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li angalia - aliangalia

**U:** Endelea na maneno; naipongeza, hupunguza, waliingiza.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 48.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **protini, vitamini, wanga.**

## Kusoma shairi

**U:** Somea mwenzako shairi.

## Sarufi

**Matumizi ya 'hiki' na 'hivi'**

**N:** Rejelea maana ya 'hiki' na 'hivi'. 'Hiki' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kikiwa karibu na majina ya vitu vinavyoanza na k i-vi. Kwa mfano: Kiti hiki kimevunjika. Cheti hiki ni chetu. 'Hivi' hutumiwa kuonyesha vitu vikiwa karibu na majina yanayoanza ki-vi. Kwa mfano: Vioo hivi ni vyetu.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye shairi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 48.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi ajaze mapengo kwa usahihi.

a) Kitabu ______ ni changu. (**hiki**/hivi).
b) Vyama ________ ni vyetu. (**hivi**/hiki)
c) Vikundi _______ ni vikubwa. (hiki/**hivi**).
d) Kitambaa _____ kinapendeza. (hivi/**hiki**)

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

Kipindi cha 50 **Lishe bora 1**

**Kipindi 50**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng l

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: li she - lishe**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| vi | li | vu | ni | ma |
| mi | ngu | ta | she | di |

◆ **Sarufi: Matumizi ya hiki na hivi**

Andika vifungu vya maneno vifuatavyo katika umoja au wingi.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Kijiko hiki | ___ |
| 2. | ___ | Viazi hivi |
| 3. | Kikapu hiki | ___ |

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Umuhimu wa chakula**



**Kuandika**

Andika sentensi mbili kuhusu matumizi ya chumvi nyumbani.

Mali ya Serikali ya Kenya 50

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

N/T/U: NG, l

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 50.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'lishe'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno kutokana na silabi zilizo kwenye jedwali.

## Hadithi ya mwalimu

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Funza maneno mapya **protini, wanga, vitamini.**

Soma hadithi. Mwanafunzi asikilize na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Umuhimu wa chakula**

Siku ya Ijumaa tulipata mgeni shuleni mwetu. Mgeni huyo alikuwa daktari Jabali. Mwalimu mkuu alikuwa amewaita wazazi ili wahutubiwe na daktari. Wazazi walipoketi na kutulia uwanjani, daktari alianza kwa kuwaeleza umuhimu wa chakula. Alisisitiza kuwa ni muhimu kwa wazazi kuwapatia watoto wao lishe bora. Kwa mfano chakula cha kujenga mwili au protini.

Hiki ni chakula muhimu sana katika kuukuza mwili. Protini hutokana na nyama, maziwa na hata maharagwe. Ukosefu wa protini humfanya mtoto kukosa kufikia kiwango kinachostahili katika kujenga mwili.

Kuna chakula cha wanga pia ambacho hupatia mwili nguvu. Chakula hiki hutokana na mazao yenye wanga kama vile mihogo, mahindi, mchele na mengineyo. Ukosefu wa chakula hiki hudhoofisha mwili na kumfanya mtu asiweze kufanya kazi yoyote. Kadhalika, kuna chakula kinachopatia mwili vitamini. Chakula hiki husaidia mwili kujikinga na magonjwa. Vitamini hutokana na mboga na matunda. Upungufu wa chakula hiki humfanya mtu kupata magonjwa. Mwili pia huhitaji kiwango kidogo cha chumvi ambayo pia huvipa vyakula ladha nzuri.

Daktari alimalizia kwa kuwahimiza wazazi wawe wakichanganya vyakula hivi kila wanapopika. Hili, alisema, litawafanya watoto kuwa na afya nzuri.

## Maswali

**T:** Kwa nini mwalimu mkuu alimwalika daktari Jabali shuleni? *(Ahutubie wazazi)*

**U:** Taja aina za vyakula vilivyotajwa na umuhimu wake mwilini. *(Protini - hujenga mwili, vitamini - hulinda mwili kutokana na magonjwa, wanga - huupa mwili nguvu)*

**U:** Eleza aina ya vyakula unavyoweza kuchanganya kuwa na lishe bora. *(Matunda, mboga, viazi)*

## Kuandika

**N:** Andika sentensi kuhusu matumizi ya chumvi.

**T:** Waongoze wanafunzi kuandika sentensi huku wakiakifisha.

**U:** Wanafunzi waandike sentensi mbili kuhusu matumizi ya chumvi nyumbani.

## Sarufi

**Matumizi ya 'hiki' na 'hivi'**

**N:** Rejelea maana ya 'hiki' na 'hivi'. 'Hiki' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kikiwa karibu na majina ya vitu vinavyoanza na k i-vi. Kwa mfano: Kijiti hiki ni kirefu.

Chombo hiki ni kichafu. 'Hivi' hutumiwa kuonyesha vitu vikiwa karibu na majina yanayoanza ki-vi. Kwa mfano: Viatu hivi ni safi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 50.**

**Majibu**

1. Vijiko hivi 2. Kiazi hiki 3. Vikapu hivi

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike jina na kuchora picha za vyakula hivi:

1. Samaki 2. Ndizi 3. Yai

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 51 na 52 **Marejeleo 1**

**Kipindi 51**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ch ng

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

che chi cho chu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| cha ku la | chu ra | ngo ma | nga no |
| **chakula** | **chura** | **ngoma** | **ngano** |

**Kipindi 52**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

CH ch

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ku m chukua | ku ta ka po nyesha | a li tu kumbusha |
| **kumchukua** | **kutakaponyesha** | **alitukumbusha** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**


Akifisha sentensi zifuatazo.

1. watalii walifika mombasa kwa meli
2. ofisi ya bi. zawadi iko karibu na gwaride
3. mzee zurua atafika jumamosi
4. dada yangu anaitwa sofia
5. mombasa ni mji mkubwa
6. kiatu changu kimepotea
7. chakula hicho kimepikwa na mama juma.

51 Hakiuzwi

Kipindi cha 51 na 52 **Marejeleo 1**

Kusoma hadithi



**Chifu mwenye hekima**

Siku moja, chifu Nyambeta alizuru shule yetu. Alitueleza kuhusu haki zetu. Kwanza alisema kuwa tuna haki ya kupewa matibabu, elimu, mavazi, vyakula na usalama. Alitukumbusha kutumia kivukio cha barabara ili kuepuka ajali. Chifu alisema ni muhimu kudumisha usafi madarasani na katika maktaba. "Nyinyi mnafaa kuwaheshimu wakubwa wenu. Kwa mfano walimu, babu, nyanya na halati," alitukumbusha. Pia alituhimiza tupande miti kutakaponyesha. Miti itakinga nyumba zetu dhidi ya upepo.

Mali ya Serikali ya Kenya 52

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ch/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno. Mwanafunzi aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno husika.

**N/T/U:** chifu, soma

**U:** Endelea na maneno; wasichana, samaki, choma, chuma.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ch, ng

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 51**.

### Kusoma silabi

Tamka sauti katika silabi. Unganisha sauti. Soma silabi.

**N/T:** /ch/ /a/ silabi ni cha.

**U:** Endelea na silabi che, chi, cho, chu

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 51.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja ili uweze kulisoma neno.

**N/T/U:** cho mbo – chombo

**U:** Endelea na maneno; chakula, chura, ngoma

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 51.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **maktaba, halati, mavazi**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 52.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

1. Chifu aliitwa nani? (Nyambeta)
2. Ni sehemu gani inafaa kuwa safi? (madarasani na maktaba)
3. Unafikiri ni nani alimwalika chifu shuleni kuzungumza na wanafunzi? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Chora vifaa vitatu vinavyopatikana darasani.

### Kazi ya ziada

Andika aina nne ya vyakula unavyovijua.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 52: Marejeleo 1

Kipindi cha 51 na 52 **Marejeleo 1**

**Kipindi 51**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ch ng

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

che chi cho chu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| cha ku la | chu ra | ngo ma | nga no |
| **chakula** | **chura** | **ngoma** | **ngano** |

**Kipindi 52**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

CH ch

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ku m chukua | ku ta ka po nyesha | a li tu kumbusha |
| **kumchukua** | **kutakaponyesha** | **alitukumbusha** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Akifisha sentensi zifuatazo.

1. watalii walifika mombasa kwa meli
2. ofisi ya bi. zawadi iko karibu na gwaride
3. mzee zurua atafika jumamosi
4. dada yangu anaitwa sofia
5. mombasa ni mji mkubwa
6. kiatu changu kimepotea
7. chakula hicho kimepikwa na mama juma.



Hakiuzwi

Kipindi cha 51 na 52 **Marejeleo 1**

**Kusoma hadithi**



**Chifu mwenye hekima**

Siku moja, chifu Nyambeta alizuru shule yetu. Alitueleza kuhusu haki zetu. Kwanza alisema kuwa tuna haki ya kupewa matibabu, elimu, mavazi, vyakula na usalama. Alitukumbusha kutumia kivukio cha barabara ili kuepuka ajali. Chifu alisema ni muhimu kudumisha usafi madarasani na katika maktaba. "Nyinyi mnafaa kuwaheshimu wakubwa wenu. Kwa mfano walimu, babu, nyanya na halati," alitukumbusha. Pia alituhimiza tupande miti kutakaponyesha. Miti itakinga nyumba zetu dhidi ya upepo.



## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** CH, ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 51**.

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** ku wa heshimu - kuwaheshimu

**U:** Endelea na maneno; kumchukua, kutakaponyesha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 51**.

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **mavazi, maktaba, halati.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya herufi kubwa**

**N:** Tunatumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi. Pia, tunatumia herufi kubwa mwanzoni mwa majina ya watu, miji na siku.

**T:** Mwanafunzi asome sentensi zenye sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 51.**

**Majibu**

1. Watalii walifika Mombasa kwa meli.
2. Ofisi ya Bi. Zawadi iko karibu na gwaride.
3. Mzee Zurua atafika Jumamosi.
4. Dada yangu anaitwa Sofia.
5. Mombasa ni mji mkubwa.
6. Kiatu changu kimepotea.
7. Chakula hicho kimepikwa na Mama Juma.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi afinyange maumbo ya herufi anazozijua huku akizitambua na kuzitaja.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 53 na 54 **Marejeleo 1**

**Kipindi 53**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

dh ch

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

dha dhe dhi dho dhu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| dha ti | dhi di | che tu | cha ngu |
| dhati | dhidi | chetu | changu |

**Kipindi 54**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

DH dh CH ch

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ku hudhuria | ku jadiliana | wa li chapwa | a li choka |
| **kuhudhuria** | **kujadiliana** | **walichapwa** | **alichoka** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma sentensi zifuatazo.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mtoto **wako** amelala. | Watoto **wenu** wamelala. |
| 2. | Jani **lako** limeanguka. | Majani **yenu** yameanguka. |
| 3. | Jina **lako** ni zuri. | Majina **yenu** ni mazuri. |
| 4. | Mkoba **wako** umeraruka. | Mikoba **yenu** imeraruka. |
| 5. | Kiti **chako** kimevunjika. | Viti **vyenu** vimevunjika. |

53 Hakiuzwi

Kipindi cha 53 na 54 **Marejeleo 1**

Kusoma hadithi



**Malezi bora**

Lotim na familia yake waliishi Kanam. Walikuwa na watoto wawili. Lotim aliwapa watoto wake malezi bora. Walipata chakula na mavazi mazuri. Lotim aliwahimiza watie bidii masomoni. Walisikiza na kuzingatia mawaidha ya wazazi. Waliongoza katika mtihani wa darasa lao. Tabia zao ziliwavutia watu wengi. Walipewa zawadi kila mara. Wakiwa nyumbani waliwasaidia wazazi wao. Katika kuwapongeza kwa bidii yao, wazazi wao waliwapeleka kuhudhuria harusi ya shangazi yao.

Mali ya Serikali ya Kenya 54

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/dh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno. Mwanafunzi aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** dhahabu, darasa

**U:** Endelea na maneno; dhati, debe, mkono, darasa, dhidi.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** dh, ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 53.**

### Kusoma silabi

Tamka sauti katika silabi. Unganisha sauti. Soma silabi.

**N/T/U:** /dh / /a/ – dha

**U:** Endelea na silabi dhe, dhi, dho, dhu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 53.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** dha ha bu – dhahabu

**U:** Endelea na maneno; dhati, dhidi, chetu.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 53.**

### Msamiati

Funza maana ya msamiati: **malezi bora, darasa, shangazi.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Lotim na familia yake waliishi wapi? *(Kanam)*

**T:** Lotim alikuwa na watoto wangapi? *(Wawili)*

**U:** Unafikiri malezi bora waliyopewa watoto hawa ni gani? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi apige mstari herufi zinazopaswa kuwa kubwa.

1. mwalimu wetu kamau amefika. (mwalimu, kamau)
2. Jiji la nairobi ni mkubwa. (nairobi)

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike haki tatu za watoto anazozijua.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 54: Marejeleo 1

Kipindi cha 53 na 54 **Marejeleo 1**

**Kipindi 53**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**dh** **ch**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**dha** **dhe** **dhi** **dho** **dhu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| dha ti | dhi di | che tu | cha ngu |
| dhati | dhidi | chetu | changu |

**Kipindi 54**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**DH** **dh** **CH** **ch**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ku hudhuria | ku jadiliana | wa li chapwa | a li choka |
| **kuhudhuria** | **kujadiliana** | **walichapwa** | **alichoka** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma sentensi zifuatazo.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mtoto **wako** amelala. | Watoto **wenu** wamelala. |
| 2. | Jani **lako** limeanguka. | Majani **yenu** yameanguka. |
| 3. | Jina **lako** ni zuri. | Majina **yenu** ni mazuri. |
| 4. | Mkoba **wako** umeraruka. | Mikoba **yenu** imeraruka. |
| 5. | Kiti **chako** kimevunjika. | Viti **vyenu** vimevunjika. |

53

Hakluzwi

Kipindi cha 53 na 54 **Marejeleo 1**

**Kusoma hadithi**



**Malezi bora**

Lotim na familia yake waliishi Kanam. Walikuwa na watoto wawili. Lotim aliwapa watoto wake malezi bora. Walipata chakula na mavazi mazuri. Lotim aliwahimiza watie bidii masomoni. Walisikiza na kuzingatia mawaidha ya wazazi. Waliongoza katika mtihani wa darasa lao. Tabia zao ziliwavutia watu wengi. Walipewa zawadi kila mara. Wakiwa nyumbani waliwasaidia wazazi wao. Katika kuwapongeza kwa bidii yao, wazazi wao waliwapeleka kuhudhuria harusi ya shangazi yao.

Mali ya Serikali ya Kenya

54

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** DH, dh, CH

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 53.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo na usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** wa li wa pelekea – waliwapelekea

**U:** Endelea na maneno; kuhudhuria, kujadiliana, walichapwa.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 53.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **malezi bora, darasa, shangazi.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya vimilikishi ; '-ako' na '-enu'.**

**N:** Tunatumia '-ako' pamoja na herufi 'ch' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano, kitabu chako ni kizuri. Tunatumia '-enu' pamoja na herufi 'vy' kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Tunga sentensi ukitumia '-ako' na '-enu'. Kwa mfano: Chakula chako ni kizuri. Vyakula vyenu ni vizuri.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi


Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi lililopo kwenye **ukurasa wa 53.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi ajaze mapengo kwa kutumia **–ako** na **–enu**

1. Chakula hiki ni ch__. Vyakula hivi ni vy___.
2. Chombo kile ni ch___. Vyombo vile ni vy___.
3. Chifu huyu ni w_____. Chifu hawa ni w____.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________



Kipindi cha 55 **Marejeleo 1**

**Kipindi 55**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

CH ch DH dh

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ma ti ba bu – matibabu**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ma | zi | cha | ba | ki |
| bu | va | ti | le | mi |

◆ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Andika na uigize vitendo hivi katika sentensi.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | **Wewe** u**li**andika. | **Nyinyi** m**li**andika. |
| 2. | **Wewe** u**li**cheza. | **Nyinyi** m**li**cheza. |
| 3. | **Wewe** u**li**simama. | **Nyinyi** m**li**simama. |

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Marafiki wa dhati**

**Kuandika**

Andika maneno haya kwa herufi kubwa.

**Kwa mfano:**

**dhambi – DHAMBI**

1. dhahabu 2. dhehebu 3. dhidi 4. dharau

55

Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** CH, ch, DH, dh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 55.**

### Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'matibabu'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

### Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **sebuleni, maktaba.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi. Mwanafunzi asikilize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

**Marafiki wa dhati**

Jumamosi Omari alimtembelea rafiki yake Anjela nyumbani kwao Ramula. Anjela alishikwa na wasiwasi sana Omari alipokawia kufika. Baba yake Anjela alienda kituo cha basi kumchukua Omari. Anjela alifurahi kumwona Omari aliyesafiri kutoka Masaku. Omari alikaribishwa na kuandaliwa vyakula vitamu.

Omari na Anjela waliketi sebuleni na kujadiliana kuhusu matukio ya shuleni. Anjela alimuuliza Omari, "Nyinyi mmesoma nini muhula huu?"

"Ooh! Mwalimu wetu ametufundisha kuhusu bendera yetu na mambo mengi kuhusu darasa letu. Zaidi ya hayo, tulienda katika maktaba jana tukasoma kuhusu usafiri. Mwalimu alitukumbusha kuwa ni vizuri kutumia kivukio cha barabara na vidaraja ili kuepuka ajali," Omari alieleza. "Je, Wewe ulisoma nini?" Omari alimuuliza Anjela.

"Mwalimu alitufundisha kuwa kila mtoto nchini ana haki ya kuishi, kupewa malezi bora, mavazi na elimu. Tulisoma pia kuwa anga yetu hubadilika kila mara. Kuna upepo, jua, mawingu na mvua wakati mwingine. Alituhimiza kuwa ni vizuri kupanda miti ili kutunza mazingira," Anjela alisema. Marafiki hawa walifurahia kuwa pamoja. Baadaye, Omari alirudi kwao.

### Maswali

**T:** Wazazi wa Anjela walimkaribisha Omari kwa njia gani? *(Walimkaribisha kwa kumuandalia vyakula vitamu.)*

**U:** Taja mambo mawili ambayo yalisomwa na Omari na Anjela. *(Walisoma kuhusu haki za watoto, usafiri na usalama wao.)*

**U:** Je, unafikiri nyumbani kwa akina Omari kulikuwa umbali gani kutoka kwa akina Anjela? Kwa nini? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Kuandika

**N:** Andika neno kwa herufi kubwa.

**T:** Waelekeze wanafunzi kuliandika kwa herufi kubwa.

**U:** Mwanafunzi aandike maneno yaliyo kwenye **ukurasa wa 55** kwa herufi kubwa.

### Sarufi

**Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

**N:** Rejelea ufafanuzi wa maana ya nafsi ya pili wakati uliopita. 'Wewe' hutumiwa katika nafsi ya pili hali ya umoja. Huonyesha mtu wa pili baada ya wa kwanza, 'mimi'. Kwa mfano: Wewe ulichana nywele. Wewe ulisoma kitabu. 'U' hutumiwa pamoja na 'wewe' kuonyesha umoja. 'Li' hutumiwa kuonyesha wakati uliopita. 'Wewe' inapotumiwa na 'li' huwa inaonyesha kuwa jambo lilitendeka wakati uliopita.

'Nyinyi' na 'm' hutumiwa katika wingi wa nafsi ya pili. 'li' hutumiwa pamoja na 'nyinyi' na 'm' kuonyesha wingi. Kwa mfano: Nyinyi mlichana nywele. Nyinyi mlisoma vitabu.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 55.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno haya.

1. Dhoruba 2. Dhuluma 3. Mawaidha

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 56: Mnyama nimpendaye 1

Kipindi cha 56 na 57 **Mnyama nimpendaye 1**

**Kipindi 56**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng** **ch**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**nga** **nge** **ngi** **ngo** **ngu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| nga mia | nyi ngi | cha fu | cha nga |
| **ngamia** | **nyingi** | **chafu** | **changa** |

**Kipindi 57**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG** **ng** **CH** **ch**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ku tengeneza | a na ye ongeza | ku changanya |
| **kutengeneza** | **anayeongeza** | **kuchanganya** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**


Onyesha mwenzako vitu mbalimbali kwa kutumia **hili** au **haya**. **Kwa mfano:** Jiwe **hili** – Mawe **haya**

1. Dawati
2. Macho
3. Sikio
4. Maembe
5. Ndizi
6. Jiwe

Mali ya Serikali ya Kenya 56

Kipindi cha 56 na 57 **Mnyama nimpendaye 1**

**Kusoma hadithi**



**Ngamia**

Ngamia ni mnyama anayefugwa nyumbani. Yeye ana shingo ndefu na miguu mirefu. Ngamia hutumia nundu yake kuhifadhi maji. Kwa hivyo, anaweza kukaa siku nyingi bila kunywa maji. Ngamia hutupatia maziwa, nyama na ngozi. Hutusaidia pia kubeba mizigo kama wafanyavyo punda na farasi. Manufaa haya ni muhimu sana.

Ngamia akikasirika anaweza kumuuma au kupiga mtu teke. Teke hili lina uzito. Unaweza kumfanya awe rafiki kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, kumpa chakula na maji. Nampenda Ngamia!

57 Hakluzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ng/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno. Mwanafunzi aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** ngamia, ng'ombe

**U:** Endelea na maneno; ngozi, karatasi, nguzo, ngao.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng, ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 56.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /ch / a/ silabi ni cha

**U:** Endelea na silabi nga, nge, ngi, ngo, ngu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 56.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: ngo zi – ngozi

**U:** Endelea na maneno; ngamia, nyingi, chafu.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 56.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **punda, farasi, ngamia.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Ni sehemu gani za mwili wa ngamia ambazo huwa ndefu? *(Shingo na miguu)*

**T:** Je, ngamia huwa na faida gani? *(Hutupatia maziwa, nyama na ngozi.)*

**U:** Unafikiri ngamia hula nini? *(Kubali jibu sahihi)*

### Zoezi

Katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili, mwanafunzi mweleze mwenzake kuhusu mnyama ampendaye.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore wanyama hawa wa nyumbani.

1. Punda 2. Ngamia 3. Ng'ombe

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

**Kipindi cha 56 na 57 — Mnyama nimpendaye 1**

**Kipindi 56**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng ch

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

nga nge ngi ngo ngu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| nga mia | nyi ngi | cha fu | cha nga |
| **ngamia** | **nyingi** | **chafu** | **changa** |

**Kipindi 57**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

NG ng CH ch

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ku tengeneza | a na ye ongeza | ku changanya |
| **kutengeneza** | **anayeongeza** | **kuchanganya** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Onyesha mwenzako vitu mbalimbali kwa kutumia **hili** au **haya**. **Kwa mfano:** Jiwe **hili** – Mawe **haya**


1. Dawati
2. Macho
3. Sikio
4. Maembe
5. Ndizi
6. Jiwe

Mali ya Serikali ya Kenya

56

**Kipindi cha 56 na 57 — Mnyama nimpendaye 1**

**Kusoma hadithi**



**Ngamia**

Ngamia ni mnyama anayefugwa nyumbani. Yeye ana shingo ndefu na miguu mirefu. Ngamia hutumia nundu yake kuhifadhi maji. Kwa hivyo, anaweza kukaa siku nyingi bila kunywa maji. Ngamia hutupatia maziwa, nyama na ngozi. Hutusaidia pia kubeba mizigo kama wafanyavyo punda na farasi. Manufaa haya ni muhimu sana.

Ngamia akikasirika anaweza kumuuma au kupiga mtu teke. Teke hili lina uzito. Unaweza kumfanya awe rafiki kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, kumpa chakula na maji. Nampenda Ngamia!

57 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NG, ng, CH, ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 56.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** wa li ngojea - walingojea

**U:** Endelea na maneno; kutengeneza, anayeongeza.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 56.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **ngamia, punda, farasi.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya 'hili' na 'haya'**

**N:** Fafanua maana na matumizi ya 'hili' na 'haya'.

'Hili' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kilicho karibu cha neno linaloanza na 'ma' katika wingi. Kwa mfano: Tunda hili. Tawi hili. Jina hili.

'Haya' hutumiwa kuonyesha vitu vilivyo karibu vya majina yanayoanza na 'ma' katika wingi. Kwa mfano: Matunda haya. Matawi haya. Majina haya.

**U:** Mwanafunzi atambue na asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 56.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aeleze mlezi wake faida ya wanyama hawa.

1. Ngamia
2. Ng'ombe
3. Kondoo

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 58: Mnyama nimpendaye 1

Kipindi cha 58 na 59 **Mnyama nimpendaye 1**

**Kipindi 58**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**mb** **ng**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**mba** **mbe** **mbi** **ngo** **ngu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| mbe le | u mbe a | nyu mba ni | ngu mu |
|---|---|---|---|
| **mbele** | **umbea** | **nyumbani** | **ngumu** |

**Kipindi 59**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**MB** **mb**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li chambua | a li omba | i na ng'ara | a li ngoa |
|---|---|---|---|
| **alichambua** | **aliomba** | **inang'ara** | **aling'oa** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Msomee mwenzako vifungu vifuatavyo.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Tawi **hili** | Matawi **haya** |
| 2. | Tunda **hili** | Matunda **haya** |
| 3. | Jino **hili** | Meno **haya** |
| 4. | Embe **hili** | Maembe **haya** |
| 5. | Teke **hili** | Mateke **haya** |

Mali ya Serikali ya Kenya 58

Kipindi cha 58 na 59 **Mnyama nimpendaye 1**

**Kusoma hadithi**



**Punda mtumishi mwema**

Je, wajua kuwa punda ni mtumishi mtiifu? Mimi ninampenda punda. Yeye hutusaidia sana nyumbani. Baba humtumia punda kubeba maji. Maji haya yanatumika nyumbani. Wanyama wengine kama kondoo na mbuzi hunywa maji haya. Punda hubeba mizigo hadi sokoni. Mama naye humtumia kwa kubeba kuni. Punda hupenda kula chakula kizuri. Chakula chake ni nyasi. Mama humpatia maji pia. Punda akishiba huwa na furaha. Si vizuri kumkasirisha punda. Akiwa na hasira humpiga mtu teke. Teke hili linaweza kuumiza. Jihadhari na punda.

59 Hakuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/mb/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U**: mbao, mpira

**U:** Endelea na maneno; mbali, bata, mbung'o, mbwa, paka.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** mb, ng

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 58.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /mb/ u/ silabi ni mbu

**U:** Endelea na silabi mba, mbe, mbi, ngo, ngu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 58.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** mbo le a - mbolea.

**U:** Endelea na maneno; mbele, umbea, nyumbani.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 58.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kondoo, punda, mbuzi.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kwa nini mwandishi humpenda punda. *(Kwa sababu punda husaidia sana nyumbani.)*

**T:** Punda hutumikaje nyumbani? *(Kubeba maji, mizigo, kuni)*

**U:** Taja wanyama wengine wanaosaidia nyumbani? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike sentensi tatu kuhusu jinsi ya kumtunza mnyama anayempenda.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi tatu ukitumia maneno haya.

1. Punda  2. Kondoo  3. Ngamia

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 59: Mnyama nimpendaye 1

Kipindi cha 58 na 59 **Mnyama nimpendaye 1**

**Kipindi 58**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**mb** **ng**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**mba** **mbe** **mbi** **ngo** **ngu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| mbe le | u mbe a | nyu mba ni | ngu mu |
| **mbele** | **umbea** | **nyumbani** | **ngumu** |

**Kipindi 59**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**MB** **mb**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a li chambua | a li omba | i na ng'ara | a li ngoa |
| **alichambua** | **aliomba** | **inang'ara** | **aling'oa** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Msomee mwenzako vifungu vifuatavyo.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Tawi **hili** | Matawi **haya** |
| 2. | Tunda **hili** | Matunda **haya** |
| 3. | Jino **hili** | Meno **haya** |
| 4. | Embe **hili** | Maembe **haya** |
| 5. | Teke **hili** | Mateke **haya** |

Mali ya Serikali ya Kenya

58

Kipindi cha 58 na 59 **Mnyama nimpendaye 1**

**Kusoma hadithi**



**Punda mtumishi mwema**

Je, wajua kuwa punda ni mtumishi mtiifu? Mimi ninampenda punda. Yeye hutusaidia sana nyumbani. Baba humtumia punda kubeba maji. Maji haya yanatumika nyumbani. Wanyama wengine kama kondoo na mbuzi hunywa maji haya. Punda hubeba mizigo hadi sokoni. Mama naye humtumia kwa kubeba kuni. Punda hupenda kula chakula kizuri. Chakula chake ni nyasi. Mama humpatia maji pia. Punda akishiba huwa na furaha. Si vizuri kumkasirisha punda. Akiwa na hasira humpiga mtu teke. Teke hili linaweza kuumiza. Jihadhari na punda.

59 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** MB, mb

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 58.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** hu bamba – hubamba

**U:** Endelea na maneno; alichambua, aaliomba, inang'ara.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 58.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **punda, kondoo, mbuzi.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya 'hili' na 'haya'**

**N:** Fafanua maana na matumizi ya 'hili' na 'haya'.

'Hili' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kilicho karibu cha neno linaloanza na 'ma' katika wingi. Kwa mfano: Ganda hili. Jani hili. Neno hili.

'Haya' hutumiwa kuonyesha vitu vilivyo karibu vya majina yanayoanza na 'ma' katika wingi. Kwa mfano: Maganda haya. Majani haya. Maneno haya.

**U:** Mwanafunzi atambue na asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 58.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi akambilishe sentensi akitumia jibu sahihi kwenye mabano.

1. Tunda ________ ni tamu. ( haya/**hili**)
2. Mayai ______ yameoza. (hili/**haya**)
3. Dawati _____ ni kubwa. (hii/**hili**)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 60 **Mnyama nimpendaye 1**

**Kipindi 60**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

NG ng MB mb

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ko ndo o – kondoo**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| o | mbu | ng'o | ndo | a |
| zi | ko | mi | mbe | nga |

◆ **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Chagua jibu sahihi kwenye mabano kujaza nafasi zilizoachwa.

1. Majina __________ yaliandikwa kitabuni. (haya, hili)
2. Goti __________ limeumia. (hili, haya)
3. Meno __________ ni meupe. (hili, haya)

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Mnyama nimpendaye**



**Kuandika**

Wanyama wa nyumbani wana umuhimu gani?

Mali ya Serikali ya Kenya 60

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NG, ng, MB, mb

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 60.**

## ★ Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na mwanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'kondoo'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza maneno mapya **ng'ombe, kondoo, mbuzi.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

**Mnyama nimpendaye**

Je, wajua kwamba ng'ombe ni mnyama anayefugwa katika sehemu nyingi za dunia? Ng'ombe ni mmojawapo wa wanyama wanaofugwa nyumbani mbali na kondoo na mbuzi. Ng'ombe ana manufaa mengi. Binadamu hupata maziwa, nyama na ngozi kutoka kwake. Pia, ng'ombe hutupatia mbolea kutoka kwa samadi. Mbolea hii hutumiwa kuongeza rutuba katika mashamba yetu.

Vilevile, kwato zake hutumiwa kutengeneza mapambo mbalimbali kama vipuli na shanga. Isitoshe, mnyama huyu hutusaidia kufanya kazi ya kulima.

Hata hivyo, ufugaji wa ng'ombe umepata tatizo la ukosefu wa lishe ya kutosha. Hili limesababishwa na ukame ulioletwa na ukataji wa miti ovyo. Wanateknolojia hata hivyo wameweka juhudi na kuleta mbinu za kisasa za kutengeneza lishe. Wafugaji wanaweza kusagia ng'ombe wao majani, yawe mabichi au yaliyokauka kwa kutumia mashine maalum. Majani haya huwasaidia ng'ombe wakati wowote. Ng'ombe anaposhiba huwa ni mnyama mtulivu, mpole na wa kupendeza.

Kwa hakika mimi nampenda ng'ombe kwani ameboresha maisha ya wengi kote ulimwenguni. Je, wewe unampenda mnyama gani?

## ? Maswali

**N:** Ni wanyama gani wengine wanaofugwa nyumbani mbali na ng'ombe? *(mMbuzi na kondoo)*

**T:** Taja manufaa manne ya ng'ombe. *(Maziwa, ngozi na nyama. Pia mbolea inayotumiwa kuongeza rotuba shambani. Kwato zake zinatumika kutengeneza mapambo.)*

**U:** Unafikiri ni kwa nini watu hukata miti? *(Kubali jibu sahihi kama: ili kutumia kwa kujenga nyumba, kupata kuni, kutengeneza vitu mbalimbali na n.k).*

## Kuandika

**N:** Andika sentensi moja kuhusu umuhimu wa wanyama wa nyumbani. Sisitiza kuhusu herufi kubwa na kikomo.

**T:** Onyesha jinsi ya kuandika sentensi kuhusu umuhimu wa wanyama wa nyumbani. Sisitiza kuhusu herufi kubwa na kikomo.

**U:** Mwanafunzi aandike sentensi kuhusu umuhimu wa wanyama wa nyumbani. Sisitiza kuhusu herufi kubwa na kikomo.

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya 'hili' na 'haya'**

Fafanua maana na matumizi ya 'hili' na 'haya'.

'Hili' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kilicho karibu cha neno linaloanza na 'ma' katika wingi. Kwa mfano: Yai hili.

'Haya' hutumiwa kuonyesha vitu vilivyo karibu vya majina yanayoanza na 'ma' katika wingi. Kwa mfano: Mayai haya.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 60.**

**Majibu**

1. haya  2. hili  3. haya

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi nne kuhusu wanyama wanaopatikana nyumbani kwao.

Tarehe: ____________________ Muda: ____________________ Idadi: ____________________

# Kipindi cha 61: Mnyama nimpendaye 2

Kipindi cha 61 na 62 **Mnyama nimpendaye 2**

**Kipindi 61**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**nd** **mb**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**nda** **nde** **ndi** **ndo** **ndu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| nda ma | ko ndo o | nyu mba ni | mba li mba li |
|---|---|---|---|
| **ndama** | **kondoo** | **nyumbani** | **mbalimbali** |

**Kipindi 62**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ND** **nd**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li andaa | a li wa omba | ku andika | ku andama |
|---|---|---|---|
| **aliandaa** | **aliwaomba** | **kuandika** | **kuandama** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Tumia **hili** au **haya** kukamilisha vifungu vifuatavyo.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Jicho ______ | Macho ______ |
| 2. | Jimbo ______ | Majimbo ______ |
| 3. | Ua ______ | Maua ______ |
| 4. | Jengo ______ | Majengo ______ |
| 5. | Jopo ______ | Majopo ______ |

61 Hakiuzwi

Kipindi cha 61 na 62 **Mnyama nimpendaye 2**

**Kusoma hadithi**



**Siri ya Ndori**

Mzee Ndori aliishi katika kijiji cha Bukuka. Alikuwa tajiri na maarufu kwa ufugaji wa wanyama. Katika zizi lake alifuga ng'ombe, kondoo na farasi. Wanakijiji walishangazwa na Ndori. Lakini yeye alicheka tu na kuendelea na ufugaji wake. Yeye aliwafuga pia wanyama pori kama fisi na simba.

Wanyama hawa waliishi kwa amani. Watu walimtembelea kutoka sehemu mbalimbali za nchi. Walikuja ili kujua siri yake. Chifu wa Bukuka aliandaa jukwaa. Ndori alitumia jukwaa hili kuwafundisha mambo mengi. Mambo haya yaliwasaidia watu sana. Waliamua kutenda jinsi walivyofundishwa.

Mali ya Serikali ya Kenya 62

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/nd/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** ndani, pwani

**U:** Endelea na maneno; ndoo, tumbo, ndama, dari, ndimi.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** nd, mb

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 61**.

### Kusoma silabi

Tamka sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /nd/ a / silabi ni nda.

**U:** Endelea na silabi nde, ndi, ndo, ndu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 61.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** pu nda – punda

**U:** Endelea na maneno; ndama, kondoo, nyumbani.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 61.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **ng'ombe, kondoo, farasi.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 62.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Taja wanyama waliokuwa katika zizi la mzee Ndori. *(Ng'ombe, kondoo na farasi)*

**T:** Ni nini kilishangaza watu kuhusu mzee Ndori? *(Walishangazwa kwa kuwa mzee Ndori aliwafuga wanyama pori kama fisi na simba.)*

**U:** Unafikiri aliwapa simba na fisi chakula gani? *(Kubali jibu sahihi kama nyama.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike kwa wingi au umoja.

1. Ng'ombe  2. Kondoo  3. Mbuzi

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike wanyama watatu anaowapenda.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 61 na 62 **Mnyama nimpendaye 2**

**Kipindi 61**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**nd** **mb**

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**nda** **nde** **ndi** **ndo** **ndu**

Soma maneno ukitumia silabi.

| nda ma | ko ndo o | nyu mba ni | mba li mba li |
|---|---|---|---|
| **ndama** | **kondoo** | **nyumbani** | **mbalimbali** |

**Kipindi 62**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ND** **nd**

Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li andaa | a li wa omba | ku andika | ku andama |
|---|---|---|---|
| **aliandaa** | **aliwaomba** | **kuandika** | **kuandama** |

**Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Tumia **hili** au **haya** kukamilisha vifungu vifuatavyo.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Jicho ____________ | Macho ____________ |
| 2. | Jimbo ____________ | Majimbo ____________ |
| 3. | Ua ____________ | Maua ____________ |
| 4. | Jengo ____________ | Majengo ____________ |
| 5. | Jopo ____________ | Majopo ____________ |

61 Hakiuzwi

Kipindi cha 61 na 62 **Mnyama nimpendaye 2**

**Kusoma hadithi**



**Siri ya Ndori**

Mzee Ndori aliishi katika kijiji cha Bukuka. Alikuwa tajiri na maarufu kwa ufugaji wa wanyama. Katika zizi lake alifuga ng'ombe, kondoo na farasi. Wanakijiji walishangazwa na Ndori. Lakini yeye alicheka tu na kuendelea na ufugaji wake. Yeye aliwafuga pia wanyama pori kama fisi na simba.

Wanyama hawa waliishi kwa amani. Watu walimtembelea kutoka sehemu mbalimbali za nchi. Walikuja ili kujua siri yake. Chifu wa Bukuka aliandaa jukwaa. Ndori alitumia jukwaa hili kuwafundisha mambo mengi. Mambo haya yaliwasaidia watu sana. Waliamua kutenda jinsi walivyofundishwa.

Mali ya Serikali ya Kenya 62

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ND, nd

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 61**.

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li wa fundisha – aliwafundisha

**U:** Endelea na maneno; aliandaa, aliwaomba, kuandamana.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 61**.

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **ng'ombe, kondoo, farasi.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya 'hili' na 'haya'**

**N:** Fafanua maana na matumizi ya 'hili' na 'haya'.

'Hili' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kilicho karibu cha neno linaloanza na 'ma' katika wingi. Kwa mfano: Dawati hili. Pato hili.

'Haya' hutumiwa kuonyesha vitu vilivyo karibu vya majina yanayoanza na 'ma' katika wingi. Kwa mfano: Madawati haya. Mapato haya.

**U:** Mwanafunzi atambue na asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 61.**

**Majibu**

1. Jicho hili – Macho haya
2. Jimbo hili – Majimbo haya
3. Ua hili – Maua haya

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore wanyama wanne anaowapenda na aandike majina yao.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 63 na 64 **Mnyama nimpendaye 2**

**Kipindi 63**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng'** **nd**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ng'a** **ng'e** **ng'i** **ng'o** **ng'u**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng'o mbe | ng'o a | se ng'e nge | ng'a mbo |
| **ng'ombe** | **ng'oa** | **seng'enge** | **ng'ambo** |

**Kipindi 64**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG'** **ng'** **ND** **nd**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a li ji unga | wa li shangazwa | hu ng'ang'ania |
| **alijiunga** | **walishangazwa** | **hung'ang'ania** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**


Tunga sentensi ukitumia **hili** au **haya** pamoja na maneno yafuatayo:

1. Machungwa
2. Jino
3. Mambo
4. Jani
5. Majangwa
6. Ndizi
7. Mapaipai

63 Hakiuzwi

Kipindi cha 63 na 64 **Mnyama nimpendaye 2**

**Kusoma hadithi**




**Maonyesho ya mifugo**

Wafula alikuwa mkulima hodari. Aliishi peke yake ng'ambo ya mto. Jambo hili lilimfurahisha. Alifuga mifugo wengi kama ng'ombe, sungura, kondoo, punda na nguruwe. Siku moja alialikwa kuhudhuria maonyesho ya kilimo. Maonyesho hayo yalifanyika mjini. Alivaa nguo nyeupe pe pe pe zilizong'ara. Alipofika mtoni, aling'oa kijiti ili apime kina cha maji. Hii ni kabla ya kuvuka mto. Alipovuka mto, alijiunga na wakulima wengine kujifunza mbinu mpya za ukulima. Baadaye alinunua seng'enge na bidhaa mbalimbali za ukulima. Alielekea kwake nyumbani Kijijini Mbeya.

Mali ya Serikali ya Kenya 64

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ng'/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** /ng'/, ng'oa, ngamia

**U:** Endelea na maneno; ngumu, ng'onda, ng'ombe, ngiri.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng', nd

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 63.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /ng'/ / a/ silabi ni ng'a

**U:** Endelea na silabi ng'e, ng'i, ng'o, ng'u.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 63.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja ukilisoma neno.

**N/T/U:** ng'a mbo – ng'ambo

**U:** Endelea na maneno; ng'ombe, ng'oa, seng'enge.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 63.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **ng'ombe, nguruwe, sungura.** Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 64.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Wafula aliishi wapi? *(Aliishi ng'ambo ya mto.)*

**T:** Taja wanyama ambao Wafula alifuga? *(Alifuga ng'ombe, sungura, kondoo, punda na nguruwe.)*

**U:** Kwa nini Wafula alinunua seng'enge? *(Kubali jibu sahihi, kwa mfano: ili kuzungusha ua shambani mwake alinde wanyama wake.)*

### Zoezi

Mwanafunzi atumie **hili** au **haya** kujaza pengo.

| | |
|---|---|
| 1. Tunda ________ | Matunda haya (hili) |
| 2. Embe hili | Maembe ________ (haya) |
| 3. Jiwe ________ | Mawe haya (hili) |

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi tatu akitumia **hili** au **haya**.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 63 na 64 **Mnyama nimpendaye 2**

**Kipindi 63**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng'** **nd**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ng'a** **ng'e** **ng'i** **ng'o** **ng'u**

- Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng'o mbe | ng'o a | se ng'e nge | ng'a mbo |
| **ng'ombe** | **ng'oa** | **seng'enge** | **ng'ambo** |

**Kipindi 64**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG'** **ng'** **ND** **nd**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a li ji unga | wa li shangazwa | hu ng'ang'ania |
| **alijiunga** | **walishangazwa** | **hung'ang'ania** |

**Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Tunga sentensi ukitumia **hili** au **haya** pamoja na maneno yafuatayo:

1. Machungwa
2. Jino
3. Mambo
4. Jani
5. Majangwa
6. Ndizi
7. Mapaipai

63

Hakiuzwi

Kipindi cha 63 na 64 **Mnyama nimpendaye 2**

**Kusoma hadithi**




**Maonyesho ya mifugo**

Wafula alikuwa mkulima hodari. Aliishi peke yake ng'ambo ya mto. Jambo hili lilimfurahisha. Alifuga mifugo wengi kama ng'ombe, sungura, kondoo, punda na nguruwe. Siku moja alialikwa kuhudhuria maonyesho ya kilimo. Maonyesho hayo yalifanyika mjini. Alivaa nguo nyeupe pe pe pe zilizong'ara. Alipofika mtoni, aling'oa kijiti ili apime kina cha maji. Hii ni kabla ya kuvuka mto. Alipovuka mto, alijiunga na wakulima wengine kujifunza mbinu mpya za ukulima. Baadaye alinunua seng'enge na bidhaa mbalimbali za ukulima. Alielekea kwake nyumbani Kijijini Mbeya.

Mali ya Serikali ya Kenya 64

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NG', ng', ND, nd

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 63.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** ya ka ongezeka – yakaongezeka

**U:** Endelea na maneno; alijiunga, walishangazwa.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 63.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **ng'ombe, sungura, nguruwe.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya 'hili' na 'haya'**

**N:** Fafanua maana na matumizi ya 'hili' na 'haya'.

'Hili' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kilicho karibu cha neno linaloanza na 'ma' katika wingi. Kwa mfano: Jiwe hili. Embe hili.

'Haya' hutumiwa kuonyesha vitu vilivyo karibu vya majina yanayoanza na 'ma' katika wingi. Kwa mfano: Mawe haya. Maembe haya.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 63.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi nne akitumia maneno yafuatayo:

1. Nguruwe
2. Sungura
3. Farasi

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 65 **Mnyama nimpendaye 2**

**Kipindi 65**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ND nd NG' ng'

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: m bwa – mbwa**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| nda | mbo | nga | o | m |
| mba | ma | bwa | ka | pa |

◆ **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Jaza mapengo ukitumia **hili** au **haya**.

1. Maumbo ____________ yanapendeza.
2. Shamba ____________ limelimwa.
3. Tunda ____________ limeiva.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Kikao cha wanyama**



**Kuandika**

Andika majina ya wanyama wanaofugwa nyumbani.

65 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ND, nd, NG', ng'

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 65.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'mbwa'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza maneno mapya: **punda, mbwa, ngamia.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Kikao cha wanyama**

Katika kijiji cha Senende kuliishi makundi mawili ya wanyama. Kulikuwa na wanyama wa nyumbani na wa porini. Kila mara wanyama hawa walilalamika kutokana na dhuluma za wanakijiji. Wanakijiji walikata miti ovyo ovyo na kuchoma makaa. Kulikuwa na kiangazi kilichosababisha ukosefu wa maji na nyasi kwa muda mrefu. Wanyama wengi wakafariki.

Siku moja mkutano wa kuwachagua viongozi uliitishwa. Kundi la wanyama wa nyumbani liliwakilishwa na ng'ombe, punda, ngamia na mbwa. Huku wanyama wa porini wakiwakilishwa na ndovu, nyati, sungura na kiboko. Wanyama walijadiliana huhusu majukumu ya viongozi. Sungura akasema, "Mimi namchagua ndovu akisaidiwa na ng'ombe, ndovu akiongea wanakijiji watamsikiliza kwa kuwa yeye ni mkubwa." Kila mnyama alikubaliana na sungura.

Ngamia naye akasema, "Ninakubaliana na sungura, ng'ombe ana uwezo wa kutetea na kuhakikisha kuwa tunapewa ulinzi wa kutosha na wanakijiji kwa sababu anapendwa sana." Ndovu na ng'ombe wakapewa majukumu ya kuhakikisha kuwa, wanakijiji hawakati miti ovyoovyo na miti itapandwa ili kuzuia kiangazi siku zijazo.

## Maswali

**N:** Taja wanyama wawili wa nyumbani waliotajwa kwenye hadithi. *(Ng'ombe, punda, ngamia na mbwa.)*

**T:** Ndovu na Ng'ombe walipewa majukumu gani? *(Ndovu na ng'ombe walipewa majukumu ya kuhakikisha kuwa, wanakijiji hawakati miti ovyoovyo na miti itapandwa ili kuzuia kiangazi siku zijayo.)*

**U:** Ni mnyama yupi unayempenda? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Kuandika

**N:** Andika jina la mnyama: ng'ombe

**U:** Mwanafunzi waandike majina matano ya wanyama wanaofugwa nyumbani.

## Sarufi

**Matumizi ya 'hili' na 'haya'**

Fafanua maana na matumizi ya 'hili' na 'haya'.

'Hili' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kilicho karibu cha neno linaloanza na 'ma' katika wingi. Kwa mfano: Chungwa hili.

'Haya' hutumiwa kuonyesha vitu vilivyo karibu vya majina yanayoanza na 'ma' katika wingi. Kwa mfano: Machungwa haya.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 65.**

**Majibu ya sarufi**

1. haya 2. hili 3. hili

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi nne akitumia 'haya'.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 66: Shuleni 2

Kipindi cha | 66 na 67 | **Shuleni 2**

**Kipindi 66**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**g** **th**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ga** **ge** **gi** **go** **gu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ga ri | i gi za | ku ga wa | ma ga i di |
|---|---|---|---|
| **gari** | **igiza** | **kugawa** | **magaidi** |

**Kipindi 67**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**G** **g** **TH** **th**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| ku igiza | tu li agiza | ku egesha | ni li gutuka |
|---|---|---|---|
| **kuigiza** | **tuliagiza** | **kuegesha** | **niligutuka** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma vifungu hivi.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Wimbo **wako** | Nyimbo **zenu** |
| 2. | Soksi **zako** | Soksi **zenu** |
| 3. | Mkoba **wako** | Mikoba **yenu** |
| 4. | Gari **lako** | Magari **yenu** |
| 5. | Shule **yako** | Shule **zenu** |

Mali ya Serikali ya Kenya

66

Kipindi cha | 66 na 67 | **Shuleni 2**

**Kusoma hadithi**



**Linda**

Linda ni msichana nadhifu. Yeye husoma katika shule ya msingi ya Gelani. Kila asubuhi Linda huvalia sare yake ya shule. Kila Jumatatu na Ijumaa Linda na wanafunzi wenzake huenda kwenye gwaride. Bendera hupandishwa na wimbo wa taifa kuimbwa. Shule yao ina uwanja mkubwa wa kuegesha magari thelathini na tisa. Pia, ina madarasa mengi. Kila Ijumaa alasiri watoto huwa na kipindi cha kuigiza mashairi.

"Sauti yako inapendeza," mwalimu humwambia Linda. Mwaka uliopita, Gelani ilikuwa shule bora kati ya shule ishirini katika mashindano ya muziki na kuigiza. "Nimefurahia kazi yenu sana," mkuu wa shule aliwaambia wanafunzi.

67

Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/g/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti katikati mwa neno. Mwanafunzi aonyeshe kidole chini asiposikia sauti katikati mwa neno.

**N/T/U:** kuigiza, gari

**U:** Endelea na maneno; kugawa, magadi, gwaride, magaidi.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** g, th

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 66.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /g / a/ silabi ni ga

**U:** Endelea na silabi ge, gi, go, gu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 66.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: gu m zo – gumzo

**U:** Endelea na maneno; gari, igiza, kugawa.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 66.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **gwaride, bendera, thelathini na tisa.** Tumia chati kurejelea tarakimu 11-50.

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 67.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U**: Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Linda alisoma shule gani? *(Alisoma katika shule ya msingi ya Gelani.)*

**T:** Kila ijumaa alasiri wanafunzi huwa na kipindi gani? *(Kipindi cha kuigiza mashairi.)*

**U:** Shuleni kwenu nyinyi hufanya nini Ijumaa na Jumatatu asubuhi? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike tarakimu hizi kwa nambari.

1. Kumi na moja
2. Ishirini
3. Thelathini na nne
4. Hamsini

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore vitu vitatu vinavyopatikana shuleni na aandike majina yake.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 67: Shuleni 2

Kipindi cha 66 na 67 **Shuleni 2**

**Kipindi 66**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**g** **th**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ga** **ge** **gi** **go** **gu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ga ri | i gi za | ku ga wa | ma ga i di |
|---|---|---|---|
| **gari** | **igiza** | **kugawa** | **magaidi** |

**Kipindi 67**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**G** **g** **TH** **th**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| ku igiza | tu li agiza | ku egesha | ni li gutuka |
|---|---|---|---|
| **kuigiza** | **tuliagiza** | **kuegesha** | **niligutuka** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma vifungu hivi.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Wimbo **wako** | Nyimbo **zenu** |
| 2. | Soksi **zako** | Soksi **zenu** |
| 3. | Mkoba **wako** | Mikoba **yenu** |
| 4. | Gari **lako** | Magari **yenu** |
| 5. | Shule **yako** | Shule **zenu** |

Mali ya Serikali ya Kenya

66

Kipindi cha 66 na 67 **Shuleni 2**

**Kusoma hadithi**



**Linda**

Linda ni msichana nadhifu. Yeye husoma katika shule ya msingi ya Gelani. Kila asubuhi Linda huvalia sare yake ya shule. Kila Jumatatu na Ijumaa Linda na wanafunzi wenzake huenda kwenye gwaride. Bendera hupandishwa na wimbo wa taifa kuimbwa. Shule yao ina uwanja mkubwa wa kuegesha magari thelathini na tisa. Pia, ina madarasa mengi. Kila Ijumaa alasiri watoto huwa na kipindi cha kuigiza mashairi.

"Sauti yako inapendeza," mwalimu humwambia Linda. Mwaka uliopita, Gelani ilikuwa shule bora kati ya shule ishirini katika mashindano ya muziki na kuigiza. "Nimefurahia kazi yenu sana," mkuu wa shule aliwaambia wanafunzi.

67

Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** G, g, TH, th

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 66.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** ku igiza – kuigiza

**U:** Endelea na maneno; tuliagiza, kuegesha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 66.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **gwaride, bendera, thelathini na tisa.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya -ako na -enu**

**N:** Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano: Kitabu chako kimepotea. '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano: Vitabu vyenu vimepotea.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 66.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atumie '–ako' au '–enu' kujaza mapengo yaliyoachwa.

1. Kitabu ______ kilipotea. (chako)
2. Madawati _____ yamevunjika. (yenu)
3. Kalamu _____ ni mzuri. (yako)

Tarehe: ____________________________ Muda: ___________________ Idadi: __________________

Kipindi cha 68 na 69 **Shuleni 2**

**Kipindi 68**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**d** **g**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**da** **de** **di** **do** **du**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| da ra sa | gwa ri de | mu da | shi da |
|---|---|---|---|
| **darasa** | **gwaride** | **muda** | **shida** |

**Kipindi 69**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**D** **G**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| i li po wadia | a li m dunisha | ku dondoka |
|---|---|---|
| **ilipowadia** | **alimdunisha** | **kudondoka** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Nakili sentensi zifuatazo.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mlingoti **wako** ni mrefu. | Milingoti **yenu** ni mirefu. |
| 2. | Meza **yako** imezeeka. | Meza **zenu** zimezeeka. |
| 3. | Kengele **yako** ni kubwa. | Kengele **zenu** ni kubwa. |
| 4. | Kitabu **chako** ni kizuri. | Vitabu **vyenu** ni vizuri. |
| 5. | Dawati **lako** limevunjika. | Madawati **yenu** yamevunjika. |

Mali ya Serikali ya Kenya 68

Kipindi cha 68 na 69 **Shuleni 2**

**Kusoma hadithi**



**Paa la shule yetu**

Kuna shule moja tu kijijini mwetu. Wiki jana, upepo mkali uliharibu paa la darasa letu, ofisi ya mwalimu mkuu na maktaba. Hivi sasa, sote tunasomea kanisani. Shida hii ni ya muda mfupi tu.

Dereva wa mbunge wetu alitumwa alete bahasha ya pesa. "Wazazi wenu watakuja kesho shuleni kuchanga pesa zaidi," dereva huyo alisema. Watanunua vifaa vya kurekebisha paa hilo. Wajenzi kumi na tisa wataitwa na kujenga paa letu kwa masaa ishirini na nne. Kwa sasa tutaendelea kusomea kanisani.

69

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/d/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** darasa, dhahabu

**U:** Endelea na maneno; dhati, debe, mkono, dawati, dhidi.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** d, g

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 68.**

### Kusoma silabi

Tamka sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /d/ / a/ silabi ni da.

**U:** Endelea na silabi de, di, do, du.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 68.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: de re va – dereva

**U:** Endelea na maneno; darasa, gwaride, muda.

Mwanafunzi asome maneno: kwenye **ukurasa wa 68.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **paa, ofisi, kumi na sita.** Tumia chati kufunza tarakimu.

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Upepo mkali uliharibu sehemu gani ya darasa? *(Upepo mkali uliharibu paa la darasa.)*

**T:** Wiki jana kulifanyika nini? *(Wiki jana, upepo mkali uliharibu paa la darasa, ofisi ya mwalimu mkuu na maktaba.)*

**U:** Upepo huleta hasara gani? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike na amsomee mzazi au mlezi wake nambari 11-50.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi tatu akitumia maneno haya kisha asome.

1. Gwaride 2. Sare 3. Bendera

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 69: Shuleni 2

Kipindi cha 68 na 69 **Shuleni 2**

**Kipindi 68**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

d g

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**da de di do du**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| da ra sa | gwa ri de | mu da | shi da |
|---|---|---|---|
| **darasa** | **gwaride** | **muda** | **shida** |

**Kipindi 69**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

D G

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| i li po wadia | a li m dunisha | ku dondoka |
|---|---|---|
| **ilipowadia** | **alimdunisha** | **kudondoka** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Nakili sentensi zifuatazo.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mlingoti **wako** ni mrefu. | Milingoti **yenu** ni mirefu. |
| 2. | Meza **yako** imezeeka. | Meza **zenu** zimezeeka. |
| 3. | Kengele **yako** ni kubwa. | Kengele **zenu** ni kubwa. |
| 4. | Kitabu **chako** ni kizuri. | Vitabu **vyenu** ni vizuri. |
| 5. | Dawati **lako** limevunjika. | Madawati **yenu** yamevunjika. |

Mali ya Serikali ya Kenya

68

Kipindi cha 68 na 69 **Shuleni 2**

**Kusoma hadithi**



**Paa la shule yetu**

Kuna shule moja tu kijijini mwetu. Wiki jana, upepo mkali uliharibu paa la darasa letu, ofisi ya mwalimu mkuu na maktaba. Hivi sasa, sote tunasomea kanisani. Shida hii ni ya muda mfupi tu.

Dereva wa mbunge wetu alitumwa alete bahasha ya pesa. "Wazazi wenu watakuja kesho shuleni kuchanga pesa zaidi," dereva huyo alisema. Watanunua vifaa vya kurekebisha paa hilo. Wajenzi kumi na tisa wataitwa na kujenga paa letu kwa masaa ishirini na nne. Kwa sasa tutaendelea kusomea kanisani.

69 Hakiuzwi

### ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** D, G

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 68.**

### ★ Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** i li badilika – ilibadilika

**U:** Endelea na maneno; ilipowadia, alimdunisha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 68.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **paa, ofisi, kumi na tisa.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### ◆ Sarufi

**Matumizi ya -ako na -enu**

**N:** Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano: Kiti chako kimevunjika. '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano: Viti vyenu vimevunjika.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 68.**

### Kazi ya ziada

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. Bendera
2. Shuleni
3. Maktaba

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

# Kipindi cha 70: Shuleni 2

Kipindi cha 70 **Shuleni 2**

**Kipindi 70**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

G g D d

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: da wa ti – dawati**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| wa | m | ma | fu | ti |
| nzi | ba | da | na | ko |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Jaza mapengo ukitumia **-ako** na **-enu**.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Bustani ______ ni kubwa. | Bustani ______ ni kubwa. |
| 2. | Chati ______ imeanguka. | Chati ______ zimeanguka. |
| 3. | Picha ______ ni nzuri. | Picha ______ ni nzuri. |

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Shule ya Kileleni**



**Kuandika**

Jaza mapengo haya.

1. Jina la shule yako ni ________.
2. Darasani mwako kuna ________, ______ na ________.

Mali ya Serikali ya Kenya 70

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** G, g, D, d

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 70.**

## ★ Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'dawati'.

**U:** Wanafunzi waunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **bendera, ofisi, maktaba.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Shule ya Kileleni**

Likizo ya Krisimasi iliisha haraka bila ya kutarajiwa. Wanafunzi pamoja na wazazi walijitayarisha kwa muhula wa kwanza. Ilikuwa furaha tele kwa Nabele kwa sababu angejiunga na shule mpya. Jumapili jioni Nabele alimkumbusha mama yake.

"Habari ya jioni mama, kesho shule zinafunguliwa." Mama yake akamjibu, "Asante sana kwa kunikumbusha, nitakupeleka kesho asubuhi."

Asubuhi ilipofika Nabele na mama yake waliandamana kwenda shuleni. Shuleni bendera ilipepea kwenye mlingoti nje ya ofisi ya shule. Madarasa yalikuwa yamepambwa kwa michoro maalum. Shule hii ilikuwa na ofisi ya mwalimu mkuu lakini haikuwa na ofisi ya naibu wake. Wazazi walipokutana, waliamua kuchanga pesa ili wajenge ofisi hiyo.

Shule hii ilikuwa na maktaba iliyokuwa na vitabu vingi. Pia kulikuwa na televisheni, redio na kamera. Kando ya gwaride, kulikuwa na bustani yenye maua ya kupendeza. Vyoo vya wavulana na wasichana vilikuwa safi. Lo! Sijaiona shule nyingine kama Kileleni. Naipenda shule yangu. Je, wewe?

## ? Maswali

**N:** Taja ofisi inayopatikana katika shule ya Kileleni kama ilivyotajwa katika hadithi. *(Ilikuwa na ofisi ya mwalimu mkuu)*

**T:** Je, unadhani kuna umuhimu gani wa vyoo shuleni kuwa safi kila wakati? *(Kubali jibu sahihi)*

**U:** Taja vitu mbalimbali vinavyopatikana katika maktaba ya shule ya Kileleni. *(Vitabu vingi, televisheni, redio na kamera)*

## Kuandika

Mwanafunzi ajaze mapengo kwa jibu sahihi kwenye **ukurasa wa 70.**

**Majibu**

1. Mwanafunzi aandike jina la shule.
2. Mwanafunzi aandike vifaa vya darasani.

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya -ako na -enu**

**N:** Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano: Kalamu yako ni nzuri. '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano: Kalamu zenu ni nzuri.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 70.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi amwelezee mlezi wake kuhusu shule yake kisha achore picha ya shule yake.

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi ajiunge katika kikundi asafishe madarasa shuleni.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 71: Shuleni 2

Kipindi cha 71 na 72 **Shuleni 2**

**Kipindi 71**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

j d

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ja je ji jo ju

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| je nga | ju a | ki ji ji | ja ri da |
|---|---|---|---|
| **jenga** | **jua** | **kijiji** | **jarida** |

**Kipindi 72**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

J j

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| tu li yo i ngojea | ki li anza | i ka ji kaza |
|---|---|---|
| **tuliyoingojea** | **kilianza** | **ikajikaza** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma vifungu hivi.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Kiranja **wako** | Viranja **wenu** |
| 2. | Fulana **yako** | Fulana **zenu** |
| 3. | Mzazi **wako** | Wazazi **wenu** |
| 4. | Mwalimu **wako** | Walimu **wenu** |
| 5. | Kiti **chako** | Viti **vyenu** |

71 Hakiuzwi

Kipindi cha 71 na 72 **Shuleni 2**

**Kusoma hadithi**



**Siku ya michezo**

Siku tuliyoingojea hatimaye ilifika. Walimu walihakikisha kila mmoja alikuwa ameketi sehemu yake. Ilikuwa ni fainali ya mchezo wa kandanda. Ilikuwa kandanda baina ya timu yetu Simba na ya shule jirani Ndovu. Kabla ya mwamuzi kupuliza kipenga alisema, "Tafadhali pangeni foleni na kusalimiana ili mchezo uanze."

"Mchezo wenu utakuwa wa kuvutia," Mwanafunzi mmoja alisema. Mwenzake alijibu, "Asante." Mchezaji wetu hodari aliitwa Wanyama. Kabla ya kipindi cha mapumziko, mchezaji Wanyama alifunga bao la kwanza. Tulisherehekea kwa furaha.

Kipindi cha pili kilianza. Lo! Ndovu wakapata bao lao. Timu yetu ilijikaza. Muda si muda, Wanyama alifunga bao la pili. Sherehe zilianza. Mwamuzi alipuliza kipenga cha kumaliza mchezo. Timu yetu Simba ilishinda. Wanyama alituzwa kama mchezaji bora. "Ushindi wako ni ushindi wetu," sote tulikubaliana.

Mali ya Serikali ya Kenya 72

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/j/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** /j/, jarida, machungwa

**U:** Endelea na maneno; jani, chama, darasa, jua.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** j, d

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 71**.

### Kusoma silabi

Tamka sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /j/ /a/ silabi ni ja.

**U:** Endelea na silabi je, ji, jo, ju.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 71.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: je mbe – jembe

**U:** Endelea na maneno; jenga, jua, jarida.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 71.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **tafadhali, asante, alituzwa.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 72.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kabla ya mchezo kuanza, walimu walihakikisha nini kimefanyika? *(Walimu walihakikisha kila mmoja alikuwa ameketi sehemu yake.)*

**T:** Ilikuwa ni fainali ya mchezo gani? *(Ilikuwa ni fainali ya mchezo wa kandanda.)*

**U:** Unafikiri mchezaji Wanyama alituzwa zawadi gani? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 71 na 72 **Shuleni 2**

**Kipindi 71**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  j   d

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  ja   je   ji   jo   ju

- ★ Soma maneno ukitumia silabi.

| je nga | ju a | ki ji ji | ja ri da |
|---|---|---|---|
| **jenga** | **jua** | **kijiji** | **jarida** |

**Kipindi 72**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  J   j

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| tu li yo i ngojea | ki li anza | i ka ji kaza |
|---|---|---|
| **tuliyoingojea** | **kilianza** | **ikajikaza** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma vifungu hivi.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Kiranja **wako** | Viranja **wenu** |
| 2. | Fulana **yako** | Fulana **zenu** |
| 3. | Mzazi **wako** | Wazazi **wenu** |
| 4. | Mwalimu **wako** | Walimu **wenu** |
| 5. | Kiti **chako** | Viti **vyenu** |

71

Hakiuzwi

Kipindi cha 71 na 72 **Shuleni 2**

**Kusoma hadithi**



**Siku ya michezo**

Siku tuliyoingojea hatimaye ilifika. Walimu walihakikisha kila mmoja alikuwa ameketi sehemu yake. Ilikuwa ni fainali ya mchezo wa kandanda. Ilikuwa kandanda baina ya timu yetu Simba na ya shule jirani Ndovu. Kabla ya mwamuzi kupuliza kipenga alisema, "Tafadhali pangeni foleni na kusalimiana ili mchezo uanze."

"Mchezo wenu utakuwa wa kuvutia," Mwanafunzi mmoja alisema. Mwenzake alijibu, "Asante." Mchezaji wetu hodari aliitwa Wanyama. Kabla ya kipindi cha mapumziko, mchezaji Wanyama alifunga bao la kwanza. Tulisherehekea kwa furaha.

Kipindi cha pili kilianza. Lo! Ndovu wakapata bao lao. Timu yetu ilijikaza. Muda si muda, Wanyama alifunga bao la pili. Sherehe zilianza. Mwamuzi alipuliza kipenga cha kumaliza mchezo. Timu yetu Simba ilishinda. Wanyama alituzwa kama mchezaji bora. "Ushindi wako ni ushindi wetu," sote tulikubaliana.

Mali ya Serikali ya Kenya

72

Mwalimu arekodi kwa kutumia kifaa cha kidijitali mazungumzo haya na kuwachezea wanafunzi darasani.

Wanafunzi wasikilize na kuandika maneno ya maamkuzi watakayoyasikia (hujambo - sijambo, habari - njema).

**Mwalimu:** Hujambo.

**Mwanafunzi:** Sijambo mwalimu.

**Mwalimu:** Habari ya asubuhi.

**Mwanafunzi:** Njema mwalimu.

**Mwanafunzi:** Tafadhali naomba ruhusa niende haja.

**Mwalimu:** Sawa, kimbia urudi darasani.

**Mwanafunzi:** Asante mwalimu.

### Kazi ya ziada

Tumia '–ako' au '–enu' kujaza mapengo.

| | –ako | –enu |
|---|---|---|
| 1. | Mwalimu _______ | Walimu wenu (wako) |
| 2. | Kiatu chako | Viatu _______ (vyenu) |
| 3. | Dawati _______ | Madawati yenu (lako) |

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

# Kipindi cha 72: Shuleni 2

Kipindi cha 71 na 72 **Shuleni 2**

**Kipindi 71**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

j d

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ja je ji jo ju**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| je nga | ju a | ki ji ji | ja ri da |
|---|---|---|---|
| **jenga** | **jua** | **kijiji** | **jarida** |

**Kipindi 72**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

J j

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| tu li yo i ngojea | ki li anza | i ka ji kaza |
|---|---|---|
| **tuliyoingojea** | **kilianza** | **ikajikaza** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma vifungu hivi.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Kiranja **wako** | Viranja **wenu** |
| 2. | Fulana **yako** | Fulana **zenu** |
| 3. | Mzazi **wako** | Wazazi **wenu** |
| 4. | Mwalimu **wako** | Walimu **wenu** |
| 5. | Kiti **chako** | Viti **vyenu** |

71 Hakiuzwi

Kipindi cha 71 na 72 **Shuleni 2**

**Kusoma hadithi**



**Siku ya michezo**

Siku tuliyoingojea hatimaye ilifika. Walimu walihakikisha kila mmoja alikuwa ameketi sehemu yake. Ilikuwa ni fainali ya mchezo wa kandanda. Ilikuwa kandanda baina ya timu yetu Simba na ya shule jirani Ndovu. Kabla ya mwamuzi kupuliza kipenga alisema, "Tafadhali pangeni foleni na kusalimiana ili mchezo uanze."

"Mchezo wenu utakuwa wa kuvutia," Mwanafunzi mmoja alisema. Mwenzake alijibu, "Asante." Mchezaji wetu hodari aliitwa Wanyama. Kabla ya kipindi cha mapumziko, mchezaji Wanyama alifunga bao la kwanza. Tulisherehekea kwa furaha.

Kipindi cha pili kilianza. Lo! Ndovu wakapata bao lao. Timu yetu ilijikaza. Muda si muda, Wanyama alifunga bao la pili. Sherehe zilianza. Mwamuzi alipuliza kipenga cha kumaliza mchezo. Timu yetu Simba ilishinda. Wanyama alituzwa kama mchezaji bora. "Ushindi wako ni ushindi wetu," sote tulikubaliana.

Mali ya Serikali ya Kenya 72

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** J, j

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 71.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** wa li kuja – walikuja

**U:** Endelea na maneno; tuliyoingojea, kilianza.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 71.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **tafadhali, asante, alituzwa.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya -ako na -enu**

**N:** Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano: Tunda lako limeiva. '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano: Matunda yenu yameiva.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 71.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunz atunge sentensi nne akitumia '-ako' na '-enu'.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

# Kipindi cha 73: Shuleni 2

Kipindi cha 73 na 74 **Shuleni 2**

**Kipindi 73**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**r** **j**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ra** **re** **ri** **ro** **ru**

- Soma maneno ukitumia silabi.

| na mba ri | ra fi ki | nu ru | ja ri da |
|---|---|---|---|
| **nambari** | **rafiki** | **nuru** | **jarida** |

**Kipindi 74**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**R** **r**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| ku tu arifu | a ta ka po rudi | ku chora |
|---|---|---|
| **kutuarifu** | **atakaporudi** | **kuchora** |

**Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Soma sentensi zifuatazo.

| | Umoja hili | Wingi haya |
|---|---|---|
| 1. | Dirisha **hili** ni dogo. | Madirisha **haya** ni madogo. |
| 2. | Jiwe **hili** ni kubwa. | Mawe **haya** ni makubwa. |
| 3. | Jicho **hili** linaona mbali. | Macho **haya** yanaona mbali. |
| 4. | Jino **hili** linauma. | Meno **haya** yanauma. |
| 5. | Tunda **hili** ni tamu. | Matunda **haya** ni matamu. |

73

Kipindi cha 73 na 74 **Shuleni 2**

**Kusoma hadithi**



**Nyota ya Amina**

Kengele ya kwanza ilipolia, sote tulielekea gwarideni. Tukasimama wima na kutulia tuli. Wimbo wa taifa ukaimbwa. Mwalimu Roda alisimama na kutuombea. Mwalimu mkuu, Bi. Faraja alikuja na kutuarifu kuwa kiranja wetu Amina amekuwa mgonjwa na hangefika shuleni. Aliendelea, "Hivyo basi, Muchiri atakuwa kiranja wenu hadi Amina atakaporudi." Muchiri alipewa nafasi azungumze. Akasema, "Asante mwalimu kwa kunichagua kuwa kiranja. Mwambie Amina pole."

Amina alikuwa mwenye bidii masomoni. Pia, alikuwa na talanta ya kuchora. Aliitumia talanta hiyo kuchora picha na chati darasani. Kuwa mgonjwa kwake kukawa pigo. Kila mwanafunzi alimwombea Amina apone haraka. Tuliondoka na kwenda darasani kusoma.

Mali ya Serikali ya Kenya 74

## Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/r/**. Tamka maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** /r/, rangi, ganda.

**U:** Endelea na maneno; rafiki, nuru, radi, kazi.

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** r, j

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 73.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /r/ /a/ silabi ni ra.

**U:** Endelea na silabi re, ri, ro, ru.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 73.**

## Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: go do ro – godoro

**U:** Endelea na maneno; nambari, rafiki, nuru.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 73.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kutuarifu, chati, talanta.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi.

## Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Kengele ya kwanza ilipolia wanafunzi walielekea wapi? *(Kengele ya kwanza ilipolia wanafunzi walielekea gwaride)*

**T:** Mwalimu gani aliomba. *(Mwalimu Roda)*

**U:** Je, wewe una talanta gani? *(Kubali jibu sahihi kwa mfano kuimba.)*

## Zoezi

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 73: Shuleni 2

Kipindi cha 73 na 74 — **Shuleni 2**

**Kipindi 73**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**r** **j**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ra** **re** **ri** **ro** **ru**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| na mba ri | ra fi ki | nu ru | ja ri da |
|---|---|---|---|
| **nambari** | **rafiki** | **nuru** | **jarida** |

**Kipindi 74**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**R** **r**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| ku tu arifu | a ta ka po rudi | ku chora |
|---|---|---|
| **kutuarifu** | **atakaporudi** | **kuchora** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Soma sentensi zifuatazo.

| | Umoja hili | Wingi haya |
|---|---|---|
| 1. | Dirisha **hili** ni dogo. | Madirisha **haya** ni madogo. |
| 2. | Jiwe **hili** ni kubwa. | Mawe **haya** ni makubwa. |
| 3. | Jicho **hili** linaona mbali. | Macho **haya** yanaona mbali. |
| 4. | Jino **hili** linauma. | Meno **haya** yanauma. |
| 5. | Tunda **hili** ni tamu. | Matunda **haya** ni matamu. |

73

Hak uzwi

Kipindi cha 73 na 74 — **Shuleni 2**

**Kusoma hadithi**



**Nyota ya Amina**

Kengele ya kwanza ilipolia, sote tulielekea gwarideni. Tukasimama wima na kutulia tuli. Wimbo wa taifa ukaimbwa. Mwalimu Roda alisimama na kutuombea. Mwalimu mkuu, Bi. Faraja alikuja na kutuarifu kuwa kiranja wetu Amina amekuwa mgonjwa na hangefika shuleni. Aliendelea, "Hivyo basi, Muchiri atakuwa kiranja wenu hadi Amina atakaporudi." Muchiri alipewa nafasi azungumze. Akasema, "Asante mwalimu kwa kunichagua kuwa kiranja. Mwambie Amina pole."

Amina alikuwa mwenye bidii masomoni. Pia, alikuwa na talanta ya kuchora. Aliitumia talanta hiyo kuchora picha na chati darasani. Kuwa mgonjwa kwake kukawa pigo. Kila mwanafunzi alimwombea Amina apone haraka. Tuliondoka na kwenda darasani kusoma.

Mali ya Serikali ya Kenya

74

Rekodi mazungumzo yafuatayo kwa kutumia kifaa cha kidijitali na kuwachezea wanafunzi darasani. Waelekeze wanafunzi kuigiza maamkuzi haya katika vikundi vya wanafunzi watatu huku wakijirekodi.

**Mwalimu Mkuu:** Habari za mchana mzazi.

**Mzazi:** Njema, mwalimu mkuu nashukuru.

**Mwalimu Mkuu:** Karibu ofisini, nikusaidie vipi?

**Mzazi:** Asante, naomba kumwona mwalimu wa darasa la pili.

**Mwalimu Mkuu:** Subiri kidogo, nimwite.

**Mzazi:** Asante.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike majibu ya salamu hizi.

1. Hujambo ____________
2. Habari ya asubuhi ____________
3. Habari ya jioni ____________

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Hakiuzwi

Kipindi cha 73 na 74 **Shuleni 2**

**Kipindi 73**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  r j

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  ra re ri ro ru

- Soma maneno ukitumia silabi.

| na mba ri | ra fi ki | nu ru | ja ri da |
|---|---|---|---|
| **nambari** | **rafiki** | **nuru** | **jarida** |

**Kipindi 74**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  R r

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| ku tu arifu | a ta ka po rudi | ku chora |
|---|---|---|
| **kutuarifu** | **atakaporudi** | **kuchora** |

**Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Soma sentensi zifuatazo.

| | Umoja hili | Wingi haya |
|---|---|---|
| 1. | Dirisha **hili** ni dogo. | Madirisha **haya** ni madogo. |
| 2. | Jiwe **hili** ni kubwa. | Mawe **haya** ni makubwa. |
| 3. | Jicho **hili** linaona mbali. | Macho **haya** yanaona mbali. |
| 4. | Jino **hili** linauma. | Meno **haya** yanauma. |
| 5. | Tunda **hili** ni tamu. | Matunda **haya** ni matamu. |

73 Hak uzwi

Kipindi cha 73 na 74 **Shuleni 2**

**Kusoma hadithi**



**Nyota ya Amina**

Kengele ya kwanza ilipolia, sote tulielekea gwarideni. Tukasimama wima na kutulia tuli. Wimbo wa taifa ukaimbwa. Mwalimu Roda alisimama na kutuombea. Mwalimu mkuu, Bi. Faraja alikuja na kutuarifu kuwa kiranja wetu Amina amekuwa mgonjwa na hangefika shuleni. Aliendelea, "Hivyo basi, Muchiri atakuwa kiranja wenu hadi Amina atakaporudi." Muchiri alipewa nafasi azungumze. Akasema, "Asante mwalimu kwa kunichagua kuwa kiranja. Mwambie Amina pole."

Amina alikuwa mwenye bidii masomoni. Pia, alikuwa na talanta ya kuchora. Aliitumia talanta hiyo kuchora picha na chati darasani. Kuwa mgonjwa kwake kukawa pigo. Kila mwanafunzi alimwombea Amina apone haraka. Tuliondoka na kwenda darasani kusoma.

Mali ya Serikali ya Kenya 74

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** R, r

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 73.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** tu li m karibisha – tulimkaribisha

**U:** Endelea na maneno; kutuarifu, atakaporudi.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 73.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **kutuarifu, talanta, chati.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya '-ako' na '-enu'**

**N:** Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano: Cheti chako kimepatikana. '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano: Vyeti vyenu vimepatikana.

**T:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 73.**


## Kazi ya ziada

Mwanafunzi apige mstari neno la heshima katika sentensi.

1. Tafadhali naomba unisaidie na kalamu.
2. Asante mwalimu kwa kutufunza.
3. Karibu tena darasani mwetu.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 75: Shuleni 2



Kipindi cha 75 Shuleni 2

Kipindi 75

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

J j R r

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ta la nta – talanta**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ku | ra | cho | ta | ki |
| nja | la | ja | nta | a |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Jaza mapengo ukitumia **-ako** na **-enu**.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Jarida ________ linapendeza. | Majarida _______ yanapendeza. |
| 2. | Kifutio _____ ni kikubwa. | Vifutio ______ ni vikubwa. |
| 3. | Maandishi _______ yanaonekana. | Maandishi _______ yanaonekana. |

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Matokeo ya muhula**

**Kuandika**

Andika sentensi mbili ukitumia neno kiranja.

75

Hakiuzwi

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** J, j, R, r

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 75.**

## ★ Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'talanta'.

**U:** Wanafunzi waunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **mapya, kengele, gwaride.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi huku wanafunzi wakisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Matokeo ya muhula**

Ijumaa ilikuwa siku ya wazazi shuleni. Wazazi wote walikuja kuwachukua watoto wao. "Nendeni pale kwenye uwanja mwangalie wazazi wenu," alisema Bi. Shina. Wanafunzi wote wa darasa la pili walitoka mbio kwa furaha. Pale uwanjani kila mwanafunzi alimpata mzazi wake isipokuwa Asha. Asha alirudi darasani akilia.

"Asha mbona unalia?" Bi. Shina aliuliza. "Sijamwona baba," akajibu Asha. "Pole, bado yuko njiani anakuja," akamjibu Bi. Shina.

Baada ya muda mfupi kengele ililia. Kila mwanafunzi alikimbia kwenda kwenye gwaride. Mwalimu mkuu aliwaambia kuwa madarasa yote yatapakwa rangi. Wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili wangepewa madawati mapya na vitabu.

"Sasa mtarudi darasani ili walimu wenu wawape wazazi matokeo yenu," alisema mwalimu mkuu. Kila mwanafunzi aliandamana na mzazi wake na kuelekea darasani. Asha naye akamkimbilia baba yake kwani alikuwa amefika. "Baba asante kwa kuja," Asha alimwambia. Baba na Asha walielekea darasani kuchukua matokeo, kisha wakaenda nyumbani.

## ? Maswali

**T:** Taja vitu ambavyo darasa la kwanza na la pili wangepewa. *(Madawati mapya na vitabu)*

**U:** Kwa nini Asha alilia? *(Kwa sababu hakumuona baba yake uwanjani)*

**U:** Je, unafikiri matokeo ya Asha yalikuwa vipi? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Kuandika

**N:** Andika sentensi moja ukitumia neno 'kiranja'.

**T:** Mwongoze mwanafunzi kuandika sentensi akitumia neno 'kiranja'.

**U:** Mwanafunzi aandike sentensi mbili akitumia neno 'kiranja'.

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya '-ako' na '-enu'**

**N:** Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano: Mjomba wako ni mzuri. '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano: Wajomba wenu ni wazuri.

## Zoezi

Mwanafunzi ajaze pengo akitumia '-ako' na '-enu'.

**Majibu:**

1. lako, yenu 2. chako, vyenu 3. yako, yenu

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atumie udongo kuunda maumbo ya herufi kubwa **J** na **R**, kisha aandike maumbo ya herufi hizi katika kitabu chake.

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi awahamasishe wengine katika jamii kuhusu umuhimu wa shule.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 76: Haki zangu 2

Kipindi cha 76 na 77 **Haki zangu 2**

**Kipindi 76**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

v f

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ve vi vo vu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| vi le vi le | vi a zi | vi mba | vu mbi |
| **vilevile** | **viazi** | **vimba** | **vumbi** |

**Kipindi 77**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

v f

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| m li poteza | tu li punguza | a li yo panga |
| **mlipoteza** | **tulipunguza** | **aliyopanga** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Jaza nafasi kwa kutumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Inafaa mwanafunzi aandike __________.
2. Juma aliteleza akaanguka __________.
3. Wezi wa mifugo walipigwa __________.
4. Nguo zilikuwa safi kwa sababu ya kuoshwa __________.
5. Gari lilianguka lilipoendeshwa __________.
6. Mumo alipigiwa makofi aliposoma __________.

Mali ya Serikali ya Kenya

76

Kipindi cha 76 na 77 **Haki zangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Mila na tamaduni**

Kila jamii kote duniani ina utamaduni wake. Kuna tamaduni nzuri na potovu. Utamaduni mzuri hujenga na kufaidi jamii na si watu binafsi. Ni vizuri jamii kuwa na tamaduni nzuri. Tamaduni potovu hunyima watoto haki zao. Tamaduni hizi ni kama ajira kwa watoto, ndoa za mapema, wizi wa mifugo na ukeketaji wa wasichana. Tamaduni hizi potovu huathiri jamii vibaya. Ni vizuri viongozi washirikiane na kuelimisha jamii. Wanaoendeleza tamaduni hizi potovu washikwe na kushtakiwa. Watoto wapewe malezi ya kutii na kuheshimu sheria na mali. Jamii na kabila zote zishirikiane kila wakati. Hii italeta maendeleo.

77 Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/v/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** /v/, viatu, tatu

**U:** Endelea na maneno; kumi, viazi, vitu, maembe.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** v, f

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 76.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T:** /v/ / a/ silabi ni va.

**U:** Endelea na silabi ve, vi, vo, vu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 76.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: vi a tu – viatu

**U:** Endelea na maneno; vilevile, viazi, vumbi.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 76.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **ajira, potovu, binafsi.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 77.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kuna aina ngapi ya tamaduni? *(Kuna tamaduni nzuri na potovu.)*

**T:** Taja aina ya tamaduni? *(Ndoa za mapema, wizi wa mifugo na ukeketaji wa wasichana.)*

**U:** Taja mambo mazuri ya kufanya ukiwa nyumbani? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi ajaze herufi sahihi kwenye mapengo. (haki, matibabu, malezi)

1. h_k_  2. m_tib_b_  3. m_l_zi

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi azungumzie tamaduni mbalimbali na mlezi wake. Wanaporejea darasani wajadiliane na wenzao.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 77: Haki zangu 2

Kipindi cha | 76 na 77 | **Haki zangu 2**

**Kipindi 76**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

v f

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ve vi vo vu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| vi le vi le | vi a zi | vi mba | vu mbi |
| **vilevile** | **viazi** | **vimba** | **vumbi** |

**Kipindi 77**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

v f

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| m li poteza | tu li punguza | a li yo panga |
| **mlipoteza** | **tulipunguza** | **aliyopanga** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Jaza nafasi kwa kutumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Inafaa mwanafunzi aandike __________.
2. Juma aliteleza akaanguka __________.
3. Wezi wa mifugo walipigwa __________.
4. Nguo zilikuwa safi kwa sababu ya kuoshwa __________.
5. Gari lilianguka lilipoendeshwa __________.
6. Mumo alipigiwa makofi aliposoma __________.

Mali ya Serikali ya Kenya

76

Kipindi cha | 76 na 77 | **Haki zangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Mila na tamaduni**

Kila jamii kote duniani ina utamaduni wake. Kuna tamaduni nzuri na potovu. Utamaduni mzuri hujenga na kufaidi jamii na si watu binafsi. Ni vizuri jamii kuwa na tamaduni nzuri. Tamaduni potovu hunyima watoto haki zao. Tamaduni hizi ni kama ajira kwa watoto, ndoa za mapema, wizi wa mifugo na ukeketaji wa wasichana. Tamaduni hizi potovu huathiri jamii vibaya. Ni vizuri viongozi washirikiane na kuelimisha jamii. Wanaoendeleza tamaduni hizi potovu washikwe na kushtakiwa. Watoto wapewe malezi ya kutii na kuheshimu sheria na mali. Jamii na kabila zote zishirikiane kila wakati. Hii italeta maendeleo.

77 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** V, F

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 76.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** wa li fedheheka – walifedheheka

**U:** Endelea na maneno; mlipoteza, tulipunguza.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 76.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **potovu, binafsi, ajira.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya vizuri na vibaya**

**N:** 'Vizuri' ni neno linalotumika kumaanisha jambo linapendeza au limefanyika kwa njia inayofurahisha. Kwa mfano: Koki alisoma hadithi vizuri. 'Vibaya' lina maana kuwa jambo halipendezi au linafanyika kwa njia isiyofurahisha. Kwa mfano: Mjomba alikata muwa vibaya.

**T:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 76.**

## Kazi ya ziada

Tunga sentensi sahihi ukitumia maneno haya:

1. Vaa
2. Wivu
3. Vizuri

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 78: Haki zangu 2

Kipindi cha 78 na 79 **Haki zangu 2**

**Kipindi 78**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

v p

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ve vi vo vu pi po pu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| wi vu | ma va zi | na pa ta | vu ma |
|---|---|---|---|
| **wivu** | **mavazi** | **napata** | **vuma** |

**Kipindi 79**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

V v P p

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li vutiwa | tu li vamiwa | u li vuta | m li vuvia |
|---|---|---|---|
| **walivutiwa** | **tulivamiwa** | **ulivuta** | **mlivuvia** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Soma sentensi na ujaze mapengo kwa kutumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Watoto wazuri huimba wimbo __________. (vizuri, vibaya)
2. Mwanafunzi aliandika __________ akaadhibiwa. (vibaya, vizuri)
3. Mwalimu alitufundisha haki zetu __________ tukaelewa. (vizuri, vibaya)

Mali ya Serikali ya Kenya 78

Kipindi cha 78 na 79 **Haki zangu 2**

**Kusoma shairi**



**Asante baba na mama**

Namwimbia mama yangu, ninaimba kwa sauti,
Pia wewe baba yangu, kunilea vizuri,
Napata elimu yangu, hata chakula mwanipa vizuri,
Hongera baba na mama, kwa kunipa haki yangu.

Ugonjwa sipati kamwe, napewa lishe bora,
Nakula ndizi na embe, matunda yote ni bora,
Wenye wivu usiwabebe, vibaya usiwatendee,
Hongera baba na mama, kwa kunipa haki yangu.

Mavazi yangu navaa, mazuri yanapendeza,
Ninakushukuru mama, kwa sauti ninasema,
Ahsante baba na mama, haki yangu kuilinda,
Hongera baba na mama, kwa kunipa haki yangu.

79 Hakiuzwi

## Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/p/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** pika, fuata

**U:** Endelea na maneno; paka, familia, pasuka, paulo.

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** p, v

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 78.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /v/ /e/ silabi ni ve

**U:** Endelea na silabi vi, vo, vu, pi, po, pu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 78.**

## Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: pa sa ka – pasaka

**U:** Endelea na maneno; pasaka, vuma, wivu, mavazi.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 78.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno: **haki, mavazi, hongera.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi.

## Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Baba na mama wamempa nini mtoto? *(Wamempa haki yake)*

**T:** Ni matunda gani anapewa mtoto? *(Ndizi na embe)*

**U:** Taja mifano ya haki zako kama mtoto. *(Kubali jibu sahihi kwa mfano, haki ya kusoma)*

## Zoezi

Mwanafunzi ajadili na mwenzake kuhusu haki za watoto.

Mwanafunzi ajadili kuhusu haki za watoto.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno matano yanayoanza kwa herufi **P.**

Tarehe: __________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 79: Haki zangu 2

Kipindi cha 78 na 79 **Haki zangu 2**

**Kipindi 78**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  v p

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  ve vi vo vu pi po pu

- Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| wi vu | ma va zi | na pa ta | vu ma |
| **wivu** | **mavazi** | **napata** | **vuma** |

**Kipindi 79**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  V v P p

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| wa li vutiwa | tu li vamiwa | u li vuta | m li vuvia |
| **walivutiwa** | **tulivamiwa** | **ulivuta** | **mlivuvia** |

**Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Soma sentensi na ujaze mapengo kwa kutumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Watoto wazuri huimba wimbo __________. (vizuri, vibaya)
2. Mwanafunzi aliandika __________ akaadhibiwa. (vibaya, vizuri)
3. Mwalimu alitufundisha haki zetu __________ tukaelewa. (vizuri, vibaya)

Mali ya Serikali ya Kenya

78

Kipindi cha 78 na 79 **Haki zangu 2**

**Kusoma shairi**



**Asante baba na mama**

Namwimbia mama yangu, ninaimba kwa sauti,
Pia wewe baba yangu, kunilea vizuri,
Napata elimu yangu, hata chakula mwanipa vizuri,
Hongera baba na mama, kwa kunipa haki yangu.

Ugonjwa sipati kamwe, napewa lishe bora,
Nakula ndizi na embe, matunda yote ni bora,
Wenye wivu usiwabebe, vibaya usiwatendee,
Hongera baba na mama, kwa kunipa haki yangu.

Mavazi yangu navaa, mazuri yanapendeza,
Ninakushukuru mama, kwa sauti ninasema,
Ahsante baba na mama, haki yangu kuilinda,
Hongera baba na mama, kwa kunipa haki yangu.

79 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** V, v, P, p

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 78.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** wa li po rudi – waliporudi

**U:** Endelea na maneno; walivutiwa, tulivamiwa, mlivuvia.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 78.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **haki, mavazi, hongera.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya vizuri na vibaya**

**N:** 'Vizuri' ni neno linalotumika kumaanisha jambo linapendeza au limefanyika kwa njia inayofurahisha. Kwa mfano: Kano alivalia nguo zake vizuri. 'Vibaya' lina maana kuwa jambo halipendezi au linafanyika kwa njia isiyofurahisha. Kwa mfano: Fundi alijenga nyumba vibaya.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi zenye kutumia vizuri na vibaya kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 78.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi ajadili na mlezi wake kuhusu haki zake na aziandike.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 80 **Haki zangu 2**

**Kipindi 80**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

P p V v

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: va zi - vazi**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ra | li | ngu | ma | bo |
| vu | zi | ji | va | she |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Chagua jibu sahihi kujaza pengo.

1. Mama yangu alinilea __________ nikamshukuru. (vizuri, vibaya)
2. Mtoto aliruka mto _______ akaanguka. (vizuri, vibaya)
3. Mpishi alipika chakula ______ kikaliwa. (vibaya, vizuri)

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Chacha**



**Kuandika**

Andika sentensi mbili ndefu kumhusu baba au mama ambaye ni mlezi wako.

Mali ya Serikali ya Kenya 80

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** P, p, V, v

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 80.**

## ★ Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'vazi'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **kuishi, haki, mavazi.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

**Chacha**

Ilikuwa alasiri, mawingu meusi yalitanda angani. Ngurumo na radi zilisikika kote. Upepo mkali ulianza kuvuma, mvua ikaanza kunyesha kwa wingi. Kando ya hospitali ya Milimani, palikuwa na mvulana mdogo aliyekuwa akinyeshewa sana. Nguo zake zililowa. "Toka hapa, nenda mbali kabisa la sivyo nitakuumiza," alisema mlinzi wa lango la hospitali.

Nilimhurumia mtoto yule alivyoteseka. Aliondoka polepole, akasimama chini ya mti. Nguo zake zilikuwa zimeraruka. Alitembea bila viatu. Alionekana mchovu asiye na afya. Nilipoenda nyumbani, nilimweleza mama yangu kuhusu mvulana huyo. Mama yangu aliamua twende kumchukua mvulana huyo. Mama alimwambia mlinzi, "Sio vyema kufukuza mtoto bila kujua shida yake. Mtoto ana haki ya kuheshimiwa na kuishi vyema." Mvulana alituambia jina lake ni Chacha. Alikuwa na maumivu mengi. Tulimchukua na kumpeleka hospitalini. Baada ya siku tatu alipata nafuu. Tulimleta nyumbani na kumpa mavazi mapya. Mama yangu alitupikia chakula kitamu. Jioni ilipofika, mama yangu alimsindikiza Chacha hadi nyumbani kwao. Wazazi wa Chacha walifurahi kumuona.

## ? Maswali

**T:** Nguo za mvulana zilifanyika nini? *(Nguo zake zililowa)*

**U:** Mama alimwambia mlinzi mtoto ana haki gani? *(Mtoto ana haki ya kuheshimiwa na kuishi vyema.)*

**U:** Taja haki zako. *(Wanafunzi wataje haki zao)*

## Kuandika

**N:** Andika sentensi moja kuhusu baba.

**T:** Mwongoze mwanafunzi kuandika sentesi kuhusu mama.

**U:** Mwanafunzi aandike sentensi mbili kumhusu mlezi wake.

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya vizuri na vibaya**

'Vizuri' ni neno linalotumika kumaanisha jambo linapendeza au limefanyika kwa njia inayofurahisha. Kwa mfano: Kano alivalia nguo zake vizuri. 'Vibaya' lina maana kuwa jambo halipendezi au linafanyika kwa njia isiyofurahisha. Kwa mfano: Fundi alijenga nyumba vibaya.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 80.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi nne kuhusu hadithi ya Chacha aliyosomewa na mwalimu.

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi awahamasishe wenzake kuhusu haki za watoto.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 81: Haki zangu 2

Kipindi cha | 81 na 82 | **Haki zangu 2**

**Kipindi 81**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**p** **d** **g**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**pi** **po** **de** **du** **ga**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ma li po | ku pe wa | da wa ti | tu li fa gi a |
|---|---|---|---|
| **malipo** | **kupewa** | **dawati** | **tulifagia** |

**Kipindi 82**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**P** **p**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li pewa | ku pendeza | ku pewa | a li wa patia |
|---|---|---|---|
| **walipewa** | **kupendeza** | **kupewa** | **aliwapatia** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Andika sentensi hizi kwa hati nadhifu.

1. Wanafunzi wanasoma **vizuri**.
2. Watoto wanacheza **vizuri**.
3. Tafadhali usiandike **vibaya**.
4. Mchezaji alikimbia **vizuri**.
5. Walimu walisomesha **vizuri**.
6. Mwanafunzi aliandika **vibaya**.
7. Kiranja alikusanya vitabu **vizuri**.

81 Hakiuzwi

Kipindi cha | 81 na 82 | **Haki zangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Kijiji cha Namboboto**

Kijiji cha Namboboto kilifahamika sana na wengi kwa kuzingatia maadili mema. Kila mwanakijiji alilinda haki za watoto. Familia nyingi zilihakikisha kuwa watoto wao walipata elimu bora. Zaidi ya hayo, watoto wote walipewa matibabu, mavazi na lishe bora. Pia walilindwa kutokana na tamaduni mbaya. Wote walijua ni vibaya kumtesa mtoto. Ilikuwa jukumu la kila mwanakijiji kuhakikisha kuwa mayatima wanalindwa. Watoto hawa walijengewa nyumba na mahitaji yao yalitimizwa. Kila mara wanakijiji walijitokeza na kukaa na watoto hao bila malipo. Ni vizuri kila mtu alinde haki za watoto.

Mali ya Serikali ya Kenya 82

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/p/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** pahali, mali

**U:** Endelea na maneno; paa, chifu, pepea, fagia, pasi, teseka.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** p, d, g

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 81**.

### Kusoma silabi

Tamka sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /p / /a/ silabi ni pa

**U:** Endelea na silabi; pi, po, de, du, ga.

Mwanafunzi aome silabi kwenye **ukurasa wa 81.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: de be – debe

**U:** Endelea na maneno; malipo, kupewa, dawati.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 81.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **haki, mavazi, matibabu.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 82.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kwa nini kijiji cha Namboboto kilijulikana? *(Kwa sababu kila mwanakijiji alilinda haki za watoto)*

**T:** Familia nyingi zilihakikisha watoto wao wanapata nini? *(Elimu bora, matibabu, mavazi na lishe bora)*

**U:** Je, unadhani ni kwa nini kila mwanakijiji alilinda haki za watoto? *(Kubali jibu sahihi kwa mfano walitaka watoto wapate malezi bora)*

### Zoezi

Mwanafunzi amtungie mwenzake sentensi kwa kutumia vibaya na vizuri. Wanafunzi watunge sentensi.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi amhadithie mlezi wake kuhusu hadithi ya kijiji cha Namboboto.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 81 na 82 **Haki zangu 2**

**Kipindi 81**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **p** **d** **g**
- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  **pi** **po** **de** **du** **ga**
- ★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ma li po | ku pe wa | da wa ti | tu li fa gi a |
|---|---|---|---|
| **malipo** | **kupewa** | **dawati** | **tulifagia** |

**Kipindi 82**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **P** **p**
- Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li pewa | ku pendeza | ku pewa | a li wa patia |
|---|---|---|---|
| **walipewa** | **kupendeza** | **kupewa** | **aliwapatia** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Andika sentensi hizi kwa hati nadhifu.

1. Wanafunzi wanasoma **vizuri**.
2. Watoto wanacheza **vizuri**.
3. Tafadhali usiandike **vibaya**.
4. Mchezaji alikimbia **vizuri**.
5. Walimu walisomesha **vizuri**.
6. Mwanafunzi aliandika **vibaya**.
7. Kiranja alikusanya vitabu **vizuri**.

81 Hakiuzwi

Kipindi cha 81 na 82 **Haki zangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Kijiji cha Namboboto**

Kijiji cha Namboboto kilifahamika sana na wengi kwa kuzingatia maadili mema. Kila mwanakijiji alilinda haki za watoto. Familia nyingi zilihakikisha kuwa watoto wao walipata elimu bora. Zaidi ya hayo, watoto wote walipewa matibabu, mavazi na lishe bora. Pia walilindwa kutokana na tamaduni mbaya. Wote walijua ni vibaya kumtesa mtoto. Ilikuwa jukumu la kila mwanakijiji kuhakikisha kuwa mayatima wanalindwa. Watoto hawa walijengewa nyumba na mahitaji yao yalitimizwa. Kila mara wanakijiji walijitokeza na kukaa na watoto hao bila malipo. Ni vizuri kila mtu alinde haki za watoto.

Mali ya Serikali ya Kenya 82

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** P, p

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 81.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li ponda – aliponda

**U:** Endelea na maneno; walipewa, kupendeza, kupewa.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 81.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **haki, matibabu, mavazi.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya vizuri na vibaya**

**N:** ‘Vizuri’ ni neno linalotumika kumaanisha jambo linapendeza au limefanyika kwa njia inayofurahisha. Kwa mfano: Shangazi alipika vizuri. ‘Vibaya’ lina maana kuwa jambo halipendezi au linafanyika kwa njia isiyofurahisha. Kwa mfano: Kanya alicheza vibaya.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 81.**

Mwanafunzi anakili sentensi katika daftari lake kwa hati nadhifu.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi nne ukitumia maneno haya:

1. Vibaya
2. Vizuri

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 83 na 84 **Haki zangu 2**

**Kipindi 83**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

f r v

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

fi fo fu ro ve

★ Soma maneno ukitumia silabi.

wa li fi ka tu li fa gi a a li fu nza wa li fu ku zwa

**walifika tulifagia alifunza walifukuzwa**

**Kipindi 84**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

F f

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

a li fanya wa li fika a li tu fungulia a li wa fuata

**alifanya walifika alitufungulia aliwafuata**

◆ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Soma sentensi na ujaze mapengo kwa kutumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Sungura alipangusa meza ________ ikachafuka.
2. Paa lilibomoka ________.
3. Mzee yule aliwalea mayatima ________ akatuzwa.
4. Jukwaa lilipambwa ________ likavutia.
5. Daraja lilijengwa ________ likabomoka.
6. Darasa lilioshwa ________ likawa safi.



Kipindi cha 83 na 84 **Haki zangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Mgeni shuleni**

Wazazi na wanafunzi wote walifika shuleni mapema. Tulifagia kila sehemu ya shule. Jukwaa lilipambwa vizuri kwa maua ya kupendeza. Mgeni aliwasili ukumbini. Tulishangilia kwa vifijo na nderemo. Mwalimu mkuu Bwana Mbokoko alimkaribisha mgeni.

Mgeni alisema, "Jina langu ni Bi. Mambo, chifu wa eneo hili. Nitawaeleza kuhusu haki zenu. Kila mtoto ana haki ya kupewa malezi bora na elimu. Watoto pia wana haki ya kutoteswa. Ni vibaya kuwatenga wasio na wazazi. Kwa hivyo, yeyote atakayemnyima mtoto haki yake atashtakiwa mahakamani na kufungwa jela. Asanteni sana. Mola awabariki."



### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/f/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwa neno. Mwanafunzi aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** sifa, fanya

**U:** Endelea na maneno; siafu, panya, fuata, usafi, sifu.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** f, r, v

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 83.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /f/ /a/ silabi ni fa.

**U:** Endelea na silabi; fi, fo, fu, ro, ve.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 83.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T:** fa gi a – fagia

**U:** Endelea na maneno; walifika, tulifagia, alifunza.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 83.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **elimu, kupewa malezi bora na kutoteswa.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 84.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Mwalimu mkuu alimkaribisha nani? *(Mwalimu mkuu alimkaribisha mgeni ambaye alikuwa chifu.)*

**T:** Je, unafikiria mtoto akinyimwa haki zake itakuwaje? *(Kubali jibu sahihi kwa mfano hatokuwa na afya nzuri, hatasoma)*

**U:** Taja haki tatu za watoto zilizotajwa kwenye hadithi? *(Haki ya kupewa malezi bora, elimu na kutoteswa)*

### Zoezi

Mwanafunzi andike maneno atakayosomewa na mwalimu.

1. fulana 2. fafanua 3. fikira

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno haya kitabuni kisha amsomee mlezi wake aendapo nyumbani.

1. Matibabu 2. Kutoteswa 3. Kupewa jina

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 81 na 82 — **Haki zangu 2**

**Kipindi 81**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

p d g

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

pi po de du ga

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ma li po | ku pe wa | da wa ti | tu li fa gi a |
|---|---|---|---|
| **malipo** | **kupewa** | **dawati** | **tulifagia** |

**Kipindi 82**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

P p

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li pewa | ku pendeza | ku pewa | a li wa patia |
|---|---|---|---|
| **walipewa** | **kupendeza** | **kupewa** | **aliwapatia** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**


Andika sentensi hizi kwa hati nadhifu.

1. Wanafunzi wanasoma **vizuri**.
2. Watoto wanacheza **vizuri**.
3. Tafadhali usiandike **vibaya**.
4. Mchezaji alikimbia **vizuri**.
5. Walimu walisomesha **vizuri**.
6. Mwanafunzi aliandika **vibaya**.
7. Kiranja alikusanya vitabu **vizuri**.

81 Hakiuzwi

Kipindi cha 81 na 82 — **Haki zangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Kijiji cha Namboboto**

Kijiji cha Namboboto kilifahamika sana na wengi kwa kuzingatia maadili mema. Kila mwanakijiji alilinda haki za watoto. Familia nyingi zilihakikisha kuwa watoto wao walipata elimu bora. Zaidi ya hayo, watoto wote walipewa matibabu, mavazi na lishe bora. Pia walilindwa kutokana na tamaduni mbaya. Wote walijua ni vibaya kumtesa mtoto. Ilikuwa jukumu la kila mwanakijiji kuhakikisha kuwa mayatima wanalindwa. Watoto hawa walijengewa nyumba na mahitaji yao yalitimizwa. Kila mara wanakijiji walijitokeza na kukaa na watoto hao bila malipo. Ni vizuri kila mtu alinde haki za watoto.

Mali ya Serikali ya Kenya 82

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** F, f

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 83.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li fagia – alifagia

**U:** Endelea na maneno; alifanya, walifika, alitufungulia.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 83.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **haki, matibabu, mavazi.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya vizuri na vibaya**

**N:** 'Vizuri' ni neno linalotumika kumaanisha jambo linapendeza au limefanyika kwa njia inayofurahisha. Kwa mfano: Mchezaji alikimbia vizuri. 'Vibaya' lina maana kuwa jambo halipendezi au linafanyika kwa njia isiyofurahisha. Kwa mfano: Kaka aliandika vibaya.

**T:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 83.**

Mwanafunzi anakili sentensi katika daftari lake kwa hati nadhifu.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno matano yanayoanza kwa herufi **F.**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 85: Haki zangu 2

Kipindi cha 85 **Haki zangu 2**

**Kipindi 85**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

P p F f V v

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ha ki – haki**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ha | va | ma | bu | ba |
| zi | ti | ngu | o | ki |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vizuri na vibaya**

Andika sentensi hizi ukipigia mstari neno **vibaya** au **vizuri**.

1. Mtoto amesoma **vizuri**.
2. Wanafunzi wameanguka **vibaya**.
3. Shangazi amepika **vizuri**.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Kanumba**



**Kuandika**

Andika sentensi fupi kueleza mambo uliyoyasoma kuhusu mgeni shuleni.

85 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** P, p, V, v, F, f

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 85.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na mwanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'haki'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **lishe bora, matibabu.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Kanumba**

Kanumba alifanya kazi katika shamba la majani la Kiboko. Alikuwa na watoto watatu; Mbone, Muchiri na Fatuma. Aliwapa wanawe malezi mema. Alihakikisha kuwa wanawe wanapata kila walichohitaji. Baada ya mwaka mmoja Kanumba alibadilika. Alianza ulevi na kuacha kuijali familia.

Ulevi wa Kanumba ulizidi. Hakujali haki za wanawe za mavazi, elimu, matibabu na lishe bora. Hali hii iliwakasirisha wanawe. Siku moja Mbone aliamua kupiga ripoti kwa chifu. Chifu alimwita Kanumba na kumwonya vikali. Kanumba aliomba msamaha kutoka kwa chifu.

Asubuhi moja chifu alimtembelea Kanumba. Chifu alimweleza kuwa ni muhimu yeye kulinda haki za watoto wake. "Ni haki ya watoto kupata elimu, lishe bora, matibabu, mavazi na kupewa muda wa kucheza. Pia, ni haki yao kuishi katika mazingira yasiyo na unywaji wa pombe au mateso," alielezea chifu.

Kuanzia siku hiyo, Kanumba alibadilika na kuwapa wanawe malezi bora.

## Maswali

**T:** Ni mambo gani Kanumba hakujali? *(Haki za wanawe za elimu, mavazi, lishe bora na matibabu)*

**U:** Je, unafikiri Mbone alifanya vizuri kupiga ripoti kwa chifu? *(Ndio. Waliweza kusaidika kupata haki zao).*

**U:** Chifu alimwambia Kanumba kufanya nini? *(Kulinda haki za watoto wake.)*

## Kuandika

**N: Andika sentensi moja kuhusu hadithi ya 'mgeni shuleni'.**

**T: Waongoze wanafunzi kuandika sentensi kuhusu 'mgeni shuleni'.**

**U: Wanafunzi waandike sentensi mbili kuhusu hadithi ya 'mgeni shuleni'.**

## Sarufi

**Matumizi ya vizuri na vibaya**

**N:** 'Vizuri' ni neno linalotumika kumaanisha jambo linapendeza au limefanyika kwa njia inayofurahisha. Kwa mfano: Watoto wanacheza vizuri. 'Vibaya' lina maana kuwa jambo halipendezi au linafanyika kwa njia isiyofurahisha. Kwa mfano: Tafadhali usiandike vibaya.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 85.**

Mwanafunzi apigie mstari neno sahihi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi ajaze mapengo akitumia vizuri au vibaya.

1. Viti vilivunjika ______________. (vibaya)
2. Mtoto anayelelewa ____________ huwa na heshima. (vizuri)
3. Vitabu vilivyonunuliwa ni ______________. (vizuri)

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 86 na 87 **Usafiri 2**

**Kipindi 86**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ch v

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

chi cho chu vo

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| chu ma | cho me ka | cha fu ka | cho mbo |
| **chuma** | **chomeka** | **chafuka** | **chombo** |

**Kipindi 87**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

CH ch V v

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a li chomeka | tu li chafua | a li chuna | a li chonga |
| **alichomeka** | **tulichafua** | **alichuna** | **alichonga** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Andika sentensi hizi. Pigia mstari herufi kubwa.

1. Shule yetu inaitwa Hekima.
2. Chifu Kitile anaishi ng'ambo ya mto.
3. Sisi hutumia boti kuvuka mto Yala.
4. Mlima wa Kilimanjaro unavutia.
5. Siku ya Jumamosi sisi hupumzika.
6. Mjomba wangu anaishi Kabuku.
7. Bawabu wetu anaitwa Mzee Kihenjo.

Mali ya Serikali ya Kenya 86

Kipindi cha 86 na 87 **Usafiri 2**

Kusoma hadithi




**Alama za barabarani**

Alama za barabarani ni muhimu. Watu wanaoendesha magari wanastahili kuzingatia alama hizo.
Alama ya kivukio cha watoto huwekwa karibu na shule. Wanaotumia barabara wanafaa kuwa waangalifu wanapokiona. Ni hatari kwa watoto kucheza au kukimbizana barabarani. Alama nyingine ni herufi H inayoonyesha hospitali. Dereva anapofika hapo, ni lazima awe mwangalifu na apunguze kasi ya gari lake. Vilevile, haruhusiwi kupiga honi ovyoovyo karibu na shule au hospitali. Alama nyingine ni kivukio cha wanyama na kivukio cha watu. Alama na sheria za barabarani zinapofuatwa, ajali hupungua.

87 Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ch/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** /ch/, chuma, shamba

**U:** Endelea na maneno; chombo, chomeka, jembe, chukua, jaza, sahani.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ch, v

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 86.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /ch/ a/ silabi ni cha

**U:** Endelea na silabi; chi, cho, chu, vo.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 86.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: cho me le a – chomelea

**U:** Endelea na maneno; chuma, chomeka, chafuka.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 86.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **kivukio cha watoto, herufi H, magari.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 87.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Ni akina nani wanaostahili kuzingatia alama za barabarani? *(Watu wote wanastahili kuzingatia alama za barabarani)*

**T:** Taja alama moja ya barabarani. *(Alama ya herufi h inayoonyesha hospitali)*

**U:** Ni wapi mtu hapaswi kupiga honi ovyoovyo? *(Karibu na shule au hospitali)*

### Zoezi

Mwanafunzi amweleze mwenzake njia za usafiri anazojua.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike baadhi ya alama za barabarani anazozijua.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 87: Usafiri 2

Kipindi cha 86 na 87 **Usafiri 2**

**Kipindi 86**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ch v

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

chi cho chu vo

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| chu ma | cho me ka | cha fu ka | cho mbo |
| **chuma** | **chomeka** | **chafuka** | **chombo** |

**Kipindi 87**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

CH ch V v

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a li chomeka | tu li chafua | a li chuna | a li chonga |
| **alichomeka** | **tulichafua** | **alichuna** | **alichonga** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Andika sentensi hizi. Pigia mstari herufi kubwa.

1. Shule yetu inaitwa Hekima.
2. Chifu Kitile anaishi ng'ambo ya mto.
3. Sisi hutumia boti kuvuka mto Yala.
4. Mlima wa Kilimanjaro unavutia.
5. Siku ya Jumamosi sisi hupumzika.
6. Mjomba wangu anaishi Kabuku.
7. Bawabu wetu anaitwa Mzee Kihenjo.

Mali ya Serikali ya Kenya

86

Kipindi cha 86 na 87 **Usafiri 2**

**Kusoma hadithi**




**Alama za barabarani**

Alama za barabarani ni muhimu. Watu wanaoendesha magari wanastahili kuzingatia alama hizo.

Alama ya kivukio cha watoto huwekwa karibu na shule. Wanaotumia barabara wanafaa kuwa waangalifu wanapokiona. Ni hatari kwa watoto kucheza au kukimbizana barabarani. Alama nyingine ni herufi H inayoonyesha hospitali. Dereva anapofika hapo, ni lazima awe mwangalifu na apunguze kasi ya gari lake. Vilevile, haruhusiwi kupiga honi ovyoovyo karibu na shule au hospitali. Alama nyingine ni kivukio cha wanyama na kivukio cha watu. Alama na sheria za barabarani zinapofuatwa, ajali hupungua.

87 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** CH, ch, V, v

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 86.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** a li chovua – alichovua

**U:** Endelea na maneno; alichomeka, tulichafua, alichuna.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 86.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **magari, herufi H, kivukio cha watoto.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya herufi kubwa**

**N:** Eleza matumizi ya herufi kubwa.

Tunatumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi.

Pia herufi kubwa hutumiwa mwanzoni mwa majina ya watu au mahali. Kwa mfano: Mji wa Ghamba, Ujerumani, Daudi.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 86.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi nne zinazo anza na herufi kubwa.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 88 na 89 **Usafiri 2**

**Kipindi 88**

- ■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

  dh ch

- ● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  dhi dho dhu cho

- ★ Soma maneno ukitumia silabi.

| dha ra u | dha ha bu | cha fu a | cha nga nya |
|---|---|---|---|
| **dharau** | **dhahabu** | **chafua** | **changanya** |

**Kipindi 89**

- ■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

  DH dh CH ch

- ▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| ku cheza | tu li chelewa | a li hudhuria |
|---|---|---|
| **kucheza** | **tulichelewa** | **alihudhuria** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Pigia mstari herufi kubwa katika sentensi zifuatazo. Soma sentensi hizi.

1. Mzee Tembo ni tajiri sana.
2. Treni ya umeme inayoitwa Maendeleo huenda kwa kasi.
3. Leo ni siku ya Jumatano.
4. Mvua ilinyesha mwezi wa Aprili.
5. Kaka yangu anaitwa Katana.

Mali ya Serikali ya Kenya 88

Kipindi cha 88 na 89 **Usafiri 2**

**Kusoma hadithi**



**Dereva Rashidi**

Rashidi alikuwa dereva ambaye hakuhitimu. Alijifundisha kuendesha gari kijijini. Siku moja Rashidi alimtembelea shangazi yake Nairobi. Alipofika huko alimdanganya kwamba yeye ni dereva stadi. Rashidi alidhamiria kuendesha gari vizuri. Shangazi yake alifurahi sana. Asubuhi iliyofuata shangazi aliamua kuenda soko la Marikiti. Rashidi alianza kuendesha gari haraka haraka. Walipofika kwenye mzunguko wa barabara, Rashidi hakujua umuhimu wa taa za trafiki. Huyo! Alifululiza moja kwa moja japo aliiona taa nyekundu. Shangazi alishangaa! Kufumba na kufumbua macho, waliligonga gari jingine.

89 Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/dh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa wa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** dhamana, thamani

**U:** Endelea na maneno; dhahabu, chuki, thelathini, dhati.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** dh, ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 88.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /dh/ a/ silabi ni dha.

**U:** Endelea na silabi; dhi, dho, dhu, cho.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 88.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: dha ti – dhati

**U:** Endelea na maneno; dharau, dhahabu, chafua.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 88.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **hakuhitimu, stadi, taa za trafiki.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 89.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Taja mji aliotembelea Rashidi. *(Rashidi alitembea Nairobi)*

**T:** Taa za trafiki zilikuwa wapi? *(Zilikuwa kwenye mzunguko wa barabara)*

**U:** Je, ungefanya nini iwapo ungekuwa shangazi? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike majina matatu ya vyombo vya usafiri.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore vyombo vitatu vya usafiri na kuvitambua kwa majina.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 89: Usafiri 2

Kipindi cha | 88 na 89 | **Usafiri 2**

**Kipindi 88**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**dh**    **ch**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**dhi**    **dho**    **dhu**    **cho**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| dha ra u | dha ha bu | cha fu a | cha nga nya |
| **dharau** | **dhahabu** | **chafua** | **changanya** |

**Kipindi 89**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**DH**    **dh**    **CH**    **ch**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ku cheza | tu li chelewa | a li hudhuria |
| **kucheza** | **tulichelewa** | **alihudhuria** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Pigia mstari herufi kubwa katika sentensi zifuatazo. Soma sentensi hizi.

1. Mzee Tembo ni tajiri sana.
2. Treni ya umeme inayoitwa Maendeleo huenda kwa kasi.
3. Leo ni siku ya Jumatano.
4. Mvua ilinyesha mwezi wa Aprili.
5. Kaka yangu anaitwa Katana.

Mali ya Serikali ya Kenya    88

Kipindi cha | 88 na 89 | **Usafiri 2**

**Kusoma hadithi**



**Dereva Rashidi**

Rashidi alikuwa dereva ambaye hakuhitimu. Alijifundisha kuendesha gari kijijini. Siku moja Rashidi alimtembelea shangazi yake Nairobi. Alipofika huko alimdanganya kwamba yeye ni dereva stadi. Rashidi alidhamiria kuendesha gari vizuri. Shangazi yake alifurahi sana. Asubuhi iliyofuata shangazi aliamua kuenda soko la Marikiti. Rashidi alianza kuendesha gari haraka haraka. Walipofika kwenye mzunguko wa barabara, Rashidi hakujua umuhimu wa taa za trafiki. Huyo! Alifululiza moja kwa moja japo aliiona taa nyekundu. Shangazi alishangaa! Kufumba na kufumbua macho, waliligonga gari jingine.

89    Hakiuzwi

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** DH, dh, CH, ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 88.**

## ▬ Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** a li dhaminiwa – a li dhaminiwa

**U:** Endelea na maneno; kucheza, tulichelewa.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 88.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **hakuhitimu, stadi, taa za trafiki.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya herufi kubwa**

**N:** Eleza matumizi ya herufi kubwa.

Tunatumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi.

Pia herufi kubwa hutumiwa mwanzoni mwa majina ya watu au mahali.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 88.**

**Majibu**

1. Mzee Tembo ni tajiri sana.
2. Treni ya umeme inayoitwa Maendeleo huenda kwa kasi.
3. Leo ni siku ya Jumatano.
4. Mvua ilinyesha mwezi wa Aprili.
5. Baba wangu anaitwa Katana.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aakifishe sentensi zifuatazo akitumia herufi kubwa.

1. baba anaendesha gari dogo.
2. siku ya jumapili nitaenda kanisani.
3. mwalimu wetu anaitwa amina.

**Majibu**

1. Baba anaendesha gari dogo.
2. Siku ya Jumapili nitaenda kanisani.
3. Mwalimu wetu anaitwa Amina.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 90 **Usafiri 2**

Kipindi 90

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

CH ch DH dh

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ba si - basi**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ba | ga | mo | pi | nde |
| shi | ki | ge | ru | si |

◆ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Akifisha sentensi zifuatazo kwa kutumia herufi kubwa.

1. alama ya kivukio cha watoto ni muhimu.
2. juma anasafiri naivasha kwa matatu.
3. mji wa nairobi ni mkubwa.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Safari ya Pemba**



**Kuandika**

Hadithi hii ya Dereva Rashidi ilifanyika wapi na ni nini kilichoendelea?

Mali ya Serikali ya Kenya 90

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** CH, ch, DH, dh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 90.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na mwanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'basi'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **meli, tuliabiri, gari dogo.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Safari ya Pemba**

Ulikuwa usiku mrefu. Tulikuwa na matumaini makubwa. Siku tuliyosubiri ilifika. Tuliabiri basi hadi bandarini. Ghafla kingo'ra kilisikika. Meli maridadi yenye rangi nyekundu ilifika.

"Naam, wajukuu wangu, safari ya Pemba imeanza," alisema babu Musa.

Baharini, tuliona samaki mkubwa. Mnamwona yule pale? Yule anaitwa papa. Yeye ni samaki hatari sana. Papa anaishi baharini," alisema babu Musa. Tuliwaona wavuvi kwenye dau wakivua samaki.

Tuliona mawimbi na meli za kubeba mizigo baharini. Baada ya saa nne, tulifika kisiwani Pemba. Tuliabiri garimoshi hadi katikati mwa mji. Majumba makubwa ya ghorofa yalipendeza sana. Mjini, kulikuwa na watu wengi. Miti ya minazi na mikarafuu ilikuwa karibu na bahari. Tuliingia kwenye hoteli moja kupata chakula cha mchana. Babu alikula samaki wa kukaanga. Mimi nilikula wali wa nazi. Vyakula vyote vilikuwa vitamu sana. Sote tulikunywa maji ya matunda. Baada ya kula tulichukua gari dogo kuelekea kijijini Soi kwa mjomba.

## Maswali

**T:** Taja vyombo vya usafiri vilivyotajwa kwenye hadithi. *(Basi, meli, garimoshi)*

**U:** Babu alikula na kunywa nini kwenye hoteli? *(Babu alikula samaki wa kukaanga na maji ya matunda)*

**U:** Je, unafikiri meli za kubeba mizigo hubeba mizigo gani? *(Kubali jibu sahihi kwa mfano chakula, nguo.)*

## Kuandika sentensi

**N: Andika sentensi moja kuhusu hadithi ya 'dereva Rashidi'.**

**T:** Waongoze wanafunzi katika kuandika sentensi kuhusu hadithi ya **'dereva Rashidi'.**

**U: Wanafunzi wafanye zoezi la kuandika kwenye ukurasa wa 90.**

## Sarufi

**Matumizi ya herufi kubwa**

N: Eleza matumizi ya herufi kubwa.

Tunatumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi.

Pia herufi kubwa hutumiwa mwanzoni mwa majina ya vitu au mahali.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 90.**

**Majibu**

1. Alama ya kivukio cha watoto ni muhimu.
2. Juma anasafiri Naivasha kwa matatu.
3. Mji wa Nairobi ni mkubwa.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya. Hakikisha kila sentensi inaanza kwa herufi kubwa.

1. Ndege 2. Basi 3. Matatu

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi atembelee shule jirani na kuwahamasisha wanafunzi kuhusu umuhimu wa elimu.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 91 na 92 **Familia 2**

**Kipindi 91**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ny** **gh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**nyi** **nyo** **nyu** **gha**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | |
|---|---|---|
| nya nya | nya ti | gha la ni |
| **nyanya** | **nyati** | **ghalani** |

**Kipindi 92**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NY** **ny**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| wa li kusanyika | wa na o fanya | a li kanyaga |
| **walikusanyika** | **wanaofanya** | **alikanyaga** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Igiza vitenzi hivi huku ukivitungia sentensi.

**Kwa mfano:** Mimi **ninaoga**.

1. Oga
2. Kimbia
3. Tabasamu
4. Cheza
5. Ruka
6. Kanyaga
7. Kusanya

91 Hakiuzwi

Kipindi cha 91 na 92 **Familia 2**

**Kusoma hadithi**



**Ukoo wetu**

Siku moja nilienda kumtembelea nyanya yangu. Yeye aliishi kijijini Ng'onda. Kijiji cha Ng'onda kilikuwa ng'ambo ya mto Ghalani. Nilivuka mto Ghalani kwenda ng'ambo. Nilipofika nyanya alinikaribisha vizuri. Alinipa kiti karibu na ghala. Jioni hiyo, nyanya alinieleza kuhusu majina ya ukoo wetu. Aliniambia kuwa yeye alikuwa na watoto watano. Aliendelea kunieleza kuwa kaka wa baba nitamwita amu naye dada wa baba ni shangazi. Watoto wa amu nitawaita binamu. Hakukomea hapo, alinikumbusha kuwa kaka wa mama yangu ni mjomba. Alimalizia kwa kunifunza dada mkubwa wa mama nitamuita mama mkubwa.

Mali ya Serikali ya Kenya 92

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ny/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** /ny/, nyanya, mbuzi

**U:** Endelea na maneno; nyama, wetu, nyimbo.

Rudia hatua ulizofuata na sauti **/gh/:** ghalani, kung'ara, ghasia, ghali

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ny, gh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 91.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /ny/ / a/ silabi ni nya.

**U:** Endelea na silabi; nyi, nyo, nyu, gha.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 91.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** nya si – nyasi

**U:** Endelea na maneno; nyanya, nyati.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 91.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **mama mkubwa, mjomba, nyanya.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 92.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Dada ya baba huitwaje? *(Dada wa baba ni shangazi.)*

**T:** Binamu ni nani? *(Watoto wa amu nitawaita binamu.)*

**U:** Taja majina mawili ya binamu wako kama unao. *(Kubali jibu sahihi, kwa mfano; Daudi, Said.)*

### Zoezi

Mwanafunzi apige mstari chini ya jina la mtu wa familia.

1. Mjomba alinipatia zawadi.
2. Twende tukamwone shangazi.
3. Amu analima shambani.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike majina manne ya jamaa wa ukoo.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 92: Familia 2

Kipindi cha | 91 na 92 | **Familia 2**

**Kipindi 91**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **ny** **gh**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  **nyi** **nyo** **nyu** **gha**

- ★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | |
|---|---|---|
| nya nya | nya ti | gha la ni |
| **nyanya** | **nyati** | **ghalani** |

**Kipindi 92**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **NY** **ny**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| wa li kusanyika | wa na o fanya | a li kanyaga |
| **walikusanyika** | **wanaofanya** | **alikanyaga** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Igiza vitenzi hivi huku ukivitungia sentensi.

**Kwa mfano:** Mimi **ninaoga**.

1. Oga
2. Kimbia
3. Tabasamu
4. Cheza
5. Ruka
6. Kanyaga
7. Kusanya

91

Hakluzwi

Kipindi cha | 91 na 92 | **Familia 2**

**Kusoma hadithi**



**Ukoo wetu**

Siku moja niliienda kumtembelea nyanya yangu. Yeye aliishi kijijini Ng'onda. Kijiji cha Ng'onda kilikuwa ng'ambo ya mto Ghalani. Nilivuka mto Ghalani kwenda ng'ambo. Nilipofika nyanya alinikaribisha vizuri. Alinipa kiti karibu na ghala. Jioni hiyo, nyanya alinieleza kuhusu majina ya ukoo wetu. Aliniambia kuwa yeye alikuwa na watoto watano. Aliendelea kunieleza kuwa kaka wa baba nitamwita amu naye dada wa baba ni shangazi. Watoto wa amu nitawaita binamu. Hakukomea hapo, alinikumbusha kuwa kaka wa mama yangu ni mjomba. Alimalizia kwa kunifunza dada mkubwa wa mama nitamuita mama mkubwa.

Mali ya Serikali ya Kenya

92

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NY, ny

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 91.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li nyunyizia – alinyunyizia

**U:** Endelea na maneno; walikusanyika, wanaofanya.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 91.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **nyanya, mjomba, mama mkubwa.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya vitenzi**

**N:** Andika maneno haya ubaoni; **simama, tembea, andika, cheka, oga na chana.**

Eleza maana ya maneno ya vitendo. Maneno ya vitendo ni yale ambayo yanaonyesha kutendeka kwa jambo fulani. Kama vile simama, tembea, cheka, chana n.k. Maneno haya huonyesha hali ya kitendo.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi, kwenye **ukurasa wa 92.**

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 91.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi zifuatazo kwa hati nadhifu, kisha amsomee mwenzake.

1. Mwalimu amesimama darasani.
2. Juma alitembea haraka.
3. Wanafunzi walicheka kwa sauti.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 93: Familia 2

Kipindi cha | 93 na 94 | **Familia 2**

**Kipindi 93**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng'**     **ny**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ng'i**    **ng'o**    **ng'u**    **nyo**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ku ng'a ra | ng'o nda | ki ng'o ra | nya ma |
| **kung'ara** | **ng'onda** | **king'ora** | **nyama** |

**Kipindi 94**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG'**     **ng'**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ku ning'inia | ku ng'ang'ania | ku nung'unika |
| **kuning'inia** | **kung'ang'ania** | **kunung'unika** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**


Jaza pengo ukitumia neno moja kati ya uliyopewa.

1. Baba ana________ ng'ombe. (fuga, kula)
2. Nyanya ata________ chakula kitamu. (oga, pika)
3. Mama ali________ sukari dukani. (simama, nunua)
4. Kaka ali________ mpira uwanjani. (cheza, kula)
5. Halati ata________ zawadi nzuri. (tupatia, tugonga)
6. Dada ali________ nguo zake. (kula, fua)
7. Amu ana________ Nairobi. (ishi, cheza)

93    Hakiuzwi

Kipindi cha | 93 na 94 | **Familia 2**

**Kusoma hadithi**



**Familia ya Ng'ang'a**

Ng'ang'a anaishi katika kijiji cha Nyanyiro. Familia yake ni kubwa sana. Ng'ang'a anaishi pamoja na nyanya yake. Nyanya huyo ana wajukuu wengi. Binti ya Ng'ang'a hung'ara kila siku. Ng'ang'a alijenga ghala kubwa. Ghala hilo hutumika kuhifadhi chakula cha ng'ombe. Ng'ombe wake wana maziwa mengi. Gharama ya chakula cha ng'ombe ni ghali sana. Ng'ang'a huuza maziwa yake katika soko la Ghele. Yeye hupata pesa nyingi sana. Ng'ang'a hutumia pesa hizo kuwalipia watoto wake karo. Yeye huipenda familia yake.

Mali ya Serikali ya Kenya    94

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ng'/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzo wa neno. Mwanafunzi aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno husika.

**N/T/U:** ng'aa, gari

**U:** Endelea na maneno; ng'ambo, nyanya, ng'ombe, nyumba, Ng'ang'a.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng', ny

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 93**.

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /ng'/ / a/ silabi ni ng'a

**U:** Endelea na silabi; ng'i, ng'o, ng'u, nyo.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 93.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** ng'o a – ng'oa

**U:** Endelea na maneno; kung'ara, ng'onda, king'ora, nyama.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 93.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **familia, wajukuu, binti.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 94.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Ng'ang'a anaishi katika kijiji gani? (Ng'ang'a anaishi katika kijiji cha Nyanyiro)

**T:** Chakula cha ng'ombe huhifadhiwa wapi? (Ghala hutumika kuhifadhi chakula cha ng'ombe)

**U:** Je, maziwa ya ng'ombe hutumiwa vipi? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Katika vikundi, wanafunzi waigize vitendo vifuatavyo.

1. Cheka    2. Keti    3. Simama

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi nne ukitumia vitenzi vifuatavyo.

1. Cheka    2. Keti    3. Simama

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 94: Familia 2

Kipindi cha 93 na 94 **Familia 2**

**Kipindi 93**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng'  ny

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ng'i  ng'o  ng'u  nyo

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ku ng'a ra | ng'o nda | ki ng'o ra | nya ma |
|---|---|---|---|
| **kung'ara** | **ng'onda** | **king'ora** | **nyama** |

**Kipindi 94**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

NG'  ng'

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| ku ning'inia | ku ng'ang'ania | ku nung'unika |
|---|---|---|
| **kuning'inia** | **kung'ang'ania** | **kunung'unika** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**


Jaza pengo ukitumia neno moja kati ya uliyopewa.

1. Baba ana________ ng'ombe. (fuga, kula)
2. Nyanya ata________ chakula kitamu. (oga, pika)
3. Mama ali________ sukari dukani. (simama, nunua)
4. Kaka ali________ mpira uwanjani. (cheza, kula)
5. Halati ata________ zawadi nzuri. (tupatia, tugonga)
6. Dada ali________ nguo zake. (kula, fua)
7. Amu ana________ Nairobi. (ishi, cheza)

93  Hakluzwi

Kipindi cha 93 na 94 **Familia 2**

**Kusoma hadithi**



**Familia ya Ng'ang'a**

Ng'ang'a anaishi katika kijiji cha Nyanyiro. Familia yake ni kubwa sana. Ng'ang'a anaishi pamoja na nyanya yake. Nyanya huyo ana wajukuu wengi. Binti ya Ng'ang'a hung'ara kila siku. Ng'ang'a alijenga ghala kubwa. Ghala hilo hutumika kuhifadhi chakula cha ng'ombe. Ng'ombe wake wana maziwa mengi. Gharama ya chakula cha ng'ombe ni ghali sana. Ng'ang'a huuza maziwa yake katika soko la Ghele. Yeye hupata pesa nyingi sana. Ng'ang'a hutumia pesa hizo kuwalipia watoto wake karo. Yeye huipenda familia yake.

Mali ya Serikali ya Kenya  94

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NG', ng'

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 93.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** a li ng'ara – aling'ara

**U:** Endelea na maneno; kuning'inia, kung'ang'ania.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 93.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **familia, wajukuu, binti.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya vitenzi**

**N:** Andika maneno haya ubaoni: keti, kula, soma, lia, osha na vuka.

Eleza maana ya maneno ya vitendo. Maneno ya vitendo ni yale ambayo yanaonyesha kutendeka kwa jambo fulani. Kama vile simama, tembea, cheka, chana n.k. Maneno haya huonyesha hali ya kitendo.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 93.**

**Majibu**

1. fuga  2. pika  3. nunua
4. cheza  5. tupatia  6. fua
7. ishi

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike vitendo vya kikazi ambavyo walezi wake hutekeleza nyumbani.

Mfano: kulima

Tarehe: ________________  Muda: ____________  Idadi: ____________

# Kipindi cha 95: Familia 2

Kipindi cha 95 **Familia 2**

**Kipindi 95**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

NY ny NG' ng'

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ng'a ri sha – ng'arisha**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ra | nya | bi | mba | ng'a |
| nti | m | ri | sha | jo |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Igiza na utunge sentensi ukitumia vitenzi hivi.

1. Fagia 2. Chana 3. Andika

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Jamaa ya Dodi**



**Kuandika**

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. Watoto 2. Binti 3. Familia 4. Mjomba

95 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NY, ny, NG', ng'

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 95.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na mwanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'ng'arisha'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **binti, mpwa, mjomba.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Jamaa ya Dodi**

Dodi anasoma shule ya msingi ya Kapu. Yeye huishi mjini na wazazi wake. Nyanya yake huishi kijijini Sabu. Mara nyingi, Dodi hutamani kumtembelea nyanya yake ili amsaidie kufanya kazi za nyumbani kama vile kuchota maji na kulima shamba.

Wakati wa likizo, Dodi aliomba ruhusa kutoka kwa wazazi ili amtembelee nyanya yake.

Siku ilipofika, Dodi alijitayarisha mapema. Mama yake alimpa zawadi ampelekee binti ya mjomba wake. Aliuchukua mkoba wake kuelekea kwenye kituo cha basi. Alipanda basi kuelekea kijijini Sabu. Mle garini, Dodi alimpata mpwa wake Nekesa " Hujambo Nekesa?" Dodi alimsalimu. "Sijambo Dodi. Nimefurahi kukuona. Unaelekea wapi?" Nekesa alimuuliza. "Ninaelekea kijijini Sabu kumuona nyanya." Dodi alisema. Walipofika kwenye kituo cha basi, gari lilisimama na wakashuka. Nekesa akaenda dukani kununua maji. Alipokuwa akirudi, Nekesa aliteguka mguu na kuanguka chini. Kwa bahati nzuri, mwenye duka alikimbia na kumsaidia Nekesa.

Dodi aliamua kumpigia nyanya yake simu baada ya kumngojea kwa muda mrefu. Nyanya yake alifika kituoni na wote wakaandamana kwenda nyumbani. Dodi alifurahi kufika kwa nyanya yake salama.

## Maswali

**T:** Dodi ni mwanafunzi wa shule gani? *(Dodi anasoma Shule ya Msingi ya Kapu.)*

**U:** Mama alimpa Dodi nini? *(Mama alimpa zawadi)*

**U:** Unafikiri Dodi na Nekesa walifika kijijini saa ngapi? *(Majibu ni kama vile saa kumi, jioni)*

## Kuandika sentensi

**N: Andika sentensi moja ukitumia neno mpwa.**

**T:** Waongoze wanafunzi katika kuandika sentensi wakitumia neno mama.

**U: Wanafunzi wafanye zoezi la kuandika kwenye ukurasa wa 95.**

## Sarufi

**Matumizi ya vitenzi**

N: Andika maneno haya ubaoni: ruka, tembea, andika, cheka, osha na kata.

Eleza maana ya maneno ya vitendo. Maneno ya vitendo ni yale ambayo yanaonyesha kutendeka kwa jambo fulani. Kama vile, simama, tembea, cheka, chana n.k. Maneno haya huonyesha kitendo.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 95.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi ajaze mapengo:

1. Mzazi wa kike anaitwa __________. (nyanya, mama)
2. Ndugu wa kiume nitamuita nani? __________ (mjomba, kaka)
3. Mama wa baba yangu nitamuita nani? __________ (nyanya, shangazi)

Tarehe: __________________ Muda: __________________ Idadi: __________________

Kipindi cha 96 na 97 **Familia 2**

**Kipindi 96**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**gh** **ny**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ghe** **ghi** **gho** **nyi** **nyu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| gha li | gha ra ma | nya ni | nyo ro ro |
|---|---|---|---|
| **ghali** | **gharama** | **nyani** | **nyororo** |

**Kipindi 97**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**GH** **gh** **NY** **ny**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li gharamika | a li ghairi | wa li nyamaza |
|---|---|---|
| **aligharamika** | **alighairi** | **walinyamaza** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Jaza pengo ukitumia maneno uliyopewa.

1. Nyanya ana________ mbegu shambani. (lima, panda)
2. Amu ali_______ miti barabarani. (ng'oa, keti)
3. Mjomba ame_______ kutoka mjini. (cheka, rudi)
4. Shangazi ame_______ kitini. (keti, panda)
5. Ndugu yake ali_______ alipoanguka. (lia, soma)
6. Wazazi wali_______ kwenye mkutano. (ng'oa, ongea)
7. Dada ata _______ mji wa Nairobi. (tembelea, pika)

Mali ya Serikali ya Kenya 96

Kipindi cha 96 na 97 **Familia 2**

**Kusoma hadithi**



**Sherehe ya kuzaliwa**

Musila ni mkaazi wa kijiji cha Mbuni. Yeye ana mke na binti mmoja. Mke wake anaitwa Sumela. Sumela alijifungua mtoto msichana. Musila aliandaa karamu ya kuzaliwa kwa mtoto wake. Kaka zake Musila walifika nyumbani kwake. Sherehe zilipoanza, mtoto alipewa jina Nyakio. Alivaa nguo nyekundu. Alipewa zawadi na dada yake. Babu alimpa zawadi ya mbuzi. Chifu aliposikia nyimbo alifika kwa Musila. Alifikiri ni ghasia za wanakijiji. Chifu alijiunga na wanakijiji kusherehekea. Vyakula vilikuwa vya bei ghali. Watu wote walifurahi.

97

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/gh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** /gh/, ghala, gari

**U**: ghadhabu, nyumba, ghorofa, geuka

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** gh, ny

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 96**.

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /ny/ / a/ silabi ni nya

**U:** Endelea na silabi; ghe, ghi, gho, nyi, nyu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 96.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: gha dha bu – ghadhabu

**U:** Endelea na maneno; ghali, gharama, nyani.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 96.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno; **dada, babu, kaka.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi: kwenye **ukurasa wa 97**.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Musila ni mkaazi wa wapi? *(Musila ni mkaazi wa kijiji cha Mbuni.)*

**T:** Mtoto aliyezaliwa alipewa jina gani? *(Nyakio)*

**U:** Kwa nini watu husherehekea kuzaliwa kwa mtoto? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi anakili sentensi zifuatazo kisha baadaye atamsomea mlezi wake.

1. Mtoto amesimama kando ya meza.
2. Wanafunzi wanasoma hadithi.
3. Baba anafyeka nyasi.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia majina haya: kaka, dada, babu.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 97: Familia 2

Kipindi cha 96 na 97 **Familia 2**

**Kipindi 96**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

gh ny

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ghe ghi gho nyi nyu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| gha li | gha ra ma | nya ni | nyo ro ro |
| **ghali** | **gharama** | **nyani** | **nyororo** |

**Kipindi 97**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

GH gh NY ny

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a li gharamika | a li ghairi | wa li nyamaza |
| **aligharamika** | **alighairi** | **walinyamaza** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Jaza pengo ukitumia maneno uliyopewa.

1. Nyanya ana________ mbegu shambani. (lima, panda)
2. Amu ali________ miti barabarani. (ng'oa, keti)
3. Mjomba ame________ kutoka mjini. (cheka, rudi)
4. Shangazi ame________ kitini. (keti, panda)
5. Ndugu yake ali________ alipoanguka. (lia, soma)
6. Wazazi wali________ kwenye mkutano. (ng'oa, ongea)
7. Dada ata ________ mji wa Nairobi. (tembelea, pika)

Mali ya Serikali ya Kenya

96

Kipindi cha 96 na 97 **Familia 2**

**Kusoma hadithi**



**Sherehe ya kuzaliwa**

Musila ni mkaazi wa kijiji cha Mbuni. Yeye ana mke na binti mmoja. Mke wake anaitwa Sumela. Sumela alijifungua mtoto msichana. Musila aliandaa karamu ya kuzaliwa kwa mtoto wake. Kaka zake Musila walifika nyumbani kwake. Sherehe zilipoanza, mtoto alipewa jina Nyakio. Alivaa nguo nyekundu. Alipewa zawadi na dada yake. Babu alimpa zawadi ya mbuzi. Chifu aliposikia nyimbo alifika kwa Musila. Alifikiri ni ghasia za wanakijiji. Chifu alijiunga na wanakijiji kusherehekea. Vyakula vilikuwa vya bei ghali. Watu wote walifurahi.

97 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** GH, gh, NY, ny

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 96.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** ku nyanyuka – kunyanyuka

**U:** Endelea na maneno; aligharamika, alighairi.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 96.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **kaka, babu, dada.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya vitenzi**

**N:** Andika maneno haya ubaoni: lala, ongea, pika, panda, lima na soma.

Eleza maana ya maneno ya vitendo. Maneno ya vitendo ni yale ambayo yanaonyesha kutendeka kwa jambo fulani, kama vile simama, tembea, cheka, chana. Maneno haya huonyesha hali ya kitendo.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 96.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi achague jibu sahihi kwenye mabano kujaza mapengo.

1. Mgeni akibisha hodi huitikiwa vipi? __________ (hodi, karibu)
2. Mzazi akikununulia zawadi unasemaje? __________ (asante, samahani)
3. __________ ni neno ambalo hutumiwa mtu akimkosea mwingine. (Pole, Karibu)

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 98 na 99 **Familia 2**

**Kipindi 98**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng'    gh

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ng'o    ng'u    ng'i    gha    ghu

▲ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng'a ra | ng'o mbe | ng'a mu a | ng'a ng'a nia |
| **ng'ara** | **ng'ombe** | **ng'amua** | **ng'ang'ania** |

**Kipindi 99**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

NG'    ng'    GH    gh

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a li ng'ara | wa li shughulika | a li nung'unika |
| **aling'ara** | **walishughulika** | **alinung'unika** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**


Msomee mwenzako sentensi zifuatazo.

1. Mjomba **alinunua** gari la bei ghali sana.
2. Kaka yangu **ameng'olewa** meno matano.
3. Binamu **anachana** nywele.
4. Amu **alitununulia** maembe.
5. Nyanya **alitupikia** mihogo.
6. Shemeji **alitutembelea** kwetu nyumbani.
7. Baba **alitupeleka** katika mbuga ya wanyama.



Kipindi cha 98 na 99 **Familia 2**

**Kusoma hadithi**



**Amina**

Amina alizaliwa mwezi wa Disemba. Mama yake anaitwa Rehema. Baba yake anaitwa Okilo. Amina alizaliwa peke yake. Hana kaka wala dada. Amina anapenda kucheza na kuendesha baiskeli. Mama ya Amina ana kaka na dada mmoja. Mwezi wa Disemba wazazi wake waliandaa karamu. Karamu hiyo ilikuwa ya kusherehekea siku ya kuzaliwa kwa Amina. Jamaa ya Amina ilifika kwenye karamu. Amina alipewa zawadi nyingi. Shangazi alimpa Amina baiskeli. Mama mdogo alimpa Amina rinda. Amu alitoa zawadi ya bei ghali. Amina alifurahi sana.



## Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ng'/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** ng'ara, gari

**U:** Endelea na maneno; ng'ombe, ngao, ng'arisha, ghala

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng', gh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 98.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /ng'/ /e/ silabi ni ng'e

**U:** Endelea na silabi; ng'o, ng'u, ng'i, gha, ghu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 98.**

## Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja ili kulisoma neno.

**N/T/U:** gha ra ma – gharama

**U:** Endelea na maneno; ng'ara, ng'ombe, ng'amua.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 98.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno: **mama mdogo, shangazi, amu.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 99.**

## Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Baba yake Amina anaitwa nani? *(Baba yake Amina anaitwa Okilo)*

**T:** Nani alimpa Amina baiskeli? *(Shangazi)*

**U:** Taja aina zingine za sherehe unazojua? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Zoezi

Mwanafunzi ajaze mapengo kwa kutumia neno sahihi.

1. Mzazi wa kike anaitwa __________.
2. Wazazi wa baba au mama wanaitwa __________.
3. Dadake baba anaitwa __________.

## Kazi ya ziada

Wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno yafuatayo:

1. Shangazi    2. Amu    3. Baba

Tarehe: ____________    Muda: ____________    Idadi: ____________

# Kipindi cha 99: Familia 2

Kipindi cha 98 na 99 | **Familia 2**

**Kipindi 98**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng' gh

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ng'o ng'u ng'i gha ghu

▲ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng'a ra | ng'o mbe | ng'a mu a | ng'a ng'a nia |
| ng'ara | ng'ombe | ng'amua | ng'ang'ania |

**Kipindi 99**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

NG' ng' GH gh

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a li ng'ara | wa li shughulika | a li nung'unika |
| aling'ara | walishughulika | alinung'unika |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Msomee mwenzako sentensi zifuatazo.


1. Mjomba **alinunua** gari la bei ghali sana.
2. Kaka yangu **ameng'olewa** meno matano.
3. Binamu **anachana** nywele.
4. Amu **alitununulia** maembe.
5. Nyanya **alitupikia** mihogo.
6. Shemeji **alitutembelea** kwetu nyumbani.
7. Baba **alitupeleka** katika mbuga ya wanyama.

Mali ya Serikali ya Kenya

98

Kipindi cha 98 na 99 | **Familia 2**

**Kusoma hadithi**



**Amina**

Amina alizaliwa mwezi wa Disemba. Mama yake anaitwa Rehema. Baba yake anaitwa Okilo. Amina alizaliwa peke yake. Hana kaka wala dada. Amina anapenda kucheza na kuendesha baiskeli. Mama ya Amina ana kaka na dada mmoja. Mwezi wa Disemba wazazi wake waliandaa karamu. Karamu hiyo ilikuwa ya kusherehekea siku ya kuzaliwa kwa Amina. Jamaa ya Amina ilifika kwenye karamu. Amina alipewa zawadi nyingi. Shangazi alimpa Amina baiskeli. Mama mdogo alimpa Amina rinda. Amu alitoa zawadi ya bei ghali. Amina alifurahi sana.

99 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NG', ng', GH, gh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 98.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** a li ghairi – alighairi

**U:** Endelea na maneno; aling'ara, walishughulika.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 98.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **shangazi, amu, mama mdogo.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya vitenzi**

**N:** Andika maneno haya ubaoni: nunua, chana, pika, tembea, peleka na ng'oa.

Eleza maana ya maneno ya vitendo. Maneno ya vitendo ni yale ambayo yanaonyesha kutendeka kwa jambo fulani. Kama vile simama, tembea, cheka, chana n.k. Maneno haya huonyesha hali ya kitendo.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi zilizo na vitenzi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 98.**

Mwanafunzi asome sentensi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi ajaze mapengo ukitumia maneno aliyopewa (alikula, aliendesha, alituletea, ilijengwa, aliiba)

1. Ng'ombe ________________ nyasi.
2. Nyumba nzuri ________________.
3. Kamau ________________ gari.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 100 **Familia 2**

**Kipindi 100**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

GH gh NY ny NG' ng'

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ha la ti - halati**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ha | gha | ti | li | a |
| ng'a | bi | mu | na | la |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Andika sentensi hizi.

1. Amina **anaendesha** baiskeli.
2. Shangazi **amenunua** rinda.
3. Mama mdogo **alimpatia** Amina zawadi.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Mkutano wa familia**



**Kuandika**

Tumia vitendo hivi kutunga sentensi.

1. Panda 2. Pika 3. Lea 4. Soma

Mali ya Serikali ya Kenya 100

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** GH, gh, Ny, ny, NG', ng'

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 100.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'halati'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno kutokana na silabi.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **mpwa, kaka.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Mkutano wa familia**

Maneno alimwita mpwa wake Abu, "Njoo hapa." Maneno na Abu waliketi chini ya mti. " Siku hizi sehemu zangu za mwili zinauma. Macho hayaoni vizuri na miguu haina nguvu. Ningependa kuwaalika jamaa zangu niwaelezee jambo muhimu, Maneno akasema."

Abu aliandika majina ya binamu zake, kaka yake, dada zake na wengine wote waliotajwa na babu. "Niandike majina ya marafiki zangu pia?" Abu aliuliza.

"La! Nataka kuwaalika jamaa tu," Mzee Maneno alimjibu.

Siku ya mkutano ilipofika, Maneno aliwachinjia ng'ombe. Familia yote ilikuwa na furaha walipokutana. Mzee Maneno aliwakaribisha wote. Kila mmoja alikuwa na hamu ya kujua waliloitiwa. Baada ya kula, wote waliketi na kunyamaza kimya.

Mzee Maneno alianza kuwasimulia jinsi anavyoteseka kwa sababu ya ugonjwa. Aliwaelezea vile alivyokuwa amejaribu tiba ya kienyeji lakini hakupata nafuu. Alimalizia kwa kutaka msaada wao wa kumtafutia matibabu ya kisasa. Jamaa zake waliamua kwa kauli moja kumpeleka kwenye Hospitali kuu ya Kitaifa ya Kenyatta. Mzee Maneno alitibiwa na akapata nafuu. Watu wote wakafurahi.

## Maswali

**T:** Babu aliyetajwa katika hadithi anaitwa nani? *(Maneno)*

**U:** Mzee Maneno alitaka kuwaalika kina nani? *(Alitaka kuwaalika jamaa zake)*

**U:** Je, unafikiri mbali na nyama ya ng'ombe mzee Maneno alinunua vyakula gani vingine? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Kuandika

**N: Andika sentensi moja ukitumia neno cheka.**

**T:** Waongoze wanafunzi katika kuandika sentensi wakitumia neno lia.

**U: Wanafunzi wafanye zoezi la kuandika kwenye ukurasa wa 100.**

## Sarufi

**Matumizi ya vitenzi**

Andika maneno haya ubaoni: panda, lea, soma, pia, funza na fungua.

Eleza maana ya maneno ya vitendo. Maneno ya vitendo ni yale ambayo yanaonyesha kutendeka kwa jambo fulani. Kama vile simama, tembea, cheka, chana. Maneno haya huonyesha hali ya kitendo.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 100.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi kuhusu hadithi waliyosomewa na mwalimu.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 101: Marejeleo 2

Kipindi cha 101 na 102 **Marejeleo 2**

**Kipindi 101**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

gh    dh

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ghe    ghi    gho    ghu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ghu la mu | gho ro fa | gha la | gha ra ma |
|---|---|---|---|
| **ghulamu** | **ghorofa** | **ghala** | **gharama** |

**Kipindi 102**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

GH    gh    DH    dh

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| i li m gharimu | a li tu ghilibu | hu ghairi |
|---|---|---|
| **ilimgharimu** | **alitughilibu** | **hughairi** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri au vibaya**

Jaza pengo ukitumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Walipewa zawadi baada ya kuimba __________.
2. Mama alipika chakula kitamu __________.
3. Mwizi akishikwa huadhibiwa __________.
4. Nyumba iliyojengwa________imebomoka.
5. Mchezaji alicheza _________akafunga bao.
6. Ukiruka________utaanguka.
7. Alipiga nguo pasi _______zikapendeza.

101 Hakiuzwi

Kipindi cha 101 na 102 **Marejeleo 2**

**Kusoma hadithi**



**Godi atuzwa**

Godi ni kiranja wa darasa la pili. Yeye husoma shule ya msingi ya Gomeni. Shule hii ina uwanja mkubwa na majengo mazuri. Mwalimu mkuu ni Bwana Bidii. Godi hupenda somo la Kiswahili. Yeye huhisi vibaya akianguka somo hili. Pia, hupenda mchezo wa mpira wa miguu. Godi na wanafunzi wengine hucheza mpira vizuri uwanjani. Siku ya wazazi shuleni, wanafunzi bora hutuzwa. Mwaka jana, wanafunzi wengi walituzwa. Godi alipokea zawadi mbili ghali. Alikuwa mwanafunzi bora katika somo la Kiswahili. Alipewa kitabu cha hadithi ya Sungura Mjanja. Vilevile, alipewa mpira mkubwa mwekundu. Godi alifurahi alipokuwa akipokea zawadi zake.

Mali ya Serikali ya Kenya 102

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/gh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** /gh/, ghala, goti

**U:** Endelea na maneno; gharama, ngumu, ghulamu, nyekundu.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** gh, dh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 101**.

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /gh/ /a / – gha.

**U:** Endelea na silabi; ghe, ghi, gho, ghu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 101.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** ghu la mu – ghulamu

**U:** Endelea na maneno; ghorofa, ghala.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 101.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **mwalimu mkuu, kiranja, hutuzwa.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 102.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Mwalimu mkuu wa shule ya Gomeni ni nani? *(Bwana Bidii)*

**T:** Taja aina ya zawadi Godi alizopokea siku ya wazazi shuleni? *(Kitabu cha hadithi ya sungura mjanja, mpira mwekundu.)*

**U:** Je, unafikiri ni kwa nini Godi alipewa mpira? *(Anapenda mchezo wa mpira.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike sentensi zifuatazo katika wingi.

1. Ulienda wapi jana? (Mlienda wapi jana?)
2. Wewe ulivuka barabara. (Nyinyi mlivuka barabara.)
3. Juzi ulinyeshewa na mvua. (Juzi mlinyeshewa na mvua.)

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi nne akitumia vizuri au vibaya.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

Kipindi cha 101 na 102 **Marejeleo 2**

**Kipindi 101**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**gh** **dh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ghe** **ghi** **gho** **ghu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ghu la mu | gho ro fa | gha la | gha ra ma |
| **ghulamu** | **ghorofa** | **ghala** | **gharama** |

**Kipindi 102**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**GH** **gh** **DH** **dh**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| i li m gharimu | a li tu ghilibu | hu ghairi |
| **ilimgharimu** | **alitughilibu** | **hughairi** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vizuri au vibaya**

Jaza pengo ukitumia **vizuri** au **vibaya**.

1. Walipewa zawadi baada ya kuimba ___________.
2. Mama alipika chakula kitamu ___________.
3. Mwizi akishikwa huadhibiwa ___________.
4. Nyumba iliyojengwa________imebomoka.
5. Mchezaji alicheza _________akafunga bao.
6. Ukiruka________utaanguka.
7. Alipiga nguo pasi _______zikapendeza.

101 Hakiuzwi

Kipindi cha 101 na 102 **Marejeleo 2**

**Kusoma hadithi**



**Godi atuzwa**

Godi ni kiranja wa darasa la pili. Yeye husoma shule ya msingi ya Gomeni. Shule hii ina uwanja mkubwa na majengo mazuri. Mwalimu mkuu ni Bwana Bidii. Godi hupenda somo la Kiswahili. Yeye huhisi vibaya akianguka somo hili. Pia, hupenda mchezo wa mpira wa miguu. Godi na wanafunzi wengine hucheza mpira vizuri uwanjani. Siku ya wazazi shuleni, wanafunzi bora hutuzwa. Mwaka jana, wanafunzi wengi walituzwa. Godi alipokea zawadi mbili ghali. Alikuwa mwanafunzi bora katika somo la Kiswahili. Alipewa kitabu cha hadithi ya Sungura Mjanja. Vilevile, alipewa mpira mkubwa mwekundu. Godi alifurahi alipokuwa akipokea zawadi zake.

Mali ya Serikali ya Kenya 102

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** GH, gh, DH, dh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 101.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo na usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li ghafilika – alighafilika

**U:** Endela na maneno; ilimgharimu, alitughilibu.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 101.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **kiranja, hutuzwa, mwalimu mkuu.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya vizuri na vibaya**

**N:** 'Vizuri' ni neno linalotumika kumaanisha jambo linapendeza au limefanyika kwa njia inayofurahisha. Kwa mfano: Mtoto aliandika vizuri. 'Vibaya' lina maana kuwa jambo halipendezi au linafanyika kwa njia isiyofurahisha. Kwa mfano: Mkulima alilima shamba vibaya.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 101.**

**Majibu**

| | | |
|---|---|---|
| 1. vizuri | 4. vibaya | 7. vizuri |
| 2. vizuri | 5. vizuri | |
| 3. vibaya | 6. vibaya | |

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi nne akitumia maneno haya:

1. Simama
2. Tembea
3. Chana
4. Oga

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 103 na 104 **Marejeleo 2**

**Kipindi 103**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **ng** **gh**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  **ngi** **ngo** **ngu** **gha**

- Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| sha nga zi | nyi ngi | nga o | ngo zi |
| **shangazi** | **nyingi** | **ngao** | **ngozi** |

**Kipindi 104**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **NG** **ng** **CH** **ch**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a li ngojea | ku bingirisha | a li angamia |
| **alingojea** | **kubingirisha** | **aliangamia** |

**Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Kamilisha sentensi ukitumia nafsi ya pili wakati uliopita na kitendo kwenye mabano.

**Kwa mfano:** Nyinyi **mlilima** shamba. (lima)

1. Wewe ________ nguo. (fua)
2. Nyinyi ________ mpira. (cheza)
3. Nyinyi ________ vitabu. (soma)
4. Wewe ________ nyumba. (panga)
5. Nyinyi ________ mto. (vuka)

103 Hakiuzwi

Kipindi cha 103 na 104 **Marejeleo 2**

**Kusoma hadithi**




**Likizo**

Likizo ya Agosti ilipoanza Tena na Tatu walifurahi. Walikuwa wameahidiwa kuwa wangemtembelea shangazi yao Bi. Shama. Jumamosi ilipofika, Tena na Tatu walianza safari.

"Nauli ndio hii. Waweke hawa wanangu pale Sangalo. Shangazi yao atawachukua wakifika kituoni," mama alimwambia dereva wa basi. Walipofika kituoni, Tena na Tatu walipokelewa na shangazi yao.

"Shikamoo shangazi," Tena alimsalimu.

"Marahaba Tena. Nimefurahi kuwaona. Mmekua sana," shangazi alisema. "Mlianza safari saa ngapi?" Shangazi aliuliza nao wakamjibu. Walipofika nyumbani walimpata mjomba wao. Alikuwa anasoma gazeti. Binamu yao Asha alikuwa akitazama televisheni. Walifurahia likizo yao.

Mali ya Serikali ya Kenya 104

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ng/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** shangazi, ngamia

**U:** Endelea na maneno; ngazi, ingia, injili, ngamia.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng, gh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 103.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /ng/ /a / silabi ni nga.

**U:** Endelea na silabi; ngi, ngo, ngu, cho.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 103.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** a nga la u – angalau

**U:** Endelea na maneno; shangazi, nyingi, ngao, ngozi.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 103.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **binamu, shangazi, mjomba.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi: kwenye **ukurasa wa 104.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Mwezi wa Agosti ulikua na nini? *(Likizo)*

**T:** Je, unadhani ni kwa nini Tina na Tatu walifurahi likizo ya Agosti ilipoanza? *(Walikuwa wameahidiwa kuwa watamtembelea shangazi yao.)*

**U:** Je, wewe hutembea wapi wakati wa likizo? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aagize maamkuzi ya mchana na usiku akiwa na rafiki yake. Mwanafunzi aigize maamkuzi.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore wanyama wawili wa nyumbani.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 104: Marejeleo 2

**Kipindi cha 103 na 104** — **Marejeleo 2**

**Kipindi 103**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng** **gh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ngi** **ngo** **ngu** **gha**

▲ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| sha nga zi | nyi ngi | nga o | ngo zi |
| **shangazi** | **nyingi** | **ngao** | **ngozi** |

**Kipindi 104**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG** **ng** **CH** **ch**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a li ngojea | ku bingirisha | a li angamia |
| **alingojea** | **kubingirisha** | **aliangamia** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Kamilisha sentensi ukitumia nafsi ya pili wakati uliopita na kitendo kwenye mabano.

**Kwa mfano:** Nyinyi **mlilima** shamba. (lima)

1. Wewe __________ nguo. (fua)
2. Nyinyi __________ mpira. (cheza)
3. Nyinyi __________ vitabu. (soma)
4. Wewe __________ nyumba. (panga)
5. Nyinyi __________ mto. (vuka)

103 Hakiuzwi

**Kipindi cha 103 na 104** — **Marejeleo 2**

**Kusoma hadithi**




**Likizo**

Likizo ya Agosti ilipoanza Tena na Tatu walifurahi. Walikuwa wameahidiwa kuwa wangemtembelea shangazi yao Bi. Shama. Jumamosi ilipofika, Tena na Tatu walianza safari.

"Nauli ndio hii. Waweke hawa wanangu pale Sangalo. Shangazi yao atawachukua wakifika kituoni," mama alimwambia dereva wa basi. Walipofika kituoni, Tena na Tatu walipokelewa na shangazi yao.

"Shikamoo shangazi," Tena alimsalimu.

"Marahaba Tena. Nimefurahi kuwaona. Mmekua sana," shangazi alisema. "Mlianza safari saa ngapi?" Shangazi aliuliza nao wakamjibu. Walipofika nyumbani walimpata mjomba wao. Alikuwa anasoma gazeti. Binamu yao Asha alikuwa akitazama televisheni. Walifurahia likizo yao.

Mali ya Serikali ya Kenya 104

### ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NG, ng, CH, ch

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 103.**

### ★ Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** i li nguruma – ilinguruma

**U:** Endelea na maneno; alingojea, kubingirisha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 103.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **shangazi, mjomba, binamu.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### ♦ Sarufi

**Matumizi ya vitenzi**

**N:** Andika maneno haya ubaoni: ruka, uza, keti na chana.

Eleza maana ya maneno ya vitendo. Maneno ya vitendo ni yale ambayo yanaonyesha kutendeka kwa jambo fulani. Kama vile ruka, ua, keti, chana n.k. maneno haya huonyesha hali ya kitendo.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi zilizo na vitenzi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 103.**

**Majibu**

1. mlifua
2. mlicheza
3. mlisoma
4. ulipanga
5. mlivuka

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike haki nne anazofaa kupata mtoto.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 105 Marejeleo 2

**Kipindi 105**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng ng' gh

Jedwali la silabi

Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ngo zi – ngozi**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| a | zi | nga | ng'a | gh | ngo |
| si | na | ma | mi | la | ra |

**Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Tumia **-ako** au **-enu** kukamilisha sentensi.

1. Kiti __________ kimevunjika.
2. Kalamu __________ zimepotea.
3. Meno __________ nyote ni meupe.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Mbuzi wa Kanini**



**Kuandika**

Andika aya fupi kueleza ulichofanya wakati wa likizo ya mwezi wa Agosti.

105 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng, ng', gh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 105.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'ngozi'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **familia, madoadoa, afya.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

Soma hadithi huku mwanafunzi akiskiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Mbuzi wa Kanini**

Kanini ni msichana wa pekee katika familia ya mzee Majomvi. Kanini ana mbuzi anayempenda sana. Mbuzi huyo alipewa na mama yake Kasyoka kama zawadi ya kuwa mtoto mtiifu. Kanini alimpa mbuzi wake jina Kapendo. Kapendo ni mbuzi anayependeza sana. Mwili wake una madoadoa mazuri. Madoadoa hayo humfanya Kapendo kuonekana mrembo.

Kapendo alijengewa nyumba nzuri na fundi Makali. Kanini hufagia na kuosha nyumba ya Kapendo. Kila asubuhi Kanini humlisha mbuzi wake. Yeye humpa chakula na maji safi. Chakula na maji humpa mbuzi wa Kanini nguvu na afya nzuri.

"Kanini, njoo hapa mwanangu," baba yake alimwita. "Naomba tumuuze huyu mbuzi wako," baba alisema. "La! Baba," Kanini alikataa. "Mbuzi huyu anaweza kutupatia pesa nyingi sana," baba alimuambia. "Mbuzi huyu hunipa maziwa. Maziwa yake ni matamu. Mama alituambia maziwa ya mbuzi yanasaidia mwili wetu kukua, " Kanini alisema. "Sawa mtoto wangu. Mlinde na umtunze mbuzi wako," baba alisema. Kanini alifurahi na kumshukuru baba yake.

## Maswali

**T:** Kanini alipewa mbuzi na nani? *(Mama yake kasyoka)*

**U:** Mwili wa mbuzi ulikuwa na nini? *(Ulikuwa na madoadoa mazuri)*

**U:** Je, wewe unampenda mnyama gani? *(Mwanafunzi aelezee jibu lake)*

## Kuandika

**N: Andika sentensi tatu kuhusu likizo yako ya Agosti.**

**T:** Muongoze mwanafunzi kuandika aya fupi kuhusu likizo ya Agosti kwa hati nadhifu.

**U: Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye ukurasa wa 105.**

## Sarufi

**Matumizi ya -ako na -enu**

N: Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano: Kitabu chako kinapendeza. '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano: Vitabu vyenu vinapendeza.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 105.**

**Majibu**

1. chako
2. zenu
3. yenu

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike vitu vitano vinavyopatikana shuleni.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

**Kipindi cha 106 na 107** **Usalama wangu 2**

**Kipindi 106**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**sh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**she** **shi** **sho** **shu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| shu le ni | m si cha na | shu sho | a na i shi |
|---|---|---|---|
| **shuleni** | **msichana** | **shusho** | **anaishi** |

**Kipindi 107**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**SH** **sh**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a na ishi | wa ki washa | wa ki hatarisha |
|---|---|---|
| **anaishi** | **wakiwasha** | **wakihatarisha** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Soma sentensi zifuatazo kwa sauti.

1. Mwanafunzi **huyo** alitumia daraja kuvuka mto.
2. Watoto **hao** wanavukishwa barabara na mwalimu.
3. Dereva **huyo** anafuata sheria za barabarani.
4. Wavulana **hao** waliogelea.
5. Ndege **huyo** alipaa angani.
6. Polisi **hao** wanalinda usalama.
7. Mtoto **huyo** alisukuma gurudumu.
8. Viwavi **hao** walivamia shamba letu.

Mali ya Serikali ya Kenya 106

**Kipindi cha 106 na 107** **Usalama wangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Mrembo Zainabu**

Zainabu ni msichana wa miaka tisa. Msichana huyo alipenda usafi. Zainabu alijiunga na shule ya msingi ya Damiano. Kila siku alikuwa nadhifu. Aliepuka uchafu na vumbi kwa vyovyote vile.

Siku moja wanafunzi walienda uwanjani kucheza. Zainabu alivaa viatu vya thamani kubwa. Wasichana walicheza mchezo wa kukimbizana. Zainabu aliteleza na kuteguka. Mwalimu wake alimpa huduma ya kwanza. Baadaye alimpeleka katika zahanati kutibiwa. Zainabu alipata nafuu na kurudi shuleni.

Mwalimu aliwafunza wanafunzi hao kuhusu usalama. Aliwaonya kutocheza matopeni wasije wakaumia. Pia aliwafunza huduma ya kwanza. Shule ilinunua dawa, bendeji, sabuni na karai.

107 Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/sh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** shuleni, chuma

**U:** Endelea na maneno; shangazi, zahanati, shanga, sahani.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 106.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /sh/ /a/ silabi ni sha

**U:** Endelea na silabi; she, shi, sho, shu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 106.**

### Kusoma maneno kwa kutumia sialbi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** sha nga – shanga

**U:** Endelea na maneno; shuleni, msichana, Shusho.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 106.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **zahanati, huduma ya kwanza, bendeji.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 107.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Zainabu alijiunga na shule gani? *(Shule ya Msingi ya Damiano.)*

**T:** Wanafunzi walifunzwa kuhusu nini? *(Mafunzo ya usalama.)*

**U:** Vitu vilivyonunuliwa na shule hutumiwa vipi? *(Wakati wa kupeana huduma ya kwanza. Waeleze matumizi ya kila kifaa.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike maneno kwa kutumia herufi zifuatazo:

1. sh    2. th    3. gh    4. ng'

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya.

1. Zahati    2. Huduma ya kwanza    3. Bendeji

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 107: Usalama wangu 2

Kipindi cha 106 na 107 **Usalama wangu 2**

**Kipindi 106**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**sh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**she** **shi** **sho** **shu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| shu le ni | m si cha na | shu sho | a na i shi |
|---|---|---|---|
| **shuleni** | **msichana** | **shusho** | **anaishi** |

**Kipindi 107**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**SH** **sh**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a na ishi | wa ki washa | wa ki hatarisha |
|---|---|---|
| **anaishi** | **wakiwasha** | **wakihatarisha** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Soma sentensi zifuatazo kwa sauti.

1. Mwanafunzi **huyo** alitumia daraja kuvuka mto.
2. Watoto **hao** wanavukishwa barabara na mwalimu.
3. Dereva **huyo** anafuata sheria za barabarani.
4. Wavulana **hao** waliogelea.
5. Ndege **huyo** alipaa angani.
6. Polisi **hao** wanalinda usalama.
7. Mtoto **huyo** alisukuma gurudumu.
8. Viwavi **hao** walivamia shamba letu.

Mali ya Serikali ya Kenya

106

Kipindi cha 106 na 107 **Usalama wangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Mrembo Zainabu**

Zainabu ni msichana wa miaka tisa. Msichana huyo alipenda usafi. Zainabu alijiunga na shule ya msingi ya Damiano. Kila siku alikuwa nadhifu. Aliepuka uchafu na vumbi kwa vyovyote vile.

Siku moja wanafunzi walienda uwanjani kucheza. Zainabu alivaa viatu vya thamani kubwa. Wasichana walicheza mchezo wa kukimbizana. Zainabu aliteleza na kuteguka. Mwalimu wake alimpa huduma ya kwanza. Baadaye alimpeleka katika zahanati kutibiwa. Zainabu alipata nafuu na kurudi shuleni.

Mwalimu aliwafunza wanafunzi hao kuhusu usalama. Aliwaonya kutocheza matopeni wasije wakaumia. Pia aliwafunza huduma ya kwanza. Shule ilinunua dawa, bendeji, sabuni na karai.

107 Hakiuzwi

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** SH, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 106.**

## ★ Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo na usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li shangiliwa – alishangiliwa

**U:** Endelea na maneno; anaishi, wakiwasha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 106.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **zahanati, bendeji, huduma ya kwanza.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## ♦ Sarufi

**Matumizi ya huyo na hao**

**N:** Fafanua maana ya 'huyo' na 'hao'.

'Huyo' hutumika kuonyesha mtu au kiumbe chenye uhai kilicho mbali kidogo katika umoja.

Kwa mfano: Kifaranga **huyo** ni wangu.

'Hao' hutumiwa kama wingi wa 'huyo'. Hutumiwa kuashiria wingi wa majina wa watu au viumbe vyenye uhai.

Kwa mfano: Vifaranga **hao** ni wetu.

**T:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi, **ukurasa wa 107.**

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 106.**

Mwanafunzi asome sentensi kwa usahihi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore maumbo ya vitu hivi.

1. Kivukio cha barabara
2. Vidaraja
3. Moto
4. Bendeji

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 108: Usalama wangu 2

Kipindi cha 108 na 109 **Usalama wangu 2**

**Kipindi 108**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

th sh

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

the thi tho thu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| the mo me ta | the la thi ni | the ma ni ni | thi bi ti |
| **themometa** | **thelathini** | **themanini** | **thibiti** |

**Kipindi 109**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

TH th SH sh

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| hu thubutu | ku thibitisha | ali thamini |
| **huthubutu** | **kuthibitisha** | **alithamini** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Chagua jibu sahihi kwenye mabano kukamilisha sentensi zifuatazo.

1. Mama _______ alituambia tusicheze mbali. (hao, huyo)
2. Wahubiri _________ walituombea juzi. (hao, huyo)
3. Mwalimu _________ alituambia tusicheze nje wakati wa mvua. (huyo, hao)
4. Mwimbaji __________alitutumbuiza. (hao, huyo)
5. Viranja ___________walikutana. (huyo, hao)

Mali ya Serikali ya Kenya

108

Kipindi cha 108 na 109 **Usalama wangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Shusho aenda mjini**

Asubuhi moja Shusho alienda kumtembelea shangazi yake. Shangazi aliishi mjini Thogoto. Njiani aliiona saa iliyometameta. Aliinama na kuiokota. Aliona ni saa ya thamani. Aliichukua na kuendelea na safari yake. Shusho aliwapata watoto wakiwasha moto njiani. Watoto hao walikuwa wakihatarisha maisha yao. Aliwaambia waache kuuchezea moto. Alipofika karibu na barabara kuu, Shusho alimpata mtu asiyemjua. Aliogopa. Mtu huyo alisema anatafuta saa yake iliyokuwa imepotea. Shusho alimwonyesha saa aliyokuwa ameokota. Mtu huyo alifurahi kuiona saa yake. Alimshukuru na kwenda zake. Shusho alifika kwa shangazi. Alimweleza kisa cha saa. Shangazi alimpongeza kwa kurudisha saa hiyo.

109

Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/th/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** dhahabu, thamani

**U:** Endelea na maneno; thawabu, thelathini, tamani, thabiti, dhania.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** th, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 108.**

### Kusoma silabi

Tamka sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /th/ / a/ silabi ni tha

**U:** Endelea na silabi; the, thi, tho, thu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 108.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja ili kulisoma neno.

**N/T/U:** tha ma ni – thamani

**U:** Endelea na maneno; themometa, thelathini, thibiti.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 108.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno; **thamani, wakiwasha moto, wakihatarisha.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi, kwenye **ukurasa wa 109.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Shusho aliokota nini njiani? *(Saa ya thamani)*

**T:** Mgeni alikuwa akitafuta nini? *(Saa yake)*

**U:** Je, unafikiri ni vizuri kuongea na wageni au watu usiowajua? *(La/ ndio. Wanafunzi watoe sababu)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike sentensi katika wingi.

1. Mwanafunzi huyo anavuka. (Wanafunzi hao wanavuka.)
2. Dereva huyo anaendesha gari. (Madereva hao wanaendesha magari.)
3. Mwalimu huyo anazima moto. (Walimu hao wanazima moto)

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi amhadithie mlezi wake hadithi ya 'Shusho aenda mjini'.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 109: Usalama wangu 2

Kipindi cha 108 na 109 **Usalama wangu 2**

**Kipindi 108**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**th** **sh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**the** **thi** **tho** **thu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| the mo me ta | the la thi ni | the ma ni ni | thi bi ti |
|---|---|---|---|
| **themometa** | **thelathini** | **themanini** | **thibiti** |

**Kipindi 109**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**TH** **th** **SH** **sh**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu thubutu | ku thibitisha | ali thamini |
|---|---|---|
| **huthubutu** | **kuthibitisha** | **alithamini** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Chagua jibu sahihi kwenye mabano kukamilisha sentensi zifuatazo.

1. Mama ________ alituambia tusicheze mbali. (hao, huyo)
2. Wahubiri __________ walituombea juzi. (hao, huyo)
3. Mwalimu __________ alituambia tusicheze nje wakati wa mvua. (huyo, hao)
4. Mwimbaji __________alitutumbuiza. (hao, huyo)
5. Viranja ___________walikutana. (huyo, hao)

Mali ya Serikali ya Kenya

108

Kipindi cha 108 na 109 **Usalama wangu 2**

**Kusoma hadithi**




**Shusho aenda mjini**

Asubuhi moja Shusho alienda kumtembelea shangazi yake. Shangazi aliishi mjini Thogoto. Njiani aliiona saa iliyometameta. Aliinama na kuiokota. Aliona ni saa ya thamani. Aliichukua na kuendelea na safari yake. Shusho aliwapata watoto wakiwasha moto njiani. Watoto hao walikuwa wakihatarisha maisha yao. Aliwaambia waache kuuchezea moto. Alipofika karibu na barabara kuu, Shusho alimpata mtu asiyemjua. Aliogopa. Mtu huyo alisema anatafuta saa yake iliyokuwa imepotea. Shusho alimwonyesha saa aliyokuwa ameokota. Mtu huyo alifurahi kuiona saa yake. Alimshukuru na kwenda zake. Shusho alifika kwa shangazi. Alimweleza kisa cha saa. Shangazi alimpongeza kwa kurudisha saa hiyo.

109

Hakiuzwi

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** TH, SH

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 108.**

## ★ Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo na usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li thibitisha — alithibitisha

**U:** Endelea na maneno; huthubutu, kuthibitisha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 108.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati: **thamani, wakihatarisha, wakiwasha moto.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya 'huyo' na 'hao'**

**N:** Fafanua maana ya '**huyo**' na '**hao**'.

'Huyo' hutumika kuonyesha mtu au kiumbe chenye uhai kilicho mbali kidogo katika umoja.

Kwa mfano: Ng'ombe **huyo** ni mkubwa.

'Hao' hutumiwa kama wingi wa 'huyo'. Hutumiwa kuashiria wingi wa majina wa watu au viumbe vyenye uhai.

Kwa mfano: Ng'ombe **hao** ni wakubwa.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi, **ulurasa wa 109.**

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 108.**

**Majibu**

1. huyo
2. hao
3. huyo
4. huyo
5. hao

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno yanayoanza na sauti /th/.

Tarehe: ________________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 110: Usalama wangu 2

Kipindi cha 110 **Usalama wangu 2**

**Kipindi 110**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

th sh

Jedwali la silabi

Tumia silabi kwenye jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: shu le ni – shuleni**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| shu | the | du | le | ma | thi |
| na | hu | zi | ni | la | sha |

◆ **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Jaza mapengo kwa kutumia **huyo** au **hao**.

1. Wanafunzi _________ wanavuka barabara katika alama ya kivukio.
2. Polisi ________ anakagua magari kando ya barabara.
3. Madereva ________ wamesimamisha magari katika alama ya kivukio.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Dereva Namu**



**Kuandika**

Andika sentensi mbili kuhusu kilichofanyika mwishoni mwa hadithi ya **Shusho aenda mjini.**

Mali ya Serikali ya Kenya

110

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** th, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 110.**

## ★ Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'shuleni'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **ramani, mikanda ya usalama, akitii.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Dereva Namu**

Namu ni dereva hodari. Siku moja aliamka asubuhi kuelekea kazini. Alisahau kubeba ramani yake ya kumuelekeza mjini. Namu alikuwa mwangalifu barabarani. Alikuwa akitii sheria za barabarani. Namu alipofika katika kivukio cha wanyama alipata ajali imetokea. Ajali hiyo ilisababishwa na dereva wa basi ambaye hakuwa mwangalifu.

Mbali na kuwa mlevi, dereva huyo alikuwa akizungumza kwa simu huku akiliendesha gari. Dereva huyo alimgonga ndovu aliyekuwa akivuka barabara.

Namu alisimamisha gari lake na kushuka. Alichukua simu yake ya mkononi na kuwapigia polisi. "Halo! Halo! Nawapigia kuripoti kuwa kuna ajali imetokea," Namu alisema. "Ajali imetokea wapi?" Polisi aliuliza. "Barabara ya kwenda Kijiwetanga, karibu na soko la Maweni," Namu alisema. Polisi walifika bila kuchelewa. Baada ya muda mfupi, abiria wote walitolewa garini. Wote walikuwa wamepata majeraha madogo madogo. Hii ni kwa sababu walikuwa wamejifunga mikanda ya usalama. Polisi walimuomba Namu awapeleke hospitalini. Namu alikuwa na wasiwasi kwa sababu hakuwa na ramani ambayo ingemwelekeza kwenda mjini. Polisi walimuonyesha ramani iliyo kwenye simu yake. Namu alifurahi sana na kuelekeza gari lake hospitalini. Tangu siku hiyo alijiamini sana katika uendeshaji wake.

## ? Maswali

**T:** Dereva Namu alisahau kubeba nini alipokuwa akienda kazini? *(Ramani yake ya kumuelekeza mjini)*

**U:** Ajali ilisababishwa na nini? *(Ajali hiyo ilisababishwa na dereva wa basi ambaye hakuwa mwangalifu)*

**U:** Je, unafikri ni kwa nini madereva wanapaswa kuwa waangalifu? *(Wanafunzi watoe hoja zao.)*

## Kuandika

**N:** **Andika sentensi moja kuhusu kilichofanyika mwishoni mwa hadithi ya 'Shusho aenda mjini'.**

**T:** Waongoze wanafunzi kuandika sentensi moja **kuhusu kilichofanyika mwishoni mwa hadithi ya 'Shusho aenda mjini' kwa hati nadhifu.**

**U:** **Wanafunzi wafanye zoezi la kuandika kwenye ukurasa wa 110.**

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya 'huyo' na 'hao'**

N: Fafanua maana ya 'huyo' na 'hao'.

'Huyo' hutumika kuonyesha mtu au kiumbe chenye uhai kilicho mbali kidogo katika umoja. Kwa mfano: Kondoo huyo ni wetu.

'Hao' hutumiwa kama wingi wa 'huyo'. Hutumiwa kuashiria wingi wa majina wa watu au viumbe vyenye uhai. Kwa mfano: Kondoo hao ni wetu.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 110.**

**Majibu**

1. hao 2. huyo 3. hao

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno yaliyo na sauti **/sh/** au **/th/.**

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 111 na 112 **Usalama wangu 2**

**Kipindi 111**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**th**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**the thi tho thu ghe**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| the ma ni ni | tha wa bu | the la thi ni | thu bu tu |
| **themanini** | **thawabu** | **thelathini** | **thubutu** |

**Kipindi 112**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**TH** **th**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a li thibiti | wa li thibitisha | tu li thubutu |
| **alithibiti** | **walithibitisha** | **tulithubutu** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Katika vikundi vya wanafunzi wawili, tunga sentensi nne ukitumia **huyo** au **hao**.



Hakiuzwi

Kipindi cha 111 na 112 **Usalama wangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Dereva Musa**

Musa alikuwa dereva wa matatu za Koma. Tangu utotoni, Musa aliyapenda magari ya abiria. Musa alipomaliza shule alisomea kazi ya udereva. Alipata cheti cha kuendesha magari ya abiria. Aliendesha matatu za mjini hadi Koma. Abiria walimpenda kwa upole na uangalifu wake. Gari lake lilikuwa na mikanda ya usalama. Pia lilienda mwendo wa kadiri. Nauli ya matatu yake haikupanda hata wakati wa mvua. Siku moja Musa aliamkia kazi yake ya udereva. Akiwa barabarani, aliliona gari la mwenzake likiyumbayumba. Kumbe dereva huyo alikuwa mlevi. Matatu ya Musa iligongwa na gari la dereva mlevi. Watu walipata majeraha madogo madogo. Watu hao hawakuwa wamefunga mikanda ya usalama.

Mali ya Serikali ya Kenya



## Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/th/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** thamani, tema

**U:** Endelea na maneo; tambua, thelathini, thabiti.

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** th, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 111.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /th / /a/ silabi ni tha

**U:** Endelea na silabi; the, thi, tho, thu, ghe.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 111.**

## Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: thi bi ti ka – thibitika

**U:** Endelea na maneno; thawabu, thelathini, thubutu.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 111.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno: **majeraha, iligongwa, mikanda ya usalama.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 112.**

## Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Musa alisomea kazi gani? *(Kazi ya udereva)*

**T:** Kwa nini watu walipata majeraha madogo madogo? *(Hawakufunga mikanda ya usalama)*

**U:** Unafikiri unapaswa kufanya nini unapovuka barabara? *(Kutazama pande za kulia na kushoto ili usigongwe na gari, tumia kivukio)*

## Zoezi

Mwanafunzi aunde maneno kwa kutumia herufi zifuatazo.

1. th 2. sh 3. ny

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya.

1. Mikanda ya usalama 2. Gari 3. Matatu

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________



Hakiuzwi

# Kipindi cha 112: Usalama wangu 2

Kipindi cha 111 na 112 **Usalama wangu 2**

**Kipindi 111**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  th

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  the thi tho thu ghe

- Soma maneno ukitumia silabi.

| the ma ni ni | tha wa bu | the la thi ni | thu bu tu |
|---|---|---|---|
| **themanini** | **thawabu** | **thelathini** | **thubutu** |

**Kipindi 112**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  TH th

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li thibiti | wa li thibitisha | tu li thubutu |
|---|---|---|
| **alithibiti** | **walithibitisha** | **tulithubutu** |

- **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Katika vikundi vya wanafunzi wawili, tunga sentensi nne ukitumia **huyo** au **hao**.

111

Hakiuzwi

Kipindi cha 111 na 112 **Usalama wangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Dereva Musa**

Musa alikuwa dereva wa matatu za Koma. Tangu utotoni, Musa aliyapenda magari ya abiria. Musa alipomaliza shule alisomea kazi ya udereva. Alipata cheti cha kuendesha magari ya abiria. Aliendesha matatu za mjini hadi Koma. Abiria walimpenda kwa upole na uangalifu wake. Gari lake lilikuwa na mikanda ya usalama. Pia lilienda mwendo wa kadiri. Nauli ya matatu yake haikupanda hata wakati wa mvua. Siku moja Musa aliamkia kazi yake ya udereva. Akiwa barabarani, aliliona gari la mwenzake likiyumbayumba. Kumbe dereva huyo alikuwa mlevi. Matatu ya Musa iligongwa na gari la dereva mlevi. Watu walipata majeraha madogo madogo. Watu hao hawakuwa wamefunga mikanda ya usalama.

Mali ya Serikali ya Kenya

112

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** TH, th.

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 111.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** a li thibiti – alithibiti

**U:** Endelea na neno; walithibitisha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 111.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **mikanda ya usalama, aligongwa, majeraha.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya huyo na hao**

**N:** Fafanua maana ya 'huyo' na 'hao'.

'Huyo' hutumika kuonyesha mtu au kiumbe chenye uhai kilicho mbali kidogo katika umoja.

Kwa mfano: Mwanafunzi **huyo** anasoma.

'Hao' hutumiwa kama wingi wa 'huyo'. Hutumiwa kuashiria wingi wa watu au viumbe vyenye uhai.

Kwa mfano: Wanafunzi **hao** wanasoma.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 111.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore vitu hivi.

1. Kivukio cha barabara
2. Vidaraja
3. Moto
4. Gari

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 113: Usalama wangu 2

Kipindi cha 113 na 114 **Usalama wangu 2**

**Kipindi 113**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**sh** **th**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**shi** **sho** **shu** **thu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| shu ghu li | u sha u ri | ku e nde sha | shu le ni |
|---|---|---|---|
| **shughuli** | **ushauri** | **kuendesha** | **shuleni** |

**Kipindi 114**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**SH** **sh** **TH** **th**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu pishana | hu shirikiana | hu athirika |
|---|---|---|
| **hupishana** | **hushirikiana** | **huathirika** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Andika sentensi tatu ukitumia **huyo** au **hao**.



Kipindi cha 113 na 114 **Usalama wangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Usalama**

Usalama ni hali ya kutokuwepo na hatari yoyote. Usalama ni muhimu katika maisha ya kila mtu. Mambo mengi yanasababisha ukosefu wa usalama. Watoto wengi wanapenda kucheza na moto. Watoto hao huhatarisha maisha yao. Kuwasha kiberiti ovyoovyo kunaweza kuanzisha moto ukachoma nyumba. Moto unapowaka, mtu anapaswa kukaa mbali.

Ajali nyingi pia husababishwa na watu kutokuwa makini. Kwa mfano, wengine hawatumii kivukio cha barabara. Kivukio cha barabara ni sehemu salama ya kuvukia. Watu wanapaswa kutumia daraja la kuvukia barabara.

Watoto wengine hupenda kucheza majini. Mtoto anayechezea majini huhatarisha maisha yake. Mtoto huyo anaweza kuwa mgonjwa. Mtoto huyo anaweza pia kuzama majini.



### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/sh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** shukuru, chakula

**U:** Endelea na maneno; shughuli, shauri, chuma, sahihi.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** sh, th

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 113.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /sh / /a/ silabi ni sha

**U:** Endelea na silabi; shi, sho, shu, thu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 113.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: m sha le – mshale

**U:** Endelea na maneno; shughuli, ushauri, kuendesha, shuleni.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 113.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **kuwasha kiberiti, daraja la kuvukia, kuzama majini.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 114.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Ajali husababishwa na nini? *(Na watu kutokuwa makini)*

**T:** Watoto wengi hupenda kufanya nini? *(Kucheza na moto, kucheza majini)*

**U:** Taja mambo yayosababisha ajali barabrani. *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi ajadili na mwenzake umuhimu wa usalama shuleni.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike hatari za kucheza kwenye mvua.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 113 na 114 **Usalama wangu 2**

**Kipindi 113**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**sh** **th**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**shi** **sho** **shu** **thu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| shu ghu li | u sha u ri | ku e nde sha | shu le ni |
|---|---|---|---|
| **shughuli** | **ushauri** | **kuendesha** | **shuleni** |

**Kipindi 114**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**SH** **sh** **TH** **th**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu pishana | hu shirikiana | hu athirika |
|---|---|---|
| **hupishana** | **hushirikiana** | **huathirika** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Andika sentensi tatu ukitumia **huyo** au **hao**.

113 Hakiuzwi

Kipindi cha 113 na 114 **Usalama wangu 2**

**Kusoma hadithi**



**Usalama**

Usalama ni hali ya kutokuwepo na hatari yoyote. Usalama ni muhimu katika maisha ya kila mtu. Mambo mengi yanasababisha ukosefu wa usalama. Watoto wengi wanapenda kucheza na moto. Watoto hao huhatarisha maisha yao. Kuwasha kiberiti ovyoovyo kunaweza kuanzisha moto ukachoma nyumba. Moto unapowaka, mtu anapaswa kukaa mbali.

Ajali nyingi pia husababishwa na watu kutokuwa makini. Kwa mfano, wengine hawatumii kivukio cha barabara. Kivukio cha barabara ni sehemu salama ya kuvukia. Watu wanapaswa kutumia daraja la kuvukia barabara.

Watoto wengine hupenda kucheza majini. Mtoto anayechezea majini huhatarisha maisha yake. Mtoto huyo anaweza kuwa mgonjwa. Mtoto huyo anaweza pia kuzama majini.

Mali ya Serikali ya Kenya 114

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** SH, sh, TH, th

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 113.**

## ★ Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** hu hatarisha – huhatarisha

**U:** Endelea na maneno; hupishana, hushirikiana.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 113.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **kuwasha kiberiti, daraja la kuvukia, kuzama majini.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya huyo na hao**

**N:** Fafanua maana ya 'huyo' na 'hao'.

'Huyo' hutumika kuonyesha mtu au kiumbe chenye uhai kilicho mbali kidogo katika umoja.

Kwa mfano: Mgeni **huyo** amefika.

'Hao' hutumiwa kama wingi wa 'huyo'. Hutumiwa kuashiria wingi wa majina ya watu au viumbe vyenye uhai.

Kwa mfano: Wageni **hao** wamefika.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 113.**

Mwanafunzi aandike sentensi sahihi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike njia nne za kudumisha usalama wake akiwa nyumbani.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 115 **Usalama wangu 2**

**Kipindi 115**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

SH sh TH th

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: sho ka – shoka**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| sho | le | tha | cho | bu |
| ke | ka | shu | wa | ma |

◆ **Sarufi: Matumizi ya huyo na hao**

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia **huyo** au **hao**.

1. Mama __________ alikuwa sokoni.
2. Wezi __________ walikuwa wameficha sura zao.
3. Mfanyibiashara __________ aliweka pesa zake benki.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Neria na Lelisho**



**Kuandika**

Tunga sentensi kwa kutumia maneno haya.

1. Mikanda
2. Iligongwa
3. Majeraha
4. Kuchoma

115

Hakiuzwi

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** SH, sh, TH, th

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 115.**

## ★ Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'shoka'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati:, **kuzama majini, ajali mchezoni.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Funza msamiati:, **kuzama majini, ajali mchezoni.**

Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Neria na Lelisho**

Neria na Lelisho ni wanafunzi wa darasa la pili. Wao hushirikiana katika shughuli nyingi za maisha. Neria humsaidia Lelisho kuvuka mto kila asubuhi na jioni wanapoenda na kutoka shuleni. "Mbona huvuki mto kwa kutumia daraja?" Neria aliuliza Lelisho.

"Nimeamua kutotumia daraja kwa sababu maji ni tulivu upande huu wa mto," Lelisho alimueleza Neria. Neria alimueleza Lelisho kuwa mtu asiyekuwa mwangalifu anaweza kuzama majini.

Wakati wa mapumziko, Neria na Lelisho walienda uwanjani kucheza na wanafunzi wenzao. Walicheza mchezo wa kandanda. Neria alikuwa mchezaji bora na alifunga mabao mawili. Lelisho alikuwa mlinda lango hodari. Hakuruhusu bao lolote lifungwe. Wanafunzi wote walifurahia mchezo huo. Kwa bahati mbaya wanafunzi wawili waligongana na kupata ajali mchezoni. Mmoja wa wale waliopata ajali alitokwa na damu nyingi. Mashabiki wa timu zote mbili walitaka kupigana. Timu iliyoshindwa ililaumu iliyoshinda. Lelisho alikimbia ofisini kumwita mwalimu wao wa darasa. Mwalimu alipofika aliwatuliza wanafunzi. "Si vyema kupigana. Ni vizuri kuishi kwa amani," mwalimu alisema. Mwalimu aliwapa huduma ya kwanza. Wawili hao walipata nafuu na kuruhusiwa kwenda darasani.

## ? Maswali

**N:** Neria humsaidia Lelisho kufanya nini? *(Kuvuka mto asubuhi)*

**T:** Wanafunzi walicheza mchezo gani? *(Kandanda)*

**U:** Ni madhara gani ambayo yanaweza kumpata mtoto asiyekuwa mwangalifu? *(Kubali jibu lolote sahihi)*

## Kuandika

**N:** **Andika sentensi moja ukitumia kifungu 'mikanda ya usalama'.**

**T:** Waongoze wanafunzi kuandika sentensi moja wakitumia neno **'iligongwa'** **kwa hati nadhifu.**

**U:** **Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika** kwenye **ukurasa wa 115.**

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya huyo na hao**

N: 'Huyo' hutumika kuonyesha mtu au kiumbe chenye uhai kilicho mbali kidogo katika umoja.

Kwa mfano: Mwalimu **huyo** alifunza.

'Hao' hutumiwa kama wingi wa 'huyo'. Hutumiwa kuashiria wingi wa majina ya watu au viumbe vyenye uhai.

Kwa mfano: Walimu **hao** walifunza.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 115.**

**Majibu**

1. huyo 2. hao 3. huyo

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya.

1. Usalama 2. Barabara 3. Ajali

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 116: Hali ya anga 2

Kipindi cha | 116 na 117 | **Hali ya anga 2**

**Kipindi 116**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

a b ch d dh

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ba cha da dha

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| za ma ni | ma to ne | ra di | ma wi ngu |
|---|---|---|---|
| **zamani** | **matone** | **radi** | **mawingu** |

**Kipindi 117**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

e f g h i

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li wa shika | wa li kusanyika | ya li kosekana |
|---|---|---|
| **waliwashika** | **walikusanyika** | **yalikosekana** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Katika vikundi vya wanafunzi wawili, msomee mwenzako sentensi zifuatazo.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | **Wewe** **ul**isoma vitabu vingi. | **Nyinyi** **ml**isoma vitabu vingi. |
| 2. | **Wewe** **ul**ipita mtihani. | **Nyinyi** **ml**ipita mtihani. |
| 3. | **Wewe** **ul**inyeshewa. | **Nyinyi** **ml**inyeshewa. |
| 4. | **Wewe** **ul**ifika mapema. | **Nyinyi** **ml**ifika mapema. |

Mali ya Serikali ya Kenya 116

Kipindi cha | 116 na 117 | **Hali ya anga 2**

**Kusoma hadithi**



**Mvua ya ajabu**

Kijiji cha Ludacho kilikosa mvua kwa siku nyingi. Mito ilikauka na maji yalikosekana. Upepo mkali ulivuma kila asubuhi. Watu wa kijiji hiki walishikwa na wasiwasi. Wanyama walianza kufa na mimea kukauka. Jioni moja wazee wa kijiji hiki walikusanyika. Waliketi chini ya mti wa *mugumo* kwa maombi ya mvua. Walipokuwa kwenye maombi, mawingu meusi yalitanda na mngurumo mkubwa wa radi ukasikika. Ghafla, matone ya mvua yalianza kuanguka. Kila mtu alikimbilia kwenye nyumba iliyokuwa karibu naye kujikinga mvua. Mvua kubwa ya ajabu ilinyesha kwa muda wa saa moja. Kila mwanakijiji alifurahi na kumshukuru Mungu. Wewe ungekuwa mmoja wao ungefurahia?

117 Hakiluzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/a/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** ama, ua

**U:** Endelea na maneno; nunua, napenda, nyoa, nyama.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** a, b, ch, d, dh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 116**. Bainisha irabu katika herufi zilizofunzwa /a/.

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /b / /a/ silabi ni ba

**U:** Endelea na silabi; cha, da, dha.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 116.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja ili kulisoma neno.

**N/T/U:** wa ze e – wazee

**U:** Endelea na maneno; zamani, matone, radi.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 116.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **upepo mkali, mawingu, matone.** Tumia nyenzo zinazoashiria hali za anga unapofunza maana ya maneno.

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 117.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kwa nini wazee wa kijiji walikusanyika? *(Kwa maombi ya mvua)*

**T:** Je, unadhani mvua ikinyesha nyingi italeta nini? *(Mafuriko, maafa)*

**U:** Kwa nini wanakijiji walifurahi? *(Walipata maji, mifugo wao walipata maji)*

### Zoezi

Soma sentensi hizi kwa sauti na aziandike kitabuni mwake.

1. Upepo mkali ulivuma kila asubuhi.
2. Mawingu meusi yalitanda angani.
3. Matone mazito ya mvua yalimwagika.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore ishara za mvua, mawingu na upepo.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 116 na 117 **Hali ya anga 2**

**Kipindi 116**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

a b ch d dh

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ba cha da dha

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| za ma ni | ma to ne | ra di | ma wi ngu |
| **zamani** | **matone** | **radi** | **mawingu** |

**Kipindi 117**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

e f g h i

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| wa li wa shika | wa li kusanyika | ya li kosekana |
| **waliwashika** | **walikusanyika** | **yalikosekana** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Katika vikundi vya wanafunzi wawili, msomee mwenzako sentensi zifuatazo.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | **Wewe ul**isoma vitabu vingi. | **Nyinyi ml**isoma vitabu vingi. |
| 2. | **Wewe ul**ipita mtihani. | **Nyinyi ml**ipita mtihani. |
| 3. | **Wewe ul**inyeshewa. | **Nyinyi ml**inyeshewa. |
| 4. | **Wewe ul**ifika mapema. | **Nyinyi ml**ifika mapema. |

Mali ya Serikali ya Kenya

116

Kipindi cha 116 na 117 **Hali ya anga 2**

**Kusoma hadithi**



**Mvua ya ajabu**

Kijiji cha Ludacho kilikosa mvua kwa siku nyingi. Mito ilikauka na maji yalikosekana. Upepo mkali ulivuma kila asubuhi. Watu wa kijiji hiki walishikwa na wasiwasi. Wanyama walianza kufa na mimea kukauka. Jioni moja wazee wa kijiji hiki walikusanyika. Waliketi chini ya mti wa *mugumo* kwa maombi ya mvua. Walipokuwa kwenye maombi, mawingu meusi yalitanda na mngurumo mkubwa wa radi ukasikika. Ghafla, matone ya mvua yalianza kuanguka. Kila mtu alikimbilia kwenye nyumba iliyokuwa karibu naye kujikinga mvua. Mvua kubwa ya ajabu ilinyesha kwa muda wa saa moja. Kila mwanakijiji alifurahi na kumshukuru Mungu. Wewe ungekuwa mmoja wao ungefurahia?

117 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** e, f, g, h, i, j

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 116.** Bainisha irabu katika herufi zilizofunzwa /e/, /i/

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li zuru – alizuru

**U:** Endelea na maneno; waliwashika, walikusanyika.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 116.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **upepo mkali, mawingu, matone.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

**N:** Fafanua maana ya nafsi ya kwanza na wakati uliopita. 'Wewe' hutumiwa katika nafsi ya pili hali ya umoja. Huonyesha mtu wa pili baada ya wa kwanza, 'mimi'.

Kwa mfano: Wewe ulikula chakula.

Wewe ulisoma kitabu. 'U' hutumiwa pamoja na 'wewe' kuonyesha umoja. 'li' hutumiwa kuonyesha wakati uliopita.

'Wewe' inapotumiwa na wakati uliopita huwa inaonyesha kuwa jambo lilitendeka wakati uliopita.

'Nyinyi' na 'm' hutumiwa kama hali ya wingi wa nafsi ya kwanza. 'li' hutumiwa pamoja na 'nyinyi' na 'm' kuonyesha wingi.

Kwa mfano: Nyinyi mlikula chakula.

Nyinyi mlisoma vitabu.

**T:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 116.**

Mwanafunzi asome sentensi kwa usahihi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi nne akitumia neno wewe kwa wakati uliopita.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 118: Hali ya anga 2

Kipindi cha | 118 na 119 | **Hali ya anga 2**

**Kipindi 118**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

j  k  l  m  n

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ja  ke  la  me  na

Soma maneno ukitumia silabi.

▲ ma wi ngu — **mawingu**   u pe po — **upepo**   tu li vu — **tulivu**   te nge ne za — **tengeneza**

**Kipindi 119**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng'  ny  o  p  r

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

ya li onekana — **yalionekana**   a ki tengeneza — **akitengeneza**   a li u penda — **aliupenda**

♦ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Tumia nafsi ya pili wakati uliopita kujaza mapengo.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Wewe ulienda shuleni. | ____________ |
| 2. | ____________ | Nyinyi mlilima shamba. |
| 3. | Wewe ulikariri shairi. | ____________ |
| 4. | ____________ | Nyinyi mlikwea milima. |
| 5. | Wewe ulitunga wimbo. | ____________ |

Mali ya Serikali ya Kenya   118

Kipindi cha | 118 na 119 | **Hali ya anga 2**

**Kusoma hadithi**



**Nelima na Kasuku**

Hali ya anga ilikuwa tulivu baada ya mvua nyingi kunyesha. Mawingu mazito bado yalionekana juu angani. Jua lilifunikwa na mawingu yaliyokuwa meusi. Nelima alikuwa akitengeneza nyumba ya udongo karibu na maua mekundu na meupe. Kasuku alitua juu ya mti na kuimba wimbo mtamu. Nelima aliupenda wimbo wa kasuku. Alimuuliza, "Ulijuaje kuimba?" Hakujibu.

"Nelima mzuri, nipatie ua jekundu. Napenda ua jekundu," kasuku aliimba. "Kasuku, wewe una kelele! Chukua ua jeupe lapendeza," Nelima alimjibu. Nelima alichukua ua jeupe na kumpa kasuku. Kasuku aliruka na kwenda zake na ua jeupe mdomoni.

119   Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/l/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** lilifunikwa, mawingu

**U:** Endelea na maneno; lapendeza, kuimba, lala, alivuka.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** y, ng, t, p

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 118.** Sisitiza kuwa herufi hizi hazina irabu.

### Kusoma silabi

Tamka sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /j /a/ silabi ni ja

**U:** Endelea na silabi; ke, la, me, na.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 118.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** ya li ta nda – yalitanda

**U:** Endelea na maneno; mawingu, upepo, tulivu.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 118.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **mvua nyingi, mawingu mazito, tulivu.** Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 119.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kasuku alitua juu ya mti na kufanya nini? *(Akiimba wimbo mtamu)*

**T:** Kwa nini Nelima alimpa kasuku ua jeupe? *(Ua jeupe lapendeza)*

**U:** Je, mvua inapokosekana kwa wakati mrefu ni nini hufanyika? *(Mito hukauka, wanyama hufa kwa kukosa chakula na maji, binadamu hukosa chakula na maji.)*

### Zoezi

Mwanafunzi ajaze mapengo kwa kutumia nafsi ya pili umoja na wingi.

1. ____________ alilima shamba. (Yeye, Nyinyi)
2. ____________ mlisoma hadithi. (Yeye, Nyinyi)
3. ____________ mlikula matunda. (Nyinyi, Yeye)

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi nne sahihi kwa kutumia **'nyinyi'**.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 119: Hali ya anga 2

Kipindi cha 118 na 119 **Hali ya anga 2**

**Kipindi 118**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

j k l m n

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ja ke la me na

Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ▲ ma wi ngu | u pe po | tu li vu | te nge ne za |
| **mawingu** | **upepo** | **tulivu** | **tengeneza** |

**Kipindi 119**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng' ny o p r

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ya li onekana | a ki tengeneza | a li u penda |
| **yalionekana** | **akitengeneza** | **aliupenda** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Tumia nafsi ya pili wakati uliopita kujaza mapengo.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Wewe ulienda shuleni. | |
| 2. | | Nyinyi mlilima shamba. |
| 3. | Wewe ulikariri shairi. | |
| 4. | | Nyinyi mlikwea milima. |
| 5. | Wewe ulitunga wimbo. | |

Mali ya Serikali ya Kenya

118

Kipindi cha 118 na 119 **Hali ya anga 2**

**Kusoma hadithi**



**Nelima na Kasuku**

Hali ya anga ilikuwa tulivu baada ya mvua nyingi kunyesha. Mawingu mazito bado yalionekana juu angani. Jua lilifunikwa na mawingu yaliyokuwa meusi. Nelima alikuwa akitengeneza nyumba ya udongo karibu na maua mekundu na meupe. Kasuku alitua juu ya mti na kuimba wimbo mtamu. Nelima aliupenda wimbo wa kasuku. Alimuuliza, "Ulijuaje kuimba?" Hakujibu.

"Nelima mzuri, nipatie ua jekundu. Napenda ua jekundu," kasuku aliimba. "Kasuku, wewe una kelele! Chukua ua jeupe lapendeza," Nelima alimjibu. Nelima alichukua ua jeupe na kumpa kasuku. Kasuku aliruka na kwenda zake na ua jeupe mdomoni.

119 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng', ny, o, p, q, r

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 118.** Bainisha irabu katika herufi zilizofunzwa **/o/.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** ya li anguka – yalianguka

**U:** Endelea na maneno; yalionekana, akitengeneza.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 118.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **tulivu, mvua nyingi, mawingu mazito.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

**N:** Fafanua maana ya nafsi ya kwanza na wakati uliopita.

'Wewe' hutumiwa katika nafsi ya pili hali ya umoja.

Huonyesha mtu wa pili baada ya wa kwanza, 'mimi'.

Kwa mfano: Wewe ulivuka barabara.

'U' hutumiwa pamoja na 'wewe' kuonyesha umoja.

'li' hutumiwa kuonyesha wakati uliopita. 'Wewe' inapotumiwa na wakati uliopita huwa inaonyesha kuwa jambo lilitendeka wakati uliopita.

'Nyinyi' na 'm' hutumiwa kama hali ya wingi wa nafsi ya kwanza. 'li' hutumiwa pamoja na 'nyinyi' na 'm' kuonyesha wingi.

Kwa mfano: Nyinyi mlivuka barabara.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 118.**

**Majibu**

1. Nyinyi mlienda shuleni.
2. Wewe ulilima shamba.
3. Nyinyi mlikariri shairi.
4. Wewe ulikwea mlima.
5. Nyinyi mlitunga nyimbo.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike vifungu vya maneno vifuatavyo katika nafsi ya pili wingi.

**Majibu**

| | |
|---|---|
| 1. Wewe ulisoma. | Nyinyi mlisoma. |
| 2. Wewe ulikula. | Nyinyi mlikula. |
| 3. Wewe ulitembea. | Nyinyi mlitembea. |

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________



Hakiuzwi

Kipindi cha 120 **Hali ya anga 2**

**Kipindi 120**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

s t th u v

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: wi ma – wima**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ngu | po | pe | vu | wi | ma |
| m | a | tu | u | to | ne |

♦ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Jaza mapengo ukitumia nafsi ya pili wakati uliopita.

**Kwa mfano:** Wewe **ulienda** (enda) nyumbani.

Nyinyi **mlienda** (enda) shuleni.

1. Nyinyi _________ (cheza) juani.
2. Wewe _________ (lima) shamba.
3. Nyinyi _________ (hesabu) nyota.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Mwezi**



**Kuandika**

Tunga sentensi tatu ukitumia maneno haya: upepo, matone, mawingu.

Mali ya Serikali ya Kenya 120

## ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** s, t, th, u, v

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 120.** Bainisha irabu katika herufi zilizofunzwa /u/.

## Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'wima'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **jua, upepo, mvua.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Mwezi**

Hapo zamani za kale palikuwa na mtu aliyeitwa Mwezi. Mwezi alikuwa na watoto watatu. Watoto hao walikuwa Jua, Nyota na Upepo. Wote waliishi pamoja angani. Kila mmoja alikuwa na kazi yake. Jua alifanya kazi ya kuleta mwangaza mchana. Nyota naye alimetameta na kufurahisha watu usiku. Kazi ya Upepo ilikuwa kusafisha na kuzoa taka. Mwezi alimpenda Jua kuliko wengine.

Hii ni kwa sababu jua alikuwa na bidii katika kazi zake. Nyota naye alimpenda ndugu yake mkubwa Jua. Hiyo ilisababisha upepo kutompenda Jua hata kidogo.

Siku moja, Mwezi alienda kuokota kuni na kuwaacha watoto wake nyumbani. Upepo alitafuta kiboko na kumfukuza Jua. Jua alipokuwa akitoroka, alianguka kwa ngurumo na radi. Alilia kwa uchungu. Machozi yake yalianguka ardhini. Hapo ndipo mvua ikanyesha kwa mara ya kwanza. Mwezi alimkaribisha mvua kwa familia yake. Hatimaye alileta watoto wake pamoja akawashauri wasameheane na waishi kwa upendo. Tangu siku hiyo watoto wa Mwezi walishirikiana kutimiza juhudi zao.

## ? Maswali

**T:** Watoto waliotajwa kwenye hadithi waliitwa nani? *(Jua, Nyota na Upepo)*

**U:** Kwa nini Upepo alimfukuza Jua? *(Kwa sababu upepo hakumpenda)*

**U:** Je, unafikiria hadithi hii ni ya ukweli au la? Eleza maoni yako. *(Wanafunzi wajibu na kueleza sababu zao)*

## Kuandika

**N: Andika sentensi moja ukitumia neno mvua.**

**T:** Waongoze wanafunzi kuandika sentensi moja wakitumia neno mvua **kwa hati nadhifu.**

**U: Wanafunzi wafanye zoezi la kuandika kwenye ukurasa wa 120.**

## ♦ Sarufi

**Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

N: 'Wewe' hutumiwa katika nafsi ya pili hali ya umoja. Huonyesha mtu wa pili baada ya wa kwanza, 'mimi'. Kwa mfano: Wewe ulifua nguo. 'U' hutumiwa pamoja na 'wewe' kuonyesha umoja. 'li' hutumiwa kuonyesha wakati uliopita.

'Wewe' inapotumiwa na wakati uliopita huwa inaonyesha kuwa jambo lilitendeka wakati uliopita.

'Nyinyi' na 'm' hutumiwa kama hali ya wingi wa nafsi ya kwanza. 'li' hutumiwa pamoja na 'nyinyi' na 'm' kuonyesha wingi. Kwa mfano: Nyinyi mlifua nguo.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 120.**

**Majibu**

1. mlicheza 2. ulilima 3. mlihesabu

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi nne kwa kutumia nafsi ya pili na **–li.**

Kwa mfano: Yeye alinunua peremende

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi awahamasishe wengine jinsi ya kuvaa kutegemea hali tofauti za anga.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 121: Hali ya anga 2

Kipindi cha 121 na 122 **Hali ya anga 2**

**Kipindi 121**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

w y z

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

wa ye za we

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ma ja ni | che ze a | ba a da ye | ba di li ka |
|---|---|---|---|
| **majani** | **chezea** | **baadaye** | **badilika** |

**Kipindi 122**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

A B CH D DH E F

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li ji tayarisha | tu ki cheza | a li wa karibisha |
|---|---|---|
| **walijitayarisha** | **tukicheza** | **aliwakaribisha** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Tunga sentensi tatu ukitumia nafsi ya pili wakati uliopita.

**Kwa mfano:** Wewe uliketi darasani.



Kipindi cha 121 na 122 **Hali ya anga 2**

**Kusoma hadithi**



**Hali ya anga**

Hali ya anga ilikuwa tulivu. Tulikuwa uwanjani tukicheza. Mara hali ya hewa ikabadilika. Mawingu meusi yalitanda angani. Muda mfupi baadaye upepo ulianza kuvuma vuuuu! Majani yalianza kuanguka. Tulifurahia kucheza nayo. Mvua ilianza kunyesha. Mimi na ndugu yangu Ongadi tuliyachezea maji ya mvua. Ongadi aliteleza na kuanguka. Nguo zake zilichafuka na kulowa maji. "Munene!" Mama aliita. "Mtakuwa wagonjwa!" Mama alisema. Baadaye tuliingia ndani ya nyumba. Tulivua nguo zilizolowa. Asubuhi iliyofuata Ongadi alianza kukohoa. Ilibidi mama ampeleke hospitalini. "Nyinyi mlichezea maji ya mvua," daktari alisema. Daktari alitushauri tusicheze kwenye mvua tena.



### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/w/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** wingu, magari

**U:** Endelea na maneno; uwanjani, aliita, zilizolowa, Jumatano.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** w, y, z

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 121.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /w/ /a/ silabi ni wa

**U:** Endelea na silabi; ye, za, we.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 121.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** ku ju a – kujua

**U:** Endelea na maneno; majani, chezea, baadaye

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 121.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **mawingu, upepo, mvua.** Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 122.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Watoto walikuwa wakichezea wapi? *(Uwanjani)*

**T:** Mawingu yalikuwa ya rangi gani? *(Meusi)*

**U:** Je,mvua ikianza kunyesha unafaa kufanya nini? *(Majibu ni kama kujikinga)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike maneno yafuatayo kwa nafsi ya pili wingi wakati uliopita.

| | Umoja | Wingi | | Umoja | Wingi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ulisoma | mlisoma | 2. | Ulikula | mlikula |
| 3. | Ulitembea | mlitembea | | | |

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi tano akitumia nafsi ya pili 'wewe'.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 122: Hali ya anga 2

Kipindi cha 121 na 122 **Hali ya anga 2**

**Kipindi 121**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  w y z

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  wa ye za we

- Soma maneno ukitumia silabi.

| ma ja ni | che ze a | ba a da ye | ba di li ka |
|---|---|---|---|
| **majani** | **chezea** | **baadaye** | **badilika** |

**Kipindi 122**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  A B CH D DH E F

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li ji tayarisha | tu ki cheza | a li wa karibisha |
|---|---|---|
| **walijitayarisha** | **tukicheza** | **aliwakaribisha** |

**Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Tunga sentensi tatu ukitumia nafsi ya pili wakati uliopita.

**Kwa mfano:** Wewe uliketi darasani.

121

Hakiuzwi

Kipindi cha 121 na 122 **Hali ya anga 2**

**Kusoma hadithi**



**Hali ya anga**

Hali ya anga ilikuwa tulivu. Tulikuwa uwanjani tukicheza. Mara hali ya hewa ikabadilika. Mawingu meusi yalitanda angani. Muda mfupi baadaye upepo ulianza kuvuma vuuuu! Majani yalianza kuanguka. Tulifurahia kucheza nayo. Mvua ilianza kunyesha. Mimi na ndugu yangu Ongadi tuliyachezea maji ya mvua. Ongadi aliteleza na kuanguka. Nguo zake zilichafuka na kulowa maji. "Munene!" Mama aliita. "Mtakuwa wagonjwa!" Mama alisema. Baadaye tuliingia ndani ya nyumba. Tulivua nguo zilizolowa. Asubuhi iliyofuata Ongadi alianza kukohoa. Ilibidi mama ampeleke hospitalini. "Nyinyi mlichezea maji ya mvua," daktari alisema. Daktari alitushauri tusicheze kwenye mvua tena.

Mali ya Serikali ya Kenya

122

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** A, B, CH, D, DH, E, F

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 121.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo na usome neno upesi.

**N/T/U:** a li m peleka – alimpeleka

**U:** Endelea na maneno; walijitayarisha, tukicheza.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 121.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **mawingu, upepo, mvua.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

**N:** Fafanua maana ya nafsi ya kwanza na wakati uliopita. 'Wewe' hutumiwa katika nafsi ya pili hali ya umoja. Huonyesha mtu wa pili baada ya wa kwanza, 'mimi'.

Kwa mfano: Wewe ulichora picha.

'U' hutumiwa pamoja na wewe kuonyesha umoja. 'li' hutumiwa kuonyesha wakati uliopita. 'Wewe' inapotumiwa na wakati uliopita huwa inaonyesha kuwa jambo lilitendeka wakati uliopita.

'Nyinyi' na 'm' hutumiwa kama hali ya wingi wa nafsi ya kwanza. 'li' hutumiwa pamoja na 'nyinyi' na 'm' kuonyesha wingi.

Kwa mfano: Nyinyi mlichora picha.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 121.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno yafuatayo:

1. Mvua
2. Upepo
3. Baridi
4. Aliteleza

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 123: Hali ya anga 2

Kipindi cha 123 na 124 **Hali ya anga 2**

**Kipindi 123**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

G H J K L M

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ve vi vo vu

- Soma maneno ukitumia silabi.

| nga zi | nyo o sha | tha mi ni | hu ha ri bu |
|---|---|---|---|
| **ngazi** | **nyoosha** | **thamini** | **huharibu** |

**Kipindi 124**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

N NG' NY O P R S

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li fika | ku hudhuria | wa li kutana | a li wa ambia |
|---|---|---|---|
| **walifika** | **kuhudhuria** | **walikutana** | **aliwaambia** |

**Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Jaza mapengo katika sentensi zifuatazo.

**Kwa mfano:** Nyinyi **mlicheza** uwanjani. (cheza)

1. Wewe __________ na mwalimu mkuu. (itwa)
2. Nyinyi __________ wimbo wa taifa. (imba)
3. Nyinyi __________ darasa. (fagia)
4. Wewe __________ gari. (abiri)
5. Wewe __________ sokoni. (enda)
6. Nyinyi __________ mto. (vuka)

123 Hakiuzwi

Kipindi cha 123 na 124 **Hali ya anga 2**

**Kusoma hadithi**



**Rita na Timo**

Ilikuwa Jumamosi. Rita na Timo waliamka mapema. Walitaka kuhudhuria maonyesho ya kilimo. Walijitayarisha na kuondoka. Jua lilichomoza. Anga ilikuwa shwari. Walifurahia kutembea. Walifika kwenye uwanja wa maonyesho saa tano. Waliona vitu vingi na kujifunza mengi. Walipokuwa wakirudi walikutana na babu yao. "Mlitoka nyumbani saa ngapi?" Babu aliwauliza. Walijibu kuwa walitoka saa mbili. Aliwaambia waende nyumbani haraka. Wakati huu jua lilikuwa limezama. Upepo mwepesi ulivuma. Walitembea haraka haraka hadi nyumbani. Mama aliwaambia wavae fulana. Walimweleza mama waliyoyaona kwenye maonyesho ya kilimo.

Mali ya Serikali ya Kenya 124

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/v/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** /v/, vua, kufua

**U:** Endelea na maneno; mvuvi, kujua, mavazi, majani.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** G, H, L, J, K, L, M

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 123.**

### Kusoma silabi

Tamka sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /v / /a/ silabi ni va

**U:** Endelea na silabi; ve, vi, vo, vu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 123.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: m vu lana – mvulana

**U:** Endelea na maneno; ngazi, nyoosha, thamini.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 123.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **upepo, anga, jua.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 124.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Watoto waliondoka nyumbani wakati gani? *(Wakati wa asubuhi)*

**T:** Ni hali gani za anga zilizotajwa katika hadithi? *(Upepo, jua)*

**U:** Je, unafikiria Rita na Timo waliona nini katika maonyesho ya kilimo? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi atunge sentensi tatu akitumia 'wewe' na 'nyinyi'.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi tatu akitumia 'wewe' na wakati uliopita 'li'.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

Kipindi cha 123 na 124 **Hali ya anga 2**

**Kipindi 123**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

G H J K L M

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ve vi vo vu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| nga zi | nyo o sha | tha mi ni | hu ha ri bu |
|---|---|---|---|
| **ngazi** | **nyoosha** | **thamini** | **huharibu** |

**Kipindi 124**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

N NG' NY O P R S

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li fika | ku hudhuria | wa li kutana | a li wa ambia |
|---|---|---|---|
| **walifika** | **kuhudhuria** | **walikutana** | **aliwaambia** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Jaza mapengo katika sentensi zifuatazo.

**Kwa mfano:** Nyinyi **mlicheza** uwanjani. (cheza)

1. Wewe __________ na mwalimu mkuu. (itwa)
2. Nyinyi __________ wimbo wa taifa. (imba)
3. Nyinyi __________ darasa. (fagia)
4. Wewe __________ gari. (abiri)
5. Wewe __________ sokoni. (enda)
6. Nyinyi __________ mto. (vuka)

123 Hakiuzwi

Kipindi cha 123 na 124 **Hali ya anga 2**

**Kusoma hadithi**



**Rita na Timo**

Ilikuwa Jumamosi. Rita na Timo waliamka mapema. Walitaka kuhudhuria maonyesho ya kilimo. Walijitayarisha na kuondoka. Jua lilichomoza. Anga ilikuwa shwari. Walifurahia kutembea. Walifika kwenye uwanja wa maonyesho saa tano. Waliona vitu vingi na kujifunza mengi. Walipokuwa wakirudi walikutana na babu yao. "Mlitoka nyumbani saa ngapi?" Babu aliwauliza. Walijibu kuwa walitoka saa mbili. Aliwaambia waende nyumbani haraka. Wakati huu jua lilikuwa limezama. Upepo mwepesi ulivuma. Walitembea haraka haraka hadi nyumbani. Mama aliwaambia wavae fulana. Walimweleza mama waliyoyaona kwenye maonyesho ya kilimo.

Mali ya Serikali ya Kenya 124

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** CH, ch, DH, dh, H, h

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 123.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo na usome neno upesi.

**N/T/U:** wa ka ondoka – wakaondoka

**U:** Endelea na maneno; walifika, kuhudhuria, walikutana.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 123.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **jua, anga, upepo.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

**N:** Fafanua maana ya nafsi ya kwanza na wakati uliopita. 'Wewe' hutumiwa katika nafsi ya pili hali ya umoja. Huonyesha mtu wa pili baada ya wa kwanza, 'mimi'. Kwa mfano: Wewe uliimba wimbo. 'U' hutumiwa pamoja na wewe kuonyesha umoja. 'li' hutumiwa kuonyesha wakati uliopita.

'Wewe' inapotumiwa na wakati uliopita huwa inaonyesha kuwa jambo lilitendeka wakati uliopita.

'Nyinyi' na 'm' hutumiwa kama hali ya wingi wa nafsi ya kwanza. 'li' hutumiwa pamoja na 'nyinyi' na 'm' kuonyesha wingi. Kwa mfano: Nyinyi mliimba nyimbo.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 123.**

**Majibu**

| | | |
|---|---|---|
| 1. uliitwa | 2. mliimba | 3. mlifagia |
| 4. uliabiri | 5. ulienda | 6. mlivuka |

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno yafuatayo katika wingi.

**Umoja**

1. Ulitabiri
2. Ulianguka
3. Uliambiwa

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 125 **Hali ya anga 2**

**Kipindi 125**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

T TH U V W Y Z

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: che za – cheza**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| che | ma | ri | a | to | vu |
| sa | ba | pe | za | di | ju |

**Sarufi: Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

Andika sentensi hizi katika umoja au wingi.

1. **Wewe** ulisoma.
2. **Nyinyi** mlicheza.
3. **Wewe** ulipita mtihani.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Natasha na Kamau**



**Kuandika**

Andika aya fupi kuhusu hadithi ya Rita na Timo uliyoisoma.

125 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Mwanafunzi aimbe wimbo wa alfabeti. Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** T, TH,U, V, W, Y, Z

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 125.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na mwanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'cheza'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **upepo, mawingu, mvua.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikilize na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Natasha na Kamau**

Jioni moja jua lilikuwa likizama. Natasha na Kamau walienda mtoni kuchota maji. Walichukua vibuyu vyao. Waliteremka polepole kuelekea mtoni. Walipofika mtoni, upepo mkubwa ulianza kuvuma. Walifikiri mvua ingenyesha ghafla. "Wewe jaza vibuyu haraka turudi nyumbani," Kamau alimwambia Natasha. Natasha alijaza vibuyu vyote maji.

"Lo!" Wewe ulisahau kubeba vifuniko vya vibuyu. Unaweza kuvikimbilia?" Natasha alimwuliza Kamau. Kamau alishangaa na kushindwa afanye nini. Alifikiri na kufikiri kwa muda. Mara akakumbuka nyanya alivyokuwa amemueleza kuhusu majani. Kamau aliingia kichakani na kutafuta majani. Aliyakunja na kuyatumia kufunika vibuyu. Natasha alifurahi sana. Alifunika vibuyu na kuviweka ndani ya kikapu. Wakaanza kurudi nyumbani. Wakiwa njiani, waliona mawingu meusi yametanda angani. Walitembea kwa haraka wakiogopa kunyeshewa. Walisaidiana kubeba vibuyu hadi nyumbani. Mama alipowaona, alishangaa, "Mlisahau vifuniko vya vibuyu jikoni. Mmebeba maji vipi?" "Tumetumia matawi mama," wakamjibu. Mama alifurahi sana na kuwashukuru.

Baada ya muda mfupi, mvua ilianza kunyesha. "Nyinyi mlifanya vizuri sana kurudi haraka kutoka mtoni. Mngenyeshewa sana. Nendeni mvae fulana msipatwe na homa," mama aliwaambia. Natasha na Kamau walivaa fulana. Walianza kufanya kazi yao ya ziada.

## Maswali

**T:** Ni kina nani walienda mtoni kuchota maji? *(Natasha na Kamau)*

**U:** Watoto walisahau nini nyumbani? *(Vifuniko vya vibuyu)*

**U:** Unatakiwa kufanya nini mvua inaponyesha? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Kuandika

**N: Andika aya fupi kuhusu hadithi ya hali ya anga.**

**T:** Mwongoze mwanafunzi kuandika aya kuhusu hali ya anga.

**U: Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye ukurasa wa 125.**

## Sarufi

**Matumizi ya nafsi ya pili wakati uliopita**

**N:** 'Wewe' hutumiwa katika nafsi ya pili hali ya umoja. Huonyesha mtu wa pili baada ya wa kwanza, 'mimi'. Kwa mfano: Wewe ulicheza mpira. 'U' hutumiwa pamoja na wewe kuonyesha umoja. 'li' hutumiwa kuonyesha wakati uliopita. 'Wewe' inapotumiwa na wakati uliopita huwa inaonyesha kuwa jambo lilitendeka wakati uliopita. 'Nyinyi' na 'm' hutumiwa kama hali ya wingi wa nafsi ya kwanza. 'li' hutumiwa pamoja na 'nyinyi' na 'm' kuonyesha wingi. Kwa mfano: Nyinyi mlicheza mpira.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 125.**

**Majibu**

1. Nyinyi mlisoma. 2. Wewe ulicheza. 3. Nyinyi mlipita mtihani.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi asome sentensi hizi.

1. Yeye ni askari.
2. Nyinyi ni walimu.
3. Yeye ana shamba kubwa.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha | 126 na 127 | **Lishe bora 2**

**Kipindi 126**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng'** **sh** **th**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ng'a** **ng'e** **ng'i** **ng'o** **ng'u**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ng'a mu a | ng'a ra | u shu ngi | u sha u ri |
|---|---|---|---|
| **ng'amua** | **ng'ara** | **ushungi** | **ushauri** |

**Kipindi 127**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG'** **ng'** **SH** **sh** **TH** **th**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li ng'oa | tu li ng'ara | i li ning'inia | hu shauriwa |
|---|---|---|---|
| **aling'oa** | **tuling'ara** | **ilining'inia** | **hushauriwa** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya hiki na hivi**

Msomee mwenzako sentensi zifuatazo ukionyesha vitu vilivyotajwa.

1. Kitabu **hiki** ni cha mwalimu.
2. Vitabu **hivi** ni vya kuandikia.
3. Kiti **hiki** kilikaliwa na mwanafunzi.


■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**a, b, ch, d, dh, e, f, g, gh, h, i, j, k, l, m, n, ng', ny, o, p, r, s, sh, t, th, u, v, w, y, z**

Mali ya Serikali ya Kenya 126

Kipindi cha | 126 na 127 | **Lishe bora 2**

**Kusoma hadithi**



**Lishe bora**

Vyakula ni muhimu katika mwili wa binadamu. Ni jukumu la kila mmoja kupata lishe bora. Lishe bora ni chakula chenye madini muhimu mwilini. Madini haya ni kama vile protini, vitamini na wanga. Protini husaidia kuujenga mwili. Vyakula vyenye protini ni kama maharagwe, samaki, mayai, nyama na maziwa. Vitamini hukinga mwili kutokana na magonjwa. Vyakula hivi vyenye vitamini ni kama matunda na mboga. Vyakula vya wanga pia ni muhimu mwilini. Ukosefu wa lishe bora husababisha magonjwa mengi mwilini.

127 Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** ng'ambo, ngamia

**U:** Endelea na maneno; ng'oa, ng'ombe, ngazi, ndama.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng', sh, th

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 126.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /sh / /a/ silabi ni sha

**U:** Endelea na silabi; ng'a, ng'e, ng'i, ng'o, ng'u.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 126.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** ng'o mbe – ng'ombe

**U:** Endelea na maneno; ng'amua, ng'ara, ushungi, ushauri.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 126.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **protini, vitamini, madini.** Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 127.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Ni vyakula vipi vina vitamini? *(Matunda na mboga.)*

**T:** Mbali na protini na vitamini ni aina nyingine gani ya chakula iliyo muhimu mwilini. *(Vyakula vya wanga.)*

**U:** Je, wewe unapenda kula chakula gani? *(Kubali majibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi arejelee majina na sauti za herufi ndogo kwa mfuatano ufaao kwenye **ukurasa wa 126.**

Mwalimu anaweza kutumia wimbo wa a,b,ch, d... kufunzia.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike na kuchora aina za matunda anayojua.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 126 na 127 **Lishe bora 2**

**Kipindi 126**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng'** **sh** **th**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ng'a** **ng'e** **ng'i** **ng'o** **ng'u**

- Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng'a mu a | ng'a ra | u shu ngi | u sha u ri |
| **ng'amua** | **ng'ara** | **ushungi** | **ushauri** |

**Kipindi 127**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG'** **ng'** **SH** **sh** **TH** **th**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a li ng'oa | tu li ng'ara | i li ning'inia | hu shauriwa |
| **aling'oa** | **tuling'ara** | **iliningi'nia** | **hushauriwa** |

**Sarufi: Matumizi ya hiki na hivi**

Msomee mwenzako sentensi zifuatazo ukionyesha vitu vilivyotajwa.

1. Kitabu **hiki** ni cha mwalimu.
2. Vitabu **hivi** ni vya kuandikia.
3. Kiti **hiki** kilikaliwa na mwanafunzi.

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**a, b, ch, d, dh, e, f, g, gh, h, i, j, k, l, m, n, ng', ny, o, p, r, s, sh, t, th, u, v, w, y, z**


Mali ya Serikali ya Kenya


126

Kipindi cha 126 na 127 **Lishe bora 2**

**Kusoma hadithi**







**Lishe bora**

Vyakula ni muhimu katika mwili wa binadamu. Ni jukumu la kila mmoja kupata lishe bora. Lishe bora ni chakula chenye madini muhimu mwilini. Madini haya ni kama vile protini, vitamini na wanga. Protini husaidia kuujenga mwili. Vyakula vyenye protini ni kama maharagwe, samaki, mayai, nyama na maziwa. Vitamini hukinga mwili kutokana na magonjwa. Vyakula hivi vyenye vitamini ni kama matunda na mboga. Vyakula vya wanga pia ni muhimu mwilini. Ukosefu wa lishe bora husababisha magonjwa mengi mwilini.

127 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NG', ng', SH, sh, TH, th

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 126.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** i li ng'oka – iling'oka

**U:** Endelea na maneno; aling'oa, tuling'ara, ilining'inia, hushauriwa.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 126.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **madini, protini, vitamini.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya 'hiki' na 'hivi'**

Fafanua maana ya 'hiki' na 'hivi'. 'Hiki' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kikiwa karibu cha majina ya vitu yanayoanza na 'ki'.

Kwa mfano; Kiatu **hiki** ni changu.

Chakula **hiki** ni chetu.

'Hivi' hutumiwa kuonyesha vitu vikiwa karibu vya majina yanayoanza na 'vi' au 'vy'.

Kwa mfano: Viatu **hivi** ni vyetu.

Vyakula **hivi** ni vyetu.

Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 126.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi achague jibu sahihi kujaza mapengo.

1. Ugali ni aina gani ya chakula?_______. (wanga, protini)
2. Matunda hutupatia____________. (vitamini, maji)
3. Ukila chakula bora utakuwa na ______. (afya bora, ugonjwa).

Tarehe: __________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 128: Lishe bora 2

Kipindi cha 128 na 129 **Lishe bora 2**

**Kipindi 128**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ny** **ng'** **gh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**nya** **nye** **nyi** **nyo** **nyu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| nya ma | nyu mba | nya ti | nyo ta |
| --- | --- | --- | --- |
| **nyama** | **nyumba** | **nyati** | **nyota** |

**Kipindi 129**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NY** **ny** **NG'** **ng'** **GH** **gh**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li fanya | hu gharimu | a li unganisha | a li ghadhabika |
| --- | --- | --- | --- |
| **alifanya** | **hugharimu** | **aliunganisha** | **alighadhabika** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya hiki na hivi**

Jaza mapengo kwa kutumia **hiki** au **hivi**.

1. Vinywaji _________ vina vitamini.
2. Kisu _________ hakina makali.
3. Vyakula _________ vina chumvi nyingi.

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**A, B, CH, D, DH, E, F, G, GH, H, I, J, K, L, M, N, NG', NY, O, P, R, S, SH, T, TH, U, V, W, Y, Z**

Mali ya Serikali ya Kenya

128

Kipindi cha 128 na 129 **Lishe bora 2**

**Kusoma hadithi**



**Vyakula mbalimbali**

Binadamu hutegemea chakula ili apate nguvu. Ni muhimu kula chakula cha kutosha. Ni lazima chakula hiki kiwe na madini. Chakula chenye madini ya wanga hutupatia nguvu mwilini. Tunahitaji nguvu ya kusoma, kuandika na kucheza. Baadhi ya vyakula vya wanga ni mahindi, mihogo, wali na ugali. Watoto wanapenda kula ugali ili wapate nguvu. Chumvi pia ni muhimu katika mwili. Chumvi huongeza ladha katika chakula. Kuna vyakula vingine ambavyo hudhuru meno. Mifano ya vyakula hivi ni biskuti, chokoleti na peremende. Tusivile vyakula hivyo. Ikibidi tuvile, tusivile kwa wingi na tupige mswaki baadaye.

129

Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ny/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** nyama, nanasi

**U:** Endelea na maneno; nyota, nyati, chakula, jani.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ny, ng', gh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 128.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /gh/ / a/ silabi ni gha

**U:** Endelea na silabi; nya, nye, nyi, nyo, nyu

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 128.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: nya nya – nyanya

**U:** Endelea na maneno; nyama, nyumba, nyati, nyota.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 128.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **wanga, chakula, chumvi.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 129.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Toa mifano ya vyakula vyenye wanga. *(Mahindi, mihogo, wali)*

**T:** chakula hutupatia nguvu ya kufanya nini? *(Kucheza, kuandika)*

**U:** Ni vyakula vipi vinapatikana kwenu? *(Mahindi, matunda, mihogo)*

### Zoezi

Mwanafunzi arejelee majina na sauti za herufi ndogo kwa mfuatano ufaao kwenye **ukurasa wa 128.**

Mwalimu anaweza kutumia wimbo wa A,B,CH, D... kufunzia.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno yafuatayo.

1. Afya 2. Chumvi 3. Chakula

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 128 na 129 **Lishe bora 2**

**Kipindi 128**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.
  **ny** **ng'** **gh**
- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.
  **nya** **nye** **nyi** **nyo** **nyu**
- Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| nya ma | nyu mba | nya ti | nyo ta |
| **nyama** | **nyumba** | **nyati** | **nyota** |

**Kipindi 129**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.
  **NY** **ny** **NG'** **ng'** **GH** **gh**
- Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a li fanya | hu gharimu | a li unganisha | a li ghadhabika |
| **alifanya** | **hugharimu** | **aliunganisha** | **alighadhabika** |

**Sarufi: Matumizi ya hiki na hivi**

Jaza mapengo kwa kutumia **hiki** au **hivi**.

1. Vinywaji __________ vina vitamini.
2. Kisu __________ hakina makali.
3. Vyakula __________ vina chumvi nyingi.

- Taja jina la herufi na utamke sauti.
  **A, B, CH, D, DH, E, F, G, GH, H, I, J, K, L, M, N, NG', NY, O, P, R, S, SH, T, TH, U, V, W, Y, Z**

Mali ya Serikali ya Kenya

128

Kipindi cha 128 na 129 **Lishe bora 2**

**Kusoma hadithi**



**Vyakula mbalimbali**

Binadamu hutegemea chakula ili apate nguvu. Ni muhimu kula chakula cha kutosha. Ni lazima chakula hiki kiwe na madini. Chakula chenye madini ya wanga hutupatia nguvu mwilini. Tunahitaji nguvu ya kusoma, kuandika na kucheza. Baadhi ya vyakula vya wanga ni mahindi, mihogo, wali na ugali. Watoto wanapenda kula ugali ili wapate nguvu. Chumvi pia ni muhimu katika mwili. Chumvi huongeza ladha katika chakula. Kuna vyakula vingine ambavyo hudhuru meno. Mifano ya vyakula hivi ni biskuti, chokoleti na peremende. Tusivile vyakula hivyo. Ikibidi tuvile, tusivile kwa wingi na tupige mswaki baadaye.

129 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NY, ny, NG', ng', GH, gh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 128.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** i li nyauka – ilinyauka

**U:** Endelea na maneno; alifanya, hugharimu, aliunganisha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 128.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **wanga, chakula, chumvi.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya 'hiki' na 'hivi'**

Fafanua maana ya 'hiki' na 'hivi'. 'Hiki' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kikiwa karibu cha majina ya vitu yanayoanza na 'ki'.

Kwa mfano; Kiti hiki ni changu.

'Hivi' hutumiwa kuonyesha vitu vikiwa karibu vya majina yanayoanza na 'vi' au 'vy'.

Kwa mfano: Viti hivi ni vyetu.

Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 128.**

**Majibu**

1. hivi
2. hiki
3. hivi

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi ajaze mapengo akitumia 'hiki' au 'hivi'.

1. Kiatu__________kimeoshwa. (hiki)
2. Kiti __________ni safi. (hiki)
3. Vijiko __________vimeoshwa. (hivi)

Tarehe: ____________________ Muda: ____________________ Idadi: ____________________

Kipindi cha 130 **Lishe bora 2**

**Kipindi 130**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng' th sh ny gh

Jedwali la silabi

Tumia silabi kwenye jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: chu ngu – chungu**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| nya | vi | ki | nyu | chu | wa |
| ngu | nga | o | ta | ng'a | mu |

**Sarufi: Matumizi ya hiki na hivi**

Jaza mapengo ukitumia jibu sahihi.

1. Mama alitumia kisu _______ (hivi, hiki) kukata mboga.
2. Shangazi alinunua vikombe ________ (hiki, hivi).
3. Kioo ________ (hiki, hivi) kilivunjwa na kaka.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Umuhimu wa chakula**



**Kuandika**

Andika sentensi nne kuhusu vyakula ulivyosoma kwenye hadithi.

Mali ya Serikali ya Kenya 130

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

N/T/U: ng', th, sh, ny, gh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 130.**

### Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na mwanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'chungu'.

U: Mwanafunzi aunde maneno.

### Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **protini, chumvi, vitamini.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Umuhimu wa chakula**

Katika kijiji cha Ruma, paliishi mzee mmoja aliyeitwa Wakene. Mke wake aliitwa Suma. Walikuwa na watoto wawili, Nekesa na Kidani. Siku moja watoto hawa walikuwa wagonjwa. Mama aliwapeleka hospitalini. Daktari alipowapima, aliwapata na ugonjwa wa ukosefu wa chakula bora. Chakula bora hujenga mwili. Daktari alimweleza Suma umuhimu wa chakula hiki.

"Vyakula hivi ni vipi daktari?" Suma aliuliza. Daktari akasema, "Vyakula hivi ni vile vyenye madini ya protini, vitamini, wanga na chumvi." Daktari alieleza kuwa protini hujenga mwili. Nekesa na Kidani waliposikia waliangaliana. Walisema, "Tulifunzwa hayo shuleni." Daktari alisema vyakula vyenye protini ni mayai, maziwa, maharagwe na nyama. Alisema vitamini hukinga mwili kutokana na magonjwa. Vyakula vinavyotupatia vitamini ni karoti, nyanya, kabeji, sukumawiki na matunda. "Mama, utatununulia matunda?" Nekesa aliuliza. "Ndio," Suma alimjibu.

Daktari alieleza kuwa wanga ni madini pia. Yanaupatia mwili nguvu. Tunahitaji nguvu ya kucheza, kusoma, kulima na kuogelea. Vyakula hivi ni mahindi, ugali, mihogo, viazi vitamu, mtama na wali. Daktari alieleza umuhimu wa chumvi pia katika chakula. Akamwandikia Suma vyakula ambavyo angewapatia watoto wake. Waliporudi nyumbani aliwapatia watoto vyakula vyenye madini. Afya yao ilikuwa nzuri. Suma alifurahi.

### Maswali

N: Taja madini matatu muhimu. *(Protini, vitamini, wanga na chumvi.)*

T: Ni vyakula gani vinavyotupatia nguvu mwilini? *(Vyakula hivi ni mahindi, ugali, mihogo, viazi vitamu, mtama na wali.)*

U: Je, ukikosa chakula bora utapatwa na shida gani mwilini? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Kuandika

N: **Andika sentensi moja kuhusu vyakula ulivyofunza.**

T: Waongoze wanafunzi kuandika sentensi kuhusu vyakula walivyosoma kwa hati nadhifu.

U: **Wanafunzi wafanye zoezi la kuandika kwenye ukurasa wa 130.**

### Sarufi

**Matumizi ya 'hiki' na 'hivi'**

Fafanua maana ya 'hiki' na 'hivi'. 'Hiki' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kikiwa karibu cha majina ya vitu yanayoanza na 'ki'.

Kwa mfano; Kikapu **hiki** ni kikubwa. 'Hivi' hutumiwa kuonyesha vitu vikiwa karibu vya majina yanayoanza na 'vi' au 'vy'.

Kwa mfano: Vikapu **hivi** ni vikubwa.

### Zoezi

Wanafunzi wafanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 130.**

**Majibu**

1. hiki 2. hivi 3. hiki

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi anakili sentensi hizi kisha amsomee mzazi/mlezi nyumbani.

1. Chakula hiki ni kitamu.
2. Viazi hivi vimeoza.
3. Vidole hivi ni safi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

Kipindi cha | 131 na 132 | **Mnyama nimpendaye 3**

**Kipindi 131**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**sh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**sha** **she** **shi** **sho** **shu**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| mi shi pi | m nya ma | shu le ni | wa na o i shi |
|---|---|---|---|
| **mishipi** | **mnyama** | **shuleni** | **wanaoishi** |

**Kipindi 132**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**SH** **sh**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li m karibisha | hu tu safirisha | hu safisha |
|---|---|---|
| **alimkaribisha** | **hutusafirisha** | **husafisha** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Chora michoro ya machungwa matatu. Tumia hili na haya kutunga sentensi.

■ Taja jina la irabu na utamke sauti.

**a** **e** **i** **o** **u**

131

Hakiuzwi

Kipindi cha | 131 na 132 | **Mnyama nimpendaye 3**

**Kusoma hadithi**



**Wanyama wetu**

Kuna wanyama wa aina nyingi. Kuna wanyama wanaofugwa nyumbani na wanaoishi msituni. Wanyama wanaofugwa nyumbani ni kama ng'ombe, mbuzi na kondoo. Mimi nampenda mbuzi. Ni mnyama mwenye faida kwetu. Mbuzi hutupatia maziwa, nyama na ngozi. Maziwa ya mbuzi yana madini muhimu kwa afya yetu. Nyama ni muhimu kwa afya yetu. Ngozi hutumiwa kutengeneza viatu, mikoba na mishipi. Watu hupenda kuvaa viatu na kufunga mishipi. Wasichana hupenda mikoba ya ngozi ya mbuzi. Mimi huvaa viatu nikienda shuleni. Ni vyema kumtunza mbuzi kwa kumpa chakula na mahali pa kulala. Mahali hapa huitwa zizi. Zizi hili huwalinda mbuzi kutokana na baridi.

Mali ya Serikali ya Kenya

132

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/sh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** shamba, choo

**U:** Endelea na maneno; shuleni, miti, shangazi, shanga, changia.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** sh, gh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 131.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /sh/ /a/ silabi ni sha.

**U:** Endelea na silabi; she, shi, sho, shu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 131.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: gha i ri – ghairi

**U:** Endelea na maneno; mishipi, mnyama, shuleni.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 131.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **ng'ombe, mbuzi, zizi.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 132.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Taja wanyama wanaofugwa nyumbani. *(Ng'ombe, mbuzi na kondoo)*

**T:** Mbuzi hutupatia nini? *(Maziwa, nyama na ngozi)*

**U:** Unatunza wanyama vipi nyumbani? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwalimu aeleze kuwa **a, e, i, o, u** ni irabu. Herufi zilizosalia ni konsonanti. Mwanafunzi ataje jina la irabu ndogo na kutamka sauti za irabu hizo, kwenye **ukurasa wa 131.**

Mwalimu anaweza kutumia wimbo wa **a, e, i, o, u** kufunzia.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore maumbo ya wanyama hawa wafugwao nyumbani.

1. Kuku. 2. Mbuzi

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 131 na 132 **Mnyama nimpendaye 3**

**Kipindi 131**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**sh**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**sha** **she** **shi** **sho** **shu**

- Soma maneno ukitumia silabi.

| mi shi pi | m nya ma | shu le ni | wa na o i shi |
|---|---|---|---|
| **mishipi** | **mnyama** | **shuleni** | **wanaoishi** |

**Kipindi 132**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**SH** **sh**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li m karibisha | hu tu safirisha | hu safisha |
|---|---|---|
| **alimkaribisha** | **hutusafirisha** | **husafisha** |

**Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Chora michoro ya machungwa matatu. Tumia hili na haya kutunga sentensi.

- Taja jina la irabu na utamke sauti.

**a** **e** **i** **o** **u**

131 Hakiluzwi

Kipindi cha 131 na 132 **Mnyama nimpendaye 3**

**Kusoma hadithi**



**Wanyama wetu**

Kuna wanyama wa aina nyingi. Kuna wanyama wanaofugwa nyumbani na wanaoishi msituni. Wanyama wanaofugwa nyumbani ni kama ng'ombe, mbuzi na kondoo. Mimi nampenda mbuzi. Ni mnyama mwenye faida kwetu. Mbuzi hutupatia maziwa, nyama na ngozi. Maziwa ya mbuzi yana madini muhimu kwa afya yetu. Nyama ni muhimu kwa afya yetu. Ngozi hutumiwa kutengeneza viatu, mikoba na mishipi. Watu hupenda kuvaa viatu na kufunga mishipi. Wasichana hupenda mikoba ya ngozi ya mbuzi. Mimi huvaa viatu nikienda shuleni. Ni vyema kumtunza mbuzi kwa kumpa chakula na mahali pa kulala. Mahali hapa huitwa zizi. Zizi hili huwalinda mbuzi kutokana na baridi.

Mali ya Serikali ya Kenya 132

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** SH, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 131.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** wa li shauri – walishauri

**U:** Endelea na maneno; alimkaribisha, hutusafirisha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 131.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **ng'ombe, mbuzi, zizi.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya 'hili' na 'haya'**

**N:** Fafanua maana na matumizi ya 'hili' na 'haya'.

'Hili' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kilicho karibu. Kwa mfano; tunda hili, jina hili, tawi hili.

'Haya' hutumiwa kuonyesha vitu vingi vilivyo karibu. Maneno huwa yanaanza na 'ma' katika hali ya wingi. Kwa mfano; matunda haya, matawi haya, majina haya.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 131.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia majina haya ya wanyama.

1. Mbuzi
2. Kuku
3. Kondoo

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha | 133 na 134 | **Mnyama nimpendaye 3**

**Kipindi 133**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

th sh

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

thi tho thu sha

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| thi bi ti sho | thi e ta | sha nga | shi nda |
|---|---|---|---|
| **thibitisho** | **thieta** | **shanga** | **shinda** |

**Kipindi 134**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

TH th SH sh

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| tu na po thibiti | a ta ku shangaza | hu tu safirisha |
|---|---|---|
| **tunapothibiti** | **atakushangaza** | **hutusafirisha** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Mkiwa wawili, tungeni sentensi tatu mkitumia **hili** au **haya**.


■ Taja jina la irabu na utamke sauti.

A E I O U

133 Hakiuzwi

Kipindi cha | 133 na 134 | **Mnyama nimpendaye 3**

**Kusoma hadithi**



**Abedi na Halima**

Abedi na Halima wanaishi katika sehemu kame. Wakati wa likizo Haruna aliwatembelea. Alipowasili, Halima alisema kwa furaha, "Abedi! Abedi! Haruna amekuja kututembelea."

"Haruna! Karibu kwetu," Abedi alimkaribisha rafiki yake. "Leo nitakueleza kuhusu ngamia wetu," Abedi aliendelea kumwambia. "Ngamia ni mnyama mzuri. Hutupa maziwa, nyama na ngozi. Hutusafirisha pia," alisema Abedi.

"Ala! kumbe ngamia ni mnyama mkubwa hivi!" Haruna alisema. "Ndio na ni mpole, Ngamia hula majani haya unayoyaona. Mbali na kutubeba tunapoenda safari, yeye hutubebea mizigo. Ngamia ni mnyama mvumilivu. Tunampenda ngamia wetu," alisema Halima.

Mali ya Serikali ya Kenya 134

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/th/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** thibitisha, tibu, tisha

**U:** Endelea na maneno; thieta, thubutu, viazi, dhamana.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** th, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 133.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /th/ /a/ silabi ni tha.

**U:** Endelea na silabi; thi, tho, thu, sha.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 133.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: the mo me ta – themometa

**U:** Endelea na maneno; thibitisho, shanga.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 133.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **kame, ngamia, mvumilivu.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 134.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Abedi na Halima waliishi wapi? *(Abedi na Halima waliishi katika sehemu kame.)*

**T:** Ni nani aliwatembelea Abedi na Halima? *(Haruna aliwatembelea)*

**U:** Unafikiri sehemu kame ni sehemu ya aina gani? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwalimu aeleze kuwa A, E, I, O, U ni irabu. Herufi zilizosalia ni konsonanti. Mwanafunzi ataje jina la irabu kubwa na kutamka sauti za irabu hizo, kwenye **ukurasa wa 133.**

Mwalimu anaweza kutumia wimbo wa A, E, I, O, U kufunzia.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore baadhi ya wanyama wa nyumbani unaowafahamu na utaje majina yao.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 134: Mnyama nimpendaye 3

Kipindi cha 133 na 134 **Mnyama nimpendaye 3**

**Kipindi 133**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **th** **sh**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  **thi** **tho** **thu** **sha**

- Soma maneno ukitumia silabi.

| thi bi ti sho | thi e ta | sha nga | shi nda |
| --- | --- | --- | --- |
| **thibitisho** | **thieta** | **shanga** | **shinda** |

**Kipindi 134**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **TH** **th** **SH** **sh**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| tu na po thibiti | a ta ku shangaza | hu tu safirisha |
| --- | --- | --- |
| **tunapothibiti** | **atakushangaza** | **hutusafirisha** |

- **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**

Mkiwa wawili, tungeni sentensi tatu mkitumia **hili** au **haya**.

- Taja jina la irabu na utamke sauti.

  **A E I O U**

133

Hakluzwi

Kipindi cha 133 na 134 **Mnyama nimpendaye 3**

**Kusoma hadithi**



**Abedi na Halima**

Abedi na Halima wanaishi katika sehemu kame. Wakati wa likizo Haruna aliwatembelea. Alipowasili, Halima alisema kwa furaha, "Abedi! Abedi! Haruna amekuja kututembelea."

"Haruna! Karibu kwetu," Abedi alimkaribisha rafiki yake. "Leo nitakueleza kuhusu ngamia wetu," Abedi aliendelea kumwambia. "Ngamia ni mnyama mzuri. Hutupa maziwa, nyama na ngozi. Hutusafirisha pia," alisema Abedi.

"Ala! kumbe ngamia ni mnyama mkubwa hivi!" Haruna alisema. "Ndio na ni mpole, Ngamia hula majani haya unayoyaona. Mbali na kutubeba tunapoenda safari, yeye hutubebea mizigo. Ngamia ni mnyama mvumilivu. Tunampenda ngamia wetu," alisema Halima.

Mali ya Serikali ya Kenya

134

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** TH, th, SH, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 133.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo na usome neno upesi.

**N/T/U:** a ta wa shauri – atawashauri

**U:** Endelea na maneno; tunapothibiti, atakushangaza, hutusafirisha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 133.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **kame, ngamia, mvumilivu.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

## Sarufi

**Matumizi ya 'hili' na 'haya'**

**N:** Fafanua maana na matumizi ya **hili na haya.**

'Hili' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kilicho karibu. Kwa mfano; jiwe hili, neno hili, embe hili.

'Haya' hutumiwa kuonyesha vitu vingi vilivyo karibu. Maneno huwa yanaanza na 'ma' katika hali ya wingi. Kwa mfano; mawe haya, maneno haya, maembe haya.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 133.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi ataje baadhi ya mambo anayoyajua kumhusu mnyama umpendaye.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 135 Mnyama nimpendaye 3

**Kipindi 135**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng th sh ng'

Jedwali la silabi


Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno.
**Kwa mfano: mbu zi – mbuzi**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ri | mbe | thu | a | nga | mbu |
| mi | sha | zi | ka | bu | ng'o |

◆ **Sarufi: Matumizi ya hili na haya**
Tunga sentensi tatu ukitumia **hili** au **haya**.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Ng'ombe**



**Kuandika**
Andika aya fupi kuhusu mnyama umpendaye.

135 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng, th, sh, ng'

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 135.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na mwanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'mbuzi'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **zizi, lishe, kudumisha.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Ng'ombe**

Amadala alisafiri kwa muda mrefu. Aliwasili kwa babu yake. Nyanya yake aliishi kijijini Mlachake. "Hodi?" Alibisha. "Karibu nyumbani," sauti nyororo ya nyanya ilisikika.

Alipokelewa kwa furaha. Alipewa maji ya machungwa. Alikunywa akamaliza. Amadala alimpa nyanya salamu kutoka kwa wazazi. "Yuko wapi babu?" Amadala aliuliza.

"Yuko katika zizi la ng'ombe," alimjibu nyanya. "Hebu niende nimsalimie," alisema Amadala.

"Shikamoo babu!" "Marahaba mjukuu wangu!" Babu aliitikia. "Njoo nikueleze kuhusu ng'ombe," alisema babu. "Tinka ni ng'ombe mzuri sana. Kila siku Tinka hutupa maziwa chupa kumi. Jioni hutupatia chupa tano. Sisi hutumia maziwa haya kupika chai. Mengine tunauza na kununua chakula na nguo. Tinka pia hutupatia mbolea. Mbolea husaidia mimea kukua vizuri shambani." Babu alieleza. "Mimi humpatia Tinka lishe bora. Nimemjengea zizi. Tinka hulala katika zizi hili. Zizi hili humkinga kutokana na jua kali na mvua. Mimi hulisafisha zizi ili kudumisha usafi. Mimi nampenda Tinka sana," akamalizia babu. Amadala alijifunza mengi kuhusu ng'ombe. "Nikiwa mkubwa, nitamfuga ng'ombe. Nitamtunza vile umemtunza Tinka," alisema Amadala.

## Maswali

**N:** Babu yake Amadala aliishi wapi? *(Aliishi kijijini mlachake)*

**T:** Tinka humpa babu maziwa chupa ngapi? *(Maziwa chupa kumi)*

**U:** Je, kufuga wanyama kuna faida gani? *(Kubali jibu sahihi)*

## Kuandika

**N:** Leo tuanze kupanga jinsi ya kuandika aya. Tutaandika aya ya kutuonyesha yale tuliyoyasoma katika hadithi. Sentensi ya kwanza itatuonyesha utangulizi wa kichwa cha hadithi. Tunapaswa kuandika nini? Tunataka kusema nini kuhusu kile tumekisoma? Hadithi ilituonyesha nini? Baadaye, tuwe na sentensi ya kuhitimisha. Ni kitu gani tunaweza kusema kinachoweza kuwa sehemu ya aya? (Wasaidie wanafunzi waweze kutoa maoni hata kama si sentensi na uziandike ubaoni). Sasa tuangalie maoni mliyo nayo. Je, tuna utangulizi? Maelezo ya kuhusu mada? Hitimisho?

**U: Wanafunzi wafanye zoezi la kuandika kwenye ukurasa wa 135.**

## Sarufi

**Matumizi ya 'hili' na 'haya'**

Fafanua maana na matumizi ya 'hili' na 'haya'.

'Hili' hutumiwa kuonyesha kitu kimoja kilicho karibu. Kwa mfano; chungwa hili.

'Haya' hutumiwa kuonyesha vitu vingi vilivyo karibu. Maneno huwa yanaanza na 'ma' katika hali ya wingi. Kwa mfano; machungwa haya.

## Zoezi

Wanafunzi wafanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 135.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya.

1. Ngombe 2. Ngamia 3. Kondoo

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi wahamasishe wengine umuhimu wa kuwahifadhi wanyama.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 136: Shuleni 3

Kipindi cha 136 na 137 **Shuleni 3**

**Kipindi 136**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

d g

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

da de do gu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| da ra sa | ku ru di | gwa ri de | go do ro |
| **darasa** | **kurudi** | **gwaride** | **godoro** |

**Kipindi 137**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

D d G g

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| hu saidia | a li geuka | a na gawa | a li rudi |
| **husaidia** | **aligeuka** | **anagawa** | **alirudi** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma sentensi hizi ukizingatia **-ako** na **-enu**.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mwalimu **wako** amefika. | Walimu **wenu** wamefika. |
| 2. | Darasa **lako** ni safi. | Madarasa **yenu** ni safi. |
| 3. | Tarakilishi **yako** inawaka. | Tarakilishi **zenu** zinawaka. |
| 4. | Mtoto **wako** amepatikana. | Watoto **wenu** wamepatikana. |

Mali ya Serikali ya Kenya

136

Kipindi cha 136 na 137 **Shuleni 3**

**Kusoma hadithi**



**Shule ya Msingi ya Masinga**

Shule ya msingi ya Masinga ina watoto mia tano. Kila darasa lina wanafunzi zaidi ya thelathini. Shule hiyo ina uwanja mkubwa. Watoto hucheza michezo mbalimbali. Kila asubuhi, watoto hukusanyika kwenye gwaride. Wanafunzi hupewa mawaidha mengi na walimu.

"Tafadhali wekeni mikono yenu ipasavyo, tunaimba wimbo wa taifa," mwalimu mkuu husema. "Lazima uheshimu taifa lako," yeye huendelea kusema. "Kuheshimu bendera ni kuonyesha upendo kwa nchi yako." Shule ya msingi ya Masinga ina basi kubwa. Watoto wanapenda kusafiri kwa basi hilo. Basi hilo huwapeleka kutembea jijini Nairobi. Watoto hufurahia ziara hizo.

137

Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/g/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** gari, ngamia

**U:** Endelea na maneno; godoro, kondoo, ganda, nguruwe, ghali.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** d, g

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 136.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /g/ /a/ silabi ni ga

**U:** Endelea na silabi; da, de, do, gu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 136.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: da wa ti – dawati

**U:** Endelea na maneno; darasa, kurudi, gwaride.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 136.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **gwaride, shule ya msingi, tafadhali.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 137.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Shule ya Msingi ya Masinga ina watoto wangapi? *(Shule ya Msingi ya Masinga ina watoto mia tano)*

**T:** Ni wakati gani watoto hukusanyika kwenye gwaride? *(Kila asubuhi, watoto hukusanyika kwenye gwaride)*

**U:** Ni kwa nini ni muhimu kuheshimu nchi yako? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi achore picha ya bendera ya Kenya na atie rangi zinazofaa.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno haya kwa hati nadhifu.

1. Darasa 2. Maktaba 3. Vyoo

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha | 136 na 137 | **Shuleni 3**

**Kipindi 136**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

d g

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

da de do gu

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| da ra sa | ku ru di | gwa ri de | go do ro |
| **darasa** | **kurudi** | **gwaride** | **godoro** |

**Kipindi 137**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

D d G g

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| hu saidia | a li geuka | a na gawa | a li rudi |
| **husaidia** | **aligeuka** | **anagawa** | **alirudi** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Soma sentensi hizi ukizingatia **-ako** na **-enu**.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mwalimu **wako** amefika. | Walimu **wenu** wamefika. |
| 2. | Darasa **lako** ni safi. | Madarasa **yenu** ni safi. |
| 3. | Tarakilishi **yako** inawaka. | Tarakilishi **zenu** zinawaka. |
| 4. | Mtoto **wako** amepatikana. | Watoto **wenu** wamepatikana. |

Mali ya Serikali ya Kenya

136

Kipindi cha | 136 na 137 | **Shuleni 3**

**Kusoma hadithi**



**Shule ya Msingi ya Masinga**

Shule ya msingi ya Masinga ina watoto mia tano. Kila darasa lina wanafunzi zaidi ya thelathini. Shule hiyo ina uwanja mkubwa. Watoto hucheza michezo mbalimbali. Kila asubuhi, watoto hukusanyika kwenye gwaride. Wanafunzi hupewa mawaidha mengi na walimu.

"Tafadhali wekeni mikono yenu ipasavyo, tunaimba wimbo wa taifa," mwalimu mkuu husema. "Lazima uheshimu taifa lako," yeye huendelea kusema. "Kuheshimu bendera ni kuonyesha upendo kwa nchi yako." Shule ya msingi ya Masinga ina basi kubwa. Watoto wanapenda kusafiri kwa basi hilo. Basi hilo huwapeleka kutembea jijini Nairobi. Watoto hufurahia ziara hizo.

137 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** D, d, G, g

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 136.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li andamana – aliandamana

**U:** Endelea na maneno; husaidia, anagawa, aligeuka.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 136.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **shule ya msingi, gwaride, tafadhali.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya -ako na -enu**

**N:** Andika '-ako' na '-enu' ubaoni.

Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano; Mti wako umemea. '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano; Miti yenu imemea.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 136.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi achague jibu sahihi.

1. Tunaamka ______ kwenda shuleni. (asubuhi, usiku)
2. Tunaenda kulala ______. (usiku, mchana)
3. Ukisalimiwa habari ya asubuhi utajibu vipi? (njema, mzuri).
4. Salamu umeshindaje hujibiwa vipi? (wema, vyema).

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 138: Shuleni 3

Kipindi cha 138 na 139 **Shuleni 3**

**Kipindi 138**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

r j

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

re ri ro jo ju

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ha ba ri | sa fa ri | ji bu | ka ri bu |
|---|---|---|---|
| **habari** | **safari** | **jibu** | **karibu** |

**Kipindi 139**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

R r J j

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu ji tayarisha | a li m shauri | a li jibu |
|---|---|---|
| **hujitayarisha** | **alimshauri** | **alijibu** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Andika sentensi hizi katika daftari lako.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| **1.** | Nchi **yako** ina amani. | Nchi **zenu** zina amani. |
| **2.** | Wimbo **wako** unapendwa. | Nyimbo **zenu** zinapendwa. |
| **3.** | Mwalimu **wako** ni mzuri. | Walimu **wenu** ni wazuri. |
| **4.** | Shati **lako** limeraruka. | Mashati **yenu** yameraruka. |

Mali ya Serikali ya Kenya 138

Kipindi cha 138 na 139 **Shuleni 3**

**Kusoma hadithi**



**Wema**

Wema huishi karibu na shule yake. Kila siku yeye huamka saa kumi na mbili asubuhi. Yeye hujitayarisha kwenda shuleni. Saa moja Wema hupata kiamshakinywa. Kisha huanza safari kwenda shuleni. Saa mbili wanafunzi hupanga foleni. Huwa na gwaride kila siku. Wakiwa kwenye gwaride, mwalimu huwasalimia, "Habari zenu wanafunzi?"

Wao hujibu, "Njema mwalimu." Wema pia humsalimu mwalimu, "Habari yako mwalimu?" Mwalimu hujibu, "Njema Wema." Wema anapokosea mwenzake yeye husema, "Samahani." Baada ya gwaride, wanafunzi huenda msalani. Kisha wao hurudi darasani kuanza masomo. Saa nne, wanafunzi huenda nje kucheza. Saa sita, mwalimu huwaongoza kuimba wimbo, "Nasikia sauti..."

139 Hakiuzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/r/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** raia, usalama

**U:** Endelea na maneno; rafiki, lango, rangi, rahisi, lima.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** r, j

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 138.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /r / / a/ silabi ni ra

**U:** Endelea na silabi; re, ri, ro, jo, ju.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 138.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: ja ngi li – jangili

**U:** Endelea na maneno; habari, safari, jibu.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 138.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **darasani, kiamshakinywa, samahani**. Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 139**.

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

N: Mwema huishi wapi? *(Mwema huishi karibu na shule yake)*

T: Watoto huenda wapi saa nne? *(Saa nne, wanafunzi huenda nje kucheza)*

U: Unajitayarisha vipi kabla ya kwenda shuleni asubuhi? *(Wanafunzi waeleze jinsi wanavyojitayarisha kabla ya kwenda shuleni)*

### Zoezi

Wanafunzi waigize jinsi ya kutumia maneno ya adabu na heshima.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno yafuatayo:

1. Darasani
2. Kiamsha kinywa
3. Gwaride

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 138 na 139 **Shuleni 3**

**Kipindi 138**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

r j

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

re ri ro jo ju

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| ha ba ri | sa fa ri | ji bu | ka ri bu |
|---|---|---|---|
| **habari** | **safari** | **jibu** | **karibu** |

**Kipindi 139**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

R r J j

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu ji tayarisha | a li m shauri | a li jibu |
|---|---|---|
| **hujitayarisha** | **alimshauri** | **alijibu** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Andika sentensi hizi katika daftari lako.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Nchi **yako** ina amani. | Nchi **zenu** zina amani. |
| 2. | Wimbo **wako** unapendwa. | Nyimbo **zenu** zinapendwa. |
| 3. | Mwalimu **wako** ni mzuri. | Walimu **wenu** ni wazuri. |
| 4. | Shati **lako** limeraruka. | Mashati **yenu** yameraruka. |

Mali ya Serikali ya Kenya 138

Kipindi cha 138 na 139 **Shuleni 3**

**Kusoma hadithi**



**Wema**

Wema huishi karibu na shule yake. Kila siku yeye huamka saa kumi na mbili asubuhi. Yeye hujitayarisha kwenda shuleni. Saa moja Wema hupata kiamshakinywa. Kisha huanza safari kwenda shuleni. Saa mbili wanafunzi hupanga foleni. Huwa na gwaride kila siku. Wakiwa kwenye gwaride, mwalimu huwasalimia, "Habari zenu wanafunzi?"

Wao hujibu, "Njema mwalimu." Wema pia humsalimu mwalimu, "Habari yako mwalimu?" Mwalimu hujibu, "Njema Wema." Wema anapokosea mwenzake yeye husema, "Samahani." Baada ya gwaride, wanafunzi huenda msalani. Kisha wao hurudi darasani kuanza masomo. Saa nne, wanafunzi huenda nje kucheza. Saa sita, mwalimu huwaongoza kuimba wimbo, "Nasikia sauti..."

139 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** R, r, J, j

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 138.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** i li raruka – iliraruka

**U:** Endelea na maneno; hujitayarisha, alijibu.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 138.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **kiamshakinywa, samahani, darasani.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya -ako na -enu**

**N:** Andika '-ako' na '-enu' ubaoni.

Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano; Kalamu yako inaandika. '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano; Kalamu zenu zinaandika.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 138.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya.

1. Bendera
2. Darasa
3. Vyoo

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 140 **Shuleni 3**

**Kipindi 140**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

g r j d

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: da ra sa – darasa**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| de | ga | nde | gwa | da | ra |
| ja | be | fa | ni | ri | sa |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Jaza mapengo ukitumia **-ako** na **-enu**.

Tumia tarakilishi yako.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mtoto _____ ni mzuri. | Watoto _____ ni wazuri. |
| 2. | Chakula _____ ni kitamu. | Vyakula _____ ni vitamu. |
| 3. | Ziara _____ imekaribia. | Ziara _____ zimekaribia. |

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Kagedo na Susa**



**Kuandika**

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. Ofisi 2. Maktaba
3. Bendera 4. Gwaride

Mali ya Serikali ya Kenya 140

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** g, r, J, d

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 140.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'darasa'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **bendera, maktaba, gwaride.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

**Kagedo na Susan**

Siku ya Jumatatu Kagedo aliamka mapema. Aliogopa kuchelewa kufika shuleni. Alioga, akanywa chai kwa mkate na kuvaa sare. Alianza safari kwa haraka kwenda shuleni. Alipofika, aligundua alikuwa ameacha kitabu cha hesabu nyumbani. Alimuita rafiki yake Susan. Alimwambia ampeleke nyumbani akachukue kitabu. "Tunafaa kuomba ruhusa," Susan alimwambia Kagedo.

Walienda katika ofisi ya mwalimu mkuu. Waliomba ruhusa. Mwalimu aliwapatia ruhusa. Aliwashauri wasicheze njiani.

Walianza safari kuelekea nyumbani kwa akina Kagedo. Walipokuwa karibu kufika, wakamwona mama yake Kagedo. Alikuwa amebeba kitabu cha hesabu. "Kagedo, uliacha kitabu chako juu ya meza. Nimekiona saa hii. Nimeamua nikuletee," mama alisema. Kagedo alifurahi na kumshukuru. Kagedo na Susan walikimbia na kurudi shuleni. Walipofika shuleni, walipata wanafunzi kwenye gwaride. Mwalimu mkuu akawaambia wanaskauti wapandishe bendera. Walipandisha bendera. Wanafunzi waliimba wimbo wa taifa. Baadaye waliomba.

"Asanteni wanaskauti kwa kazi yenu nzuri," mwalimu mkuu alisema. Aliendelea kuwashauri. "Ni lazima mtumie muda wenu vizuri shuleni. Msipofanya bidii, hamuwezi kufaulu masomoni." Aliwaeleza kuwa ni muhimu kusoma vitabu katika maktaba. Hili husaidia kuongeza ujuzi. Ni muhimu kufika darasani bila kuchelewa. Gwaride liliisha. Wanafunzi walienda madarasani. Walianza masomo ya siku hiyo.

## Maswali

**T:** Kagedo alisahau kitabu kipi nyumbani? *(Alisahau kitabu cha hesabu nyumbani)*

**U:** Ni nani aliwapatia Kagedo na Susan ruhusa? *(Mwalimu mkuu)*

**U:** Kwa nini ni muhimu kufanya bidii shuleni? *(Wanafunzi watoe majibu sahihi)*

## Kuandika

**N:** Mwanafunzi atunge sentensi moja ukitumia neno gwaride.

**T:** Waongoze wanafunzi kutunga sentensi moja wakitumia neno gwaride.

**U:** Wanafunzi wafanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa**

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 140 **Shuleni 3**

**Kipindi 140**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

g r j d

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: da ra sa – darasa**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| de | ga | nde | gwa | da | ra |
| ja | be | fa | ni | ri | sa |

**Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Jaza mapengo ukitumia **-ako** na **-enu**.

Tumia tarakilishi yako.

| | Umoja -ako | Wingi -enu |
|---|---|---|
| 1. | Mtoto _____ ni mzuri. | Watoto _____ ni wazuri. |
| 2. | Chakula _____ ni kitamu. | Vyakula _____ ni vitamu. |
| 3. | Ziara _____ imekaribia. | Ziara _____ zimekaribia. |

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Kagedo na Susa**



**Kuandika**

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. Ofisi
2. Maktaba
3. Bendera
4. Gwaride

Mali ya Serikali ya Kenya

140

wa 140.

## Sarufi

**Matumizi ya -ako na -enu**

Andika '-ako' na '-enu' ubaoni.

Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako. Kwa mfano; Jino lako linauma. '-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako. Kwa mfano; Meno yenu yanauma.

## Zoezi

Wanafunzi wafanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 140.**

**Majibu**

1. Watoto wenu ni wazuri.
2. Vyakula vyenu ni vitamu.
3. Ziara zenu zimekaribia.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya ya heshima.

1. Asante
2. Tafadhali
3. Samahani

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 141 na 142 **Usafiri 3**

**Kipindi 141**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

dh g d

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

dhe dhi dho dhu gi

- Soma maneno ukitumia silabi.

| dha ha bu | dha mbi | ga ri | da ra sa |
|---|---|---|---|
| **dhahabu** | **dhambi** | **gari** | **darasa** |

**Kipindi 142**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

DH dh G g D d

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa na dhalilika | wa li ji dhalilisha | a li ganda |
|---|---|---|
| **wanadhalilika** | **walijidhalilisha** | **aliganda** |

**Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Weka herufi kubwa panapofaa katika sentensi hizi.

1. ndege ya rais ni ya dhahabu.
2. watu wengi husafiri mwezi wa desemba.
3. wageni watafika siku ya jumamosi.
4. karamu imeandaliwa.
5. mpira wa ali umeletwa.
6. mkono wake ulivishwa saa.
7. wendy huishi karibu na shule.

141 Hakiuzwi

Kipindi cha 141 na 142 **Usafiri 3**

**Kusoma shairi**

**Vyombo vya usafiri**



Safari zote ni ajabu, leo nitakupa jibu,
Maswali yote nitajibu, nawe usishangae,
Safari kweli yasisimua, na pia yavutia.

Ndege kama dhahabu, angani yaangaza,
Safari kama umeme, haraka wanawasili,
Safari kweli yasisimua, na pia yavutia.

Barabarani kuna matatu, na magari madogo,
Matatu yabeba watu, kusafirisha vitongojini,
Safari kweli yasisimua, na pia yavutia.

Baiskeli na pikipiki, pia zasafirisha watu,
Majumbani na shuleni, huwafikisha salama,
Safari kweli yasisimua, na pia yavutia.

Chombo kipi cha safari, wapenda kusafiria?
Ndege, meli na gari, zote twasafiria,
Safari kweli yasisimua, na pia yavutia.

Mali ya Serikali ya Kenya 142

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/dh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** dhamini, thamini

**U:** Endelea na maneno; dhahabu, dhati, thelathini.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** dh, g, d

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 141**.

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /dh/ / a/ silabi ni dha

**U:** Endelea na silabi; dhe, dhi, dho, dhu, gi.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 141.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** dha ru ra – dharura

**U:** Endelea na maneno; dhahabu, dhambi, gari, darasa.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 141.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **ndege, matatu, meli.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 142.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha shairi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Kusoma shairi

**N/T/U:** Soma shairi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Ni vyombo gani vya usafiri vimetajwa? *(Gari, meli, pikipiki, ndege, baiskeli)*

**T:** Matatu husafirisha nini? *(Watu)*

**U:** Mnatumia vyombo vipi vya usafiri katika eneo lenu? *(Wanafunzi wataje vyombo tofauti tofauti)*

### Zoezi

Mwanafunzi achore picha ya gari la usafiri- matatu

### Kazi ya ziada

Chora maumbo ya vyombo hivi vya usafiri.

1. Pikipiki 2. Baiskeli 3. Meli

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha | 141 na 142 | **Usafiri 3**

**Kipindi 141**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**dh** **g** **d**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**dhe** **dhi** **dho** **dhu** **gi**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| dha ha bu | dha mbi | ga ri | da ra sa |
| **dhahabu** | **dhambi** | **gari** | **darasa** |

**Kipindi 142**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**DH** **dh** **G** **g** **D** **d**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| wa na dhalilika | wa li ji dhalilisha | a li ganda |
| **wanadhalilika** | **walijidhalilisha** | **aliganda** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Weka herufi kubwa panapofaa katika sentensi hizi.

1. ndege ya rais ni ya dhahabu.
2. watu wengi husafiri mwezi wa desemba.
3. wageni watafika siku ya jumamosi.
4. karamu imeandaliwa.
5. mpira wa ali umeletwa.
6. mkono wake ulivishwa saa.
7. wendy huishi karibu na shule.

141 Hakiuzwi

Kipindi cha | 141 na 142 | **Usafiri 3**

**Kusoma shairi**

**Vyombo vya usafiri**



Safari zote ni ajabu, leo nitakupa jibu,
Maswali yote nitajibu, nawe usishangae,
Safari kweli yasisimua, na pia yavutia.

Ndege kama dhahabu, angani yaangaza,
Safari kama umeme, haraka wanawasili,
Safari kweli yasisimua, na pia yavutia.

Barabarani kuna matatu, na magari madogo,
Matatu yabeba watu, kusafirisha vitongojini,
Safari kweli yasisimua, na pia yavutia.

Baiskeli na pikipiki, pia zasafirisha watu,
Majumbani na shuleni, huwafikisha salama,
Safari kweli yasisimua, na pia yavutia.

Chombo kipi cha safari, wapenda kusafiria?
Ndege, meli na gari, zote twasafiria,
Safari kweli yasisimua, na pia yavutia.

Mali ya Serikali ya Kenya 142

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** DH, dh, G, g, D, d

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 141.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** a li ghairi – alighairi

**U:** Endelea na maneno; wanadhalilika, aliganda.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 141.**

## Msamiati

Wakumbushe wanafunzi maana ya msamiati **ndege, matatu, meli.**

## Kusoma shairi

**U:** Somea mwenzako shairi.

## Sarufi

**Matumizi ya herufi kubwa**

**N:** Eleza matumizi ya herufi kubwa.

Tunatumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi.

Pia herufi kubwa hutumiwa mwanzoni mwa majina ya vitu au mahali.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 141.**

**Majibu**

1. Ndege ya rais ni ya dhahabu.
2. Watu wengi husafiri mwezi wa Disemba.
3. Wageni watafika siku ya Jumamosi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi asome sentensi zifuatazo.

1. Lori kubwa linabeba mizigo.
2. Usafiri wa ndege ulifurahisha Limo.
3. Matatu nyingi huendeshwa vibaya.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 143 na 144 **Usafiri 3**

**Kipindi 143**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  ch dh sh

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  che chi cho dhu shi

- Soma maneno ukitumia silabi.

| che ma | shu le ni | dha ru ra | sha mba |
|---|---|---|---|
| **chema** | **shuleni** | **dharura** | **shamba** |

**Kipindi 144**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  CH ch DH dh SH sh

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| ya li chacha | ma shambulizi | a li dhalilisha |
|---|---|---|
| **yalichacha** | **mashambulizi** | **alidhalilisha** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Mkiwa wawili, someni sentensi kisha mpigie mistari herufi kubwa.


1. Chombo hiki ni cha usafiri.
2. Ndege ya Kenya ni kubwa.
3. Mimi husafiri kwa matatu.
4. Maimuna alifika Voi kwa ndege.
5. Barabara hii ilijengwa na Toma.
6. Safari yake imevunjika.
7. Meli ilielea majini.

143

Kipindi cha 143 na 144 **Usafiri 3**

**Kusoma hadithi**

**Chema**



Chema aliamka mapema. Alijitayarisha haraka. Basi la shule lilifika. Chema aliliabiri. Wanafunzi wengine walikuwa kwenye basi. "Je, kila mtu ameketi?" Dereva aliuliza. "Ndio," wote walijibu. "Kila mtu afunge mkanda wa usalama," alisema dereva. "Kwa nini tufunge mkanda wa usalama tukisafiri?" Cherono aliuliza.

"Hii ni kwa usalama wako, usije ukaanguka na kuumia," alijibu dereva.

Safari ilianza. Kulikuwa na magari mengi barabarani. Askari wa trafiki alisimamisha basi na kuingia ndani. "Kwa nini hujafunga mkanda?" Askari alimuuliza Chema. "Samahani sitarudia tena," alisema Chema. "Lazima ufunge mkanda wa usalama unaposafiri," askari aliendelea. Chema aliufunga mkanda na aliomba msamaha. Safari ikaendelea.

Mali ya Serikali ya Kenya 144

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ch/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** chema, shamba

**U:** Endelea na maneno; chati, shati, chakula.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ch, dh, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 143.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /ch/ /a/ silabi ni cha

**U:** Endelea na silabi; che, chi, cho, dhu, shi.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 143.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** cha ma – chama

**U:** Endelea na maneno; chema, shuleni, dharura.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 143.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **basi, dereva, mkanda wa usalama.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 144.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Basi lilipofika Chema alifanya nini? *(Aliabiri)*

**T:** Dereva alimwambia kila mtu afanye nini? *(Afunge mkanda wa usalama)*

**U:** Taja mambo mengine unayotakiwa kufanya wakati unasafiri. *(Wanafunzi wataje mambo k.m. kutotoa mkono nje ya dirisha)*

### Zoezi

Mwanafunzi ajadiliane na mwenzake umuhimu wa vyombo vya usafiri.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya.

1. Lori 2. Gari dogo 3. Basi

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 144: Usafiri 3

Kipindi cha 143 na 144 **Usafiri 3**

**Kipindi 143**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ch** **dh** **sh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**che** **chi** **cho** **dhu** **shi**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| che ma | shu le ni | dha ru ra | sha mba |
| **chema** | **shuleni** | **dharura** | **shamba** |

**Kipindi 144**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**CH** **ch** **DH** **dh** **SH** **sh**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ya li chacha | ma shambulizi | a li dhalilisha |
| **yalichacha** | **mashambulizi** | **alidhalilisha** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Mkiwa wawili, someni sentensi kisha mpigie mistari herufi kubwa.


1. Chombo hiki ni cha usafiri.
2. Ndege ya Kenya ni kubwa.
3. Mimi husafiri kwa matatu.
4. Maimuna alifika Voi kwa ndege.
5. Barabara hii ilijengwa na Toma.
6. Safari yake imevunjika.
7. Meli ilielea majini.

143 Hakiuzwi

Kipindi cha 143 na 144 **Usafiri 3**

**Kusoma hadithi**

**Chema**



Chema aliamka mapema. Alijitayarisha haraka. Basi la shule lilifika. Chema aliliabiri. Wanafunzi wengine walikuwa kwenye basi. "Je, kila mtu ameketi?" Dereva aliuliza. "Ndio," wote walijibu. "Kila mtu afunge mkanda wa usalama," alisema dereva. "Kwa nini tufunge mkanda wa usalama tukisafiri?" Cherono aliuliza.

"Hii ni kwa usalama wako, usije ukaanguka na kuumia," alijibu dereva.

Safari ilianza. Kulikuwa na magari mengi barabarani. Askari wa trafiki alisimamisha basi na kuingia ndani. "Kwa nini hujafunga mkanda?" Askari alimuuliza Chema. "Samahani sitarudia tena," alisema Chema. "Lazima ufunge mkanda wa usalama unaposafiri," askari aliendelea. Chema aliufunga mkanda na aliomba msamaha. Safari ikaendelea.

Mali ya Serikali ya Kenya 144

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** CH, ch, DH, dh, SH, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 143.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo na usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li chakura – alichakura

**U:** Endelea na maneno; yalichacha, mashambulizi.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 143.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **basi, dereva, mkanda wa usalama.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Sarufi

**Matumizi ya herufi kubwa**

**N:** Eleza matumizi ya herufi kubwa.

Tunatumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi.

Pia herufi kubwa hutumiwa mwanzoni mwa majina ya vitu au mahali.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 143.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore umbo la lori ambalo limebeba mizigo na utie rangi.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 145 **Usafiri 3**

**Kipindi 145**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

DH dh CH ch SH sh

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: cho ma – choma**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| cha | ma | ka | ni | a |
| cho | dha | che | li | sha |

**Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Akifisha sentensi zifuatazo kwa herufi kubwa.

1. baba ataninunulia gari dogo ijumaa.
2. ali na asha walipanda meli.
3. tutazuru ziwa victoria jumatano.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Safari ya Talai**



**Kuandika**

Andika majina ya vyombo vya usafiri unavyovijua.

145 Hakluzwi

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** DH, dh, CH, ch, SH, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 145.**

### Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na mwanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'choma'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

### Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **pikipiki, meli, ndege.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Safari ya Talai**

Shule zilifungwa siku ya Ijumaa. Juma alifunga safari. Alienda kwa shangazi yake Maria. Shangazi aliishi mjini Talai. "Mara hii, nitasafiri kwa matatu," aliwaza Juma. Juma alijitayarisha. Alipomaliza aliondoka nyumbani. Alienda kwenye kituo cha magari. Juma aliabiri matatu. Matatu ilikuwa na runinga. Alijua angefurahia safari.

Mara safari ikaanza. Juma alianza kutazama runinga. Runinga ilionyesha aina mbalimbali za usafiri. Aliona ndege kubwa za abiria. Zilielekea nchi za mbali. Alishangaa jinsi ndege ingepaa angani bila kuanguka. Kipindi hicho pia kilionyesha meli kubwa. Zilionekana zikielea juu ya maji. "Angalia hiyo meli. Ni kubwa kama nyumba!" Juma alitamka. Ghafla, gari lao likasimamishwa kando ya barabara. "Kwani tumefika?" Juma aliuliza mwenzake. "Tumepata panchari. Shukeni nibadilishe gurudumu," dereva akasema. Dereva alibadilisha gurudumu na safari iliendelea.

Barabarani kulikuwa na magari mengine ya usafiri. Kulikuwa na mabasi, malori na magari madogo. Watu wengine walitumia pikipiki na baiskeli. Wengine walitembea kwa miguu. Baada ya muda, Juma aliwasili kwa shangazi yake. "Karibu Juma," shangazi akasema kwa furaha. Juma alifurahi kukutana na shangazi na binamu yake. Juma alikaa na kucheza na binamu yake. Alikaa mpaka shule zikafunguliwa.

### Maswali

**T:** Shule ilifungwa siku gani? *(Shule ilifungwa siku ya Ijumaa)*

**U:** Taja vyombo mbali mbali vya usafiri. *(Matatu, ndege, meli, pikipiki, baiskeli)*

**U:** Je, unafikiri ni njia zipi tunaweza kuzuia ajali tunaposafiri? *(Ajali zinaweza kuzuiwa kwa kuwa makini, kufunga mikanda, kuzingatia sheria za barabarani.)*

### Kuandika

**N:** Mwanafunzi atunge sentensi moja ukitumia neno 'garimoshi'.

**T:** Mwongoze mwanafunzi kutunga sentensi moja akitumia neno 'garimoshi'.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 145 **Usafiri 3**

**Kipindi 145**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

DH dh CH ch SH sh

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: cho ma – choma**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| cha | ma | ka | ni | a |
| cho | dha | che | li | sha |

♦ **Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

Akifisha sentensi zifuatazo kwa herufi kubwa.

1. baba ataninunulia gari dogo ijumaa.
2. ali na asha walipanda meli.
3. tutazuru ziwa victoria jumatano.

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Safari ya Talai**




**Kuandika**

Andika majina ya vyombo vya usafiri unavyovijua.

145 Hakiuzwi

## ♦ Sarufi

**Matumizi ya herufi kubwa**

N: Eleza matumizi ya herufi kubwa.

Tunatumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi.

Pia herufi kubwa hutumiwa mwanzoni mwa majina ya vitu au mahali.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 145.**

**Majibu**

1. Baba ataninunulia gari dogo Ijumaa.
2. Ali na Asha walipanda meli.
3. Tutazuru Ziwa Victoria Jumatano.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya.

1. Ndege
2. Matatu
3. Meli

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 146 na 147 **Marejeleo 3**

**Kipindi 146**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng' ng gh

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ng'e ng'i ngo ngu gha

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng'a tu ka | ngu ru mo | gha la | ma zi ngi ra |
| **ng'atuka** | **ngurumo** | **ghala** | **mazingira** |

**Kipindi 147**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

NG' ng' NG ng GH gh

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| wa li ng'ara | wa li po angalia | wa li gharamika |
| **waling'ara** | **walipoangalia** | **waligharamika** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vizuri, vibaya na hivi**

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. Vizuri
2. Vibaya
3. Hivi
4. Hiki
5. Hawa
6. Huyu
7. Changu
8. Chenu

Mali ya Serikali ya Kenya 146

Kipindi cha 146 na 147 **Marejeleo 3**

**Kusoma hadithi**



**Mazingira**

Siku moja Diba na Habiba walimfuata mama yao sokoni. Walipofika sokoni waliona watu wengi. Watu wengine walikula ndizi na kutupa maganda ovyoovyo. Diba na Habiba walisikia mshindo mkuu. Walipoangalia waliona mama yao ameanguka chini tifu! Walisema, "Pole mama." Walipotazama zaidi waliona ganda la ndizi lilikuwa limetupwa chini. Ganda hili lilimfanya mama akateleza na kuanguka vibaya. Mama alipoamka, aliwaeleza wanawe umuhimu wa kutunza mazingira. Aliwaambia kuwa maganda huchafua mazingira. Takataka inafaa kutupwa mahali panapofaa, kama kwenye pipa la taka. Takataka hazifai kutupwa ovyoovyo barabarani.

147 Hakizuwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ng'/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** ng'onda, ngozi

**U:** Endelea na maneno; ng'atuka, ng'oa, angalau.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ng', ng, gh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 146.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /ng'/ /a/ silabi ni ng'a.

**U:** Endelea na silabi; ng'e, ng'i, ngo, ngu, gha.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 146.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: a nga la u – angalau

**U:** Endelea na maneno; ng'atuka, ngurumo, ghala.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 146.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **maganda, taka, akateleza.**

Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 147.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Ni nani hupenda kufuata wazazi wao wanapoenda sokoni? *(Watoto)*

**T:** Ni akina nani walifuata wazazi wao sokoni. *(Diba na Habiba)*

**U:** Wewe hutupa takataka wapi? *(Wanafunzi watoe majibu yao)*

### Zoezi

Katika vikundi vya watu watano, imbeni wimbo wa taifa.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi akifika nyumbani ashiriki katika shughuli za kudumisha usafi wa mazingira kama vile kuokota takataka au kuosha vyombo.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 147: Marejeleo 3

Kipindi cha 146 na 147 **Marejeleo 3**

**Kipindi 146**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng'** **ng** **gh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**ng'e** **ng'i** **ngo** **ngu** **gha**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ng'a tu ka | ngu ru mo | gha la | ma zi ngi ra |
| **ng'atuka** | **ngurumo** | **ghala** | **mazingira** |

**Kipindi 147**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG'** **ng'** **NG** **ng** **GH** **gh**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| wa li ng'ara | wa li po angalia | wa li gharamika |
| **waling'ara** | **walipoangalia** | **waligharamika** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vizuri, vibaya na hivi**

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. Vizuri
2. Vibaya
3. Hivi
4. Hiki
5. Hawa
6. Huyu
7. Changu
8. Chenu

Mali ya Serikali ya Kenya



Kipindi cha 146 na 147 **Marejeleo 3**

**Kusoma hadithi**



**Mazingira**

Siku moja Diba na Habiba walimfuata mama yao sokoni. Walipofika sokoni waliona watu wengi. Watu wengine walikula ndizi na kutupa maganda ovyoovyo. Diba na Habiba walisikia mshindo mkuu. Walipoangalia waliona mama yao ameanguka chini tifu! Walisema, "Pole mama." Walipotazama zaidi waliona ganda la ndizi lilikuwa limetupwa chini. Ganda hili lilimfanya mama akateleza na kuanguka vibaya. Mama alipoamka, aliwaeleza wanawe umuhimu wa kutunza mazingira. Aliwaambia kuwa maganda huchafua mazingira. Takataka inafaa kutupwa mahali panapofaa, kama kwenye pipa la taka. Takataka hazifai kutupwa ovyoovyo barabarani.



Hakiuzwi

### ■ Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NG', ng', NG, ng, GH, gh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 146.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** wa li ng'atuka – waling'atuka

**U:** Endelea na maneno; waling'ara, walipoangalia.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 146.**

### Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **maganda, akateleza, taka.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Somea mwenzako hadithi.

### ◆ Sarufi

**Matumizi ya 'vizuri' na 'vibaya'**

**N:** 'Vizuri' ni neno linalotumika kumaanisha jambo linapendeza au limefanyika kwa njia inayofurahisha.

Kwa mfano: Mwalimu alitufundisha **vizuri.**

'Vibaya' lina maana kuwa jambo halipendezi au linafanyika kwa njia isiyofurahisha.

Kwa mfano: Dereva aliendesha gari **vibaya.**

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 146.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi ataje mambo matano anayoweza kufanya ili kudumisha usafi wa mazingira nyumbani.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Hakiuzwi

# Kipindi cha 148: Marejeleo 3

Kipindi cha 148 na 149 **Marejeleo 3**

**Kipindi 148**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ny** **dh** **sh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

**nye** **nyi** **dho** **dhu** **sho**

★ Soma maneno ukitumia silabi.

| nyu ngu | u nge dha ni | ma i sha | kwi sha |
|---|---|---|---|
| **nyungu** | **ungedhani** | **maisha** | **kwisha** |

**Kipindi 149**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NY** **ny** **DH** **dh** **SH** **sh**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li nyanyuka | wa li ji dhalilisha | u ta hatarisha |
|---|---|---|
| **alinyanyuka** | **walijidhalilisha** | **utahatarisha** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Andika sentensi hizi kitabuni.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Nchi **yako** ina amani. | Nchi **zenu** zina amani. |
| 2. | Ni kipindi **chako** cha kusoma. | Ni vipindi **vyenu** vya kusoma. |
| 3. | Mwalimu **wako** ni mzuri. | Walimu **wenu** ni wazuri. |
| 4. | Mshipi **wako** umekatika. | Mishipi **yenu** imekatika. |

Mali ya Serikali ya Kenya

148

Kipindi cha 148 na 149 **Marejeleo 3**

**Kusoma shairi**



**Dawa**

Dawa za kila aina, naomba usichezee,
Ugonjwa wa kila namna, daktari wako mueleze,
Kuna chungu na tamu sana, mtoto sisherehekee,
Dawa msinywe dawa, bila wazazi wenu kuwepo.

Dawa za maji twazipenda, ni tamu kama asali,
Za tembe zinatushinda, ungedhani pilipili,
Sindano zinatulinda, kutoka kwa homa kali,
Dawa msinywe dawa, bila wazazi wenu kuwepo.

Dawa usiweke ovyo, ni hatari kwa maisha,
Mtoto akila sivyo, uzima huenda kwisha,
Dawa ukiwacha hivyo, maisha utahatarisha,
Dawa msinywe dawa, bila wazazi wenu kuwepo.

149

Hakluzwi

### Utambuzi wa sauti

Tamka sauti **/ny/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** /nyamaza, nane

**U:** Endelea na maneno; nyangumi, nyani, ngoja, nahodha.

### Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** ny, dh, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 148.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /ny/ /a/ silabi ni nya

**U:** Endelea na silabi; nye, nyi, dho, dhu, sho.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 148.**

### Kusoma maneno kwa kutumia silabi

Tamka kila silabi katika neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U**: nya ngu mi – nyangumi

**U:** Endelea na maneno; nyungu, ungedhani, maisha, kwisha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 148.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **dawa, tembe, utahatarisha.** Mwanafunzi asome msamiati kwenye hadithi kwenye **ukurasa wa 149.**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha shairi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Kusoma shairi

**N/T/U:** Soma shairi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Taja aina za dawa zilizotajwa kwenye shairi hili. *(Maji, tembe, tamu, chungu)*

**T:** Shairi hili linatuelezea kwamba tunywe dawa vipi? *(Mzazi akiwepo)*

**U:** Ukinywa dawa ovyo, nini kitafanyika? *(Utayahatarisha maisha yako)*

### Zoezi

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya:

1. Dawa 2. Maganda 3. Sindano

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike vitu vitatu vinavyopatikana nyumbani.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 149: Marejeleo 3

Kipindi cha 148 na 149 **Marejeleo 3**

**Kipindi 148**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.
  ny dh sh
- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.
  nye nyi dho dhu sho
- Soma maneno ukitumia silabi.
  nyu ngu — u nge dha ni — ma i sha — kwi sha
  **nyungu** — **ungedhani** — **maisha** — **kwisha**

**Kipindi 149**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.
  NY ny DH dh SH sh
- Soma sehemu za neno na neno lote.
  a li nyanyuka — wa li ji dhalilisha — u ta hatarisha
  **alinyanyuka** — **walijidhalilisha** — **utahatarisha**

◆ **Sarufi: Matumizi ya -ako na -enu**

Andika sentensi hizi kitabuni.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Nchi **yako** ina amani. | Nchi **zenu** zina amani. |
| 2. | Ni kipindi **chako** cha kusoma. | Ni vipindi **vyenu** vya kusoma. |
| 3. | Mwalimu **wako** ni mzuri. | Walimu **wenu** ni wazuri. |
| 4. | Mshipi **wako** umekatika. | Mishipi **yenu** imekatika. |

Mali ya Serikali ya Kenya

148

Kipindi cha 148 na 149 **Marejeleo 3**

**Kusoma shairi**



**Dawa**

Dawa za kila aina, naomba usichezee,
Ugonjwa wa kila namna, daktari wako mueleze,
Kuna chungu na tamu sana, mtoto sisherehekee,
Dawa msinywe dawa, bila wazazi wenu kuwepo.

Dawa za maji twazipenda, ni tamu kama asali,
Za tembe zinatushinda, ungedhani pilipili,
Sindano zinatulinda, kutoka kwa homa kali,
Dawa msinywe dawa, bila wazazi wenu kuwepo.

Dawa usiweke ovyo, ni hatari kwa maisha,
Mtoto akila sivyo, uzima huenda kwisha,
Dawa ukiwacha hivyo, maisha utahatarisha,
Dawa msinywe dawa, bila wazazi wenu kuwepo.

149

Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** NY, ny, DH, dh, SH, sh

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 148.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo usome neno upesi.

**N/T/U:** wa li m nyanyasa – walimnyanyasa

**U:** Endelea na maneno; alinyanyuka, walijidhalilisha.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 148.**

## Msamiati

Mkumbushe mwanafunzi maana ya msamiati **dawa, tembe, utaharisha.**

## Kusoma shairi

**U:** Somea mwenzako shairi.

## Sarufi

**Matumizi ya -ako na -enu**

**N:** Tunatumia '-ako' kuonyesha kitu cha mwenzako.

Kwa mfano; Jani **lako** ni kubwa.

'-enu' hutumiwa kuonyesha wingi wa vitu vya wenzako.

Kwa mfano; Majani **yenu** ni makubwa.

**U:** Mwanafunzi asome sentensi za sarufi kwenye hadithi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 148.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi andike mambo matatu ambayo hafai kufanya anapopewa dawa hospitalini.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 150 **Marejeleo 3**

**Kipindi 150**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

gh ng ng' ny sh th

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: shu ngi – shungi**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| sho | o | ngi | zi | ka |
| nyo | ngu | shu | nga | sha |

◆ **Sarufi: Matumizi ya vitenzi**

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. Jenga 2. Kula 3. Vuka

Tazama picha. Sikiliza mwalimu akisoma hadithi.

**Shule yangu**



**Kuandika**

Andika mambo ambayo umejifunza kutokana na shairi la **Dawa**.

Mali ya Serikali ya Kenya 150

## Ufahamu wa herufi

Onyesha herufi. Taja jina la herufi. Tamka sauti.

**N/T/U:** gh, ng, ng', ny, sh, th

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti kwenye **ukurasa wa 150.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi kuunda neno 'shungi'.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno.

## Hadithi ya mwalimu

Funza msamiati; **madawati, mihogo, kucha.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

Soma hadithi huku mwanafunzi akisikiliza na kutazama picha. Hakiki utabiri.

**Shule yangu**

Shule yangu inaitwa Bondeni. Mimi ni mwanafunzi katika darasa la pili. Darasa letu lina madawati, vitabu, kalamu na vifutio. Sisi huketi darasani tunaposoma. Mwalimu wetu hutufunza masomo mengi. Sisi husoma Hesabu, Kiingereza, Kiswahili na mengine.

Darasa letu lilikuwa karibu na choo. Mara kwa mara tulitatizika na harufu ya choo. Choo hicho kilibomolewa na kujengwa mbali na darasa. Somo nilipendalo ni la Kiswahili. Mwalimu wetu hutufunza mambo mengi. Sisi husoma kuhusu sehemu za mwili. Sehemu hizi ni macho, pua, mdomo, mikono na miguu. Mwalimu hutufunza usafi wa mwili. Yeye husema," Kila mwanafunzi akate kucha ndefu, anyoe nywele, aoge na kusafisha nguo zake."

Sisi husoma kuhusu vyakula vya kiasilia. Vyakula hivi ni muhimu kwa afya yetu. Vyakula hivi ni kama mihogo, viazi, mahindi na maharagwe. Mbali na hayo mwalimu hutufunza siku za wiki. Ninazijua siku zote. Mwalimu wetu hutufunza kuwa wiki ina siku saba. Wazazi wangu hufanya kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Sisi hatuendi shuleni siku ya Jumamosi. Jumapili, sisi huenda kumwomba Mungu. Sisi huwatembelea wagonjwa na mayatima baada ya kuomba. Mimi huongea lugha ya Kiswahili. Ninaipenda lugha yangu.

## Maswali

**T:** Ni vitu gani vinavyopatikana darasani? *(Darasani kuna madawati, vitabu, kalamu na vivutio)*

**U:** Ni vyakula gani vilivyotajwa kwenye hadithi? *(Mihogo, viazi, mahindi na maharagwe)*

**U:** Kwa nini watu humwomba Mungu? *(Majibu ni kama, ili kupata Baraka na kadhalika)*

## Kuandika

**N:** Mwanafunzi atunge sentensi moja kuhusu ulichofunza kutokana na shairi la dawa.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika lililopo kwenye **ukurasa wa 150.**

## Sarufi

**Matumizi ya vitenzi**

Andika maneno haya ubaoni: chora, panda, na vua.

Eleza maana ya maneno ya vitendo. Maneno ya vitendo ni yale ambayo yanaonyesha kutendeka kwa jambo fulani. Kama vile chora, panda, na vua. Maneno haya huonyesha hali ya kitendo.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 150.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aigize vitendo hivi.

1. Ruka 2. Soma 3. Kimbia

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

JAMHURI YA KENYA
Mali ya
Serikali ya Kenya
HAKIUZWI

# Kiswahili 2

## Mazoezi ya Lugha

### Mwongozo wa Mwalimu

Mwongozo huu wa mwalimu wa gredi ya 2 umetayarishwa kwa kurejelea pakubwa mbinu za utafiti ili kumsaidia mwalimu anapofundisha kuwasaidia wanafunzi kukuza ujuzi wao katika lugha ya Kiswahili. **Mwongozo huu umeshughulikia uhusiano na maadili, uhusiano na masuala mutambuko, sehemu nne za ujifunzaji lugha – kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika, vilevile mada zote na maadili yaliyojadiliwa katika mtaala.** Mwongozo huu unamwezesha mwalimu kuwapa wanafunzi wa gredi ya 2 mbinu tofauti za kusoma, kujifundisha na kujitathmini na hivyo basi kuakifia malengo lengwa kwa kurejelea sehemu husika za kipindi/somo.

Mwongozo huu unarejelea yaliyojiri wakati wa muda wa majaribio ya Tusome. Tusome imedhaminiwa na USAID na kutekelezwa na Wizara ya Elimu. Malengo ya kitabu hiki ni kuwa wanafunzi watakaokamilisha vipindi na masomo kwenye vitabu vya wanafunzi watakuwa wamejikimu na ujuzi wa kuweza kusoma katika gredi ya 2. Pia, wanafunzi wataweza kusoma kwa ufasaha na kuelewa wanachokisoma na kuandika. Hivyo, wanafunzi wakimaliza masomo ya gredi ya 2 watakuwa na uwezo wa kusoma na kujifunza kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya ujifunzaji katika gredi za juu.

Vipengele muhimu vilivyopewa kipao mbele kwenye mwongozo huu wa gredi ya 2 ni:

- Shughuli za ufundishaji ambazo ni za kufurahisha wakati wa kufundisha mada zilizomo kwenye mtaala KICD.
- Mpangilio maalum wa shughuli za ufundishaji zilizopangwa kwa mtiririko na msambao ufaao kwa kurejelea utafiti uliofanywa katika kufunza na kujifunza Kiswahili.
- Nakala za kitabu cha mwanafunzi kenye mwongozo huu ili kumwenzesha mwalimu kufanya marejeleo ya moja kwa moja na kwa urahisi anapofundisha.
- Hadithi tamu zinazolandana na tamaduni na umri wa mwanafunzi zitakazo msaaidia pakubwa katika kukuza ujuzi wake wa kusoma.
- Maelekezo yaliyopangwa vizuri kumwongoza mwalimu katika kuutumia mwongozo kwa urahisi.
- Hadithi zilizoandikwa za kiwango cha mwanafunzi na rahisi kusoma ambazo zitamwenzesha mwanafunzi kusoma na kuelewa hadithi husika.
- Hadithi za mwalimu ambazo zinalenga kukuza msamiati na ujuzi wa kusikiliza wa mwanafunzi.

Mwongozo huu umetayarishwa na wataalamu wenye tajriba kubwa kutoka Wizara ya Elimu, Tume ya Huduma ya Walimu, Taasisi ya Masomo Maalumu ya Kenya, na Taasisi ya usimamizi wa Elimu nchini Kenya.

USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa U.S. Agency for International Development (USAID) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

ISBN 978-9966-110-17-4

© 2018